**14 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 14 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO, NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Na. 304

### Kulinda Maslahi ya Watumishi Wanawake kwenye Sekta Binafsi

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza: -

Je, kiasi gani Serikali inalinda haki ya kufanya kazi kwa Watumishi Wanawake wa Sekta Binafsi na zisizo rasmi wanaoachishwa baada ya ujauzito?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kulinda haki za wafanyakazi wote nchini wakiwemo wanawake. Hatua hizo ni pamoja na: -

(a) Kuzifanyia marekebisho Sheria ya Kazi ikiwemo iliyopitishwa na Bunge mwezi Februari 2025, ambayo pamoja na mambo mengine imeboresha haki ya likizo ya uzazi kwa wafanyakazi wanawake wanaojifungua Watoto Njiti;

(b) Kutoa Mwongozo kwa waajiri wa kuandaa sera ya kuondoa ubaguzi katika maeneo ya kazi;

(c) Kuendelea kufanya kaguzi maeneo ya kazi na kuchukua hatua stahiki pindi inapobainika kuwepo kwa ukiukwaji; na

(d) Kutoa elimu kwa wafanyakazi ili kuwawezesha kufahamu haki zao, ikiwemo haki ya kufungua mashauri *CMA* endapo wameachishwa kazi isivyo halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu na mamlaka zinazohusika na wananchi kwa ujumla, kushirikiana na Serikali kutoa elimu ili kuhakikisha watumishi wanawake katika sekta zilizotajwa wanazielewa vizuri haki zao, ikiwemo haki ya kuwasilisha changamoto wanazokabiliana nazo kwenye vyombo vya utatuzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa vile kumekuwa na wimbi kubwa sana la

wafanyakazi wanawake wa Sekta Binafsi na zisizo rasmi wanawake kupata ujauzito au kujifungua, huwa hawarejeshewi mikataba yao kwa sababu wanahofia hiyo likizo ndefu ya uzazi. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani kuwatetea wanawake hawa wa Sekta Binafsi na zisizo rasmi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ninapongeza kwa sheria nzuri za kazi ambazo tumezipitisha, lakini Serikali ina mpango gani kuongeza nguvu ya rasilimali watu na fedha kwenye vyombo vya ukaguzi mahali pa kazi, ili waende kwa wingi wakaone *compliance* ya sheria zile za waajiri kwa wanawake hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Dkt. Kaijage kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza, amekuwa mfuatiliaji mzuri wa masuala ya haki za wafanyakazi na wanawake lakini katika sekta zote. Ukweli ni kwamba, tayari kwenye mazingira ambayo mwanamke anapata ujauzito kazini, kwanza ni haki yake ya kisheria na imelindwa na msingi wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na imetambua kwamba inapotokea anapata ujauzito anayo haki ya kupewa likizo ya uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo, kwa umuhimu ambao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliuona, tulifanya mapitio ya sheria kuangalia hata wale wanawake wanaojifungua Watoto Njiti wakaongezewa siku, ukiacha zile siku za kawaida. Ikitokea amepelea katika kujifungua ndani ya wiki 36 labda imefika mpaka 40 na ndipo inaanza kuhesabika likizo yake ya uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine pia anayo haki wakati wa baada ya kuwa amejifungua kupewa hii likizo, ni pamoja na mwenza wake kupewa siku za kuweza kumhudumia.

Sambamba na haki hiyo, inaendana na haki ya mjamzito kupewa muda wa kwenda kunyonyesha katika kipindi chote ambacho atakuwa ananyonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ikitokea kuna mwajiri ambaye anamfukuza mfanyakazi kwa sababu ya kupata ujauzito au mtoto labda pengine kwamba amejifungua na hiyo kwenye sheria inatajwa kuwa ni *unfair termination* na hatua zipo ambazo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashauri, ikitokea mwananchi yeyote au mwanamke yeyote ameona sababu za kufukuzwa kwake kazi zinapelekea au kuna viashiria vya kwamba imesababishwa na yeye kupata ujauzito au kujufungua, alifikishe shauri hilo mara moja kwa Afisa Kazi wa Mkoa husika na baadaye ashauriwe namna ya kupeleka shauri lake *CMA (Commission for Mediation and Arbitration)* kwa ajili ya hatua zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Iddi Kassim.

Na. 305

**Hitaji la Mabweni Shule ya Msingi Segese – Msalala**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mabweni ya Watoto wenye Mahitaji Maalum katika Shule ya Msingi Segese?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa Fedha 2022/2023 – 2023/2024, Shule ya Msingi Segese ilipokea shilingi milioni 308 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya watoto wenye mahitaji

maalum. Ujenzi wa bweni la wasichana umekamilika, ujenzi wa bweni la wavulana upo hatua za mwisho za ukamilishaji. Aidha, kibali cha matumizi ya bweni la wasichana chenye barua Kumb. Na. EA.295/315/22/139 kilitolewa tarehe 4 Machi, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, shilingi milioni 323.7 zimetengwa kupitia *CSR* kwa ajili ya ujenzi wa uzio na nyumba ya mlezi. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji kwa watoto wenye mahitaji maalum ikiwemo watoto wa Shule ya Msingi Segese kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ninawapongeza Serikali kwa hatua hiyo. Swali langu la kwanza la nyongeza; kwa kuwa tayari Ofisi ya Mbunge kupitia Mfuko wa Jimbo mmeshatenga shilingi milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la shule ya sekondari Kata ya Shilela. Ni lini sasa Serikali na yenyewe itatenga fedha kwa ajili ya kuweza ku-*support* na kumalizia ujenzi wa bweni hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa wadau wa Kata ya Bulyan'hulu wako tayari na wameshatenga eneo nami kama Mbunge niko tayari kuchangia kiasi cha shilingi milioni 10, Nini *commitment* ya Serikali sana kuleta fedha kwa ajili ya kumalizia bweni hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Iddi Kassim kwa kazi kubwa anayoifanya na yeye mwenyewe akiunga jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba Sekta ya Elimu inaweza kuimarika na hasa kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana wa kuendelea kuboresha miundombinu katika Sekta hii muhimu ya Elimu Msingi. Katika kipindi cha miaka minne tayari Serikali ya Awamu ya Sita imejenga mabweni mapya 738 lakini imefanya ukamilishaji wa mabweni 1,216, na Serikali inaendelea na jitihada hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba niyajibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja. Napenda kumhakikishia kwamba jitihada zake hizi za kuunga mkono Serikali kwa kutenga fedha, kupitia Mfuko wa Jimbo shilingi milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni aliyoyataja, Serikali itaunga mkono na itafika katika maeneo haya aliyoyataja kwa ajili ya kuhakikisha mabweni yanajengwa ili kuendelea kuimarisha Sekta ya Elimu Msingi katika jimbo lake na kwa Tanzania kwa ujumla wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kata ya Masama Magharibi wametenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa mabweni, wameweka matofali wameweka na mawe na kuna uhitaji mkubwa sana wa kujenga mabweni ya wavulana na wasichana katika shule hii. Serikali ina mpango gani wa kutuletea fedha za kujenga mabweni katika shule hii ya Kyuu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambaye amekuwa akifuatilia kwa ukaribu kabisa Sekta hii muhimu sana ya Elimu Msingi na hasa kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niendelee kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita za kufanya uwekezaji na kuimarisha miundombinu katika Sekta muhimu hii ya Elimu Msingi zitaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua jitihada kubwa sana na ninatumia nafasi hii kuwapongeza ndugu zetu wa Masama Magharibi kwa kuonyesha jitihada za kuunga mkono juhudi za kimaendeleo katika jimbo lake. Ninamhakikishia kwamba Serikali itafika kuunga mkono na kuweka fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika Kata hii ya Masama Magharibi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa Shule ya Dakama *Secondary* iliyoko katika Halmashauri ya Ushetu iko barabarani na haina uzio. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga uzio? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava ambaye amekuwa akiuliza maswali na akifanya ufuatiliaji wa kuhakikisha kwamba katika mkoa anaouwakilisha Sekta ya Elimu Msingi inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava kwamba, kupitia fedha za ndani za halmashauri Serikali itafika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inajenga uzio katika shule hii ya Dakama *Secondary* aliyoitaja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaendelea kuimarisha usalama wa wanafunzi, lakini usalama wa mali za shule.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ngassa.

Na. 306

### Usambazaji wa Umeme Vitongoji vya Igunga

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kusambaza umeme kwenye Vitongoji vya Jimbo la Igunga?

**NIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Igunga lina jumla ya vitongoji 337 ambapo kati ya hivyo, vitongoji 95 vimepatiwa umeme, vitongoji 15 wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa miradi kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Pili A na vitongoji 69 zabuni imetangazwa kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya IIB. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* itaendelea kutenga fedha za kuvipelekea umeme vitongoji 158 vilivyosalia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuishukuru Serikali hususan Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na hatimaye wameweza kutupatia vitongoji vipya 69 kuingia kwenye mchakato, vikiwepo Vitongoji vya Mwalunju, Mwakule, Mwahobelo, Kagera, lakini pia na vitongoji vingine mpaka kule kwetu Mwamatiga, Mwamashimba. Ninaishukuru sana Wizara kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, changamoto kubwa ambayo imekuwa ikipatikana kwenye uunganishaji wa umeme kwenye ngazi za vitongoji ni lile suala la lazima umeme wa *Line* ya *MV* uwepo, kwa maana ya *line* kubwa. Sasa, wameshatangaza hivi vitongoji na kuna uwezekano wakakuta baadhi ya maeneo hakuna hyo *line*. Ipi kauli ya Wizara katika kuhakikisha wananchi wote wa Jimbo la Igunga wanafikiwa na umeme na kwa bei ya shilingi 27,000? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge na tunashukuru kwa pongezi zake. Kuhusiana na vitongoji hivi 69 ambavyo vinaenda kutekelezwa katika Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya IIB.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika awamu ya vitongoji 15 vya kila Mbunge ulikuwa ni mradi wa ujazilizi na tulikuwa tunapeleka umeme na tunaendelea kupeleka umeme katika vitongoji ambavyo vimepitiwa na *line* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ambao utaenda kuanza hivi karibuni ni wa tofauti kidogo. Ni mradi ambao ni *hybrid*, unahusisha vitongoji ambavyo havina *line* kubwa, lakini na vitongoji ambavyo vilevile vina *line* kubwa. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa vitongoji vyake 69, vile ambavyo pia havitajipitiwa na *line* kubwa na vyenyewe vitanufaika katika mradi huu. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Gharama ya kuweka umeme vijijini ni shilingi 27,000 na Chemba ipo kwenye orodha ya vijiji Tanzania. Sasa, ni kwa nini kwenye Kijiji cha Chemba wanatoza shilingi laki tatu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika maeneo ya vijiji gharama ya kuunganisha umeme ni shilingi 27,000. Kwa kijiji ambacho Mheshimiwa Mbunge amekizungumza mahsusi, nikitoka hapa nitafuatilia na kisha nitampa majibu ambayo yatamridhisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini

mkandarasi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vya Manyoni ataanza kazi? Ninashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge na ninaamini anazungumzia Vitongoji 15 vya kila Mbunge. Iko mikoa mitatu ambayo tulichelewa kupata wakandarasi ikiwemo Mikoa ya Mbeya, Tanga na Singida. Hata hivyo, jambo la heri ni kwamba, tumeshapata mkandarasi na hivi tunavyoongea timu yetu ya Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* tayari wako kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida wakitambulisha mradi huo na wakimtambulisha mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge mradi huu utaanza hivi karibuni kwa sababu mkandarasi leo atakabidhiwa *site*. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kajege nilikuona umesimama.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi ni muhimu sana katika uchumi wa Jimbo la Mwibara lakini unahitaji sana umeme ili uweze kuendelea. Je, ni lini Serikali itasambaza umeme katika vitongoji vilivyobakia? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Serikali ilikuwa ina mradi wa kimkakati wa kupeleka umeme katika maeneo ya uzalishaji, ikiwemo maeneo ya migodi midogo, viwanda, maeneo ya uvuvi na maeneo yote ambayo yanachagiza shughuli za kiuchumi. Mradi huu umefikia zaidi ya maeneo 3,000 ikiwemo vituo vya afya na visima vya maji vilevile, kwa maeneo ambayo yanatoa huduma za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali ilishaanza kupeleka umeme katika maeneo ya kimkakati yanayochagiza shughuli za kiuchumi na shughuli za kijamii. Kwa maeneo ya vitongoji, Serikali inayo miradi. Sasa hivi tuna mradi wa takribani vitongoji 3,000 vya kupeleka umeme, kwenye vitongoji 15 vya kila Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunaenda kuanza mradi mkubwa wa vitongoji 9,000 kwa majimbo mbalimbali. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge jimbo lake na lenyewe litanufaika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Jonas Zeeland.

Na. 307

**Kupeleka Umeme Vitongoji vya Mvomero**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye Vitongoji vyote vilivyobaki katika Wilaya ya Mvomero?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mvomero lina jumla ya Vitongoji 687 ambapo kati ya hivyo, Vitongoji 385 vimepatiwa umeme, vitongoji 20 Wakandarasi wanaendelea na kazi ya utekelezaji wa miradi kupitia Mradi wa Ujazilizi *(Densification IIB)* na Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya IA. Vitongoji 97 zabuni imetangazwa kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya IIB. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kupeleka umeme katika Vitongoji 185 vilivyosalia kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja dogo la nyongeza.

Wilaya ya Mvomero ina vijiji 130, vijiji 60 havikuwa na umeme, tunamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassana, katika kipindi chake vijiji 59 tayari umeme umeshakwenda, vingine vimewashwa, vingine vipo kwenye utaratibu wa kuwasha. Kuna kijiji kimoja cha Mkata, kipo katika Kata ya Msongozi, nilifuatilia kwa nini mpaka leo umeme haujapelekwa wanasema eti walikisahau kwenye mkataba wa Mkandarasi! Je, nini kauli ya Serikali juu ya hiki Kijiji cha Mkata? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kijiji hicho kwa bahati mbaya kilisahaulika, lakini ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tulishakichukua na tumeshaongea na Mkandarasi, nitaendelea kuwafuatilia *REA* na kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, nimwelekeze Mkurugenzi Mkuu wa *REA* afuatilie kijiji hicho apeleke Mkandarasi na umeme uweze kuwaka katika Kijiji cha Mkata. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, vitongoji vya Kabatini, Mtapenda, Kahelele na Ntumba ni miongoni mwa vitongoji vikubwa ndani ya Wilaya ya Tanganyika vyenye hadhi ya kijiji. Ni lini Wizara itapeleka umeme kwenye vitongoji hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mradi ambao unakuja wa kupeleka umeme katika vitongoji wa awamu ya IIB unahusisha pia Jimbo la Tanganyika. Katika vitongoji ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge tutaenda kuvitazama kama vipo katika mpango ambao tumeuweka sasa hivi. Kama havipo basi tutashauriana kuona

namna gani tunaweza tukaviongeza katika mradi huo ambao tunategemea utaanza hivi karibuni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mchungahela.

Na. 308

**Kuwatumia Wafungwa katika Kuzalisha Chakula**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuwatumia Wafungwa kuzalisha chakula chao wenyewe badala ya kununua?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Magereza limeandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2025/2026 hadi 2029/2030 wa kujitosheleza kwa chakula cha Wafungwa na Mahabusu. Mpango huo unatekelezwa kwa kuboresha kilimo cha umwagiliaji ambacho kitaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula hadi kufikia tani 46,267 za mahindi, tani 6,359 za mpunga, tani 7,757 za maharage na tani 1,750 za mafuta ya kula ifikapo Juni, 2030. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa kwa sasa hivi wamekuwa wakiishi kwa kutegemea ruzuku wakiwa gerezani, hali kadhalika hata wakitoka nje wamekuwa wakiishi kwa shida sana. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha sasa kwamba wanafanya uzalishaji wenye tija ambao utawapatia mazao mengi ili kusudi waweze kuuza, wapate kutosheleza mahitaji yao yote pia na kupata mitaji pale wanapoweza kutoka nje. Serikali wana mkakati gani kwenye hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, mkakati madhubuti wa Serikali ni huu wa miaka mitano wa kuhakikisha kwamba tunazalisha chakula cha kutosha, kwanza kuwatosheleza wafungwa na mahabusu waliopo magerezani lakini pia hata kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali ndiyo huu, ndani ya miaka mitano tuhakikishe kwamba uzalishaji unakuwa na tija na wa kutosheleza chakula cha Wafungwa na Mahabusu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Mawasiliano ya Habari na Teknolojia. Waheshimiwa Wabunge leo hamna maswali ya nyongeza?

Waheshimiwa Wabunge, leo hamtaki maswali ya nyongeza? au mnawasiliana na majimboni? Mheshimiwa Gallos Tauhida, kwa niaba Dkt. Mnzava. *(Kicheko)*

Na. 309

**Kudhibiti Ukatili Unaofanywa kwa Wanawake kupitia Mitandao ya Kijamii**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti udhalilishaji na ukatili kwa Wanawake unaofanywa kupitia Mitandao ya Kijamii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendesha kampeni za kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii. Elimu hii imetolewa kwa makundi mbalimbali yaliyojumuisha wanafunzi wa Shule za Sekondari pamoja na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na wadau wengine wamefanya majadiliano kuhusu njia za kuimarisha usalama wa mitandao na kupambana na uhalifu mitandaoni, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022 zilizotungwa mahsusi kwa ajili ya kulinda watumiaji wa mtandao, hasa wanawake, dhidi ya unyanyasaji na ukatili wa mtandaoni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, kumekuwa na matukio mbalimbali katika mitandao ya kijamii ikionesha baadhi ya shule wanafunzi wakifanya matukio ambayo ni kinyume cha sheria na ni udhalilishaji. Je, Serikali imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, kumekuwa na matukio mengi ambayo yanaashiria udhalilishaji katika mitandao. Je, Serikali imeshawachukulia hatua kwa kiasi gani wale ambao wanafanya uhalifu huo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Dada yangu Daktari, kwa kuuliza maswali yenye afya kwa ajili ya umma kwa lengo la kuona kabisa pamoja na ulimwengu sasa

unashuhudia ukuaji mkubwa na kasi ya teknolojia, lakini vilevile matumizi yawe sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ambazo Serikali imechukua kwa hawa ambao wanafanya makosa ya kijinai, maana kufanya matendo ambayo hayana adabu na yote ambayo tumeweza kuyashuhudia mengi tumeona yanashughulikiwa na Jeshi la Polisi, wameshachukuliwa hao ambao wamefanya hayo na sheria inafuata mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kiasi ambacho tumeweza kukifanyia kazi kwa makosa mbalimbali ya mtandaoni ni zaidi ya 50% ya makosa yaliyojitokeza yameweza kufanyiwa kazi na taratibu mbalimbali za kisheria zimeweza kuchukuliwa dhidi yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Baadhi ya wahanga wa ukatili mitandaoni wamekuwa wakitolewa picha zao bila ridhaa yao. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na jambo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali kutoka kwa Mheshimiwa Fatma Toufiq, kauli ambayo ninaweza kuitoa kwa kutumia Bunge lako Tukufu ni kuendeleza kutoa elimu, wataalam wetu waendelee kutoa elimu bila kuchoka, hasa wataalam wetu kutoka *TCRA* vilevile na Jeshi la Polisi. Kwa sababu kutumia taarifa za mtu bila idhini yake ni kosa la jinai na tunamshukuru Mheshimiwa Rais, ameweza kuunda taasisi maalum inayolinda taarifa za mtu binafsi, hivyo sheria itachukua mkondo wake bila kuona aibu kwa yeyote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mtinga.

Na. 310

**Kuwa na Maafisa Ugani Katika Kila Kijiji**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kupeleka Maafisa Ugani katika kila Kijiji nchini kwa kuwa bajeti ya kilimo imeongezeka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Lengo la Serikali ni kuajiri Maafisa Ugani kwa Vijiji 12,333 na Kata 3,956 za Tanzania ili kutoa huduma za ugani zitakazosaidia kuongeza tija na uzalishaji. Hata hivyo, Maafisa Ugani waliopo ni 6,748 sawa na 41.43% ya mahitaji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya kuongeza tija na uzalishaji, Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Ugani kwa awamu ambapo kati ya mwaka 2021 na 2024, imeajiri Maafisa Ugani 941. Pia, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na sekta binafsi, inatekeleza programu mbalimbali ikiwemo *BBT,* ambapo wahitimu wa vyuo katika fani ya kilimo hupata ajira za muda.

Mheshimiwa Naibu Sika, hadi kufikia Machi 2025, ajira 1,237 zimetolewa kupitia *BBT* Ugani katika tasnia za pamba 737 na korosho 500. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya kidijiti na kuwapatia Maafisa Ugani vitendea kazi ili kuwafikia wakulima wengi kwa muda mfupi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, kama jibu linavyosema 41% tu ya vijiji ndiyo ina Maafisa Ugani na hii ndiyo muajiri mkuu wa Tanzania suala la Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali imekuwa ikifanya jambo zuri la kupeleka mbolea ya ruzuku, mbegu za

ruzuku kwenye mikoa yote na hasa Mkoa wangu wa Singida, Serikali haioni sasa kwamba ni jambo la dharura kuhakikisha kwamba Maafisa Ugani wanakwenda kwenye vijiji vyote ili hii mbolea ya ruzuku na hizi mbegu za ruzuku wakulima waweze kupanda vizuri na kutumia hizi mbegu vizuri ili tija iweze kuonekana, kuliko kuendelea kupeleka ruzuku wakati wananchi wanapanda alizeti wengine wanamwaga, wengine wanapanda vile vipimo, hili ni jambo la dharura. Je, Serikali haioni kwamba ni dharura sasa kupeleka Maafisa Ugani katika vijiji vyote, kwa sababu hili ni jambo la muhimu na ni ajira kwa Watanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na maoni ya Mheshimiwa Mbunge Mtinga, kwamba Serikali tunaona hiyo haja na ndiyo maana tunatambua wote kwamba ajira zinazingatia bajeti ambayo tunayo na mahitaji. Ndiyo maana moja ya jambo kubwa ambalo sasa hivi Wizara ya Kilimo tunalifanya, tunatengeneza kama *application* ile ama mfumo ambao mwananchi wa kawaida anaweza kum-*trace* Afisa Ugani mahali popote alipo na akam-*request* kama unavyofanya kwenye *Uber* akaja katika eneo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huo mfumo tunaendelea kuu-*develop* wakati huu kukiwa na hilo *gap* la Maafisa Ugani, lakini wakati huo huo Serikali itaendelea kuajiri katika vijiji vyote kulingana na fedha itakapokuwa inapatikana na bajeti tunavyotengewa, lakini na mahitaji katika maeneo yote. Hivyo jambo hilo sisi tunalizingatia na lipo katika mipango ya Serikali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Simiyu tuna upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani, Wilaya ya Busega, Bariadi, Itilima, Meatu na Maswa. Je, ni lini Serikali italeta Maafisa Ugani wa kutosha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi, Serikali tutaendelea kuajiri katika Mikoa, hususani Simiyu na ndiyo maana ukiona kwenye jibu la msingi hapa utaona katika Tasinia ya Pamba tumeajiri Maafisa Ugani 737 ambao wapo katika Mikoa hiyo inayozalisha pamba, hususani Simiyu ambako pamba zaidi ya 60% inatoka huko. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusiana na ajira za Maafisa Ugani, nilitaka kujua Serikali imejipangaje kwa ajili ya kuwapatia usafiri Maafisa Ugani hao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Malembeka kwamba, moja ya kazi nzuri aliyofanya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake ni kugawa pikipiki kwa Maafisa Ugani wote nchini kama sehemu ya usafiri kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, kwa niaba Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

Na. 311

**Kiwanda cha Viuatilifu Kibaha**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA K.n.y. MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, ni faida kiasi gani inapatikana katika Kiwanda cha Viuatilifu Kibaha na je, Kiwanda hicho kimefikia malengo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kiwanda cha Viuadudu cha Tanzania *Biotech Products Limited* cha Kibaha kimepata mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na vijana wa Kitanzania 83 kupata ajira na ujuzi wa teknolojia ya bidhaa za kibailojia, lakini pia kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa malaria nchini kwa kuzalisha na kusambaza dawa ya viuadudu katika kipindi cha miaka minne 2021 mpaka 2025, ambapo jumla ya lita 754,423 zimezalishwa na kusambazwa katika Halmashauri mbalimbali nchini na wadau wengine. Pia kuuza dawa za Viuadudu kwa nchi nyinginezo ikiwemo Kenya, Angola, Niger, Botswana, Namibia, Eswatini, Mozambique na Uganda ambapo jumla ya lita 288,444 zenye thamani ya zaidi shilingi bilioni 3.6 zimeuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kiwanda hicho kinafikia lengo la uzalishaji wa lita milioni sita kwa mwaka. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kuna taarifa kwamba bidhaa hii inachangamkiwa sana nchi za nje kuliko hapa nchini kwetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuitangaza rasmi hasa ili iweze kueleweka dawa hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Wizara ya Biashara imewahi kukaa pamoja na TAMISEMI na Wizara ya Afya ili kwa pamoja kupanga mkakati maalum wa kuweza kuitumia bidhaa hii ili kutokomeza Malaria ambayo yameenea sana katika nchi yetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninatumia nafasi hii kwanza kumpongeza sana muuliza swali, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, ambaye amekuwa akifuatilia sana lakini pia Mheshimiwa Khalifa, ambaye ameuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli dawa hii ya viuadudu ambayo inaua mazalia ya malaria inauzwa sana nje kama nilivyosema kwenye takwimu hapa, lakini pia hata sisi tunafanya hiyo kazi. Kwa hiyo moja, tunaendelea kuitangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la la pili ambalo linahusisha kabla tulikuwa tunauza kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI ambao tuna mkataba mahsusi wa kusambaza viuadudu au viuatilifu hivi kwenye Halmashauri zetu. Sasa nini tunafanya badala ya kutumia tu Serikali tumeanza kuhamasisha na wananchi wa kawaida, binafsi waanze kununua ili waweze kunyunyiza kwenye mazalia, ndiyo maana sasa tunazalisha kwa kiwango kidogo, ambacho unaweza kununua kwa shilingi elfu moja, elfu mbili, elfu tatu ili kila mmoja majumbani humu aweze kununua na kunyunyiza kuua mazalia ya mbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi katika swali lake la pili, tayari Serikali inaendeleza mpango huo wa kushirikiana kama nilivyosema kupitia Wizara ya Afya na TAMISEMI. Zaidi ya fedha shilingi milioni 700 kwa mfano, Mwaka wa Fedha 2023/2024 zilitengwa kwa ajili ya kununua viuadudu hivi na sasa tunaendelea kufanya hiyo kazi kutenga fedha zaidi ili kudhibiti mazalia ya mbu katika Halmashauri zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa 2025 Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa zaidi ya shilingi bilioni 4.5 kwenye Shirika letu la Maendeleo la Taifa *(NDC)* ambao ndiyo wanasimamia uzalishaji wa viuadudu hivyo. Kwa hiyo maana yake ni nini, mwaka huu tunazalisha zaidi na tunaamini tutasambaza zaidi kwenye Halmashauri zetu hapa nchini. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Tarimo.

Na. 312

**Ukarabati wa Uwanja wa Ndege Moshi**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, lini ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Moshi utakamilika ikiwa ni pamoja na kuwalipa fidia wale waliopisha upanuzi?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi unatekelezwa kupitia fedha za Serikali *(GoT)* ambapo utekelezaji wake kwa sasa umefikia 66%. Wizara inaendelea na ufuatiliaji wa fedha hizo kutoka Serikalini kwa ajili ya kumlipa mkandarasi ili aweze kukamilisha kazi zilizosalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi huu, taratibu zinaendelea na mara baada ya taratibu hizo kukamilika Serikali italipa fedha hizo kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Kwanza, niipongeze Serikali kwa majibu haya mazuri, lakini mpango huo na niwatakie utekelezaji mwema, lakini ninalo swali moja la nyongeza. Je, baada ya kukarabati haya maeneo ya nje pamoja na *run way,* Serikali itaanza lini ukarabati wa lile jengo la wageni ili liendane na ukarabati unaofanyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Tarimo, kwa sababu amekuwa ni mfuatiliaji wa karibu sana wa maendeleo ya Jimbo lake, lakini kipekee ujenzi wa uwanja huu muhimu kwa kihistoria na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaanza taratibu za ujenzi kama nilivyosema *run way* na miundombinu mingine. Hebu tumalize kwanza hili la kwanza, likikamilika tuchukue swali lake la nyongeza kama moja kati ya mambo muhimu ambayo tuanze kuchakata Serikalini ili tuje tuanze sasa pia na ukarabati wa jengo hilo lakini kwa sasa hivi hebu tumalize kwanza kazi ambazo tumeshaanza tayari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi hii. Uwanja wa Ndege wa Newala ulitumiwa sana wakati wa harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika lakini uwanja ule sasa ulishakuwa makazi ya watu na Halmashauri ya Mji wa Newala imetenga eneo kubwa kwa ajili ya uwanja wa ndege mpya. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Newala ili kufidia ule ambao ulitumika hapo mwanzo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Maimuna Mtanda, kwa jinsi anavyofuatilia Uwanja wa Ndege wa Newala. Nimhakikishie baada ya taratibu za ndani Serikalini kukamilika, Serikali itafanya mchakato kutazama kiwanja hiki ambacho tayari amesema Halmashauri imekabidhi Serikali ili tuweze kutumia kwa ajili ya uwanja wa ndege kwa sababu tunatambua na kuzingatia mchango mkubwa wa Newala pamoja na maeneo haya katika ukombozi wa Taifa letu, lakini pia katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, Uwanja wa Ndege wa Mwanza umekuwa katika programu ya upanuzi kwa muda mrefu ili uweze kukubalika kama uwanja wa Kimataifa. Changamoto kubwa iliyopo pale kuna watu zaidi ya 1,400 ambao wamekuwa

wakidai fidia yao mpaka leo Serikali bado haijatoa maamuzi na vikao vimekuwa vikikaa mara kwa mara. Je, ni lini sasa watu hawa watafidiwa ili uwanja ule uweze kupanuliwa na uweze kufanya kazi na tukiangalia kwamba ni eneo ambalo ni *hub* kwa Nchi za Maziwa Makuu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inao mpango wa dhati wa kuufanya Uwanja wa Ndege wa Mwanza kuwa wa Kimataifa. Hatua mbalimbali zimeshaanza kufanyika ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la abiria ambalo yeye wenyewe maboresho hayo amekuwa akiyashuhudia yameendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili uwanja huu uweze kukidhi *standard* hiyo ya Kimataifa, ni lazima pia tutazame vitu vingine muhimu ikiwa ni pamoja na ulinzi na usalama. Wapo wananchi ambao wamevamia maeneo ya uwanja huo ambao taratibu za ndani Serikalini zinaendelea ili kuweza kutazama namna bora wanavyoweza kuondoka kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge taratibu zitakapokamilika basi tutaweza kuupanua uwanja huo na kuufanya wa Kimataifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini uwanja wa ndege utaanza kujengwa katika Mkoa wa Simiyu kwa sababu ni ahadi ambayo ipo katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Minza kwa swali lake la nyongeza kuhusiana na Mkoa wa Simiyu. Kama ilivyo Mikoa mingine, Serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia, inayo nia ya dhati ya kujenga uwanja wa ndege mkubwa wa kisasa katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi tupo katika hatua mbalimbali za utoaji wa ardhi ili baadaye tuanze mchakato kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Hivyo, nimwombe yeye pamoja na Mkoa washirikiane na Wizara ili kukamilisha michakato hiyo ya upatikanaji wa ardhi hatimaye tuweze kuanza kuweka fedha kwa ajili ya kuanza kujenga Uwanja huo wa Simiyu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Mshua.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Uwanja wa Ndege wa Tanga ni muhimu sana kuimarisha Muungano wetu kwani abiria kutoka Pemba, Zanzibar, Dar es Salaam na Tanga kwenyewe wanatumia sana. Je, ni lini Uwanja huu pamoja na majengo yake yaliyochoka utakarabatiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mshua juu ya umuhimu wa Uwanja wa Tanga. Kwanza tunayo bandari kubwa pale ambayo imeshakarabatiwa kwa shilingi bilioni 429.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tuna Bomba la Mafuta linajengwa pale. Tatu, tuna viwanda mbalimbali ambavyo vimejengwa na vingine vinaendelea kujengwa. Pia, tunao mpango wa kujenga Reli ya Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kwamba uwanja wa ndege haujadiliki juu ya kuboreshwa. Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa kutambua umuhimu huo na jinsi

ambavyo wananchi wa Tanga wanavyohitaji pia usafiri, tumekwishaanza taratibu mbalimbali za ndani na zitakapokamilika tutakwenda kuanza kufanya maboresho ya uwanja huo pengine siyo muda mrefu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Ritta.

Na. 313

**Maeneo yaliyotumiwa na Wapigania Uhuru kuwa Vivutio**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuyafanya maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika kama Kihesa Mgagao kuwa Vivutio vya Utalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii hufanya zoezi la kubainisha vivutio vya Utalii ambavyo vingi vinamilikiwa na Halmashauri za Manispaa, Halmashauri za Wilaya, Taasisi za Serikali, taasisi binafsi, jamii na familia. Mara baada ya kubaini maeneo hayo, Serikali hufanya majadiliano na wamiliki wa maeneo yaliyobainishwa ili kuona namna ya kuyaendeleza kuwa vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika kama Kihesa Mgagao, Kilolo, Mazimbu, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine Kampasi ya Mazimbu tayari yamepata ridhaa kutoka kwa wamiliki ili yaweze kutangazwa kuwa urithi wa Taifa. Kwa sasa Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kutangaza maeneo hayo kuwa urithi wa Taifa. Mara baada ya kutangazwa, taratibu za kuyaendeleza kiutalii zitafuata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa eneo hilo la Kihesa Mgagao waliishi Marais waliopigania uhuru wa Vyama vya Namibia, *ZANU PF* (Zimbambwe), *UNC* na *UPS (South Africa)* na tayari wenzetu wa *South Africa* gereza alilokuwa amefungwa Mandela limekuwa kivutio kizuri sana cha utalii. Je, Serikali sasa ipo tayari kuongeza jitihada za kuhakikisha kwamba lile eneo la Kihesa Mgagao linakuwa kivutio kizuri cha utalii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Mkoa wetu wa Iringa ni kitovu cha utalii kwa Nyanda za Juu Kusini na kumekuwa na vivutio vizuri sana katika Nyanda za Juu Kusini ukiwemo Mkoa wetu wa Iringa na Kilolo; je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuja kutembelea katika Mkoa wetu ili uone vivutio vizuri vilivyopo katika mkoa wetu ili sasa viweze kutusaidia na kuweza kuongeza uchumi katika utalii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi tayari sasa hivi Serikali imekwishapata ridhaa kutoka kwa wamiliki wa maeneo haya na kwamba sasa kinachofanyika ni michakato ya ndani ya kuwezesha eneo hili kutangazwa kuwa urithi wa Taifa. Baada ya kutangazwa mambo yote haya ya kuliendeleza eneo hili kuwa sehemu ya kivutio cha utalii yatafuata. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira tupo katika hatua ya mwisho kabisa ya jambo hili kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii katika Ukanda huu kama unavyofahamu kwamba ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, Serikali

imejielekeza katika kufungua ukanda huo kuwa sehemu ya utalii. Nipo tayari kwenda kutembelea maeneo haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru nami kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na wapigania uhuru wetu, Mkoa wa Kilimanjaro kuna vivutio vikubwa ikiwemo maeneo waliyoishi Mangi wetu, (Mangi Meli, Marealle, Mandara na Mangi Sina, ambavyo maeneo hayo yangetumika kama vivutio na kuliongezea pato la Taifa letu na mtu mmoja mmoja, lakini maeneo haya hayafikiki na nyumba walizoishi zimebomoka na vitu walivyotumia. Ni lini Serikali itafanya ukarabati wa vitu hivi ili kuweza kudumisha utalii Mkoa wa Kilimanjaro? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo yanamilikiwa na familia ambayo ni ya kihistoria, jukumu la kuyaendeleza na kuyasimamia mara nyingi linakuwa chini ya familia hizo, lakini pale ambapo tunafanya majadiliano na familia hizo na wao wakakubali kwamba Serikali tuweze kushirikiana kuyaendeleza tunafanya hivyo. Kwa hiyo, sasa hivi Serikali ipo katika mazungumzo na wamiliki wa maeneo haya na wale ambao watakuwa tayari Serikali kushirikiana nao tutafanya hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Rehema na Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Moja ya kumbukumbu ya Vita vya Majimaji ni uwepo wa jengo la Mjerumani pale Liwale Mjini lenye ghorofa moja. Je, nini mpango wa Serikali wa kulifanya lile jengo la Mjerumani pale Liwale liwe moja ya vivutio vya utalii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pale Liwale kuna jengo, Serikali ilishatuma timu ya kwenda kuona jinsi ambavyo jengo lile linaweza kutumika kama kivutio cha utalii. Tupo katika mazungumzo na wenzetu wa halmashauri ili kuona namna bora ya zaidi ya kulitumia eneo lile.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali dogo la nyongeza. Eneo alilozikwa Mtemi wa Wanyamwezi (Mtemi Mirambo) lililopo katika eneo la Kata ya Kanindo, Wilayani Kaliua - Ulyankulu, limepotea kabisa na halitunzwi, lakini mpaka sasa watalii na wageni kutoka maeneo mbalimbali nchini na ndani ya nchi wanakuja pale kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kujua historia ya Tanzania. Je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa hili eneo la Mtemi Mirambo kwenye kaburi hili ili liweze kuwa ni kivutio cha utalii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, timu yetu ya malikale ilifanya kazi ya kupitia maeneo yote kulipokuwa na njia ya kusafirishia watumwa kutoka kule Tabora mpaka kufika kule Bagamoyo na miongoni mwa maeneo yaliyotembelewa ni pamoja na eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliulizia. Ninaomba awe na subira, tunafanyia kazi maeneo haya ili kuongeza mazao ya utalii katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na makabila zaidi ya 120 yenye tamaduni mbalimbali, lakini makabila haya au tamaduni hizi hazifahamiki kwa kiasi kikubwa na watalii isipokuwa kabila la Kimasai. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kujenga

*center* ambayo itakuwa inatangaza tamaduni hizi na hivyo kuvutia watalii na kukuza uchumi wa nchi yetu? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa wingi wa makabila tuliyonayo yapo mambo mengi ambayo tunaweza kuyatumia kama vivutio vya utalii. Ndani ya Wizara sasa hivi tuna mkakati wa kuja na mazao tofauti ya utalii ambayo yatatambulisha mila, tamaduni zetu lakini vilevile na vyakula vyetu. Hivi karibuni tumefanya kongamano kubwa la utalii wa vyakula katika nchi yetu. Tunayo mipango ya kufanya haya anayoyapendekeza, ninaomba atupe muda tutayakamilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Sylvia, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Florence.

Mheshimiwa Asenga.

Na. 314

**Wanafunzi Wanaopata Ujuzi Sekta Binafsi Kutambuliwa na *VETA***

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuhuisha Sekta Binafsi na *VETA* ili Wanafunzi wanaopata ujuzi waweze kutambuliwa na *VETA*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutumia Mfumo wa Utambuzi na Urasimishaji Ujuzi *(Recognition of Prior Learning)*

imeendelea kuwatambua vijana wanaopata ujuzi kupitia mazingira yasiyo rasmi ambapo baada ya utambuzi huo wahusika hutunukiwa Vyeti vinavyotambulika na *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa, zaidi ya Vijana 20,000 wametambuliwa na *VETA* na kutunukiwa Vyeti katika mfumo nilioutaja hapo juu, ikijumuisha wanagenzi 1,275 wanaoshiriki miradi ya kimkakati kama vile *SGR* na Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere *(JNHPP)* pamoja na wafungwa 214 wamefanyiwa tathmini na kutunukiwa vyeti ili kutambuliwa rasmi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini bado inaonekana elimu ya kutosha haijafika kwa wananchi wetu kuhusu mkakati huu wa Serikali kuwatambua hasa mafundi tunaowaita mafundi mchundo *especially* kule Jimbo la Kilombero. Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya *operation* maalum kwa mfano; Mkoa wa Morogoro ili mafundi mchundo wote wakafahamu *operation* hii nzuri ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba tunaendelea kutoa elimu na kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba tunatambua makundi mbalimbali yaliyoshiriki katika miradi mbalimbali ya kimkakati. Vilevile, bado tumeanzisha kampeni mbalimbali na moja ya Shirika lipo pale Iringa ambalo limeingia mkataba na *VETA* kwa ajili ya ku-*improve* wale mafundi ambao ni wa kawaida kutambuliwa na taasisi mbalimbali kwa maana ya *VETA*. Kwa hiyo, Kilombero tutafika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Shonza.

Na. 315

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nne Igawa – Tunduma**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Njia Nne kutoka Igawa hadi Tunduma utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Igawa – Uyole – Songwe – Tunduma yenye urefu wa kilometa 218 inaendelea kujengwa kwa awamu. Kwa kuanzia, Serikali imeanza na upanuzi kwa njia nne sehemu ya Nsalaga (Uyole) – Ifisi – *Songwe Airport* yenye urefu wa kilometa 36 ambapo kwa sasa utekelezaji wake umefikia 25%. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya kuijenga sehemu iliyobaki ya barabara hii kwa utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi *(PPP)*. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Wananchi wa Mkoa Songwe tunaendelea kuiomba Serikali ujenzi wa kipande kilichobaki utakapoanza uanzie katika Mji wa Tunduma kuja mpaka Nanyala ili tuweze kuondokana na changamoto ya foleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa nina swali moja la nyongeza. Mkoa wa Songwe tunazo barabara mbili za kimkakati (Barabara ya Mlowo - Kamsamba na Barabara ambayo inatoka Mbalizi kwenda Mkwajuni). Wananchi wa Mkoa wa Songwe wanataka kufahamu ni lini hasa ujenzi wa barabara hizi utaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba yamekuwa ni maombi ya Mkoa wa Songwe kupitia *RCC* lakini hata Viongozi wa Kitaifa wameshauri kwamba wakati tunanza na hii barabara ni ndefu. Kwa hiyo, tutakapoanza tunategemea tutaanza siyo tu Tunduma ama Igawa, lakini tungetamani tuanze sehemu mbili ama tatu ikiwepo na Tunduma kwa sababu ya kupunguza msongamano mkubwa sana ambao upo katika mpaka wa Nchi ya Tanzania na Zambia (mpaka wa Tunduma).

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, swali lake la nyongeza, kuhusu Barabara ya Kamsamba ama Mlowo kwenda Kamsamba pamoja na Mbalizi kwenda Mkwajuni, tumeshapata mkandarasi. Sasa hivi tupo kwenye hatua za mwisho kabisa ili aweze kuanza kazi ya kujenga na bahati nzuri hizo barabara ni za bajeti ya mwaka huu, lakini hata bajeti inayokuja, barabara hizo zimewekewa bajeti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Sasa je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopisha barabara ya *by pass* ya Uyole - Songwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *By pass* ya Uyole - Songwe ni sehemu ya barabara ambayo ipo kwenye swali la msingi na tunavyoongea sasa hivi eneo hilo thamani yake ya fidia ni shilingi bilioni 27.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshapokea kutoka Wizara ya Fedha shilingi bilioni 10 ambazo zimepokelewa siku za karibuni. Kwa hiyo, tunafanya taratibu za kuanza kulipa hizo fedha kwa wale watakaoathirika na tunategemea Wizara ya Fedha itafanya haraka kwa sababu tayari hiyo barabara Mhandisi

Mshauri wa mkandarasi ambaye atafanya hiyo kazi ameshaenda *site. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare, jiandae Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayojengwa na mkandarasi anayeitwa Chiko, kilometa 25 na kilometa 31.6, zote zimesimama. Je, nini Kauli ya Serikali kuhusu kumrudisha mkandarasi huyu barabarani, ili aendeleze kipande hiki ambacho kimeharibika sana, hata kupitika tu ni tabu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, lakini barabara hiyo mkandarasi, kama anavyosema, amesimama. Kama tulivyosema hapa wakati wa bajeti, wakandarasi wengi waliokuwa wamesimama sasa hivi fedha imeshaanza kutoka, ili waweze kuendelea na kazi, ikiwemo hiyo barabara ya Mheshimiwa katika Jimbo lake la Itigi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi. Wajiandae Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Bupe na Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mvua zinazoendelea kunyesha zimeharibu miundombinu ya barabara, hasa kutoka Mkuzi hadi Mlola na barabara hii tuliahidiwa kwamba, itajengwa kwa kiwango cha lami. Je, Serikali haioni kwamba, hiki ndiyo kipindi cha kutengeneza barabara ile ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wangu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, maeneo mengi katika Nchi ya Tanzania, ambayo yapo na mvua sasa hivi barabara zimekuwa za shida kupitika na hasa zile ambazo ni za kiwango cha changarawe. Nitoe tu maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Tanga, kuhakikisha kwamba,

anapeleka mkandarasi ama mkandarasi ambaye yupo pale anahakikisha kwamba, anasimamia hizo barabara ziweze kupitika kwa muda wote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara. Wajiandae Mheshimiwa Bupe, Mheshimiwa Ishengoma na Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi anayejenga Barabara kutoka Tarime kwenda Nayamungo, kilometa 25, *Nyanza Works* ameandika barua ya kusimama ujenzi kwa sababu, hajalipwa. Je, Serikali ipo tayari kuongea na mkandarasi huyu aendelee kufanya kazi ya ujenzi? Barabara hii ni mbaya sana wakati huu wa mvua na kuna maneno mengi sana watu wanalalamika kwa sababu, ni njia pekee ya kwenda mjini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachofahamu mimi ni kwamba, Mkandarasi wa Nyanza ameshalipwa pesa ambayo alikuwa anadai baadhi ya *certificate* na tumeshamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Mara ahakikishe kwamba, mkandarasi huyo anarudi *site,* kama alikuwa hayupo, lakini pia, kuhakikisha kwamba, zile barabara zinapitika kwa sababu, hiyo ni sehemu ya mkataba kwamba, isije barabara ikafunga wakati mkandarasi yupo *site*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Ntendo – Muze na Matai – Kasesha ni barabara za kimkakati sana katika Mkoa wa Rukwa, mkandarasi ameondoka hakuna kinachoendelea. Ni lini Serikali itajenga barabara hizi kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hizi barabara mbili tofauti, za Ntendo – Muze na hiyo ya Matai –

Kasesha na barabara zote, zina wakandarasi. Ambacho ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, wakandarasi hawa wameshaleta madai yao na Serikali inayafanyia kazi walipwe, ili waendelee na kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ishengoma. Jiandae Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara ya njia nne kuanzia Kibaha Maili Moja – Morogoro, ili kupunguza msongamano wa magari na hasa malori?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara za Mji wa Morogoro, hizo za njia nne, ni kati ya barabara ambazo kwa sasa tunategemea kuzipeleka kwenye Mpango wa *PPP,* ikiwa ni kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro na zitakuwa ni za njia nne. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Mkandarasi wa Barabara ya Mbande – Kisewe – Mgongola, aliyesimama, atasambaza vifusi na hatimaye kuweka zege/lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kipande kilichobaki ni kidogo sana na nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge wa Mbagala kwamba, namwelekeza Meneja wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba, ahakikishe anasambaza kifusi, japo tunajua Dar es Salaam mvua zinanyesha, lakini ahakikishe anakisambaza, ili baada ya mvua kupungua, basi hicho kipande chote kikamilike kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mbulu – Garababi, ambayo ilikuwa inajengwa kwa kiwango cha lami, mkandarasi wake hachongi ile njia ya kupita, sasa barabara hiyo haipiti kabisa na wewe Waziri uliahidi ukimwambia meneja amwelekeze mkandarasi. Barabara ile haichongwi, tufanyeje ile barabara ichongwe watu wapite, kwa maana Hospitali ya Hydom ipo katika maeneo hayo? Tufanyeje, ili mkandarasi achonge barabara ile, ili wananchi tuweze kupita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri Mkandarasi wa Mbulu Galbadi tulishamlipa *IPC* aliyokuwa anadai. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha tunamsimamia meneja na mkandarasi mwenyewe achonge hiyo barabara iweze kupitika katika kipindi hiki cha mvua.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee. Mheshimiwa Komanya.

Na. 316

**Ujenzi wa Daraja la juu la Mto Chobe, Lyusa na Nkoma, Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga madaraja ya juu Mto Chobe, Lyusa na Nkoma, kwani upembuzi yakinifu umekamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Madaraja ya Mto Chobe, Lyusa na Nkoma, yaliyopo katika Barabara ya Mwangongo – Lalago – Meatu – Mto Sibiti (km 120.78). Kwa sasa Serikali inatafuta fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, katika barabara tajwa hapo, upo mradi mkubwa wa daraja wa shilingi bilioni nane na milioni 400. Mkandarasi ameshindwa kuendelea kutokana na changamoto ya fedha. Je, ni lini Serikali itamlipa huyo mkandarasi ili aweze kukamilisha kipande kidogo kilichobaki cha 15%.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika barabara hiyo ya kilometa 120 iliyotajwa inatakiwa zijengwe kilometa 65. Ni lini Serikali itaanza kujenga hizo kilometa 25 zilizopo ndani ya barabara tajwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, daraja alilolitaja ni Daraja la Itembe, lenye mita 150, lipo 55%. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunavyoongea sasa hivi mkandarasi amesharudi eneo la kazi na tunategemea yale madai yote yaweze kulipwa, kama alivyokuwa amedai, ili tuweze kulikamilisha hilo daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ambayo ameitaja, ambayo tumeitaja kwenye jibu letu, kuanzia Nkoma – Lalago, kilometa 65, ilikuwa ni sehemu ya Barabara ya *EPC*. Sisi tutajenga kipande hicho cha kutoka Nkoma – Lalago, kilometa 65 na tunavyoongea sasa hivi mkandarasi ameshasaini na yupo kwenye maandalizi ya kuanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANSIC K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nangurukuru – Liwale ilikamilika kufanyiwa upembuzi

yakinifu miaka miwili iliyopita. Je ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami na madaraja na makalavati, ili kuchechemua uchumi na maendeleo katika Wilaya za Kilwa na Liwale? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilometa 10 hizo zipo kwenye maandalizi ya manunuzi kuzijenga, kama tulivyokuwa tumeahidi. Tutaendelea pia na mwaka unaokuja. Kuhusu maeneo yale ambayo ni korofi, ama yenye madaraja; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Liwale kwamba, tupo tayari tunajenga hayo madaraja kupitia zile fedha za dharura. Kwa hiyo, madaraja yote yaliyokuwa na changamoto, wakandarasi tayari wanaendelea kuyajenga, ili kuondoa hiyo adha ikiwa ni pamoja na kuchechemua shughuli za kibiashara katika miji na Mji wa Liwale ukiwemo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Daraja la Mto Lukosi kwenye Barabara inayotoka Ilula – Mkaranga – Kising'a – Kilolo lina mkandarasi, lakini amesimama muda mrefu sana, hafanyi kazi yoyote pale na ni daraja kubwa. Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba, mkandarasi yule anaendelea na kazi katika daraja lile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Mikoa ya Nyanda za Juu kusini, hiki ni kipindi cha mvua nyingi sana kwa hiyo, wakati fulani zipo shughuli nyingi ambazo wakandarasi hawawezi kuendelea nazo. Kama ni tofauti na changamoto ya mvua ambazo zipo na maji yamekuwa mengi sana kwenye mto, nitaomba nionane na Mheshimiwa Mbunge ili tuone tatizo ni nini. Kama changamoto itakuwa siyo hiyo ya maji mengi, ambayo sasa hivi yapo kwenye mito mingi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Tumekuwa tukiomba ujenzi wa Daraja la Songolo pamoja na Kelema Maziwani. Ni lini Serikali mnaenda kuanza kujenga madaraja hayo mawili kuokoa maisha ya wananchi wa Wilaya ya Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja aliyoyataja na hasa hilo la Kelema, tumeyapangia bajeti hata katika bajeti ya huu tunaouanza mwaka wa fedha, 2025/2026. Kwa hiyo, nina hakika tutaanza kuyajenga hayo madaraja katika mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli.

**MHE. *ENG.* SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nanga – Isambala – Kondoa kuna Daraja la Munguri B ambalo nimelisemea, huu mwaka wa tano sasa. Je, Serikali ina kauli gani kwa wananchi wa Kondoa na Hanang ambao wanatumia hiyo barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, daraja alilolitaja, ambalo linaunganisha Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Dodoma, Kondoa na Hanang, ni daraja ambalo tulikuwa tumelifanyia usanifu, lakini baada ya mvua likawa limeongezeka sana, kwa hiyo, tukatakiwa tufanye tena usanifu. Tunaamini tutakamilisha usanifu katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 ili tuweze kulijenga sasa daraja lote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Mariam Nyoka.

Na. 317

**Ujenzi wa Barabara ya Azimio – Makande – Songea**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Azimio - Mtinga – Lukumbile - Songea hadi Makande kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Azimio – Mtinga – Lukumbile yenye urefu wa kilometa 68.65 inafanyiwa matengenezo mbalimbali na *TANROADS,* ili iweze kupitika vizuri majira yote ya mwaka. Serikali imepanga kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Azimio – Mtinga – Lukumbile (kilometa 68.65) kwa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Mwaka wa Fedha 2026/2027. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Nalafu Mashariki – Lukala kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya kutoka Mbesa – Mbati – Malumba kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara alizozitaja ni kati ya vipande ambavyo vinatoka Mtwara Pachani – Lingusenguse – Tunduru kilometa 300. Tumeshakamilisha

usanifu na kwa sasa cha kwanza tunachofanya ni kuhakikisha kwamba, yale maeneo yote korofi tunayajenga kwa kiwango cha lami wakati Serikali inatafuta fedha kujenga barabara yote, yakiwemo na hayo maeneo aliyoyataja, kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Barabara ya Murushaka Karagwe – Benako Ng'ara, mkandarasi amesimama mpaka leo. Ninapenda kujua, kwa nini mkandarasi amesimama, kama ni pesa ili Serikali iweze kulipa pesa yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba arudie kuitaja hiyo barabara, ili niweze kuielewa vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver rudia tena barabara yako.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Barabara ya Karagwe, inapitia Murushaka – Benako - Ng'ara; inajengwa kwa kiwango cha lami, lakini mkandarasi amesimama kwa kutokulipwa pesa yake. Ninapenda kujua, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi yule ili aweze kumalizia barabara ile?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, *CRDC* ndiyo Mkandarasi ambaye anajenga hiyo barabara na ameshaleta maombi, kwa ajili ya kumlipa haki zake. Serikali inaandaa malipo hayo ili aweze kukamilisha kazi ambayo alikuwa hajaikamilisha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, lini Barabara ya Tabora – Hambali – Ishihemulwa – Shitage na Bulele – Ushege itatiwa lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara hiyo, kwanza imepandishwa hadhi na Mheshimiwa Waziri kutoka Barabara ya Mkoa kwenda *Trunk Road*. Sasahivi Serikali inakamilisha vipande vilivyokuwa vimebaki kutofanyiwa usanifu, ikiwa barabara hiyo ilijengwa kwa kiwango cha lami, na hasa baada ya kupata hiyo hadhi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, tumekuwa na maombi ya muda mrefu ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Njiapanda – Mang'ola – Matala – Lalagu na kwa kuwa, hatuoni utekelezaji utaanza lini, lakini barabara ile inahitaji madaraja, ili kuokoa maisha ya watu. Ni lini sasa Serikali, angalau kwa kuanzia, tutakuwa na madaraja kwa yale maeneo korofi, hasa kipindi hiki, ili kuokoa maisha ya wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, bahati nzuri hiyo barabara nimepita. Ni barabara ambayo ina mabonde mengi, ambayo yanashindwa kupitika. Katika bajeti yetu na mpango wetu kwa sasa tumesema barabara zote, hata kama hatutazijenga kwa kiwango cha lami, tunaagiza mameneja wa mikoa waainishe maeneo yale yote korofi, ambayo huwa yanafanya barabara zisipitike, ikiwemo na hiyo barabara ili tuhakikishe kwamba, hata kama si kwa kiwango cha lami, maeneo ambayo yanakwamisha kufanya usafiri kati ya eneo na eneo tuweze kuyajenga, ikiwepo hiyo Barabara ya Sibiti – Matala - Karatu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

Na. 318

**Kutunga Sera ya Taifa ya Bima**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatunga Sera ya Taifa ya Bima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha, kwa kushirikiana na wadau, inaendelea na zoezi la kuandaa Sera ya Taifa ya Bima ya Mwaka 2025 kwa lengo la kuweka mfumo madhubuti wa usimamizi wa masuala ya bima nchini, ikiwa ni pamoja na namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali, ili kuboresha maisha ya wananchi na kuongeza mchango wa Sekta Ndogo ya Bima katika pato la Taifa. Kwa sasa, Wizara imekusanya maoni ya wadau wa Sekta ya Bima na inaendelea kuyafanyia kazi maoni yaliyotolewa ili kuboresha rasimu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninakubaliana na majibu ya Serikali na niwaombe sasa waharakishe huo mchakato, ili kunusuru maisha ya Watanzania wanaokabiliana na majanga, hasa ya barabarani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua ushauri huo wa Mheshimiwa Kikoyo na nitaufanyia kazi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, watumiaji wa bima sasa hivi wameshafikia zaidi ya milioni nane na makusanyo ya bima ni zaidi ya shilingi bilioni 900 kwa mwaka. Je, kwa nini Serikali inaruhusu udanganyifu unaoendelea wa baadhi

ya wafanyabiashara ku-*claim* fidia na baadaye bidhaa hizo, zilizolipwa fidia, zinaenda kuuzwa sokoni na wananchi kupata madhara makubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kusema kwamba kuna udanganyifu. Hili ni suala la kuchukua, kwenda kulifuatilia na kulifanyia kazi ili tuone; kama huo udanganyifu upo tutaufanyia kazi na sheria itachukua mkondo wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, maswali yamekwisha. Sasa ni kipindi cha kutangaza wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; Wageni wa Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara; Dkt. Hashil Abdallah, Katibu Mkuu; Dkt. Suleiman Serera, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu khamis Shauri, Mkurugenzi wa Biashara Zanzibar; Balozi Meja Jenerali Wilbert Ibuge, Mkuu wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa *(NDC)*; Mhandisi Bashir Juma Mrindoko, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda *(TIRDO);* Mhandisi Musa Nyamsingwa, Mwenyekiti wa Bodi, Shirika la Maendeleo ya Viwanda *(SIDO);* Kanali Mstaafu Joseph Simbakalia, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania; na Profesa Elizabeth Mwakasungula, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala Vipimo, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni Bwana Elias Kimath, Mjumbe wa Bodi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA);* Mhandisi Profesa Valerian Silayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Uhandisi wa Kilimo na Teknolojia; Profesa Othman Chande Othman, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Viwango Tanzania; Profesa Zacharia Mganilwa, Mwenyekiti wa Bodi, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE);* Dkt. Aggrey Mlimka, Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ushindani; Profesa Mkumbukwa Ntambo, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda; Mhandisi Profesa

Sylvester Mpanduji, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Viwanda Vidogo *(SIDO);* na Mhandisi Profesa Frederick C. Kahimba, Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania *(TEMDO),* karibuni. *(Makofi)*

Wapo vilevile Latipha M. Khamis, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TANTRADE);* Bwana Godfrey Nyaisa, Afisa Mtendaji Mkuu Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA);* Dkt. Ashura Katunzi, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Viwango Tanzania *(TBS);* Dkt. Nicolaus Shombe, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Taifa la Maendeleo; Mhandisi Godfrey Mwinama, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uhandisi wa Kilimo na Teknolojia za Vijijini; Profesa Edda Lwoga, Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE);* Bwana Willam Erio, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani *(FCC)*; Bwana Alban Kihulla, Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo; na Bwana Wema Kaskaz, Msajili wa Baraza la Ushindani Tanzania *(FCT),* karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni Bwana Asagye Bangu, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani; Ndugu Leodgar Tenga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Viwanda Nchini *(CTI);* Profesa Fortunata Makene, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii; na Dkt. Lucas Katera, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini Tanzania. *(Makofi)*

Ipo pia Familia ya Mheshimiwa Dkt. Jafo, Ndugu Rehema Disanura, Mke wake Mheshimiwa Waziri; Ndugu Sadik Seleman Jafo, Mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Rahma Seleman Jafo, Mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Lutfi Jafo, Mtoto wa Mheshimiwa Waziri; na Ndugu Ally Saidi Jafo, kaka wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Jafo; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Idara kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni familia yake; Ndugu Rehema Henry Mponzi, Mke wake Mheshimiwa Naibu

Waziri; Ndugu Junior Exaud Kigahe, Mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Maico Kastory Kigahe, Kaka wa Mheshimiwa Naibu Waziri; na Ndugu Daudi Silaoneka Kigahe, kaka wa Mheshimiwa Naibu Waziri, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Wageni 21 wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wanafunzi 19 na walimu wawili wa Shule ya Msingi Baybridge kutoka Masaki Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mwalimu Laoni Sandetwa wa Shule ya Awali Ibihwa kutoka Wilaya ya Bahi Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Ndugu Kakarase Makuru rafiki yake kutoka Serengeti, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ndugu zake kutoka Manyoni, Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, Wachungaji wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mara kutoka Chuo cha Biblia, Bunda. *(Makofi)*

Wageni 29 wa Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Halmashauri ya Kondoa Mji, Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 40 wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Wadau kutoka Taasisi ya Itambue Thamani Yako ya Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Sister Mechtilda Charles wa Shirika la Masister Moyo Safi wa Maria Afrika kutoka Jijini Dodoma. Karibu. *(Makofi)*

Wanafunzi 101 na Walimu watano wa Shule ya Msingi ya Carmel kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* Wanachama wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi *(UVCCM)* Ndaki ya Elimu. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba hotuba yangu yote iingie katika *Hansard* kama nilivyoiwasilisha hapa mezani asubuhi leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara mnamo tarehe 25 Machi, 2025, sasa ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, mwomba Mungu siyo mtovu. Hivyo, ninapenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na fadhili kwa fanaka zake na afya njema zilizotuwezesha kumudu kutekeleza majukumu haya niliyopewa kwa mamlaka ya umma wote wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chanda chema huvikwa pete. Nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri mkubwa, uzalendo na umakini wa hali ya juu. Ninamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema, siha njema, hekima na busara ili aendelee kuyatekeleza yale yote aliyoyapanga kwa manufaa ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuendelea kunipa dhamana hii ya kuongoza Wizara ya Viwanda na Biashara. Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, hakika kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu sitomwangusha hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumshukuru, hasa kwa ushirikiano na wenzangu, Ndugu yangu Exaud Kigahe, Naibu Waziri wangu ambaye kwa pamoja tumeendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba jambo hili tulilopewa dhamana linaenda mbele hali kadhalika Dkt. Hashil Twaibu Abdallah, Katibu Mkuu wa Wizara yangu na Dkt. Suleiman Hassan Serera, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, ninawashukuru watumishi wote wa Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na wadau ambao wameniwezesha kutekeleza majukumu yangu niliyokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isiyo kongwe haivushi. Ninapenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa namna walivyonipatia miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamekuwa chachu na mali zaidi kwangu katika kufanikisha majukumu yangu. Kama wahenga wanavyosema, “elimu bila amali ni kama nta bila asali.” Hivyo, ninawashukuru sana kwa kuwa amali ambayo wamenipa, kwangu imenisaidia kutekeleza majukumu yangu kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msiba haupigi hodi. Ninaomba nichukue fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Waheshimiwa Wabunge wote, familia na ndugu na jamaa wa marehemu tulioondokewa na wapendwa wetu. Kwanza ni Makamu wa Rais wetu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye hivi jana tu tumekamilisha msiba wake, Mheshimiwa Cleopa David Msuya aliyefariki dunia tarehe 7 Mei, 2025; pili, Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni Mkoa wa Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani kwa Ukanda wa Afrika ambaye alifariki dunia tarehe 27 Novemba, 2024 akiwa Nchini India alikokuwa akipatiwa matibabu. Kwa hakika vifo vya viongozi hawa ni pigo kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuyaenzi maisha yao tunapojifunza kutoka kwa viongozi hao waliotukuka katika utendaji wao wa kazi. Tunaungana na familia zao, ndugu, jamaa na Watanzania wote katika kipindi hiki cha maombolezo tukiomba Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninaungana na viongozi wenzangu kutoa pole kwa Watanzania wenzetu waliofikiwa na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali, ikiwa ni pamoja na kuporomoka kwa jengo la ghorofa katika Eneo la Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Ninawapa pole wote kwa maafa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar; na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa jitihada zao za kuendelea kusimamia uimarishaji wa Muungano na shughuli za maendeleo hapa nchini. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar kwa ushirikiano

wake uliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Sekta ya Viwanda na Biashara kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge Bingwa sana wa Ilala. Hongera sana, Mungu akuhifadhi na akulipe kwa kazi kubwa unayoendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Mbeya Mjini na Rais wa Umoja wa Mabunge Dunia kwa kazi kubwa anayofanya kuliongoza Bunge letu. Hali kadhalika Wenyeviti wa Kamati kwa kumsaidia Mheshimiwa Spika na Bunge letu limeweza kushamiri vizuri. Bunge la 12 limekuwa Bunge la viwango na Bunge la mfano. Ahsanteni sana na Mungu awalipe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninaomba kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini kwa umakini mkubwa na maelekezo yake. Hali kadharika Makamu Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa Mariam Ditopile mwana wa Mzuzuri, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma. Hakika hawa wamefanya kazi kubwa. Ninaomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati, wamekuwa wakitoa maelekezo ambayo yameisaidia Wizara ya Viwanda na Biashara kutimiza wajibu wake. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, ninawapongeza watoa hoja wote waliotangulia kutoa hotuba zao hapa Bungeni. Kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba yake ya bajeti aliyoiwasilisha hapa Bungeni mnamo tarehe 9 Aprili, 2025. Hotuba hiyo ilitoa hali ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kuonesha Dira na Mwelekeo wa Taifa letu katika mwaka wa fedha 2025/2026 katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, hotuba ninayoiwasilisha imegawanyika katika maeneo makuu manne, ambayo ni; taarifa ya hali ya mwenendo wa Sekta ya Viwanda na Biashara hapa nchini, utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na mafanikio makuu yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita na vipaumbele mbalimbali vya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na shughuli zitakazotekelezwa katika Wizara na taasisi mbalimbali katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali na mwenendo wa Sekta ya Viwanda hapa nchini. Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi na upanuzi wa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo pamoja na vile vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi hapa nchini. Bidhaa hizo ni pamoja na saruji, mbolea, huduma za kuunganisha magari, sukari, mabati na vioo kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wake, uzalishaji wa ajira, kukuza mauzo ya nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia jitihada hizo, mchango wa Sekta ya Viwanda pamoja na biashara kwa pamoja ukuaji wake umeendelea kuimarika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la Taifa kwa mwaka 2024 ulikuwa asilimia 7.3 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2023. Aidha, ukuaji wa sekta ya viwanda ulikuwa asilimia 4.8 mwaka 2024 ukilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2023. Vilevile, mchango wa Sekta ya Biashara katika pato la Taifa kwa mwaka 2024, ulikuwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na asilimia 8.4 kwa mwaka 2023. Halikadhalika kasi ya ukuaji wa Sekta ya Biashara ulikuwa ni asilimia 4.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.2 katika mwaka 2023. Ukuaji huu umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji wa biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina fursa mbalimbali za masoko ya kuuza mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini

ambapo katika mwaka 2025 mwenendo wa baadhi ya masoko ya biashara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa mauzo ya nje ya katika nchi yetu katika Bara la Afrika kwa mwaka 2024 yalikuwa Dola za Marekani Bilioni 3.9 ikilinganishwa na Dola za Marekani Bilioni 2.3 katika mwaka 2023 ambayo ni sawa na ongezeko la 40%. Ongezeko hilo, lilitokana na kuongezeka kwa masoko mapya chini ya Soko Huru la Bara la Afrika yanayojumuisha nchi za Morocco, Nigeria, Senegal, Ghana, Misri, Ethiopia, Algeria, Djibuti, Somalia na Guinea. Bidhaa zilizochangia mauzo hayo kwa kiwango kikubwa ni zao la kahawa, tumbaku, vioo, nafaka (mchele na mahindi), viungo na nyuzi za mkonge. Aidha, kwa mwaka 2024 bidhaa zilizoagizwa kutoka katika nchi za Afrika zilikuwa na thamani ya Dola za Marekani Bilioni 1.37 ikilinganishwa na Dola za Marekani Bilioni 1.4 kwa mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 4.04. Upungufu huo umechangiwa na kupungua kwa uagizaji wa sukari za viwandani, dawa za binadamu na *plasters gypsum* kutoka nchi ya Misri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa jumla wa ufanyaji biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine katika Soko Huru la Afrika kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024 umeendelea kuwa urari chanya wa kibiashara katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Soko la Umoja wa Ulaya, kwa mwaka 2024 thamani ya mauzo ya bidhaa katika Soko la Jumuiya ya Umoja wa Ulaya ilikuwa Dola za Marekani Millioni 686 ikilinganishwa Dola za Marekani Milioni 633.5 mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.6. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za kakao, parachichi, tumbaku, kahawa na madini. Aidha, mwaka 2024 uagizaji wa bidhaa kutoka Soko la Jumuiya ya Umoja wa Ulaya ulikuwa Dola za Marekani Bilioni 1.2 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 1.17 kwa mwaka 2023, sawa ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hilo linachangiwa na uhitaji wa malighafi na mitambo ya kuzalisha bidhaa za viwandani na migodini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa Soko la Bara la Asia, kwa mwaka 2024 thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda baadhi ya nchi za Bara la Asia hususani kwa nchi za China, India, Japan, Singapore na Umoja wa Falme za Kiarabu ilikuwa dola za Marekani bilioni 2.8 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2.9 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 2.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu huo ulichangiwa na mabadiliko ya mahitaji ya Soko na ushindani mkubwa kutoka katika nchi nyingine zinazouza bidhaa kama hizo. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na madini, mazao jamii ya kunde, korosho, parachichi, pamba, nyama ya mbuzi, mbogamboga, tumbaku, ufuta pamoja na kakao na karanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, uingizaji wa bidhaa kutoka baadhi ya nchi za Bara la Asia ulikuwa na thamani ya dola za Marekani bilioni 5.5 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 8.8 kwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa 34.4%. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za mitaji, plastiki na usafirishaji. Bidhaa zilizonunuliwa kwa wingi ni pamoja na magari, pikipiki, mafuta ya gesi na petroli, simu, sukari kwa ajili ya matumizi ya viwandani, saruji nyeupe na bidhaa za chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imeendelea majukumu yake kulingana na fedha zilizoidhinishwa na kupokelewa. Utekelezaji wa Bajeti kulingana na fedha zilizopokelewa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 110,899,722,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 81,115,206,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, fedha hizo zinajumuisha shilingi 12,762,260,000 za Matumizi Mengineyo na shilingi 68,352,946,000 za Mishahara. Aidha, shilingi 29,784,516,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 75,747,677,767.85, sawa na 68.30% ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 9,170,635,771.78 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na 71.86% na shilingi 52,800,269,874.07 kwa ajili ya Mishahara sawa na 77.25% ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 13,776,772,122 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na 46.25% ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imeendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele yakiwemo: Kuendelea na miradi ya maendeleo ya kielelezo ya Magadi Soda - Engaruka kule Wilayani Monduli; Makaa ya Mawe ya Mchuchuma; Chuma cha Liganga; kuendeleza Kiwanda cha Kilimanjaro *Machine Tool*; Kuratibu majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa; Kuboresha mazingira kibiashara; Kuendelea na utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania; Kuendelea na kongani za viwanda; Kukuza uboreshaji wa hali ya ushindani wa soko; na Kuendelea na Ubunifu, Uhawilishaji na Ukuzaji wa Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali baada ya kukamilisha malipo ya malipo ya fidia ya kiasi cha shilingi bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 waliopisha eneo la utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Serikali inaendelea na majadiliano na mwekezaji ambaye ni Kampuni ya "*Shudao Investment Group Company Limited*" inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Kwanza ya majadiliano na mwekezaji ilifanyika Januari, 2025, Awamu ya Pili ilifanyika Februari, 2025 na Awamu ya Tatu ilifanyika Aprili, 2025. Masuala yaliyokubalika hadi sasa katika majadiliano hayo ni pamoja na makubaliano katika vipengele muhimu vya mikataba ikiwemo misingi sahihi ya mgawanyo wa hisa na muundo wa uwekezaji *(Financing structure);* kiwango cha mtaji wa uwekezaji unaohitajika; muundo wa usimamizi na uendeshaji wa mradi;

muda wa Mkataba wa Uwekezaji; uhuishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi; na uandaaji wa modeli ya kifedha ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mradi wa Magadi Soda. Wizara kupitia *NDC* imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kimkakati na Kielelezo wa Magadi soda uliopo katika Bonde la Engaruka Wilayani Monduli Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 6.3 kwa ajili ya mradi huo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 5.89 ni kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi 595 waliopisha mradi na kiasi cha shilingi milioni 408.7 ni kwa ajili ya malipo ya ada ya mwaka ya leseni ya uchumbaji wa madini. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya shilingi bilioni 5.702 sawa na 97% ya fedha zote za fidia zililipwa kwa wafidiwa 528 kati ya wafidiwa 595. Aidha, ukamilishaji wa zoezi la ulipaji fidia wa kiasi kilichobaki cha shilingi milioni 194.3 unaendelea kwa wafidiwa 67 waliobakia ambao wanakamilisha nyaraka muhimu zikiwemo taratibu za mirathi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mradi upo katika hatua za mwisho za kupata wawekezaji wawili watakaojenga viwanda viwili vya kuchenjua magadi. Uamuzi wa kuwa na wawekezaji wawili ni kutokana na uwepo wa mashapo mengi ya magadi katika mfumo wa maji kiasi cha mita za ujazo bilioni 3.2 ambazo zinaendelea kuongezeka kila mwaka. Uwekezaji wa viwanda viwili na miundombinu yake inatarajiwa kutumia dola za Marekani milioni 700 ambapo utawezesha nchi kuwa mzalishaji namba moja wa magadi soda katika Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unatarajia kuiingizia Serikali mapato ya dola za Marekani milioni 42 kutokana na tozo na kodi mbalimbali. Aidha, utazalisha ajira 1,000 - 1,400 za moja kwa moja na kati ya ajira 4,000 - 5,600 zisizokuwa za moja kwa moja. Vilevile, mradi utachochea uanzishwaji wa viwanda vinavyotumia magadi kama malighafi katika uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mradi wa Chuma cha Maganga Matitu. Wizara ilisaini Mkataba wa Ubia na mwekezaji *Fujian Hexingwang Industry Tanzania Company Limited* kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Chuma Ghafi cha Maganga Matitu Agosti, 2024. Uwekezaji katika mradi huo unakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 77.45 na utadumu kwa miaka 25 na kusababisha Tanzania kuwa nchi ya nne katika Afrika kwa uzalishaji wa chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uzalishaji wa mgodi unatarajiwa kuwa wa tani milioni moja kwa mwaka za chuma ghafi, tani milioni moja kwa mwaka za *Titanium concentrate* na tani 483,000 kwa mwaka za mabaki ya madini. Hadi kufikia Machi, 2025, Kampuni ya Ubia ya Maganga Matitu *Minerals Corporation Limited* ilianzishwa kati ya *NDC* na mwekezaji huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo utaanza baada kulipa fidia wananchi wanaozunguka eneo hilo. Ambapo ulipaji huo utakamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2024/2025. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuzalishwa kwa ajira 1,000 ambapo kati ya ajira hizo, ajira 300 ni za moja kwa moja na ajira 700 zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mradi utaiwezesha nchi kutumia rasilimali za ndani kuzalisha bidhaa mbalimbali za chuma ambazo zitawezesha uanzishwaji wa viwanda vingine vitakavyoongeza mnyororo wa thamani. Vilevile, mradi utaokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza bidhaa za chuma nje ya nchi na utaondoa na kupunguza uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na matumizi ya chuma chakavu ambavyo wakati mwingine vinakosa ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Makaa ya Mawe wa Katewaka. Wizara inaendelea kuratibu maandalizi ya Mradi wa Makaa ya Mawe wa Katewaka ambao upo katika hatua za mwisho kuanza utekelezaji. Mradi huo ni muhimu katika uendelezaji wa Sekta ya Viwanda, kuongeza ajira nchini pamoja na kuokoa fedha nyingi zinazotokana na zinazotumika kuagiza malighafi hiyo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo ambao utadumu kwa miaka 100 una tani milioni 100 za makaa ya mawe na utazalisha tani milioni 1.5 kwa mwaka. Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imefanikiwa kufanya kikao cha majadiliano na mwekezaji na kukamilisha kuandaa Rasimu ya Mpango Kazi wa utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha uzalishaji wa viwanda vipya na Kongani za Viwanda. Wizara imefanikiwa kuvutia uwekezaji wa ujenzi wa kongani ya Viwanda ya *Sino Tan Industrial Park* iliyopo Kwala Mkoa wa Pwani inayotarajiwa kuwa na viwanda vikubwa 200 na viwanda vidogo 300 pindi ujenzi utakapokamilika. Aidha, Mwekezaji katika mradi huo ambaye ni *Sino Tan* anatarajia kukamilisha ujenzi wote wa kongani ifikapo mwaka 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya awali ya ujenzi imehusisha ekari 500 kati ya ekari 2,500 ambapo ujenzi umefikia 80%. Kukamilika kwa kongani hiyo kunatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja 100,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 500,000 na kuzalisha bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mradi wa Kongani ya Kisasa ya Viwanda *(Modern Industrial Park)* iliyopo katika eneo la Mlandizi Mkoani Pwani. Mradi huu ulianza ujenzi Septemba, 2021 na unatarajiwa kugharimu shilingi trilioni 3.5. Ujenzi huo umechukua jumla ya eneo lenye ukubwa wa ekari 1,077.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025, jengo la utawala, kituo cha huduma za pamoja kwa ajili ya Taasisi za Serikali *(one stop centre)*, ujenzi wa kituo cha zimamoto, ujenzi wa kituo cha afya na uzio wa kilomita tisa umekamilika. Aidha, viwanda vitano ambavyo ni: *Sulphur and minerals sulphur pesticides* (vitazalisha pembejeo); *Tan smart* (vilainishi vya magari na mashine mbalimbali); Nadeem (Kusindika vyakula aina mbalimbali); Mohamed Maaz Abdul (bidhaa mbalimbali); na *Tan Turk* (Kutengeneza na kuunganisha majenerata), vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, jumla ya wawekezaji 11 wamesaini mikataba na wanatarajia kuanza ujenzi pindi watakapokamilisha malipo. Kukamilika kwa kongani hiyo kutatoa ajira za moja kwa moja 30,000 na zisizo za moja kwa moja 200,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TIRDO* imeendelea na zoezi la kufanya tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji nchini. Hadi kufikia Machi, 2025 zoezi la ukusanyaji taarifa na uainishaji wa fursa za uwekezaji limefanyika Kanda ya Ziwa katika Mkoa wa Mwanza na Shinyanga. Tathmini hiyo ilibaini uwepo wa viwanda vikubwa 50, vya kati 109, vidogo 1,156 na vidogo sana 1,776 katika Mkoa wa Mwanza; na viwanda vikubwa 40 vya kati 92, vidogo 931 na vidogo sana 780 kwa Mkoa wa Shinyanga. Aidha, Wizara imeunda mfumo wa Kanzidata ya Taarifa za Viwanda Nchini *(National Industrial Information Management System)* ambao utakua na moduli nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025, Awamu ya Kwanza ya utengenezaji wa mfumo huo kwa upande wa moduli ya Viwanda umefikia 95%. Taarifa za viwanda kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Kilimanjaro, Tanga, Shinyanga na Mwanza zimeingizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ukamilishaji wa matengenezo ya mfumo huo kwa moduli tatu zilizobaki unaendelea. Mfumo huo utaimarisha uwazi wa taarifa, kurahisisha ufuatiliaji wa Sekta ya Viwanda na kutoa mwongozo kwa wawekezaji kuhusu maeneo yenye fursa bora za uwekezaji na hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Taasisi ya *CAMARTEC*. Hadi Machi, 2025 Wizara imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za ubunifu na tafiti tumizi zinazosababisha kupatikana kwa zana sahihi za kilimo na teknolojia za vijijini. *CAMARTEC* imefanya tathmini ya ufanisi na uhimili wa sampuli mbalimbali zikiwemo: Mashine za kuparura mazao mbalimbali katika Wilaya ya Chemba; Mashine za kutenganisha maganda na viini vya makokwa ya chikichi katika Wilaya ya Buhigwe; na

Mtambo wa kukaushia mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi Jijini Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya tathmini zote zilizofanyika yameonesha mafanikio makubwa yanayoruhusu sampuli vifani husika kuandaliwa kwa hatua inayofuata ambayo ni uzalishaji mkubwa wa zana na teknolojia hizo. Aidha, *CAMARTEC* imeunda mtambo wa kuzalisha hewa yenye joto unaotumia nishati mbadala kwa ajili ya kulitumia joto hilo kwenye makaushio ya mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TEMDO* inaendelea kutekeleza mradi wa usanifu na uundaji wa vifaa tiba vya hospitali Awamu ya Tatu ambapo hadi kufikia Machi, 2025 usanifu huo umekamilika kwa 100%. Mradi huo unalenga kuipunguzia nchi gharama kutokana na kuagiza vifaa tiba nje ya nchi. Kifaa tiba kilichosanifiwa na kuundwa ni jokofu la ngazi sita la kuhifadhi maiti; usanifu wa vifaa mbalimbali ikiwemo: *stretchers; theatre trolleys; and Autoclave* na mashine za kufulia; mitambo ya kuongeza thamani ya mazao ya korosho na chikichi; na mtambo wa kuzalisha nishati mbadala ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TEMDO* imeendelea kufanya juhudi za kuwasaidia wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya kwa kuwapa huduma kama vile maeneo ya kufanyia kazi; mashine na mitambo; ushauri wa kiufundi; na kuwaunganisha na watoa mitaji ili wakue kufikia kiwango cha kujitegemea. Hadi kufikia Machi 2025, wajasiriamali wanne ambao ni *Bivac Company Ltd, Rest Food Process Limited, Upendo Food Process Limited* na *Simba and Alice Food Process Limited* wameendelea kuzalisha bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo kwenye viatamizi hivyo kwa Mkoa wa Arusha. Bidhaa zilizobuniwa, kutengenezwa na kuuzwa na wajasiriamali hao ni pamoja na siagi ya karanga, unga lishe, vyakula lishe na mbegu mbalimbali za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *SIDO* imeendelea kuwapatia wajasiriamali teknolojia mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Teknolojia hizo zimekuwa ni msingi wa kuwawezesha

kuanzisha na kukuza miradi ya uzalishaji hususani kuongeza ufanisi, kuleta tija na kuhakikisha bidhaa zinazalishwa kwa viwango na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025 teknolojia mpya 17 zilibuniwa na *SIDO* na wajasiriamali katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga, Iringa na Mbeya. Teknolojia hizo ni: Teknolojia ya kuteketeza taka; Mashine iliyoboreshwa kwa ajili ya ubanguzi wa korosho; Mtambo wa kuongeza virutubisho kwenye unga; Tenki la umwagiliaji; Teknolojia ya kukamua mafuta kutoka kwenye viungo; Tenki la kuongeza virutubisho kwenye mafuta ya alizeti; na Mashine ya kusaga viungo inayohamishika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya mashine 463 na vipuri 3,028 vilitengenezwa na kuuzwa kwa wajasiriamali. Vilevile, Wizara imetoa huduma za matengenezo ya mashine na mitambo kwa viwanda 87 na kusaidia karakana binafsi 127 na kuzalisha mashine 127.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Chuo cha *CBE*. Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya atamizi za biashara kwa lengo la kusaidia ukuaji na maendeleo ya biashara changa *(Startups)* na wajasiriamali walioko katika hatua za awali. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya wanafunzi 361 wapo katika mafunzo ambapo kupitia mafunzo hayo, jumla ya wanafunzi 260 wamesajiliwa katika Awamu ya Kwanza, wanafunzi 75 wapo katika hatua ya Atamizi na wanafunzi 26 wapo katika hatua ya baada ya Atamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 54.24 kwa njia ya moja kwa moja na shilingi bilioni 11.96 kupitia Mfuko wa Dhamana wa Wakulima Wadogo. Kati ya fedha zilizotolewa kwa njia ya moja kwa moja, shilingi bilioni 6.15 zilitolewa kwa ajili ya uendeshaji wa viwanda 37 vya mazao ya Kahawa, Korosho, Pamba, Parachichi, Mpunga, Mkonge, Miwa, Zabibu, Mafuta ya Alizeti na Mawese pamoja na Usindikaji wa Nyama na Maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shilingi bilioni 11.96 ambazo zilitolewa kupitia Mfuko wa Dhamana wa Wakulima Wadogo zilielekezwa kwenye viwanda 26 vya uchakataji wa mazao ya nafaka, usindikaji wa zabibu, uchakataji wa kahawa na ukamuaji wa mafuta ya alizeti. Mikopo hiyo imewezesha uchakataji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza biashara Wizara imeendelea kuwezesha na kuimarisha wananchi kushiriki katika biashara ndani na nje ya nchi yetu. Wizara imeendelea hatua mbalimbali za kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinapata masoko ya kikanda na kimataifa. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea na majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa. Baadhi ya matokeo ya majadiliano hayo ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mfumo Rahisi wa Ufanyaji Biashara wa Wafanyabiashara Wadogo *(STR)* wanaovuka mipaka ya Tanzania na Zambia. Jumla ya bidhaa 51 zilikubaliwa kuingia katika Mfumo Rahisi wa Ufanyaji Biashara kwa Wafanyabiashara Wadogo wanaovuka mpaka wa Tanzania na Zambia kutoka bidhaa 22 za awali. Bidhaa hizo mpya ni pamoja na maharage, njegere, matunda mbalimbali, viazi mviringo, soya na mboga mboga za kukausha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa Tanzania na Malawi, majadiliano ya uwili ya kuanzisha Mkataba wa Taratibu Zilizorahisishwa za Kiforodha yamekamilika, ikiwa ni pamoja na jumla ya bidhaa 61 za Viwandani na Kilimo zimekubalika kuingia katika Mfumo huo wa *STR*; ukomo wa tathmini ya bidhaa ya dola za Kimarekani 2,000 umekubalika; na idadi ya uvukaji usiozidi ukomo wa thamani hiyo umekubalika pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shughuli za kikanda Wizara ilishiriki Mkutano wa 46 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara; Viwanda; Fedha na Uwekezaji uliofanyika Novemba, 2024 Jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo uliidhinisha kuongezeka kwa orodha ya bidhaa mpya 198 katika

orodha ya bidhaa zinazotumia Mfumo Rahisi wa Bidhaa Mpakani wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kufikia bidhaa 568.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika. Serikali imeanza kunufaika na utekelezaji wa mkataba huo kupitia biashara ya bidhaa za Kundi 'A' ambapo usafirishaji wa shehena ya kwanza ya bidhaa chini ya mwamvuli na kanuni za *AfCFTA* ulifanyika Julai 2023. Hadi kufikia Machi, 2025, Serikali imehamasisha wafanyabiashara kusafirisha shehena ya bidhaa 21 tofauti, ambapo kiasi cha takribani tani 1,000 zenye thamani zaidi ya Dola za Marekani Milioni 9.36 zimeuzwa katika nchi 18 za Afrika ambazo tulikuwa hatufungamani nazo. Hadi kufikia Machi, 2025, Tanzania imetoa jumla ya vyeti vya uasili wa bidhaa vipatavyo 131 kwa kampuni kuu katika soko huru la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ufuatiliaji wa masoko ya bidhaa zinazozlishwa nchini Wizara Wizara iliratibu Maonesho ya Pili ya Kimataifa ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania *(TIMEXPO 2024)* yaliyofanyika Uwanja wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Dar es Salaam Septemba hadi Oktoba, 2024. Katika maonesho hayo, kampuni 257 zilipata nafasi ya kutangaza bidhaa zao, kutanua wigo wa biashara zao na kujifunza teknolojia mpya za uzalishaji wa bidhaa. Aidha, Wizara iliratibu maonesho ya 11 ya biashara yaliyoambatana na sherehe ya miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar, yaliyofanyika Januari, 2025, katika viwanja vya Dimani Zanzibar. Katika maonesho hayo, jumla ya washiriki 338 walipata nafasi ya kutangaza huduma na bidhaa wanazozalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara vilevile iliratibu maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, 2024 yaliyofanyika Juni hadi Julai, 2024, kwa lengo la kutoa fursa kwa washiriki kutangaza bidhaa na huduma. Matokeo yaliyopatikana kutokana na maonesho hayo ni kuwezesha kampuni 3,954 kushiriki maonesho zinazojumuisha kampuni za ndani 3,503 na kampuni 551 kutoka nchi 28, kwa kufanikisha mauzo ya papo kwa papo ya kiasi cha shilingi bilioni 3.62 kilichangiwa zaidi na wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishiriki katika maonesho ya Saba Saba, Wiki ya Viwanda *SADC* yaliyofanyika Nchini Zimbabwe Agosti 2024. Kupitia maonesho hayo, nchi ilifanikiwa kuonesha bidhaa zinazozalishwa na baadhi ya viwanda na wajasiriamali wanawake. Viwanda hivyo ni pamoja na Kiwanda cha Kahawa cha *AMIMZA;* Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha, Kiwanda cha Kuchakata Mkonge cha *Aja International Limited; Mohamed Enterprises Tanzania Limited (METL); na CAPS Limited.* Maonesho hayo yaliiwezesha nchi kupokea tuzo za ubora kupitia kampuni za *METL* na *CAPS Limited* ambazo zilipewa Tuzo ya Ubora ya Viwango ya *SADC (SADC Quality Award)* kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo mengine ni kufanyika kwa makongamano ya maadhimisho ya miaka 50 ya mahusiano baina ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) yaliyofanyika Desemba, 2024 Tanzania na UAE. Katika makongamano hayo jumla ya wafanyabiashara 22 kutoka Tanzania walishiriki kongamano lililofanyika nchini *UAE* na wadau 391 walishiriki kongamano lililofanyika nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* imeendelea na juhudi za kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinapata utambulisho maalum katika masoko. Kupitia juhudi hizo, yaliyofanyika ni kukamilika kwa utengenezaji wa alama ya asali *(Tanzania Honey Brand Mark)* pamoja na kuandaa taratibu na kanuni za kupata alama hiyo na kukamilika kwa zoezi la kutafuta nembo maalum itakayotambulisha bidhaa za Tanzania *(National Brand Mark – Made in Tanzania)* katika masoko ya Kimataifa, ambapo jumla ya nembo 93 ziliwasilishwa katika zoezi hilo. Kati ya hizo, nembo tatu bora na bunifu zaidi zilishinda katika shindano hilo la Nembo ya Bidhaa na Huduma *(Made in Tanzania)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* imekamilisha viwango muhimu katika kilimo, chakula, uhandisi na aina nyingine mbalimbali za viwango. Jumla ya viwango 278 vilitayarishwa sawa na 40.3% ya lengo la kutayarisha viwango 690 kwa mwaka. Uandaaji wa viwango hivyo vimesaidia wazalishaji wa bidhaa

nchini kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuendana na mahitaji ya soko na hatimaye kutanua wigo wa masoko ndani na nje ya nchi ya Tanzania. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya leseni 482 za nembo ya ubora ya *TBS* zilitolewa ambayo ni sawa na 53.6% ya lengo la kutoa leseni 900 kwa mwaka. Vilevile *TBS* imesajili bidhaa za chakula na vipodozi 1,672 ambavyo ni sawa na 79.6% ya lengo la kusajili na kutoa vibali 2,100 kwa mwaka, kati ya bidhaa hizo, bidhaa 1,208 ni za chakula na bidhaa 464 ni za vipodozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2025, *TBS* ilifanikiwa kutoa jumla ya vyeti vya ubora 91,558 vimetolewa kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi ambayo ni sawa na 70.4% ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 130,000. Aidha, jumla ya magari 37,764 yaliyotumika nje ya nchi yalikaguliwa, sawa na 78.7% ya lengo la kukagua magari 48,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2025 *TBS* ilifanikiwa kupima jumla ya sampuli 28,642 kwa lengo la kuhakikisha ubora wake. Sampuli hizo ni sawa na 75.4% ya lengo la kupima sampuli 38,000 kwa mwaka. Aidha, *TBS* imefanikiwa kufanya ugezi wa vifaa/mashine mbalimbali ambapo jumla ya vifaa 8,052 vilifanyiwa ugezi sawa na 70% ya lengo la kufanya ugezi wa vifaa 11,500 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *TBS* imeendelea kutekeleza majukumu ya kuweka kinasaba kwenye mafuta ambapo jumla ya lita bilioni 3.5 za mafuta ya *petrol*, dizeli na mafuta ya taa ziliwekewa kinasaba sawa na 87.4% ya lengo la kuweka kinasaba katika lita bilioni 4.15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Ushindani *(FCC)* imeendelea kuchukua hatua katika kuboresha hali ya ushindani sokoni, ambapo jumla ya mashauri 27 yapo katika hatua mbalimbali za utatuzi. Kati ya mashauri hayo, mashauri matano yanahusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko, mashauri 16 yanayohusu miungano ya kampuni ambayo haikuidhinishwa na *FCC* na mashauri sita yanahusu ukiritimba sokoni. Aidha,

mashauri saba yamekamilika na yamechukuliwa hatua na mashauri 20 yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kumlinda mlaji dhidi ya mienendo potofu, uhalifu na kandamizi katika soko la bidhaa na huduma na kupambana na bidhaa bandia. Hadi kufikia Machi, 2025, malalamiko 87 ya walaji wadogo wadogo yalichukuliwa hatua ambapo, malalamiko 69 yalitatuliwa na malalamiko 14 yaliwasilishwa katika mamlaka zingine ambazo ni Mahakama, Jeshi la Polisi na *TCRA*. Vilevile, kaguzi za kushtukiza 35 zilifanyika sokoni, ambapo bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 3.3 zilikamatwa kwa kuvunja Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010. Tume imefanikiwa kukagua kontena 5,265, kati ya kontena hizo, kontena 411 sawa na asilimia 7.8 zenye thamani ya shilingi bilioni 10 zilikamatwa kwa kukiuka sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *FCC* imefanikiwa kupata Cheti cha Ithibati *ISO 9001:2015*, kinachoonesha dhamira ya ubora katika mifumo ya usimamizi wa ubora na utoaji wa huduma *(Quality Management System)*. Cheti hicho kinachotambulika Kimataifa kinaonyesha msisitizo wetu katika kuongeza ufanisi wa kiutendaji, kuridhika kwa wateja na ushirikishwaji wa wafanyakazi katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa wadau. Vilevile, cheti hicho kinaimarisha uaminifu wa *FCC* Kimataifa, kuongeza tija na kuendeleza maendeleo endelevu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Baraza la Ushindani, hadi kufikia Machi, 2025, Wizara imepokea jumla ya kesi 28 zinazoendelea kusikilizwa na kuamuliwa. *FCT* liliweza kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi tano na kesi 23 zinaendelea kusikilizwa katika hatua mbalimbali. Utatuzi wa mashauri hayo umeweza kupunguza migogoro ya wafanyabiashara, wawekezaji na walaji inayohusu ushindani wa kibiashara na udhibiti wa soko. kupitia Wakala wa Vipimo *(WMA)* Wizara imekagua na kuhakiki vipimo 1,013,859 sawa na 99.2% ya lengo la kukagua vipimo 1,022,342 vilivyopangwa kukaguliwa kwa mwaka. Kati ya vipimo hivyo, vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa, vipimo 10,898 vilirekebishwa na vipimo 761 vilikataliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *WMA* imeendelea kufanya kazi ya udhibiti wa bidhaa zilizofungashwa mipakani na bandarini katika vituo vya ukaguzi 13 ambavyo ni Sirari, Mtukula, Namanga, Holili, Tunduma, Tarakea, Horohoro, Kasumulu, Kwala na Bagamoyo, Manyovu, Mbweni na Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Wakala wa Biashara na Leseni *(BRELA)* imefanikiwa kusajili jumla ya kampuni 13,794 kati ya 16,200 zilizopangwa ikiwa ni sawa na 85%. *BRELA* imefanikiwa kutoa vyeti vya usajili wa viwanda 37 na 48 vilivyopangwa sawa na 77%. Pia *BRELA* imefanikiwa kutoa leseni za viwanda 298 kati ya 236 zilizopangwa ikiwa ni sawa na 126% na kutoa leseni za biashara, kundi "A'' 17,595 kati ya 15,120 zilizopangwa ikiwa ni sawa na 113%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala *(WRRB)* imekagua jumla ya maghala 237 ya kuhifadhia mazao na kutoa jumla ya leseni 237 ambazo ni za waendesha ghala katika bidhaa za korosho, mbaazi, ufuta, kakao, dengu na choroko. Kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghalani, Bodi ya Maghala imeweza kuratibu uuzwaji wa tani 872,844 za mazao ya kahawa, korosho, kakao, maharage, mihogo, mpunga, mbaazi, choroko, mchele, ufuta, chai, soya pamoja na dengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita. Kwa kipindi cha miaka minne (4) cha Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imepata mafanikio katika maeneo mbalimbali yakiwemo uendelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati, upanuzi na ujenzi wa viwanda, uendelezaji wa teknolojia mbalimbali, atamizi na ubunifu, utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania ndani na nje ya nchi, ubora wa bidhaa na ushindani wa kibiashara na utatuzi wa migogoro. Muhtasari wa baadhi ya mafanikio hayo kwa uchache sana ni kama ifuatavyo:-

Moja, Serikali imefanikiwa kulipa fidia ya shilingi bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 wanaopisha utekelezaji wa Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga. Aidha, Serikali kuanza hatua za

utekelezaji wa mradi huo hali kadhalika Mradi wa Magadi Soda Engaruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC)* Serikali imefanikiwa kufufua Kiwanda cha Kilimanjaro *Machine Tools (KMTC)* ambacho kwa sasa kinaendelea na uzalishaji. Kiwanda hicho kilisimama uzalishaji kwa zaidi ya miaka 30 ambapo katika kipindi cha miaka minne (4) ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan jumla ya shilingi bilioni 4.07 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali katika kiwanda hicho. Kiwanda hicho sasa kimefanikiwa uzalishaji wa jumla ya mashine 47 na vipuri 132. Aidha, kwa sasa kiwanda kimekuwa ni tegemeo kubwa la vipuri kutoka kwenye viwanda vya ndani vikiwemo kiwanda cha sukari (*TPC),* Kiwanda cha Bia *(TBL), Kili Leather,* viwanda vya mkonge na mashamba ya maua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji wa viwanda nchini. Kupitia juhudi hizo za Serikali, viwanda vikubwa vimejengwa na kupanuliwa vikiwemo *Kiwanda cha Wild Flower and Grains Limited; Kiwanda cha Chokaa cha Maweni,* Viwanda vya kuunganisha magari (*Kiwanda cha GF Trucks and Equipment Limited* kilichopo Kibaha – Pwani na Kiwanda cha *Saturn Corporation Limited)* kilichopo Kigamboni – Dar es Salaam, Kiwanda cha kutengeneza vioo (*Sapphire Float Glass (Tanzania) Company Limited),* Kiwanda cha Sukari cha Kilombero; Kiwanda cha Sukari Kagera na ujenzi wa viwanda vipya vya Sukari vya Mkulazi na Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, *TEMDO* imefanikiwa kutengeneza vifaa kadhaa vya hospitali ikiwemo majokofu nane ya kuhifadhia maiti, vitanda vya kawaida 452, kabati 426, *drip stand* 306, *hospital screen* 24 *na* vichomea taka ngumu 30 ambavyo vimesambazwa katika hospitali mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, *TEMDO* imefanikiwa kuunda mfumo wa Kitaifa wa kuhifadhi na kuchakata taarifa za viwanda nchini ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, SIDO imefanikiwa kuzalisha mashine 3,091 na vipuri 9,643 ambavyo vitasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati katika uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Wizara kupitia taasisi zake za *TIRDO, TEMDO, SIDO na CBE* imeanzisha na kuendeleza programu atamizi na uanagenzi ambapo katika kipindi cha miaka minne taasisi hizo zimeendelea na programu atamizi kwa wabunifu 808 ambao wako katika hatua mbalimbali za uendelezaji wa bunifu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Wizara imefanikiwa kukamilisha marejeo ya Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, Wizara kupitia *TANTRADE* imeratibu ushiriki wa Tanzania katika matukio mbalimbali ya ukuzaji biashara ndani na nje ya nchi yakiwemo Maonesho ya 45 hadi 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (*DITF)*, Maonesho ya Bidhaa za Viwanda, Maonesho ya *Expo* 2020 Dubai na Maonesho ya Kimataifa ya Mbogamboga na Matunda ya *Expo 2020 Doha*. Hati za Makubaliano 46 baina ya Kampuni mbalimbali za ndani na nje ya nchi zenye thamani ya shilingi trilioni 17.52 zilisainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano *(FYDP III)*, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Sera za Kisekta, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), Maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na mipango mbalimbali ya Kitaifa).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

(a) Kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa Viwanda nchini;

(b) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ya nchini;

(c) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mitaa ya viwanda (*Industrial Clusters*) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati;

(d) Kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa Sekta binafsi;

(e) Kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini;

(f) Kuchochea maendeleo ya watu kwa kuboresha miradi na programu kwa jamii inayohusisha elimu na mafunzo ya ujuzi; na

(g) Kuimarisha usimamizi wa ubora na usalama wa bidhaa nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vipodozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake ni kama ifuatavyo:

(a) Kukamilisha marejeo na kutekeleza Sera Endelevu ya Maendeleo ya Viwanda.

(b) Kuandaa mpango kabambe wa maendeleo ya viwanda hapa nchini.

(c) Kuandaa mkakati na muongozo wa kuunda na kunganisha magari.

(d) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya Mchuchuma, Liganga na mradi wa Magadi Soda Engaruka kule Mkoani Wilayani Monduli, Mkoani Arusha.

(e) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya Kimkakati ya Chuma Maganga Matitu, Makaa ya mawe Katewaka, Makaa ya Mawe Mhukuru pamoja na kulipia leseni za uchimbaji.

(f) Kufufua Kiwanda cha Mang'ula.

(g) Kuendelea kufanya tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji katika kanda za ziwa (Kagera, Geita, Mara na Simiyu) na Kanda ya Kaskazini.

(h) Kusanifu na kuendeleza utengenezaji wa vifaa tiba vya hospitali.

(i) Kuimarisha na kuanzisha mitaa ya viwanda na viwanda darasa kwa ajili ya kongani za viwanda na biashara katika Wilaya moja kila Mkoa.

(j) Kutayarisha viwango 740 vya Kitaifa katika sekta mbalimbali.

(k) Kusajili makampuni na majina ya biashara.

(l) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

(m) Kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania;

(n) Kuboresha hali ya ushindani na ulinzi wa mlaji katika soko.

(o) Kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri mbalimbali.

(p) Kujenga madarasa ili kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika eneo la Nzuguni - Kampasi ya Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani; Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka

wa fedha 2024/2025. Ufanisi huo ulipatikana kutokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Wizara wakiwemo washirika wa maendeleo, sekta binafsi, benki mbalimbali na wananchi kwa ujumla. kwa kuwa kidole kimoja hakivunji chawa, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru viongozi na Watendaji wote wa Sekta Binafsi wakiwemo Baraza la Taifa la Biashara, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania, Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania, Chemba ya Wafanyabiashara ya Wanawake (*Tanzania Chambers of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA)*, Jumuiya za Wafanyabiashara Tanzania ikiwemo Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kariakoo, Wamachinga, Wazalishaji wa Bidhaa za Ujenzi wakiwemo wazalishaji wa Nondo, Saruji, Bati, *Wallput, Gypsum, Gypsum board*, mbao kwa michango yao ambayo imesaidia sana Sekta ya Viwanda kuweza kunawiri na kushamiri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natambua kwa dhati mchango wa wajasiriamali wa kada zote, wakiwemo mafundi mchundo, mafundi seremala, mafundi uashi, wabunifu wa kazi za mikono na watoa huduma wa viwango mbalimbali ambao wanachangia kuinua uchumi kupitia Sekta ya Viwanda na Biashara. Wahenga walinena "akili ni mali; "jasho ni mtaji" na pia "kidole kimoja hakivunji chawa", hivyo mafanikio tunayoyashuhudia leo ni matokeo ya jitihada za pamoja baina ya Serikali na Sekta binafsi. Ahsanteni sana sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia Wamiliki na Waandishi wa Vyombo vya Habari na Wasanii wote kwa mchango wao katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zake kwa ujumla. Nawaomba tuendeleze ari hiyo ili tuweze kupanua wigo wa elimu kwa umma na hatimaye tushiriki kikamilifu katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara na kutia chachu zaidi katika mafanikio tuliyoyapata. Kwa hakika, neno likitumiwa vyema, hujenga Taifa na mchango wao katika kutoa taarifa sahihi, kuelimisha na kushirikisha jamii ni sehemu muhimu ya maendeleo ya viwanda na biashara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya kisima hayachimbiwi mbali. Ninawapongeza sana na kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe kwa ushirikiano walionipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa na yale ya Jimbo kwani ukaribu wetu ndiyo msingi wa mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza kwa jitihada zao za kuleta maendeleo katika Jimbo la Kisarawe na kunisaidia katika kutekeleza majukumu haya. Madiwani na wananchi wote wa Jimbo la Kisarawe ninawashukuru sana. Mkono mmoja hauchinji ng'ombe, kwa unyenyekevu mkubwa ninawaomba waendelee kushirikiana nami kuungana mkono kufanikisha kwa pamoja. Hakika ninawapenda sana na ninawathamini sana wananchi wangu wa Kisarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtumbwi mmoja huvushwa kwa pamoja, Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, wakiwemo Mheshimiwa Exaud S. Kigahe, Naibu Waziri wangu na Mbunge wa Mufindi Kaskazini (ninawaomba ndugu zangu wa Mufindi Kaskazini wamwangalie kwa jicho la wema Naibu Waziri wangu, ananisaidia sana), Dkt. Hashil T. Abdallah, Katibu Mkuu, Dkt. Suleiman H. Serera, Naibu Katibu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Taasisi, Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake; ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru wachapishaji wote akiwemo Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha nyaraka mbalimbali za Wizara kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano mkubwa kwa muda wote, Mungu awalipe mema wajumbe wote wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenda tezi na omo, marejeo ngamani. Maneno haya ya wahenga hutufundisha kuwa, licha ya shughuli na majukumu ya kitaifa ya kila siku, familia ni mahali pa faraja, nguvu na matumaini makubwa. Utekelezaji wa majukumu

yangu usingekuwa rahisi bila maombi na dua njema kutoka kwa watu wangu wa karibu. Nawaombea Pepo ya Firdaus wazazi wangu Saidi Ally Jafo, baba yangu na Khadija Amiri Madega ambao wametangulia mbele ya haki kwa malezi yao bora kwa kipindi chote cha uhai wao. Vilevile, walifanya kazi kubwa ya malezi, Mungu awalipe pepo huko walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninapenda kuwashukuru wake zangu, Rehema binti Disanura, Aisha binti Shame na Salma binti Dibibi. Hakika upendo wao umekuwa wa dhati sana kwangu, wamenisaidia kwa vipindi vyote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaffo, hawa ni watatu, siyo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru kwa msaada wao ambao hakika wamekuwa wake bora kwangu. Pia, ninaomba niwashukuru watoto wangu kwa upendo, faraja na subira wakati wote ninapotimiza majukumu yangu ya kitaifa. Hakika wananipa nguvu sana na ari ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo wa uzalendo na weledi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana vilevile, viongozi wangu wa Dini kwa mapenzi yao makubwa na dua. Pia, ninawashukuru ndugu zangu, jamaa na marafiki wote kwa kuendelea kuniombea kwa Mola ili niendelee kutimiza vyema majukumu yangu katika Taifa. Niwaahidi Watanzania wote kwa ujumla kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa kutanguliza maslahi ya Taifa mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa sana ninaomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wabunge wenzangu wote wa Bunge hili la Kumi na Mbili na watumishi wa Bunge kwa msaada, ushirikiano, upendo na mahaba ya dhati juu yangu, ahsanteni sana. Hakika wamenipenda, wamenithamini sana tena wakati wote kwa miaka yote minne ya Bunge hili la Kumi na Mbili. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika nami ninawapenda na kuwathamini sana kutoka ndani ya moyo wangu. Ninaomba Mungu anijalie hekima na unyenyekevu usio na kikomo, Mungu awalipe Waheshimiwa Wabunge malipo mema na *Inshallah* Mungu kwa uweza wake na mapenzi yake aturudishe Wabunge sote katika Bunge hili katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Mungu awabariki Wabunge wote warudi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya shilingi 135,788,232,000 katika Fungu 44. Kati ya fedha hizo, shilingi 93,900,697,000 ni matumizi ya kawaida na shilingi 41,887,535,000 ni matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya shilingi 93,900,697,000 za matumizi ya kawaida, shilingi 75,819,380,000 ni mishahara na shilingi 18,081,317,000 ni matumizi mengineyo. Aidha, kati ya shilingi 41,887,535,000 zinazoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na shilingi 27,870,710,000 ni fedha za ndani na shilingi 14,016,825,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika Tovuti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ni *www.mit.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania, Mbariki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**14 MEI, 2025**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SELEMANI SAIDI JAFO (MB.), WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 25 Machi, 2025, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2025/2026.

***2. Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote, muomba Mungu si mtovu, hivyo napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na fadhili kwa fanaka zake na afya njema zinazotuwezesha kumudu kuyatekeleza yale tuliyokasimiwa na Mamlaka na Umma wa Watanzania wote.

***3. Mheshimiwa Spika;*** Chanda chema huvikwa pete. Nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri, uzalendo na umakini wa hali ya juu. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya na siha njema, hekima na busara ili aendelee kuyatekeleza yale yote aliyoyapanga kwa manufaa ya nchi yetu. Aidha, namshukuru kwa dhati kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi ya kuongoza Wizara ya Viwanda na Biashara. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais ya kuwa, kwa kushirikiana na Naibu Waziri wangu, Viongozi wenzangu, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na wadau wote wa Wizara nitatekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia ili tuweze kufikia malengo mahsusi ya kuendeleza sekta ya Viwanda na Biashara. Nitaendelea kuwa msikivu kwake wakati wote kwani Mtoto msikivu ndiye abarikiwaye.

***4. Mheshimiwa Spika;*** Isiyo kongwe haivushi! Napenda kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa namna wanavyonipatia miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamekuwa chachu na amali za ziada kwangu katika kufanikisha majukumu yangu, kama Wahenga walivyosema elimu bila amali ni kama nta bila asali, hivyo nawashukuru sana kwa kuwa amali kwangu ya kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kikamilifu,

***5. Mheshimiwa Spika;*** Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar; na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa jitihada zao za kuendelea kusimamia na kuimarisha Muungano wetu na hatimaye kuleta maendeleo kwa Watanzania wote kwa ujumla. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (SMZ) kwa ushirikiano wake unaoniwezesha kutekeleza majukumu ya Sekta ya Viwanda na Biashara. Kwa hakika "kazi ya pamoja huzaa matunda", na mafanikio tunayoyaona leo ni zao la mshikamano na dhamira ya dhati kati ya pande mbili za Muungano.

***6. Mheshimiwa Spika;*** Ninapenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini na umahiri wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Nawaombea kwa Mola awaongoze, awalinde na awasimamie ili muweze kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa, kusimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. Maana kama walivyosema Wahenga, "Palipo na uongozi bora, hakuna jambo linaloshindikana." Kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Deodatus Philip

Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Viti Maalum. Sanjari na viongozi hao wa kamati niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Kamati hii imeendelea kutoa maelekezo na ushauri wenye tija kwa Wizara. Nikiri kuwa, kamati hii imekuwa chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara. Aidha, napenda kuishukuru Kamati kwa uchambuzi makini wakati wa kujadili Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026. Waswahili husema "Tano mkononi ni bora kuliko kumi porini", na hakika, ushauri na maelekezo waliotoa ni hazina halisi tuliyonayo katika safari ya maendeleo, na yametupatia muongozo mzuri katika kuandaa Hotuba hii ninayoiwasilisha leo. Ninawaahidi kuwa tutaendelea kupokea ushauri wao na kuufanyia kazi ili kuiendeleza sekta yetu pamoja.

***7. Mheshimiwa Spika***; Msiba haupigi hodi, na ni wajibu wetu kuwa pamoja katika huzuni kama tulivyo katika furaha. Naomba nichukue fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwako Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, familia, ndugu na jamaa wa marehemu kwa kuondokewa na wapendwa wetu, kwanza, Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia aliwahi kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa vipindi viwili tofauti Mhe. Cleopa David Msuya, aliyefariki dunia tarehe 7 Mei 2025, pili, Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani ukanda wa Afrika ambaye alifariki dunia tarehe 27 Novemba 2024 akiwa nchini India alipokuwa akipatiwa matibabu. Kwa hakika, vifo vya viongozi hawa ni pigo kubwa kwa taifa letu. Tutaendelea kuyaenzi maisha yao, tunapojifunza kutoka kwa uongozi wao uliotukuka. Tunaungana na familia zao, ndugu, jamaa na Watanzania wote katika kipindi hiki cha maombolezo, tukiomba Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema peponi, Amina. Vilevile, naungana na viongozi wenzangu kutoa pole kwa Watanzania wenzetu waliofikwa na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali ikiwa ni

pamoja na kuporomoka kwa jengo la ghorofa katika eneo la Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Nawapa pole kwa maafa hayo.

***8. Mheshimiwa Spika;*** Hali kadhalika, nawapongeza watoa hoja wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya Bajeti aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 9 Aprili, 2025. Hotuba hiyo inatoa hali ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa Mwaka 2024/2025 pamoja na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa Mwaka 2025/2026 katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Viwanda na Biashara. Safari ya pamoja haichoshi, hotuba hiyo imesaidia kuweka mwanga wa hatua tulizopiga na tunazotarajia ili sote kwa nafasi zetu tuendelee kushirikiana katika kujenga Taifa.

***9. Mheshimiwa Spika;*** Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 na mpango wa mwaka 2025/2026.

## 2. HALI NA MWENENDO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

### 2.1. Viwanda

**10.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi na upanuzi wa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo pamoja na vile vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi na zinazotumia malighafi zinazopatikana nchini kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wake, kuzalisha ajira na kukuza mauzo ya nje ya nchi. Kupitia jitihada hizo, viwanda vipya vimejengwa na vingine vimefanyiwa upanuzi kama ifuatavyo: -

### A. Viwanda vya Marumaru

***11. Mheshimiwa Spika*** Tanzania ina viwanda viwili (2) ambavyo ni kiwanda cha *Goodwill (Tanzania) Ceramic Company Ltd* na *KEDA (Tanzania) Ceramics Company Ltd*. Viwanda hivyo vina jumla ya uwezo uliosimikwa wa kuzalisha marumaru mita za

mraba 149,000 kwa siku sawa na mita za mraba 40,230,000 kwa mwaka (wastani wa siku 270 kwa mwaka/ siku za kazi). Hata hivyo, viwanda hivyo kwa sasa vinazalisha jumla ya mita za mraba 125,000 kwa siku sawa na mita za mraba 33,750,000 kwa mwaka. Mahitaji ya marumaru nchini ni mita za mraba 80,000 kwa siku. Viwanda hivyo vina ziada ya marumaru mita za mraba 45,000 ambapo kati ya hizo, marumaru zenye mita za mraba 25,000 huuzwa katika nchi za Kenya, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Zambia na Uganda.

***12. Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *Goodwill (T) Ceramic Company Ltd* kipo katika Wilaya ya Mkuranga, Mkoani Pwani na kinazalisha bidhaa za aina mbalimbali za marumaru. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha mita za mraba 100,000 za marumaru kwa siku sawa na mita za mraba 27,000,000 kwa mwaka. Kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha mita za mraba 78,000 kwa siku sawa na mita za mraba 21,060,000 kwa mwaka. Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 1,269 wa ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 6,500 ambao ni ajira zisizo za moja kwa moja. Kiwanda cha KEDA (Tanzania) *Ceramics Company Limited (Twyford)* kilichopo katika Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani, kinazalisha bidhaa za aina mbalimbali za marumaru. Uwezo uliosimikwa wa kiwanda ni kuzalisha mita za mraba 49,000 za marumaru kwa siku sawa na mita za mraba 13,230,000 kwa mwaka. Kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha mita za mraba 47,000 kwa siku sawa na mita za mraba 12,690,000 kwa mwaka. Kiwanda hicho kimetoa ajira 1,000 za moja kwa moja na ajira 6,000 zisizo za moja kwa moja.

### B. Viwanda vya Saruji

***13. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 14 vya kuzalisha saruji. Kati ya hivyo, viwanda saba (7) vinazalisha *clinker* na saruji na viwanda saba (7) vinazalisha saruji pekee. Viwanda vya saruji nchini huzalisha *clinker* ambayo ni malighafi muhimu kwa ajili ya kutengeneza bidhaa ya saruji. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha malighafi ya *clinker* tani 8,096,375 kwa mwaka. Uzalishaji halisi wa *clinker* nchini ni tani 7,104,000 na mahitaji ya malighafi ya *clinker* nchini ni tani 5,549,901. Hivyo, kuna ziada ya tani 1,554,099 ambayo huuzwa katika nchi za Jumuiya ya

Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

***14. Mheshimiwa Spika,*** Uzalishaji wa saruji nchini kwa mwaka 2024 ulikuwa tani 10,929,567.60 ambapo mahitaji ya ndani ya nchi ni takribani tani 8,500,000 kwa mwaka. Hivyo, kuna ziada ya tani 2,429,567.60 ambayo huuzwa katika masoko ya Rwanda, Malawi, Msumbiji, Burundi, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia. Viwanda vinavyozalisha saruji na kuuza nje ya nchi ni pamoja na *Dangote Industries Ltd, Tanzania Portland Cement PLC, Lake Cement Co. Ltd, Mbeya Cement Co. Ltd,* na *Tanga Cement PLC*. Sekta hiyo imetoa ajira 12,500 ambapo kati ya hizo, 5,220 ni ajira za moja kwa moja na 17,280 ni ajira zisizo za moja kwa moja.

**C. Viwanda vya Mbolea**

***15. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 36 vya kuzalisha mbolea. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa ni viwili (2) ambavyo ni Minjingu na *Itracom Fertilizer Limited,* kiwanda cha kati ni kimoja (1) cha YARA na viwanda vidogo 33 (***Jedwali Na. 1***) ambavyo hutengeneza mbolea za maji kwa kuchanganya mbolea za chumvichumvi. Viwanda hivyo vimetoa jumla ya ajira 1,910 za moja kwa moja na ajira 6,425 zisizo za moja kwa moja.

***16. Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha mbolea cha *Itracom Fertilizer Limited* ambacho ni kiwanda cha kimkakati kwa ukanda wa Afrika Mashariki kipo Eneo la Viwanda la Nala katika Jiji la Dodoma. Kiwanda kimewekeza shilingi bilioni 78.4 na kinaendelea na usimikaji wa mitambo minne (4) ya kuzalisha mbolea aina FOMI ambayo ni mseto wa mbolea asili na mbolea za chumvi chumvi. Hadi kufikia Machi, 2025 usimikaji wa mitambo hiyo yenye uwezo wa kuzalisha tani 800,000 kwa mwaka umekamilika na mitambo imeanza kufanya kazi ambapo tani za mbolea 72,600 zimezalishwa na kutoa ajira za moja kwa moja 827. Mbolea inayozalishwa huuzwa ndani na nchi za Burundi, Kenya na Uganda. Aidha, mtambo mwingine mmoja (1) wenye uwezo wa kuzalisha tani 200,000 za mbolea kwa mwaka unaendelea

kusimikwa. Vilevile, kiwanda kimesimika mitambo kwa ajili ya kuzalisha virekebishi udongo wenye uwezo wa kuzalisha tani 300,000 kwa mwaka. Pindi usimikaji wa mitambo yote utakapokamilika na uzalishaji utakapofikia uwezo uliosimikwa, kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 1,000,000 za mbolea kwa mwaka na kitatoa ajira za moja kwa moja 3,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 8,000.

***17. Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha mbolea cha Minjingu kipo eneo la Minjingu katika Mkoa wa Manyara. Kiwanda kimewekeza shilingi bilioni 50 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 250,000 za mbolea kwa mwaka. Hadi kufikia Machi 2025, kiwanda kimezalisha tani 59,600 za mbolea aina ya *Phosphate* ambazo ni sawa na asilimia 23.84 za uwezo uliosimikwa. Kiwanda kimetoa ajira 200 za moja kwa moja na ajira 560 zisizo za moja kwa moja. Aidha, kwa mwaka 2025/2026 kiwanda kina mpango wa kuongeza mitambo ya kuzalisha mbolea ya kukuzia ya NPK hadi kufikia tani 400,000 kwa mwaka.

***18. Mheshimiwa Spika;*** Kwa sasa mahitaji ya mbolea ni tani 1,000,000 ambapo zaidi ya asilimia 60 ni mbolea ya chumvi chumvi ambayo huagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa ujumla uzalishaji wa mbolea unaendelea kuimarika ambapo uwezo uliosimikwa wa viwanda unatarajiwa kuwa zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka. Malighafi zinazotumika kuzalisha mbolea katika viwanda vyetu hupatikana hapa nchini na nyingine huagizwa nje ya nchi hususan mbolea ya chumvi chumvi. Ili kupunguza uagizaji wa mbolea ya chumvi chumvi ambayo kiambato kikubwa ni kemikali zitokanazo na mazao ya petroli, juhudi zinaendelea kumpata mwekezaji atakaye anzisha kiwanda cha mbolea ya chumvi chumvi kinachotumia malighafi ya gesi asilia. Aidha, Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kupitia kiwanda cha Bidhaa za Kibaiolojia – Kibaha, lipo katika hatua za mwisho za kuanza uzalishaji wa mbolea ya kibaiolojia isiyo ya kemikali. Mbolea hiyo inatarajiwa kuingizwa sokoni kuanzia Mwezi Disemba 2026. Ili kupunguza uagizwaji mbolea nje ya nchi, juhudi zinaendelea kufanyika kumpata mwekezaji mahiri ambae anaweza kutumia gesi asilia kuzalisha mbolea ya chumvichumvi.

**D. Viwanda vya Kutengeneza Vioo**

***19. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda vinne (4) vya kuzalisha bidhaa za vioo. Viwanda hivyo ni Kioo Ltd; *Salehbhai Glass Industries* Ltd; *Sapphire Glass Industrial limited; na Keda Float Glass T. Ltd.* Kiwanda cha Kioo Ltd huzalisha chupa za vinywaji na viwanda vilivyosalia huzalisha vioo vya majumbani. Zaidi ya asilimia 95 ya malighafi zinazotumiwa na viwanda vya *Sapphire, Kioo Ltd na Keda* kuzalisha bidhaa zinapatikana nchini. Malighafi hizo ni pamoja na *dolomite, silca sand, limestone* na *feldspar*.

***20. Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *Sapphire Glass Industrial Limited* kimewekeza mtaji wa bilioni 800.1. Kiwanda hicho kilianza uzalishaji mwezi Septemba, 2023 baada ya kuzinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kiwanda `kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 700 kwa siku. Hadi kufikia Machi, 2025 kiwanda kimezalisha vioo tani 225,000 ambapo asilimia 60 ya vioo vinavyozalishwa huuzwa nje ya nchi. Nchi hizo ni pamoja na Madagascar, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) na Afrika Kusini. Kiwanda kimetoa ajira za moja kwa moja 1,012 na ajira zisizo za moja kwa moja 3,857. Aidha, kiwanda hicho kitakapokamilika kitatoa ajira za moja kwa moja 1,650 na ajira zisizo za moja kwa moja 6,000. Kiwanda kingine cha *Keda Float Glass T. Ltd* kimewekeza mtaji wa kiasi cha dola za Marekani milioni 309 na kina uwezo wa kuzalisha tani 600 kwa siku za vioo sawa na tani 220,000 kwa mwaka. Kiwanda kilianza uzalishaji mwezi Agosti, 2024 na kimetoa ajira za moja kwa moja 1,400 na ajira zisizo za moja kwa moja zaidi ya 6,000.

**E. Viwanda vya Kuunganisha Magari**

**21.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 13 vya kuunganisha magari. Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) vinaunganisha magari ambavyo ni *GF Trucks and Equipment Ltd* kilichopo eneo la TAMCO Kibaha, Pwani na *Saturn Corporation Limited* kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam. Viwanda 11 vilivyosalia vinatengeneza matrela. Kiwanda cha *GF Truck and*

*Equipment Ltd* kina uwezo uliosimikwa wa kuunganisha magari 200 kwa mwezi na kimewekeza kiasi cha shilingi bilioni 13 na kimetoa ajira 167. Kiwanda cha *Saturn Corporation Limited* kilichopo Kigamboni jijini Dar es salaam kina uwezo uliosimikwa wa kuunganisha vichwa vya magari 900 na magari aina ya tipa 270 kwa mwezi ambapo kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 64.3. Kiwanda kimetoa ajira za moja kwa moja 250 na ajira zisizo za moja kwa moja 1,800. Aidha, kiwanda cha TATA ambacho ujenzi wake unaendelea katika eneo la TAMCO Kibaha, Pwani kimewekeza jumla ya shilingi bilioni 19. Kiwanda hicho kitakapokamilika kinatarajia kuunganisha vichwa vya magari, tipa pamoja na pikipiki. Hadi kufikia Machi 2025 ujenzi wa kiwanda ulikuwa umefikia asilimia 70.

**F. Viwanda vya Sukari**

***22. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda saba (7) vya sukari ambavyo ni *Kilombero Sugar Company Limited (KSCL), Mtibwa Sugar Limited*, Kiwanda cha Sukari Mkulazi, *Kagera Sugar Limited*, *TPC Limited* Moshi, *Bagamoyo Sugar Limited* na Manyara *Sugar Company Limited*. Viwanda vya sukari vimetoa ajira za moja kwa moja takribani 34,200 na ajira zisizo za moja kwa moja 200,000. Aidha, Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha sukari tani 638,486.6 kwa mwaka, ambapo mahitaji ya sukari nchini ni tani 900,000. Kati ya tani hizo, tani 650,000 ni kwa matumizi ya kawaida na tani 250,000 ni kwa matumizi ya viwandani. Hadi kufika Machi, 2025 uzalishaji wa sukari ya matumizi ya kawaida ulikuwa tani 446,332.

***23. Mheshimiwa Spika;*** Katika jitihada za kupunguza uagizaji wa sukari ya viwandani ambayo haizalishwi hapa nchini, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa kufanya upanuzi wa kiwanda cha Mkulazi kitakachozalisha sukari ya viwandani. Aidha, Serikali imeendelea na mikakati ya kuanzisha miradi mipya ya viwanda vya sukari vikiwemo Kiwanda cha Sukari cha Rufiji na mradi wa kiwanda cha Sukari Kasulu katika Mkoa wa Kigoma. Kiwanda cha Sukari cha Rufiji kinachojengwa na Kampuni ya "Lake Agro" kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 30,000 za sukari kwa mwaka na mradi wa kiwanda cha sukari Kasulu unaotekelezwa na

kampuni ya "Mufindi Paper Mill" unatarajiwa kuzalisha tani 100,000 kwa mwaka na kufikia uzalishaji wa juu wa tani 300,000 kwa mwaka baada ya upanuzi. Kwa uwekezaji unaoendelea kufanyika katika viwanda vya sukari, ndani ya kipindi kifupi nchi yetu itaondokana kabisa na changamoto ya upungufu wa sukari.

**G. Viwanda vya Mabati**

**24.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 54 vya kuzalisha mabati ambapo viwanda vikubwa ni vinne (4) Lodhia, *MMI Steel, ALAF Limited* na *Kinglion* na viwanda 50 vilivyosalia ni viwanda vya kati. Viwanda hivyo vimetoa ajira 1,500 za moja kwa moja na ajira 8,500 zisizo za moja kwa moja. Viwanda vya mabati vya Lodhia, *ALAF Limited* na *MMI Steel* vimefanya upanuzi ambao umehusisha ujenzi wa majengo na kusimika mitambo mipya yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 200,000 kwa mwaka. Upanuzi wa kiwanda cha Lodhia umegharimu kiasi cha dola za Marekani million 60. Kutokana na upanuzi huo, kiwanda kimetoa ajira mpya za moja kwa moja 500 na ajira zisizo za moja kwa moja 1,000. Kwa upande wa kiwanda cha *ALAF Limited*, upanuzi umegharimu kiasi cha dola za Marekani million 25 na kutoa ajira mpya za moja kwa moja 75. Aidha, katika kiwanda cha *MMI Steel,* upanuzi umegharimu kiasi cha dola za Marekani million 60 na umewezesha upatikanaji wa ajira mpya za moja kwa moja 300. Upanuzi huo umewezesha kuzalisha mabati ya rangi kuanzia hatua ya awali hadi kuweka rangi. Kwa sasa uzalishaji wa mabati ya rangi umefikia tani 260,000 kwa mwaka, wakati mahitaji ya mabati ya rangi kwa mwaka nchini ni tani 130,000. Hivyo, kuna ziada ya tani 130,000.

**H. Viwanda vya Kubangua Korosho**

**25.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 57 vya kubangua korosho. Viwanda hivyo vipo katika mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Pwani, Singida, Katavi na Dar es salaam. Viwanda vina uwezo uliosimikwa wa kubangua korosho jumla ya tani 103,395 kwa mwaka. Hata hivyo, kati ya viwanda hivyo 57, ni viwanda 36 pekee vinavyofanya kazi. Viwanda hivi vimetoa ajira 6,702 za moja kwa moja na ajira 15,000 zisizo za moja kwa moja.

Sababu zilizopelekea viwanda 21 kutofanyakazi ni pamoja na ukosefu wa mitaji, uchakavu wa mitambo, teknolojia kupitwa na wakati, ukosefu wa utaalamu wa masoko ya nje na baadhi kushindwa kuhimili ushindani katika ununuzi wa korosho ghafi. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa ubanguaji wa korosho umekuwa ukiongezeka nchini kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali za kuhamasisha wawekezaji. Juhudi hizo zimewezesha kujengwa viwanda vitatu vikubwa vya kubangua korosho ambavyo ni Coastal Nuts (T) Ltd, Akofa East Africa (T) Ltd na Tankom (T) Ltd. Mathalani, ubanguaji wa korosho nchini ulikuwa tani 6,628.46 kwa msimu wa mwaka 2020/2021; tani 14,955.94 mwaka 2021/2022; tani 10,773.10 mwaka 2022/2023 na tani 26,656 mwaka 2023/2024

**i. Kiwanda cha Coastal Nuts(T) Ltd**

**26.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha kubangua korosho cha Coastal Nuts (T) Ltd kipo Wilaya ya Mtwara na kimewekeza mtaji wa dola za Marekani Milioni 6. Kiwanda hicho kilianza uzalishaji mwaka 2022 na kina uwezo wa kubangua korosho tani 6,000 kwa mwaka. Kiwanda kimetoa ajira 200 za moja kwa moja na 450 zisizo za moja kwa moja. Katika msimu wa 2022/2023 na 2023/2024 kiwanda kilibangua tani 1,000 na 1,500 mtawalia. Kwa msimu wa 2024/2025 kiwanda kinatarajia kubangua tani 4,000.

**ii. Kiwanda cha Akofa East Africa (T) Ltd**

**27.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha kubangua korosho cha Akofa East Africa (T) LTD kipo Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani na kimewekeza mtaji wa kiasi cha shilingi bilioni 6. Kiwanda hicho kilianza uzalishaji mwaka 2022 na kina uwezo wa kubangua korosho tani 8,000 kwa mwaka. Kiwanda kimetoa ajira 500 za moja kwa moja na 300 zisizo za moja kwa moja. Katika msimu wa 2022/2023 na 2023/2024 kiwanda kilibangua tani 800 na 3000 mtawalia. Kwa msimu wa 2024/2025 kiwanda kinatarajia kubangua tani 4,500.

**iii. Kiwanda cha Tankom (T) Ltd**

**28.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha kubangua korosho cha Tankom (T) LTD kipo Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani na kimewekeza mtaji wa kiasi cha dola za Marekani milioni 2. Kiwanda hicho kilianza uzalishaji mwaka 2022 na kina uwezo wa kubangua korosho tani 3,000 kwa mwaka. Kiwanda kimetoa ajira 180 za moja kwa moja na 340 zisizo za moja kwa moja. Kiwanda kilianza ubanguaji wa korosho msimu wa 2023/204 na kiliweza kubangua tani 125. Kwa msimu wa 2024/2025 kiwanda kinatarajia kubangua tani 2,500.

**I. Viwanda vya Wanga na Glukosi ya Maji**

**29.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *East African Starch Limited* ni kiwanda pekee nchini Tanzania kinachozalisha wanga na glukosi ya maji kutoka kwenye mahindi. Kiwanda hicho kilichopo Mkoa wa Mbeya kilianza uzalishaji wa majaribio mwaka 2022 na uzalishaji rasmi mwaka 2024. Kiwanda kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 20 na kinazalisha glukosi ya maji ambayo hutumika kama malighafi ya kuzalisha bidhaa mbalimbali za viwandani ikiwemo biskuti, pipi, *ice cream* na madawa. Uwezo uliosimikwa wa kiwanda ni kuzalisha tani 15,000 za wanga na tani 12,000 za glukosi ya maji kwa mwaka kutokana na mahindi tani 40,000 hadi tani 45,000. Hadi kufikia Machi, 2025 kiwanda kimezalisha tani 187 za wanga na tani 700 za glukosi ya maji. Aidha, kiwanda kimetoa ajira 80 za moja kwa moja na 20 zisizo za moja kwa moja. Kiwanda kitakapojiendesha katika uwezo wake uliosimikwa, kitakuwa na uwezo wa kutoa ajira 300 za moja kwa moja na 50 zisizo za moja kwa moja.

**J. Viwanda vya Kuzalisha Vipuri vya Magari na Pikipiki**

**30.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kampuni ya Kitanzania ya *Oasis Group* iliyopo Mikocheni Dar es Salaam chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) imeanzisha mradi wa kipekee wa kutengeneza betri za umeme (lithium) zitakazotumika katika magari na pikipiki hapa nchini wenye thamani ya dola za Marekani milioni 4.8. Mradi huo pia

utahusisha utengenezaji wa fremu za pikipiki 50,000 kwa mwaka pamoja na ujenzi wa vituo vya kuchajia betri. Uzalishaji wa betri na fremu hizo ndani ya nchi unatarajiwa kukuza uwezo wa viwanda nchini kupitia uhamishaji wa teknolojia, kuongeza ajira zenye ujuzi na kupunguza uchafuzi wa hewa. Kwa sasa, mradi upo katika hatua ya maandalizi ya uzalishaji, na shughuli za uzalishaji zinatarajiwa kuanza Agosti, 2025.

**2.2. Biashara**

**31.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina fursa mbalimbali za masoko ya nje ya kuuza mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini. Katika kutumia fursa hizo, Wizara imeendelea kushiriki majadiliano ya biashara baina ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa lengo likiwa ni kupanua wigo wa fursa za masoko yenye masharti nafuu ya bidhaa na huduma na kuvutia biashara na uwekezaji. Katika mwaka 2023/2024 mwenendo wa biashara ulikuwa kama ifuatavyo:

**A. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)**

**32.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2024, Tanzania iliendelea kuboresha mahusiano ya kibiashara na nchi mbalimbali duniani. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa zilizouzwa kwenye soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ilikuwa dola za Marekani milioni 1,163.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,180.5 mwaka 2023 sawa na upungufu ya asilimia 1.4. Upungufu huo umechangiwa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za viwanda, nafaka, mbolea, chumvi, samaki na mazao ya samaki katika nchi za Rwanda na Burundi; na kuongezeka kwa mauzo katika kanda nyingine hususan SADC na AfCFTA.

**33.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2024 bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 527.3 ziliagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 523.6 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 0.7. Ongezeko hilo limetokana na urahisi wa upatikanaji wa baadhi ya bidhaa kutoka nchi jirani kwa masoko ya mipakani na utashi wa walaji. **(Jedwali Na. 2)**. Mwenendo wa

jumla wa ufanyaji biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024 umeendelea kuwa urari chanya wa biashara.

**B. Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)**

**34. *Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2024, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ilikuwa ni dola za Marekani milioni 2,968 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,727.5 mwaka 2023 sawa na ongezo la asilimia 71.8. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa mbalimbali kama vile vile madini, parachichi, kahawa, tumbaku, vigae, mavazi, vyandarua, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka. Aidha, kwa mwaka 2024, bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 786.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 786.1 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 0.04 **(Jedwali Na. 3)**. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa uagizaji wa kemikali za kuzalisha mbolea, juisi mchanganyiko, mabati na bidhaa za chuma. Mwenendo wa jumla wa ufanyaji biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine za SADC kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024 umeendelea kuwa urari chanya wa biashara.

**C. Mwenendo wa Biashara Kati ya Tanzania na Nchi za Afrika – AfCFTA**

**35. *Mheshimiwa Spika;*** Mwenendo wa mauzo ya nje ya Tanzania katika nchi za Bara la Afrika kwa mwaka 2024 yalikuwa dola za Marekani milioni 3,946.76 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,341.37 kwa mwaka 2023 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 40. Ongezeko hilo, lilitokana na kuongezeka kwa masoko mapya chini ya AfCFTA yanayojumuisha nchi za Morocco, Nigeria, Senegal, Ghana, Misri, Ethiopia, Algeria, Djibuti, Somalia na Guinea. Bidhaa zilizochangia mauzo hayo ni pamoja na kahawa, tumbaku, vioo, nafaka (mchele na mahindi), viungo na nyuzi za mkonge **(Jedwali Na. 4)**. Aidha, kwa mwaka 2024 bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani Milioni 1,374.97 ikilinganishwa na dola za Marekani

milioni 1,430.58 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 4.04. Upungufu huo ulichangiwa na kupungua kwa uagizaji wa sukari za viwandani, madawa ya binadamu na *plasters* za *gypsum* kutoka Misri. Mwenendo wa jumla wa ufanyaji biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine za soko la AfCFTA kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024 umeendelea kuwa urari chanya wa biashara.

**D. Soko la Umoja wa Ulaya (EU)**

**36. *Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2024 thamani ya mauzo ya bidhaa katika soko la Jumuiya ya Umoja wa Ulaya ilikuwa dola za Marekani millioni 686.3 ikilinganishwa dola za Marekani milioni 633.5 mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.6. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za kakao, parachichi, tumbaku, kahawa na madini. Aidha, mwaka 2024 uagizaji wa bidhaa kutoka soko la Jumuiya ya Umoja wa Ulaya ulikuwa dola za Marekani milioni 1,267.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,174.9 kwa mwaka 2023, sawa ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hilo lilichangiwa na uhitaji wa malighafi na mitambo ya kuzalisha bidhaa viwandani na migodini **(Jedwali Na. 5)**.

**E. Bara la Asia**

***37. Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda baadhi ya nchi za Bara la Asia hususan kwa nchi za China, India, Japan, Singapore na Umoja wa Falme za Kiarabu ilikuwa dola za Marekani milioni 2,840.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,924.1 mwaka 2023 **(Jedwali Na. 6)** sawa na upungufu wa asilimia 2.9. Upungufu huo ulichangiwa na mabadiliko ya mahitaji ya Soko na ushindani mkubwa kutoka katika nchi nyingine zilizouza bidhaa kama hizo. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na madini, mazao jamii ya kunde, korosho, parachichi, pamba, nyama ya mbuzi, mbogamboga, tumbaku, ufuta, kakao na karanga.

***38. Mheshimiwa Spika;*** Aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka baadhi ya nchi za Bara la Asia ulikuwa na thamani ya dola za

Marekani milioni 5,514.2 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,409.3 kwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 34.4. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za mitaji, Plastiki na usafirishaji. Bidhaa zilizonunuliwa kwa wingi ni pamoja na magari, pikipiki, mafuta ya gesi na petroli, simu, sukari kwa ajili ya matumizi ya viwandani, saruji nyeupe na bidhaa za chuma.

**2.3. Mchango wa Sekta ya Viwanda na Biashara Nchini**

***39. Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2024 ulikuwa asilimia 7.3 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2023 (Jedwali Na. 7). Aidha, ukuaji wa Sekta ya Viwanda ulikuwa asilimia 4.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2023 **(Jedwali Na. 8).**

***40. Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa kwa mwaka 2024 ulikuwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2023. Aidha, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Biashara ilikuwa asilimia 4.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2023. Ukuaji huo umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara.

**3. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025**

**41. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kutekeleza maeneo ya kipaumbele yakiwemo kuendeleza miradi ya Kielelezo ya Magadi Soda Engaruka; Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Chuma cha Liganga; Kuendeleza Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools Company (KMTC); Kuratibu majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa; na Kuboresha mazingira ya biashara. Maeneo mengine ya kipaumbele ni: Kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania; Kuendeleza mitaa ya viwanda; Kukuza na kuboresha hali ya ushindani sokoni, ubunifu, uhawilishaji na ukuzaji wa teknolojia.

## 3.1. Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

### *3.1.1 Fedha Zilizoidhinishwa*

**42. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 110,899,722,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 81,115,206,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, zinazojumuisha shilingi 12,762,260,000.00 za Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi 68,352,946,000.00 za Mishahara. Aidha, shilingi 29,784,516,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

### 3.1.2 Fedha Zilizopokelewa

***Fedha za Matumizi ya Kawaida***

**43. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 75,747,677,767.85, sawa na asilimia 68.30 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 9,170,635,771.78 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na asilimia 71.86 na shilingi 52,800,269,874.07 kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 77.25 ya fedha zilizotengwa.

***Fedha za Maendeleo***

**44. *Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 13,776,772,122.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 46.25 ya fedha zilizotengwa.

## 3.2. Utekelezaji wa Mipango

### *3.2.1. Maendeleo ya Viwanda*

***A. Kuendeleza Miradi ya Kimkakati na Kielelezo***

***Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga***

**45. *Mheshimiwa Spika;*** Serikali baada ya kukamilisha malipo ya fidia ya kiasi cha shilingi bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142

waliopisha eneo la utekelezaji wa mradi. Serikali inaendelea na majadiliano na mwekezaji ambaye ni Kampuni ya "Shudao Investment Group Company Limited (SDIG)" inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Awamu ya kwanza ya majadiliano na mwekezaji ilifanyika Januari, 2025, awamu ya pili ilifanyika Februari, 2025 na awamu ya tatu ilifanyika Aprili, 2025. Masuala yaliyokubalika hadi sasa katika majadiliano hayo ni pamoja na makubaliano katika vipengele muhimu vya mikataba ikiwemo misingi sahihi ya mgawanyo wa hisa na muundo wa uwekezaji (Financing structure); kiwango cha mtaji wa uwekezaji unaohitajika; muundo wa usimamizi na uendeshaji wa mradi; muda wa Mkataba wa Uwekezaji; uhuishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi; na uandaaji wa modeli ya kifedha ya pamoja.

**ii. Mradi wa Magadi Soda Engaruka**

***46. Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia NDC imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kimkakati na kielelezo wa Magadi soda uliopo katika bonde la Engaruka wilayani Monduli. Katika mwaka 2024/2025, Serikali imetoa jumla ya shilingi 6,304,672,959 kwa ajili ya mradi huo. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,895,890,224 ni kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi 595 waliopisha Mradi, na kiasi cha shilingi 408,782,735 ni kwa ajili ya malipo ya ada ya mwaka ya leseni ya uchimbaji madini. Zoezi la ulipaji fidia lilizinduliwa rasmi Januari, 2025 katika eneo la Engaruka Mkoa wa Arusha. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya shilingi 5,702,104,241.70 sawa na asilimia 97 ya fedha zote za fidia zililipwa kwa wafidiwa 528 kati ya wafidiwa 595. Aidha, ukamilishaji wa zoezi la ulipaji fidia wa kiasi kilichobaki cha shingi 194,303,812.31 unaendelea kwa wafidiwa 67 waliobaki ambao wanakamilisha nyaraka muhimu zikiwemo taratibu za mirathi.

***47. Mheshimiwa Spika;*** Kwa sasa mradi upo katika hatua za mwisho za kupata wawekezaji wawili watakaojenga viwanda vya kuchenjua Magadi. Uamuzi wa kuwa na wawekezaji wawili ni kutokana na uwepo wa mashapo mengi ya Magadi katika mfumo wa maji kiasi cha mita za ujazo bilioni 3.2 ambazo zinaendelea kuongezeka kila mwaka. Uwekezaji wa viwanda viwili

na miundombinu yake inatarajiwa kutumia dola za Marekani milioni 700 ambapo utawezesha nchi kuwa mzalishaji namba moja wa Magadi soda katika Afrika. Mradi huu unatarajia kuiingizia Serikali mapato ya dola za Marekani milioni 42 kutokana na tozo na kodi mbalimbali. Aidha, utazalisha ajira 1,000 - 1,400 za moja kwa moja na kati ya ajira 4,000 - 5,600 zisizokuwa za moja kwa moja. Vilevile, Mradi utachochea uanzishwaji wa viwanda vinavyotumia magadi kama malighafi katika uzalishaji.

**iii. Mradi wa Chuma cha Maganga Matitu**

***48. Mheshimiwa Spika****;* Wizara kupitia NDC ilisaini Mkataba wa Ubia na mwekezaji *Fujian Hexingwang Industry Tanzania Co.Ltd* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Chuma ghafi cha Maganga Matitu Agosti, 2024. Uwekezaji katika mradi huo unakadiriwa kuwa dola za Marekani million 77.45 na utadumu kwa miaka 25 na kupelekea Tanzania kuwa nchi ya nne (4) Afrika kwa uzalishaji wa chuma. Hatua zote za utekelezaji wa mradi zimekamilika ikiwa ni pamoja na Upembuzi Yakinifu, uliobaini uwepo wa kiwango cha mashapo ya chuma (*Iron ore*) tani milioni 100 katika kiwango cha *inferred* chenye ubora wa chuma (44.6%), *Titanium Oxide* (11.2%) na *Vanadium Pentoxide* (0.41%). Aidha, uzalishaji wa mgodi unatarajiwa kuwa tani milioni 1.0 kwa mwaka za chuma ghafi, tani 100,000 kwa mwaka za *Titanium concentrate* na tani 483,000 kwa mwaka za mabaki ya madini tajwa (*tailings)*. Hadi kufikia Machi, 2025, Kampuni ya Ubia ya *Maganga Matitu Minerals Corporation Limited (MMCL)* imeanzishwa kati ya Serikali kupitia Msajili wa Hazina, NDC na mwekezaji huyo.

***49. Mheshimiwa Spika;*** Utekelezaji wa mradi huo utaanza baada kulipa fidia wananchi wanaozunguka eneo hilo. Zoezi la ulipaji wa fidia linatarajiwa kufanyika kabla ya mwaka 2024/2025 kuisha ambapo kiasi cha shilingi 4,215,600,214 kinatarajiwa kulipwa kwa wananchi 385. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kupatikana ajira 1,000 ambapo kati ya ajira hizo, ajira 300 ni za moja kwa moja na ajira 700 zisizo za moja kwa moja. Aidha, mradi utaiwezesha nchi kutumia rasilimali za ndani kuzalisha bidhaa mbalimbali za chuma ambazo zitawezesha uanzishwaji wa viwanda vingine vitakavyoongeza mnyororo wa

thamani (*downstream processing industries*). Vilevile, mradi utaokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza bidhaa za chuma nje ya nchi na utaondoa au kupunguza uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na matumizi ya vyuma chakavu ambavyo wakati mwingine vinakosa ubora.

**iv. Mradi wa Makaa ya Mawe Katewaka**

***50. Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia NDC imefanikiwa kusimamia mradi wa makaa ya mawe Katewaka ambao upo katika hatua za mwisho kuanza utekelezaji. Mradi huo ni muhimu katika uendelezaji wa sekta ya viwanda, kuongeza ajira nchini pamoja na kuingiza fedha za kigeni kwa mauzo ya makaa ya mawe nje ya nchi. Mradi huo ambao una mashapo tani milioni 100 za makaa ya mawe unatarajiwa kuzalisha wastani wa tani milioni 1.5 kwa mwaka. Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imefanikiwa kufanya vikao vya majadiliano na mwekezaji na kukamilisha kuandaa Rasimu ya Mpango Kazi wa utekelezaji wa mradi huo. Aidha, Serikali imefanikiwa kukamilisha uthamini wa wananchi 693 watakaopisha mradi ambapo kiasi cha fidia ya shilingi 2,089,642,544 kinatarajiwa kulipwa kabla ya mwezi Septemba 2025.

**B. Kuwezesha Uanzishwaji wa Viwanda Vipya na Kongani za Viwanda**

**Kongani ya Viwanda Sino Tan Industrial Park- Kwala Mkoani Pwani**

***51. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kuvutia uwekezaji wa ujenzi wa kongani ya Viwanda *Sino Tan Industrial Park* iliyopo Kwala Mkoa wa Pwani inayotarajiwa kuwa na viwanda vikubwa 200 na viwanda vidogo 300 pindi ujenzi utakapokamilika. Aidha, Mwekezaji katika mradi huo ambaye ni *Sino Tan* anatarajia kukamilisha ujenzi wote wa kongani ifikapo mwaka 2027. Hatua ya awali ya ujenzi imehusisha ekari 500 kati ya ekari 2,500 ambapo ujenzi umefikia asilimia 80. Kukamilika kwa kongani hiyo kunatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja 100,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 500,000 na kuzalisha bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 6.

***52. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi 2025, ujenzi wa miundombinu iliyokamilika ni barabara kuu ya ndani, miundombinu ya maji, jengo la utawala, jengo la zimamoto, jengo la hosteli, majengo sita (6) ya viwanda na jengo la kufundishia mafundi. Vilevile, miundombinu ya umeme mkubwa (50 MW) ipo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Kutokana na kukamilika kwa miundombinu hiyo, viwanda vinne (4) vimeanza uzalishaji ambavyo ni Kiwanda cha nguo cha *House of Garments*; Kiwanda cha vipodozi cha *KVS Chemicals*; Kiwanda cha *Snowsea* kinachozalisha vifaa vya umeme vya majokofu na kabati maalum ya kuhifadhia bidhaa baridi. Aidha, wawekezaji sita (6) wa viwanda tayari wamesaini mikataba na wanaendelea na taratibu za kuanza ujenzi.

**Kongani ya Kisasa ya Viwanda Modern Industrial Park –Mlandizi, Pwani**

***53. Mheshimiwa Spika;*** Mradi wa kongani ya kisasa ya viwanda ulianza ujenzi Septemba, 2021 na unatarajiwa kugharimu shilingi trilioni 3.5. Ujenzi huo umechukua jumla ya eneo lenye ukubwa wa ekari 1,077, ambapo eneo hilo limegawanywa katika viwanja 210. Kati ya viwanja hivyo, viwanja 202 ni kwa ajili ya viwanda, viwanja viwili (2) ni kwa ajili ya vituo vya umeme (54MW) na (400MW), viwanja viwili (2) ni vya maeneo ya biashara, viwanja vitatu (3) ni kwa ajili ya huduma za jamii na kiwanja kimoja (1) ni kwa ajili ya bandari kavu.

***54. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 jengo la utawala, kituo cha huduma za pamoja kwa ajili ya Taasisi za Serikali (one stop centre), ujenzi wa kituo cha zimamoto, ujenzi wa kituo cha Afya na uzio wa kilomita 9 zimekamilika. Aidha, viwanda vitano (5) ambavyo ni *Sulphur and mineralssulphur pesticides* (vitazalisha pembejeo) *Tan smart lyf- lubricants for machines and vehicles* (Vilainishi vya magari na mashine mbalimbali), *Nadeem-food processing* (Kusindika vyakula aina mbalimbali), *Mohamed Maaz Abdul – General industry*; na *TanTurk- generator assembly* (Kutengeneza na kuunganisha majenerata) vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Vilevile, jumla ya wawekezaji 11 wamesaini mikataba na wanatarajia kuanza ujenzi pindi watakapomaliza

malipo. Kukamilika kwa kongani hiyo kutatoa ajira za moja kwa moja 30,000 na zisizo za moja kwa moja 200,000.

**C. Kuimarisha Ufanisi katika Sekta ya Viwanda na Biashara kupitia Falsafa ya KAIZEN**

***55. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya ufanisi ya KAIZEN kupitia Mradi wa Huduma za Maendeleo ya Biashara (BDS). Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imetoa mafunzo ya huduma za maendeleo ya biashara kwa wakufunzi 97 na wajasiriamali 884 katika Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Singida, Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Kisiwa cha Zanzibar. Aidha, Wizara imeshiriki mashindano ya KAIZEN yaliyofanyika nchini Tunisia Oktoba, 2024 ambapo kampuni na viwanda 60 zilishiriki mashindano hayo. Vilevile, kupitia mradi huo, Wizara iliratibu ushiriki wa mafunzo ya KAIZEN yaliyofanyika nchini Mauritius ambapo washiriki 10 walishiriki mafunzo hayo.

**D. Kufanya Tathmini ya Viwanda na Kuainisha Fursa za Uwekezaji**

***56. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO inaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji nchini. Hadi kufikia Machi, 2025 zoezi la ukusanyaji taarifa na uainishaji wa fursa za uwekezaji katika viwanda limefanyika Kanda ya Ziwa (Mwanza na Shinyanga). Tathmini hiyo ilibaini uwepo wa viwanda vikubwa 50, vya kati 109, vidogo 1,156 na vidogo sana 1,776 katika Mkoa wa Mwanza na viwanda vikubwa 40 vya kati 92, vidogo 931 na vidogo sana 780 kwa Mkoa wa Shinyanga. Aidha, Wizara imeunda mfumo wa Kanzidata ya Taarifa za Viwanda Nchini (National Industrial Information Management System (NIIMS)) ambao utakua na moduli nne (4) ambazo zitawezesha kupata taarifa za viwanda, maghala, masuala ya leseni, malighafi za viwanda, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji katika viwanda, taarifa za rasilimali watu, ujuzi na ajira.

***57. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 awamu ya kwanza ya matengenezo ya mfumo upande wa moduli ya Viwanda umefikia asilimia 95 na taarifa za viwanda kutoka Mikoa

ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Kilimanjaro, Tanga, Shinyanga na Mwanza zimeingizwa. Vilevile, ukamilishaji wa matengenezo ya mfumo huo kwa moduli zilizobaki unaendelea. Mfumo huo umeimarisha uwazi wa taarifa, kurahisisha ufuatiliaji wa sekta ya viwanda na kutoa mwongozo kwa wawekezaji kuhusu maeneo yenye fursa bora za uwekezaji na hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini.

**E. Kuimarisha Maabara kwa Ajili ya Utoaji Huduma**

**58.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuimarisha utoaji wa huduma za maabara, Wizara kupitia TIRDO inaendelea na hatua za kupata ithibati za maabara za ngozi na nguo; mazingira; kemia; teknolojia ya kupima vifaa vya kihandisi bila kuharibu (*Non Distructive Testing)*; maabara za nishati; na madini ambazo zinabadili ithibati za awali kutoka Bodi ya *Southern African National Accreditation System* (SANAS) kwenda Bodi ya *Southern African Development Community Accreditation Service* (SADCAS). Aidha, tarehe 20 Machi 2025, Maabara ya Chakula ya TIRDO imefanikiwa kupata Ithibati Na. *TEST-1 0033 ya ISO 17025-2017* ambapo itawezesha maabara hiyo kupima sampuli kwa kiwango cha kimataifa. Maabara zilizobaki zinatarajia kukamilisha taratibu za kupata ithibati ifikapo mwaka 2027. Kukamilika kwa maabara hizo kutasaidia shirika kutoa huduma zitakazoweza kutambulika kimataifa na kuongeza uwezo wa viwanda katika maeneo husika. Aidha, Wizara imekamilisha mchakato wa kumpata mzabuni kwa ajili ya uanzishaji wa maabara ya nishati na madini katika Mkoa wa Njombe ambayo inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2026.

**F. Uvumbuzi, Utafiti na Uendelezaji wa Teknolojia**

***59. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara kupitia CAMARTEC imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za ubunifu na tafiti tumizi zinazopelekea kupatikana kwa zana sahihi za kilimo na teknolojia za vijijini. Wizara imefanya tathmini ya ufanisi na uhimili wa sampuli mbalimbali zikiwemo:- Mashine za kupura mazao mbalimbali katika Wilaya ya Chemba; Mashine za kutenganisha maganda na viini vya makokwa ya chikichi katika Wilaya ya Buhigwe; na Mtambo wa kukaushia mazao ya kilimo,

mifugo na uvuvi jijini Arusha. Matokeo ya tathmini zote zilizofanyika yameonesha mafanikio makubwa yanayoruhusu sampuli vifani husika kuandaliwa kwa hatua inayofuata ambayo ni uzalishaji mkubwa wa zana na teknolojia hizo.

***60. Mheshimiwa Spika;*** Mafanikio ya tathmini yameonekana katika upuraji wa dengu, alizeti na mbaazi; kutenganisha maganda na viini vya mbegu za matunda ya michikichi (mise); na ukaushaji wa korosho zilizobanguliwa na parachichi. Aidha, majaribio ya kukamua mafuta ya parachichi kwa kutumia mashine za mkono yameonesha mafanikio makubwa na hivyo kuleta suluhu ya kudumu kwenye kuongeza thamani ya parachichi zinapozalishwa kwa wingi na kukosa soko la uhakika. Wizara pia imeunda mtambo wa kuzalisha hewa yenye joto unaotumia nishati mbadala kwa ajili ya kulitumia joto hilo kwenye makaushio ya mazao mbalimbali. Majaribio ya awali ya mtambo huo yameonesha mafanikio makubwa kwa kufua joto hadi kufikia nyuzi joto 65 kwa dakika 5.

***61. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika masuala mbalimbali yakiwemo utengenezaji wa zana za kilimo na uongezaji thamani wa mazao. Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara imefanikiwa kuunda zana tatu (3) zinazotumika kupasua tabaka gumu la udongo (sub-soiler) kwa kuzingatia uhitaji wa Wizara ya Kilimo. Zana hizo zimeanza kutumika katika mradi wa Jenga Kesho Iliyobora (BBT) Chinangali na Ndogowe ambapo zimeonesha ufanisi mzuri kwa kulima ekari 120 wakati wa majaribio ya kukabidhiana. Aidha, Wizara inatarajia kuzalisha zana nyingine saba (7) (sub-soiler) kwa ajili ya mradi wa BBT; Kuunda vipandio vitano (5) vinavyotumia injini ya pikipiki (RAFIKI cotton seed planter) zinazotumika na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya *Tanzania Agriculture Research Institute* (TARI – UKILIGURU); na kuendelea na ushirikiano na TARIUyole kwa ajili ya kuunda kipandio cha ngano kinachoendeshwa kwa trekta.

***62. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TEMDO inaendelea kutekeleza mradi wa usanifu na uundaji wa vifaa tiba vya hospitali awamu ya III ambapo hadi kufikia Machi, 2025 usanifu huo umekamilika kwa asilimia 100. Mradi huo unalenga kuipunguzia

nchi gharama kutokana na kuagiza vifaa tiba nje ya nchi. Kifaa tiba kilichosanifiwa na kuundwa ni jokofu la ngazi sita la kuhifadhi maiti. Vilevile, Wizara imekamilisha usanifu wa vifaa mbalimbali ambavyo ni:'stretchers', 'theatre trolleys', 'Autoclave', na mashine za kufulia; mitambo ya kuongeza thamani ya mazao ya korosho na chikichi; na mtambo wa kuzalisha nishati mbadala ya kupikia.

***63. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia FCC inaendelea na juhudi za kufanya utafiti kuhusu ushindani na ulinzi wa mlaji. Wizara imekamilisha utafiti katika soko la nyaya za umeme na tayari matokeo ya utafiti huo yameidhinishwa. Utafiti huo ulibaini uwepo wa viashiria vya ukiukwaji wa misingi ya ushindani na ulinzi wa mlaji. Kufuatia matokeo ya utafiti huo, Wizara ilifanya uraghbishi kwa wadau wa soko hilo kwa ajili ya kujadili matokeo ya utafiti huo pamoja na mapendekezo yake. Wizara inaendelea kufuatilia soko hilo kwa ajili ya kuhakikisha misingi na haki za walaji zinalindwa.

### *G. Kuanzisha Vitovu vya Teknolojia za Kihandisi* (VITEKI) katika Wilaya za Maswa na Karatu

***64. Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia CAMARTEC imeendelea na shughuli za ugani wa zana za kilimo na teknolojia mbalimbali ambapo imefanikiwa kuanzisha Vitovu vya Teknolojia za Kihandisi (VITEKI) katika Wilaya ya Maswa, Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha. VITEKI hivyo vina jumla ya vifaa 119 ambapo kwa upande wa Maswa vipo 70 na Karatu vipo 49. Vifaa hivyo vinatumika kwa ajili ya kazi mbalimbali kama vile kupanda mazao, usafirishaji na uchakataji wa awali wa mazao ya kilimo.

***65. Mheshimiwa Spika;*** Kupitia VITEKI hivyo, wadau hususani wakulima wameweza kuhudumiwa kupitia mifumo rafiki ya matumizi ya zana za kilimo na teknolojia za vijijini kwa kuzikodi na hivyo kuwaondolea ulazima wa kuzinunua. Aidha, vijana 30 wametumia fursa hiyo kujipatia ajira na kipato kwa kukodi zana hizo na kwenda kutoa huduma kwa malipo kwenye vijiji mbalimbali. VITEKI hivyo pia vimekuwa vikitoa mafunzo kwa wadau mbalimbali ambapo jumla ya wadau 45 kutoka vijiji vya

Mwandete, Lalago, Sangamwalugesha na Shinyamwenege walipata mafunzo ya matumizi sahihi ya zana za kupukuchua mahindi, mtama na alizeti.

**3.2.2. Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

**Kubuni, Kutengeneza na Kusambaza Teknolojia Mpya kwa Ajili ya Matumizi ya Viwanda Vidogo na vya Kati**

***66. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kuwapatia wajasiriamali teknolojia mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Teknolojia hizo zimekuwa ni msingi wa kuwezesha kuanzisha na kukuza miradi ya uzalishaji hususan kuongeza ufanisi, kuleta tija na kuhakikisha bidhaa zinazalishwa kwa viwango na ubora unaotakiwa. Hadi kufikia Machi, 2025 teknolojia mpya 17 zilibuniwa na SIDO na wajasiriamali katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga, Iringa na Mbeya. Teknolojia hizo ni: Teknolojia ya kuteketeza taka; Mashine iliyoboreshwa kwa ajili ya ubanguzi wa korosho; Mtambo wa kuongeza virutubisho kwenye unga; Tenki la umwagiliaji; Teknolojia ya kukamua mafuta kutoka kwenye viungo; Tenki la kuongeza virutubisho kwenye mafuta ya alizeti; na Mashine ya kusaga viungo inayohamishika.

***67. Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, Wizara inamiliki vituo na karakana saba (7) katika Mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga. Vituo hivyo vinajihusisha na uendelezaji wa teknolojia na utengenezaji wa mashine/vifaa na kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wa mijini na vijijini kwa kuzingatia Mkakati wa Wilaya Moja, Bidhaa Moja (ODOP). Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Mashine 463 na Vipuri 3,028 vilitengenezwa na kuuzwa kwa wajasiriamali. Vilevile, Wizara imetoa huduma za matengenezo ya mashine na mitambo kwa viwanda 87 na kusaidia karakana binafsi 127 kuzalisha mashine 127.

**Kuendeleza Ubunifu wa Teknolojia na Mawazo ya Bidhaa Mpya Chini ya Programu ya Kiatamizi**

***68. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kuwasaidia wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya kwa kuwapa huduma wezeshi ikiwa ni pamoja na maeneo ya kufanyia kazi, ushauri wa kiufundi na mitaji ili wakue na kufikia viwango vya kujitegemea. Hadi kufikia Machi, 2025 mawazo bunifu matatu (03) yamehitimu katika Mkoa wa Arusha, Dar es salaam na Kilimanjaro. Mawazo hayo bunifu ni utengenezaji wa mbolea kutokana na nywele za binadamu, mashine ya kukatakata mchaichai kwa ajili ya kusindika, na mashine ya kurutubisha unga. Aidha, mawazo bunifu 22 kutoka kwa wabunifu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Mwanza, Singida na Morogoro yanaendelea kuatamiwa. Vilevile, katika kuwaendeleza na kuwawekea mazingira rafiki wabunifu, Wizara kupitia SIDO imeingia makubaliano na Tume ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Uatamizi Jijini Dar es Salaam. Hali kadhalika, moja ya makubaliano hayo ni kukarabati vituo vya uatamizi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Mwanza, Lindi na Tanga.

***69. Mheshimiwa Spika;*** Kwa upande wa TEMDO, juhudi zimefanyika za kuwasaidia wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya kwa kuwapa huduma kama vile maeneo ya kufanyia kazi,machine na mitambo, ushauri wa kiufundi na kuwaunganisha na watoa mitaji ili wakue na kufikia viwango vya kujitegemea. Hadi kufikia Machi, 2025 wajasiriamali wanne (4) ambao ni *Bivac Co. Ltd, Rest Food Process Ltd, Upendo Food Process Ltd* na *Simba and Alice Food Process Ltd* wameendelea kuzalisha bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo kwenye viatamizi hivyo kwa Mkoa wa Arusha. Bidhaa zilizobuniwa, kutengenezwa na kuuzwa na wajasiriamali hao ni pamoja na siagi ya karanga, unga lishe, vyakula lishe na mbegu mbalimbali za mazao.

***70. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Chuo cha CBE imeendelea kutoa mafunzo ya atamizi za biashara kwa lengo la kusaidia ukuaji na maendeleo ya biashara changa (Startups) na

wajasiriamali walioko katika hatua za awali. Mafunzo hayo yamegawanyika katika hatua tatu (3) ambazo ni:- Hatua Kabla ya Atamizi (Pre- Incubation); Hatua ya Atamizi (Incubation Stage) na Hatua Baada ya Atamizi (Post- Incubation). Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya wanafunzi 361 wapo katika mafunzo ambapo kupitia mafunzo hayo, jumla ya wanafunzi 260 wamesajiliwa katika awamu ya kwanza, wanafunzi 75 wapo katika hatua ya atamizi na wanafunzi 26 wapo katika hatua ya baada ya Atamizi.

### *C. Kuhamasisha Wajasiriamali Wadogo na wa Kati* Kuchangamkia Masoko ya Ndani na ya Nje

**71.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuelimisha wajasiriamali wadogo na wa kati kuhusu umuhimu wa kuzalisha na kutoa huduma kadri ya mahitaji ya soko la ndani na nje yanavyohitaji. Katika jitihada hizo, Wizara iliwezesha wajasiriamali 299 kushiriki katika maonesho ya Afrika Mashariki maarufu kwa jina la Nguvu Kazi au Jua Kali yaliyofanyika Juba, Sudani ya Kusini Oktoba hadi Novemba, 2024. Katika maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 1,700 kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliweza kushiriki. Maonesho hayo yamekuwa ya manufaa kwa wajasiriamali kwa kupata fursa za kupanua wigo wa soko la bidhaa zao pamoja na kubadilishana maarifa ya biashara kwa kuboresha bidhaa na mbinu mpya za teknolojia. Aidha, katika maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 158 walipata mikataba ya biashara yenye thamani ya shilingi milioni 176.

### Kutoa Huduma za Kifedha kwa Wajasiriamali

***72. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara kupitia mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF) imetoa jumla ya mikopo 841 yenye thamani ya shilingi blioni 2.4 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, ambapo asilimia 34 ya mikopo hiyo ilitolewa katika miradi ya vijijini. Kati ya mikopo hiyo, asilimia 51.5 ilitolewa kwa wanawake na asilimia 48.5 ilitolewa kwa wanaume. Mikopo hiyo iliwezesha kupatikana kwa ajira 1,395 ambapo wanawake ni asilimia 42.5. Aidha, wastani wa kiwango cha urejeshaji mikopo kimeimarika na kufikia asilimia 92 mwaka

2024 kutoka asilimia 90.1 mwaka 2023. Vilevile, kupitia Programu ya Uwezeshaji Viwanda Vidogo (SANVN Viwanda Scheme), Wizara imewezesha jumla ya wajasiriamali nane (08) kuunganishwa na Benki ya Azania na kupata mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 735. Halikadhalika, kupitia Mfuko wa Dhamana ya Serikali (CGS), wajasiriamali wanne (04) waliweza kupata mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 140.

***73. Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2024/25, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 54.24 kwa njia ya moja kwa moja (direct lending) na shilingi bilioni 11.96 kupitia Mfuko wa Dhamana wa Wakulima Wadogo (Smallholder Farmers Credit Guarantee Scheme). Kati ya fedha zilizotolewa kwa njia ya moja kwa moja, shilingi bilioni 6.15 zilitolewa kwa ajili ya uendeshaji (working capital) wa viwanda 37 vya mazao ya Kahawa, Korosho, Pamba, Parachichi, Mpunga, Mkonge, Miwa, Zabibu, Mafuta ya Alizeti, na Mawese pamoja na Usindikaji wa Nyama na Maziwa. Aidha, shilingi bilioni 11.96 ambazo zilitolewa kupitia Mfuko wa Dhamana wa Wakulima Wadogo zilielekezwa kwenye viwanda 26 vya uchakataji wa mazao ya nafaka, usindikaji wa zabibu, uchakataji wa kahawa, na ukamuaji wa mafuta ya alizeti. Mikopo hiyo imewezesha uchakataji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi katika mikoa mbalimbali nchini.

***74. Mheshimiwa Spika;*** Katika kutatua changamoto ya utoshelevu wa mafuta ya kula nchini, Benki ya TADB imewezesha ujenzi wa kiwanda kikubwa na cha kisasa chenye uwezo wa kukamua lita 70,000 za mafuta kwa siku kwa kutumia mbegu za soya, alizeti, pamba na chikichi. Kiwanda hicho kinachojengwa katika Mkoa wa Pwani kinatarajiwa kupunguza utegemezi wa Taifa wa uagizaji mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Ili kujenga uchumi wa viwanda unaoweza kushindana na kuiletea nchi yetu maendeleo, katika mwaka 2025/26, Serikali kupitia Benki ya TADB itaendelea kuchagiza uwekezaji wa sekta binafsi kwa kutoa mikopo kwa wadau wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Mikopo hiyo itazingatia mahitaji na fursa zilizopo katika mnyororo mzima wa thamani, ikiwemo kwa waongezaji wa thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

### 3.2.3. Mtangamano wa Biashara

**75. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kama ifuatavyo:

### A. Nchi na Nchi

#### *i. Utekelezaji wa Mfumo Rahisi wa Ufanyaji Biashara kwa Wafanyabiashara Wadogo Wanaovuka Mpaka wa Tanzania, Zambia na* Malawi

**76. *Mheshimiwa Spika;*** Katika kutekeleza Mfumo Rahisi wa Ufanyaji Biashara kwa Wafanyabiashara Wadogo (STR) wanaovuka mipaka ya Tanzania na Zambia, jumla ya bidhaa 51 zilikubalika kuingia katika mfumo rahisi wa ufanyaji biashara kwa wafanyabiashara wadogo wanaovuka mpaka wa Tanzania na Zambia kutoka bidhaa 22 za awali ikiwa ni ongezeko la bidhaa mpya 29. Bidhaa hizo mpya ni pamoja na Maharage, Njegere, Matunda mbalimbali, Viazi Mviringo, Soya na Mboga mboga za kukausha. Aidha, bidhaa hizo zilijadiliwa na kukubaliwa katika Mkutano wa Makatibu Wakuu wa Tanzania na Zambia, kupitia kikao kilichoratibiwa na Wizara kilichofanyika Nakonde Zambia Oktoba, 2024. Aidha, kwa upande wa Tanzania na Malawi, majadiliano ya uwili ya kuanzisha Mkataba wa Taratibu Zilizorahisishwa za Kiforodha yamekamilika, ambapo jumla ya bidhaa 61 na ukomo wa thamani ya mzigo wa bidhaa usiozidi dola za Marekani 2,000 kwa siku umekubalika kutumia mfumo wa STR.

#### *ii. Jukwaa la Ushirikiano Kati ya Afrika na Urusi*

**77. *Mheshimiwa Spika;*** Katika kuimarisha uhusiano wa biashara na Urusi, Wizara ilishiriki katika mkutano wa kwanza wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya Afrika na Urusi uliofanyika Novemba, 2024. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni mwenendo na matarajio ya ushirikiano wa biashara na uchumi. Ili kuwepo mwenendo na matarajio chanya ya ushirikiano wa biashara na uchumi baina ya Afrika na Urusi pande zote mbili zilikubaliana

yafanyike yafuatayo:- Kutumia sarafu/pesa na mifumo ya malipo ya nchi husika pale zinapofanyika biashara baina ya nchi za Afrika na Urusi; Kuwa na ushirikiano wa kibiashara kwa kuweka huduma za kifedha na zisizo za kifedha kusaidia mauzo ya nje ya Afrika; Kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji; Kujenga uwezo kwa wataalam wanaohusika na masuala ya majadiliano; Upatikanaji wa teknolojia za kisasa; Kukuza ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi; Kuboresha miundombinu ya uwekezaji na usafirishaji; na Kuanzisha tovuti ya huduma za usambazaji (Supply services portal).

**B. Kikanda**

**i. Mkutano wa 46 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

***78. Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 46 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji uliofanyika Novemba, 2024 Jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo uliidhinisha kuongeza orodha ya bidhaa mpya 198 katika orodha ya bidhaa zitakazotumia mfumo rahisi wa biashara katika mipaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kufikia bidhaa 568. Vilevile, mkutano huo ulipitia pendekezo la Kenya la kufanya mabadiliko ya kanuni za uasili wa bidhaa za EAC ili sukari ya viwandani inayozalishwa kwa kutumia malighafi kutoka nje ikidhi vigezo vya uasili na kupata msamaha wa ushuru wa forodha.

***79. Mheshimiwa Spika;*** Pendekezo hilo lilikataliwa na ikapendekezwa kuwa, kunapokuwa na upungufu wa sukari katika nchi wanachama, kipaumbele cha kununua sukari kiwe ni ndani ya EAC na kwamba mapitio ya vigezo vya uasili wa sukari kwa matumizi ya viwandani yajadiliwe kupitia mikutano ya mapitio ya jumla ya vigezo vya uasili wa bidhaa kwa bidhaa zote. Hivyo, Tanzania iliweza kusimamia na kulinda sekta ya sukari kwa kutoruhusu sukari kutoka nje kutokana na jitihada zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuvutia uwekezaji wa viwanda vya sukari nchini. Vilevile, mkutano ulipitisha Kanuni za Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya EAC ambapo ilikubalika

kuwa kanuni husika zimezingatia maoni ya nchi wanachama hususan maoni ya Tanzania ya kutenganisha vivutio kwa wawekezaji na wafanyabiashara waliopo ndani na nje ya SEZ.

**ii. Kusimamia na Kuratibu Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA)**

***80. Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeanza kunufaika na utekelezaji wa mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) kupitia biashara ya bidhaa za Kundi A ambapo usafirishaji wa shehena ya kwanza ya bidhaa chini ya mwamvuli na kanuni za AfCFTA ulifanyika Julai 2023. Hadi kufikia Machi, 2025, Serikali imehamasisha wafanyabiashara kusafirisha shehena ya bidhaa 21 tofauti ambapo kiasi cha takribani tani 1,000 zenye thamani zaidi ya dola za Marekani milioni 9.36 zimeuzwa katika nchi 18 za Afrika ambazo tulikuwa hatufungamani nazo. Bidhaa hizo ni pamoja na nyuzi za mkonge, kahawa, viungo, parachichi, tumbaku, mchele na vioo. Vilevile, utekelezaji wa mkataba wa AfCFTA umeonesha mafanikio ya biashara baina ya nchi za Afrika kwa kutumia taratibu na vigezo vya uasili vya AfCFTA. Hadi kufikia Machi, 2025, Tanzania imetoa jumla ya vyeti vya uasili wa bidhaa vipatavyo 131 kwa kampuni kuuza katika soko la AfCFTA.

***81. Mheshimiwa Spika;*** Ili kuongeza manufaa yanayotokana na soko hilo, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji uliofanyika Novemba, 2024 Arusha kwa ajili ya kulijadili mapendekezo ya ufunguaji wa soko la bidhaa chini ya Mkataba wa AfCFTA. Aidha, mkutano huo ulikuwa ni maalum kwa ajili ya kujadili na kukubaliana na orodha ya bidhaa ambazo zitawekwa kwenye Kundi B *(Sensitive Products)* la bidhaa ambazo zitaondolewa ushuru kidogo kidogo kwa kipindi cha miaka 13 na Kundi C *(Exclusion List)* la bidhaa ambazo hazitaondolewa ushuru wa forodha katika ufunguaji wa biashara ya bidhaa katika AfCFTA.

**C. Kimataifa**

***i. Kuwezesha Wafanyabiashara Kufikia Masoko ya* Nje ya Nchi**

**82.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara iliratibu warsha na ziara ya kubaini na kuwezesha wafanyabiashara kufikia masoko ya nje ya nchi iliyofanyika mwaka 2024 katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Tanga na Kilimanjaro. Warsha hizo zililenga kubainisha wafanyabiashara ambao wanaweza kutumia vyema fursa zinazotokana na majadiliano ya kikanda na kimataifa ikiwemo Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Soko la Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA), Masoko baina ya nchi na nchi na masoko mengine ya upendeleo kama vile Soko la Marekani kupitia mpango wa AGOA na China. Aidha, kupitia warsha hiyo, jumla ya kampuni 120 zimepatikana na zimejengewa uwezo wa namna ya kufikia masoko husika. Vilevile, Wizara inaendelea na jitihada za kuhakikisha wafanyabiashara wananufaika na masoko ya nje hususan yenye fursa nafuu.

**3.2.4. Maendeleo ya Biashara**

**A. Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini**

***83. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeshiriki katika mkutano wa tatu (3) wa majadiliano ya kisera baina ya sekta binafsi na sekta ya umma kuhusu biashara ya nafaka na mazao jamii ya mikunde uliofanyika Desemba, 2024 Jijini Nairobi Kenya. Kupitia mkutano huo, wawakilishi kutoka Serikali za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana ya kuendelea kuweka mazingira bora na wezeshi ya biashara kwa kufanya mikutano ya uwili (Bilateral Meetings); na kuboresha miundombinu ya biashara kama vile barabara, reli na bandari zinazounganisha mataifa; na kujenga maghala ya kuhifadhia mazao.

***84. Mheshimiwa Spika;*** Masuala mengine yaliyokubaliwa ni kuboresha vituo vya pamoja mipakani kwa kusimika vifaa vitakavyoongeza ufanisi katika utendaji kama vile *Scanners;* kujenga uelewa wa masuala ya usalama wa chakula kwa

wananchi; kujenga utamaduni wa kubadilishana taarifa za kibiashara baina ya nchi na nchi, wafanyabiashara, mashiriki yasiyo ya kiserikali na wadau wengine katika minyororo ya thamani ya mazao; kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo; Kuhamasisha urasimishaji wa biashara hususan katika maeneo ya mipakani ili kudhibiti biashara zisizo rasmi; na Kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ambao humpatia mkulima soko la uhakika na bei shindani.

**B. Kukusanya, Kuchambua na Kusambaza Taarifa za Masoko**

**85.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kukusanya na kuchambua taarifa za mwenendo wa bei na masoko ya bidhaa zikiwemo:- Taarifa za bei za mazao makuu ya chakula (mahindi, mchele, mtama, uwele, ulezi, maharage, ngano na viazi mviringo) kutoka katika masoko makuu ya Mikoa Tanzania Bara na kuzisambaza taarifa hizo kila siku ya Jumatatu, Jumatano na Ijumaa. Taarifa hizo husambazwa kwa wadau na ofisi mbalimbali za Serikali ikiwemo: - Ofisi ya Rais – Ikulu; Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu; Benki Kuu ya Tanzania (BOT); Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Shirika la Chakula Duniani (WFP); National Microfinance Bank (NMB); Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA); Wizara ya Kilimo; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; na wadau wengine mbalimbali zikiwemo taasisi za Utafiti. Aidha, taarifa hizo hutangazwa na Redio ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na kuchapishwa katika magazeti ya -The Guardian na Mwananchi. Lengo ni kuwawezesha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watumiaji wa bidhaa hizo kupata taarifa za bei za bidhaa zitakazowasaidia kufanya ulinganifu wanapotaka kununua bidhaa hizo na hatimaye kufanya maamuzi sahihi.

***C. Kuwajengea Uwezo Wafanyabiashara Wadogo na* Wa kati Kutumia Mifumo Katika Ufanyaji Biashara**

***86. Mheshimiwa Spika;*** Wizara iliratibu programu sita (6) za mafunzo zilizoratibiwa kwa washiriki 311 katika Mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam kwa lengo la kuimarisha ushindani katika kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi. Programu hizo ni; usimamizi na uendeshaji wa biashara, namna ya kufikia masoko ya ndani na

nje, kutambua na kutumia fursa za biashara katika soko la AfCFTA na kuongeza thamani ya bidhaa. Wadau walioshiriki ni pamoja na Wanachama wa Chama cha Walemavu Tanzania (CHAWATA), Kampuni ya Msosi *Daily Catering* na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kariakoo nchini.

**Kutayarisha Viwango vya Kitaifa Katika Sekta/Nyanja Mbalimbali**

***87. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imekamilisha viwango muhimu katika kilimo, chakula, uhandisi na aina nyingine mbalimbali za viwango. Jumla ya viwango 278 vilitayarishwa sawa na asilimia 40.3 ya lengo la kutayarisha viwango 690 kwa mwaka. Aidha, kati ya viwango 278 vilivyokamilika, 62 ni katika nyanja ya kemikali, vinne (4) nyanja ya ujenzi, 97 nyanja ya kilimo na chakula, 33 nyanja ya nguo na ngozi, 23 nyanja ya mazingira, 8 nyanja ya madini, 33 nyanja ya uhandisi mitambo na 18 katika sekta mtambuka. Viwango 154 viko katika hatua mbalimbali za uandaaji. Uandaaji wa viwango hivyo vimesaidia wazalishaji wa bidhaa nchini kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuendana na mahitaji ya soko na hatimaye kutanua wigo wa masoko ndani na nje ya nchi.

**E. Kutoa Leseni ya Ubora Kutoka Katika Sekta Mbalimbali**

***88. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya leseni 482 za nembo ya ubora ya TBS zilitolewa ambayo ni sawa na asilimia 53.6 ya lengo la kutoa leseni 900 kwa mwaka. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 205 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa mbalimbali kama vile siagi ya karanga, asali, maji ya kunywa, pombe kali (spirit), vifungashio, mchele na pombe. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

**F. Kusajili Majengo, Maeneo ya Uzalishaji, Uuzaji na Usambazaji wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi**

***89. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TBS imeendelea na huduma za kusajili majengo yanayohifadhi bidhaa za chakula na vipodozi kwa lengo la kuhakiki ubora na ufanisi wa maeneo hayo ili kuendelea kulinda afya za walaji. Hadi kufikia Machi, 2025, TBS imesajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 10,923 ambavyo ni sawa na asilimia 84 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 13,000 kwa mwaka. Kati ya maeneo yaliyosajiliwa, maeneo 8,748 yanajihusisha na chakula na maeneo 2,175 yanajihusisha na vipodozi.

**G. Kusajili Bidhaa za Chakula na Vipodozi**

***90. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, TBS imesajili bidhaa za chakula na vipodozi 1,672 ambavyo ni sawa na asilimia 79.6 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 2,100 kwa mwaka. Kati ya bidhaa hizo, bidhaa 1,208 ni za chakula na bidhaa 464 ni za vipodozi.

**H. Kukagua na Kutoa Vibali kwa Bidhaa na Magari Yatokayo Nje ya Nchi**

**91.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya vyeti vya ubora 91,558 vimetolewa kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi ambayo ni sawa na asilimia 70.4 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 130,000. Kati ya vibali hivyo, vibali 26,339 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nje ya nchi na vibali 65,219 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nchini. Aidha, jumla ya magari 37,764 yaliyotumika nje ya nchi yalikaguliwa, sawa na asilimia 78.7 ya lengo la kukagua magari 48,000 kwa mwaka.

**I. Kutoa Mafunzo na Semina Kuhusu Viwango na Udhibiti Ubora kwa Wadau**

***92. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TBS imeendelea kutoa elimu kwa wazalishaji wa bidhaa za viwandani, wasindikaji na umma wote wa Watanzania kuhusu dhana nzima ya viwango na

ubora. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya wadau 1,113 walipewa mafunzo kuhusu masuala ya viwango ambayo ni sawa na asilimia 69.6 ya lengo la kutoa mafunzo kwa wadau 1,600 kwa mwaka. Mafunzo hayo yalifanyika katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita, Mara, Mbeya, Iringa, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Tabora na Mtwara. Aidha, Shirika limeendelea kutoa mafunzo hayo kwa wajasiriamali wadogo (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima ya kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama ili kuwezesha kukidhi ushindani wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

**J. Kuthibitisha Kampuni Chini ya Mifumo ya Ubora na Uongozi**

**93. *Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya kampuni nane (8) zilithibitishwa mifumo ya ubora ya kimenejimenti sawa na asilimia 53.3 ya lengo la kuthibitisha kampuni 15 kwa mwaka.

**K. Kupima Sampuli za Bidhaa Mbalimbali Pamoja na Kufanya Ugezi wa Vifaa/mashine mbalimbali**

***94. Mheshimiwa Spika;*** Katika kusimamia ubora wa bidhaa, Wizara kupitia TBS hupima ubora wa bidhaa kwa kupitia sampuli zinazoletwa kwenye maabara za zake. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya sampuli 28,642 zilipimwa katika maabara mbalimbali za TBS sawa na asilimia 75.4 ya lengo la kupima sampuli 38,000 kwa mwaka. Aidha, Shirika hupima bidhaa za wazalishaji ili kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa hizo kabla ya matumizi.

***95. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, Shirika limefanya ugezi wa vifaa/ mashine mbalimbali ambapo hadi kufikia Machi 2025, jumla ya vifaa 8,052 vilifanyiwa ugezi sawa na asilimia 70 ya lengo la kufanya ugezi wa vifaa 11,500 kwa mwaka. Lengo la kufanya ugezi (calibration) wa mitambo au vifaa mbalimbali vinavyotumika katika uzalishaji wa bidhaa au utoaji huduma mbalimbali ni kuweka mazingira rafiki ya biashara, ili kuhakikisha usawa/usahihi wa vipimo wakati wa matumizi ya vifaa hivyo.

### L. Kuweka Kinasaba Katika Mafuta ya Petrol, Dizeli na Mafuta ya Taa

**96.** ***Mheshimiwa Spika;*** Shirika limeendelea kutekeleza jukumu la kuweka kinasaba kwenye mafuta ambapo hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya lita 3,581,643,081 za mafuta ya petrol, dizeli na mafuta ya taa ziliwekewa kinasaba sawa na asilimia 87.4 ya lengo la kuweka kinasaba katika lita 4,150,000,000 za mafuta kwa kipindi cha mwaka mzima. Shirika linatekeleza shughuli hiyo kwa lengo la kuendelea kudhibiti ubora wa mafuta (uchakachuaji) pamoja na upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuuza mafuta yasiyolipiwa kodi katika soko la ndani. Mafuta ambayo hayawekewi kinasaba ni yale yanayosafirishwa kwenda nchi jirani (transit products) na mafuta yenye msamaha wa kodi yanayotumika kwenye miradi maalum.

### *M. Kutambulisha Rajamu ya Kitaifa kwa Bidhaa za* Tanzania

**97.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) imeendelea na juhudi za kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinapata utambulisho maalum katika masoko. Kupitia juhudi hizo, yaliyofanyika ni kukamilika kwa utengenezaji wa Alama ya Asali (*Tanzania Honey Brand Mark*) pamoja na kuandaa taratibu na kanuni za kupata alama hiyo; na kukamilika kwa zoezi la kutafuta nembo maalum itakayotambulisha bidhaa za Tanzania (Nation Brand Mark – Made in Tanzania) katika masoko ya Kimataifa, ambapo jumla ya nembo 93 ziliwasilishwa katika zoezi hilo. Kati ya hizo, nembo tatu (3) bora na bunifu zaidi zilishinda katika shindano hilo la Nembo ya Bidhaa na Huduma (Made in Tanzania).

### N. Kukusanya na Kusambaza Taarifa Muhimu za Fursa za Biashara

**98.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za biashara nchini kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara kufanya maamuzi ya kibiashara kwa wakati kwa kutekeleza yafuatayo:

(1) Kukusanya na kusambaza majarida 38 ya taarifa za bei za bidhaa kutoka masoko 13 ya Mkoa wa Dodoma, Dar es Salaam, Songwe, Manyara, Shinyanga, Singida, Pwani, Ruvuma, Mbeya, Rukwa, Tanga, Arusha na Kilimanjaro na kusambazwa kwa jumla ya wadau 426,579 wa biashara nchini kupitia mitandao ya kijamii pamoja na *TanTrade Biashara App*;

(2) Kuhuisha taarifa za kampuni 112 katika Kanzidata ya Mamlaka yenye jumla ya kampuni 1,839. Kanzidata hiyo inasaidia Mamlaka kuwa na taarifa sahihi za kampuni ili kuunganishwa na fursa zinazopatikana ndani na nje ya nchi;

(3) Kuhuisha taarifa za taratibu za usafirishaji wa bidhaa tano (5) katika Mfumo wa *Trade Portal* kutoka Bodi ya Chai, Tume ya Nguvu za Atomic (TAEC), Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), Mamlaka ya Usimamizi wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bodi ya Nyama (TMB), pamoja na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (COPRA);

(4) Kufanya uchambuzi na kuandaa taarifa ya hali ya biashara na fursa zilizopo baina ya Tanzania na nchi mbalimbali. Taarifa ya masoko kutoka nchi 64 (22 za Bara la Afrika, 14 za Bara la Ulaya, 25 za Bara la Asia na tatu (3) za Mashariki ya Kati) zimeandaliwa; Uchambuzi wa mwenendo wa bei nchini katika bidhaa za mahindi, mchele, mtama, uwele, ulezi, ngano, maharage na viazi mviringo. Uchambuzi ulionesha kupanda kwa bei ya bidhaa za mchele kwa asilimia 4.98, ulezi 3.36, mtama 0.22 na ngano 0.40. Vilevile, uchambuzi ulionesha kushuka kwa bei za bidhaa za mikunde kama maharage kwa wastani wa asilimia 0.66;

(5) Kuhuisha taratibu za kuuza nje kwa bidhaa tano (5) ikiwemo asali, ngozi, viungo, kahawa na parachichi kwenye mfumo wa *Trade Portal*; na

(6) Kukusanya taarifa kutoka kwa Taasisi wezeshi tatu (3) ambazo ni ZSTC, ZASCO na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, ili kuboresha taarifa za taratibu za kukidhi vigezo vya Biashara ya nje kwa upande wa Zanzibar katika mfumo wa *Trade Portal* (*trade.tanzania.go.tz)*.

### *O. Kuendeleza na Kusimamia Mifumo ya Masoko* Nchini

**99.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuboresha na kusimamia mfumo wa *TanTrade Biashara App* uliosanifiwa wa taarifa za masoko pamoja na mwenendo wa bei za bidhaa katika masoko mbalimbali nchini. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya watumiaji 1,477 wamejisajili katika mfumo huo ili kupata taarifa na kufuatilia mwenendo wa bei za bidhaa nchini. Mfumo huo unatoa bei ya jumla na rejareja kwa bidhaa za mazao ya mifugo, nafaka, mbogamboga, asali, bidhaa za ujenzi na mafuta (petroli na dizeli) kwa masoko 67 katika Mkoa wa Mtwara, Dar es Salaam, Dodoma, Shinyanga, Mara, Manyara, Mwanza, Iringa, Kagera na Morogoro.

### P. Utatuzi wa Mashauri ya Ushindani Sokoni

**100.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeendelea kuchukua hatua katika kuboresha hali ya ushindani sokoni, ambapo jumla ya mashauri 27 yapo katika hatua mbalimbali za utatuzi. Kati ya mashauri hayo, mashauri matano (5) yanahusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko, mashauri 16 yanayohusu miungano ya kampuni ambayo haikuidhinishwa na FCC, na Mashauri sita (6) yanahusu ukiritimba sokoni. Kati ya mashauri hayo yaliyopo katika hatua mbalimbali za utatuzi, mashauri saba (7) yamekamilika na yamechukuliwa hatua na mashauri 20 yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

### Q. Kuchunguza Maombi ya Miungano ya Kampuni

**101.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilichunguza maombi 51 ya miunganiko ya kampuni yaliyowasilishwa FCC. Kati ya maombi hayo, maombi 35 ya miunganiko yaliidhinishwa ambapo 31

yaliidhinishwa bila masharti na manne (4) yaliidhinishwa kwa masharti. Miungano hiyo ilitoka katika Sekta za Kilimo (9), Uzalishaji (9), Fedha (4), Afya (2), Ardhi na Majengo (5), Burudani na michezo (1), Madini (5), Biashara (2), Utalii (2), Mawasiliano (4) na Huduma (3). Aidha, maombi 15 yaliyobaki yako katika hatua tofauti za uchunguzi.

### R. Kuendelea Kuchukua Hatua za Kumlinda Mlaji

***102. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na juhudi za kumlinda mlaji dhidi ya mienendo potofu, hadaifu na kandamizi katika soko la bidhaa na huduma na kupambana na bidhaa bandia. Hadi kufikia Machi, 2025, malalamiko 83 ya walaji wadogo wadogo yalichukuliwa hatua ambapo, malalamiko 69 yalitatuliwa na malalamiko 14 yaliwasilishwa katika mamlaka zingine ambazo ni mahakama, jeshi la polisi na TCRA. Aidha, mikataba 63 inayoandaliwa na upande mmoja ilisajiliwa kwa lengo la kuondoa masharti kandamizi kwa walaji.

***103. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, kaguzi za kushtukiza 35 zilifanyika sokoni, ambapo bidhaa zenye thamani ya shilingi 3,380,598,900 zilikamatwa kwa kuvunja Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010. Bidhaa hizo ni pamoja na *Oraimo, Gillette, Oral-B, Lapaix, Castrol, Missfiah, Whitedent, ORS, Dove, Rinju, Dettol, Tyrolit and Cathy*. Pamoja na kaguzi za kushtukiza, Tume imeendelea kufanya kaguzi za kila siku za makontena ya bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam na Bandari kavu zote katika Jiji la Dar es Salaam. Kutokana na kaguzi hizo, Tume imefanikiwa kukagua kontena 5,265, kati ya kontena hizo, kontena 411 sawa na asilimia 7.8 zenye thamani ya shilingi 10,810,589,276 zilikamatwa kwa kukiuka Sheria hiyo.

**104.** ***Mheshimiwa Spika;*** Aidha, FCC imefanikiwa kupata Cheti cha Ithibati ISO 9001:2015, kinachoonesha dhamira ya ubora katika mifumo ya usimamizi wa ubora na utoaji wa huduma (Quality Management System). Cheti hicho kinachotambulika kimataifa kinaonyesha msisitizo wetu katika kuongeza ufanisi wa kiutendaji, kuridhika kwa wateja, na ushirikishwaji wa wafanyakazi

katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa wadau. Vilevile, cheti hicho kinaimarisha uaminifu wa FCC kimataifa, kuongeza tija, na kuendeleza maendeleo endelevu.

### S. *Kutoa Maamuzi ya Mashauri ya Rufaa* Yanayowasilishwa katika Baraza

**105.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) imepokea jumla ya kesi 28 zinazoendelea kusikilizwa na kuamuliwa. Kati ya kesi hizo, 11 ni kesi mpya na 17 ni kesi zilizokuwa hazijaamuliwa katika kipindi cha mwaka 2023/2024. Wizara imeweza kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi tano (5) na kesi 23 zinaendelea kusikilizwa katika hatua mbalimbali. Utatuzi wa mashauri hayo umeweza kupunguza migogoro ya wafanyabiashara, wawekezaji na walaji inayohusu ushindani wa kibiashara na udhibiti wa soko. Matokeo ya mashauri yaliyoamuliwa, yameongeza uwajibikaji na kuimarisha ushindani wa kweli katika sekta ya biashara na udhibiti wa soko. Hatua hiyo imeongeza ufanisi na uzalishaji, usambazaji wa huduma na bidhaa, kukuza ubunifu, kuwezesha matumizi ya rasilimali yenye ufanisi na kumlinda mlaji.

### T. Kusimamia na Kuhakiki Vipimo Vyote Vitumikavyo na Viingiavyo Nchini

**106.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) hadi kufikia Machi, 2025 imekagua na kuhakiki vipimo 1,013,859 sawa na asilimia 99.2 ya lengo la kukagua vipimo 1,022,342. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa, vipimo 10,898 vilirekebishwa na vipimo 761 vilikataliwa. Aidha, Wizara iliendelea kufanya kaguzi za kawaida na kaguzi za kushtukiza ambapo jumla ya kaguzi 3,293 kati ya kaguzi 3,000 kwa vipimo mbalimbali vitumikavyo kwenye biashara, afya, usalama na mazingira zimefanyika, sawa na asilimia 109.8. Vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni pampu za kuuzia mafuta ya nishati, *Flowmeters* zitumikazo kupimia mafuta kwenye bohari na maghala ya kuhifadhia mafuta, tenki za kuhifadhia na kusafirishia mafuta, dira za maji, mizani inayotumika kupimia bidhaa mbalimbali, vipimo vya urefu pamoja na malori yabebayo kokoto, mchanga na vifusi.

**U. Kuendelea na Ukaguzi wa Bidhaa Zilizofungashwa Kwenye Maeneo ya Mipakani, Bandarini na Viwandani**

**107.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 Wakala imeendelea kufanya kazi ya udhibiti wa bidhaa zilizofungashwa mipakani na bandarini katika vituo vya ukaguzi 13 ambavyo ni Sirari (Mara), Mtukula (Kagera), Namanga (Arusha), Holili (Kilimanjaro), Tunduma (Songwe), Tarakea (Kilimanjaro), Horohoro (Tanga), Kasumulu (Mbeya), Kwara na Bagamoyo (Pwani), Manyovu (Kigoma) na Mbweni na Temeke (Dar es Salaam). Baadhi ya bidhaa zilizokaguliwa ni mbao, mbegu za mimea, mafuta ya kula, sabuni, maziwa, matunda, sukari, dawa ya meno, chumvi, vinywaji vya pombe, mbolea, vifaa vya ujenzi, gesi, waya na maji.

***V. Kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za* Biashara na Huduma, Hataza na vyeti vya Viwanda**

**108.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara kupitia Wakala wa Biashara na Leseni (BRELA) imefanikiwa kusajili jumla ya kampuni 13,794 kati ya 16,200 zilizopangwa ikiwa ni sawa na asilimia 85, kusajili majina ya biashara 23,644 kati ya 29,912 yaliyopangwa ikiwa ni sawa na asilimia 79, Kusajili alama za biashara na huduma 2,601 kati ya 4,410 zilizopangwa ikiwa ni sawa na asilimia 60, na kupokea maombi ya Hataza 93, kuchakata maombi 50 na kufanikiwa kutoa Hataza 37 kati ya 40 zilizopangwa sawa na asilimia 93. Vilevile, Wizara ilifanikiwa kutoa vyeti vya usajili wa viwanda 37 kati ya 48 vilivyopangwa sawa na asilimia 77.

**W. Kutoa leseni za Biashara kundi ‘A’ na za Viwanda**

**109.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara kupitia BRELA imefanikiwa kutoa leseni za viwanda 298 kati ya 236 zilizopangwa ikiwa ni sawa na asilimia 126 na kutoa leseni za biashara kundi “A’’ 17,595 kati ya 15,120 zilizopangwa ikiwa ni sawa na asilimia 113. Matokeo haya yanatokana na jitihada za Serikali katika kusimamia taratibu za ufanyaji wa Biashara unaozingatia Sheria.

### *X. Kuendelea Kuboresha na Kuimarisha Mifumo na* **Miundombinu ya TEHAMA**

**110.** ***Mheshimiwa Spika;*** BRELA kwa kushirikiana na wataalam kutoka Kituo cha Taifa cha kuhifadhi Data kimtandao imeendelea kufanya maboresho ya mfumo wa usajili kwa njia ya Mtandao ili kuondoa kero zinazoathiri kasi ya utekelezaji wa majukumu ya usajili kwa njia ya mtandao. Hadi kufikia Machi, 2025, moduli za usajili wa kampuni na majina ya biashara, leseni za biashara na viwanda zimekamilika, kwa sasa moduli za hataza na alama za biashara na huduma zinakamilishwa ili kuwa na mfumo kamili kwa moduli zote. Aidha, Wizara imefanikiwa kufunga vifaa vipya kwa ajili ya kuhifadhi data kupitia Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kujikinga na Majanga ya kimtandao ambacho kimejengwa katika Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data za Mtandao (NIDC), na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Hadi kufikia Machi, 2025, mifumo yote inaendeshwa kupitia *Data Center* ya Serikali.

### Y. Kutoa Leseni na Kufanya Ukaguzi wa Ghala

***111. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imefanya kaguzi kwenye ghala kabla ya msimu kuanza na wakati msimu unaendelea. Aidha, Wizara ilifanikiwa kukagua jumla ya ghala 237 za kuhifadhia mazao na kutoa jumla ya leseni 237 ambazo ni za waendesha ghala katika bidhaa za korosho, mbaazi, ufuta, kakao, dengu, na choroko. Kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, Wizara imeweza kuratibu uuzwaji wa tani 872,844 za mazao. Kati ya tani hizo, Kahawa ni tani 94,499.859, Korosho tani 639,403.8, Kakao tani 9,332.2, Maharage tani 74.112, Mihogo tani 22,112.970, Mpunga tani 1,563.924, Mbaazi tani 99,682.909, Choroko tani 10,701, Mchele tani 186.353, Ufuta tani 85,810.4, Chai tani 48.380, Soya tani 775.7 na Dengu tani 21,666.567. Kupitia mauzo hayo, zaidi ya shilingi bilioni 87 zimelipwa katika halmashauri zilizotumia mfumo huo na hivyo kuongeza mapato ya ndani na uwezo wa halmashauri kuboresha huduma kwa wananchi, hususan katika sekta ya kilimo na biashara.

***112. Mheshimiwa Spika;*** Aidha, Wizara imeandaa miongozo ya biashara ambayo inabainisha mifumo ya uuzaji wa mazao ya dengu, soya, mbaazi, choroko, maharage, ufuta pamoja na miongozo ya mauzo kwa Meneja Dhamana na Ukaguzi wa Ghala. Mifumo hiyo inampatia mnunuzi na muuzaji wigo mpana wa kuchagua soko lenye manufaa zaidi kwa kuzingatia bei, uharaka wa malipo, ubora na wingi wa mazao kulingana na mahitaji ya soko.

***Z. Elimu na Mafunzo Mbalimbali***

***i. Kufanya Kaguzi Elimishi za Leseni za* Biashara Kundi 'A' na Viwanda**

***113. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara imefanya kaguzi elimishi nne (4) ambapo mbili (2) ni za viwanda na mbili (2) za leseni za biashara katika mikoa ya Pwani na Mtwara. Katika kaguzi hizo, elimu kuhusu Sheria ya Viwanda vya Taifa (Leseni na Usajili) Sura ya 46 na Sheria ya Leseni za biashara Sura 208 ilitolewa. Vilevile, elimu ya matumizi ya mifumo inayotumika kutoa leseni za viwanda na leseni za biashara kundi "A" kwa njia ya mtandao ilitolewa. Jumla ya biashara 397 zilikaguliwa ambapo kati ya hizo, 236 zilikuwa na leseni halali za biashara, 82 hazikuwa na leseni ya biashara, 71 leseni za biashara zilikuwa zimeisha muda wake na nane (8) zilikuwa na leseni za biashara kundi 'B' badala ya kundi 'A'.

***114. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, kwa upande wa leseni za viwanda jumla ya viwanda 153 vilikaguliwa ambapo kati ya hivyo, 50 vilikuwa na leseni, 99 havikuwa na leseni, na vinne (4) havifanyi kazi na vimefungwa. Hatua zilizochukuliwa kwa biashara ambazo hazina leseni pamoja na Viwanda ni pamoja na: - Kuwaelekeza wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda waliokuwa hawana leseni kuwasilisha maombi ya leseni kwenye mamlaka husika na kuhuisha zile zilizoisha muda wake; Kuwaelekeza kuomba leseni za biashara na kuwasaidia kupata leseni hizo papo kwa papo; na Kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kufanya biashara kwa kufuata sheria za nchi.

### ii. Mafunzo ya Ujasiriamali na Usimamizi wa Biashara

***115. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 wajasiriamali 14,532 kutoka mikoa yote Tanzania bara walipata mafunzo mbalimbali na kutunukiwa vyeti ambavyo ni muhimu katika kurasimisha biashara zao. Mafunzo yaliyotolewa ni ya ujuzi maalum wa kiufundi katika uzalishaji mali kama vile usindikaji wa vyakula; ujasiriamali; KAIZEN; utengenezaji wa sabuni, batiki na vipodozi; Mafunzo ya afya na usalama viwandani; ufungashaji; na elimu ya mikopo. Mafunzo hayo yamewezesha, viwanda 271 kurasimishwa.

***116. Mheshimiwa Spika;*** Katika kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe 2021/2022 – 2025/2026, Wizara imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wanaozalisha vyakula kwa kutumia teknolojia ya kuongeza virutubisho kwenye vyakula. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati 275 wanaojihusisha na uzalishaji wa unga wa mahindi kutumia teknokojia ya kuongeza virutubisho katika chakula katika mikoa ya Arusha, Geita, Tanga, Tabora, Kilimanjaro, Simiyu na Shinyanga. Kupitia mafunzo hayo, wajasiriamali wataweza kuzalisha bidhaa zenye ubora unaokidhi soko la ndani na nje ya nchi.

### iii. *Elimu na Kuhamasisha Matumizi ya Mfumo* wa Stakabadhi kwa Wadau Wote

**117.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara imeendelea kutoa elimu ya mfumo wa stakabadhi kwa wafanyabiashara wa mazao katika mikoa mbalimbali. Uhamasishaji huo umepelekea kufanyika kwa minada ya mazao sehemu mbalimbali ikiwemo mnada wa mbaazi Tunduru-Ruvuma ambapo wakulima wa Wilaya ya Tunduru waliuza mbaazi zao kwa bei ya juu ya shilingi 1,722; mnada wa mbaazi Dodoma ambapo wakulima waliuza mbaazi zao kwa bei ya juu ya shilingi1,840; mnada wa kakao Mbeya ambapo wakulima waliuza kakao zao kwa bei ya juu ya shilingi 18,620; mnada wa korosho kwa Mikoa ya Kusini ambapo bei ya juu ilikuwa shilingi 4,070 kwa

kilo; na mnada ya choroko kwa Mikoa ya kanda ya ziwa ambapo bei ya juu ilikuwa shilingi 1,450 kwa kilo.

### iv. *Kuelimisha Umma Juu ya Umuhimu wa* Kufanya Sajili Mbalimbali za Kibiashara

***118. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari, matamasha, semina, maonesho na mikutano. Hadi kufikia machi, 2025 Wizara imeshiriki katika maonesho 10 ya biashara kwa lengo la kutoa elimu kwa wadau na huduma za papo kwa papo. Maonesho hayo yanajumuisha: Maonesho ya bidhaa za kilimo, Maonesho ya Afrika Mashariki, Maonesho ya Sekta ya madini, Maonesho ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, wiki ya vijana, kliniki ya biashara wakati wa mashindano ya michezo (SHIMIWI), *Tanzania International Manufacturers Expo 2024*, Maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Dodoma na Maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Dar es Salaam. Aidha, Wizara ilifanikiwa kufanya vipindi 16 vya televisheni, vipindi nane (8) vya redio na kuchapisha taarifa mbalimbali 40 kwenye magazeti.

***119. Mheshimiwa Spika;*** Katika utoaji elimu, Wizara imeweka msisitizo katika usajili, urasimishaji wa biashara, mapitio na maboresho ya sheria zinazosimamiwa na BRELA ikiwemo Sheria ya Makampuni Sura ya 212 kuhusu kuboresha daftari la kuwatambua wamiliki manufaa wa majina ya biashara na kampuni.

### v. Elimu kwa Umma Kuhusu Matumizi Sahihi ya Vipimo

**120.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imetoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na maonesho mbalimbali. Wadau waliopata elimu ni pamoja na TAKUKURU Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam na Jiji la Dodoma; Jeshi la Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala; DIT; NSSF; na Wauzaji wa gesi za ORYX. Pia, imeandaa habari 75 za Magazeti, Graphics 120 pamoja na video fupi 62 kuhusu majukumu ya WMA. Hali kadhalika, katika kuendelea kuboresha kuhabarisha umma kuhusu majukumu ya

Wakala, tovuti na mitandao ya kijamii kama vile *instagram* na *facebook* vimeendelea kuhusishwa sambamba na kuwepo kwa namba ya simu 0800110097 ya bure kwa ajili ya huduma kwa mteja. Aidha, Wizara imefanikiwa kurusha matangazo mubashara katika vyombo vya Habari vitano (5) vya Chaneli Ten, TBC, Redio Uhuru na Redio one, pamoja na kufanya Mkutano na Wahariri na Waandishi wa Habari.

### *AA. Uratibu na Ushiriki wa Maonesho na* Majukwaa Mbalimbali

***121. Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea kusimamia matukio ya ukuzaji Biashara katika kutangaza bidhaa na huduma yaliyoratibiwa na Sekta Binafsi na Umma kwa lengo la kuimarisha mwenendo wa tasnia ya ukuzaji biashara nchini. Kupitia jitihada hizo, Wizara imefanikiwa kuratibu matukio ya ukuzaji biashara na kuwezesha ushiriki wa wafanyabiashara katika kupata masoko ya bidhaa na huduma na kujitangaza kupitia maonesho, majukwaa na kliniki kama ifuatavyo:

#### *i. Uratibu na Ushiriki wa Maonesho Mbalimbali*

***122. Mheshimiwa Spika;*** Wizara iliratibu Maonesho ya Pili ya Kimataifa ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania (TIMEXPO 2024) yaliyofanyika Uwanja wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Dar es Salaam Septemba hadi Oktoba, 2024. Katika maonesho hayo, kampuni 257 zilipata nafasi ya kutangaza bidhaa zao, kutanua wigo wa biashara zao na kujifunza teknolojia mpya za uzalishaji wa bidhaa. Aidha, Wizara kupitia TanTrade iliratibu maonesho ya 11 ya biashara yaliyoambatana na sherehe ya miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar, yaliyofanyika Januari, 2025, katika viwanja vya Dimani Zanzibar. Katika maonesho hayo, jumla ya washiriki 338 walipata nafasi ya kutangaza huduma na bidhaa wanazozalisha.

***123. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, Wizara iliratibu Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, 2024 (48$^{th}$ DITF) yaliyofanyika Juni hadi Julai, 2024 kwa lengo la kutoa fursa kwa washiriki kutangaza bidhaa na huduma. Matokeo yaliyopatikana

kutokana na maonesho hayo ni kuwezesha kampuni 3,954 kushiriki maonesho ambapo kampuni za ndani 3,503 na kampuni 451 kutoka nchi 28; na kufanikisha mauzo ya papo kwa papo ya kiasi cha shilingi bilioni 3.62 yakichangiwa zaidi na wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa. Matokeo mengine ni uratibu wa siku za mataifa saba (7) ambapo fursa za biashara na uwekezaji zilipatikana ikiwa ni pamoja na Kampuni ya Shandong Oasis Food Co. Ltd iliainisha mahitaji ya kununua tani 20,000 za mihogo na tani 20,000 za viazi vitamu kwa matumizi ya binadamu na chakula cha Wanyama zenye thamani ya shilingi bilioni 6 za Kitanzania; na kampuni ya *AJA Limited* ilifanikiwa kuuza mkonge wenye thamani ya dola za Marekani 108,000.

***124. Mheshimiwa Spika;*** Katika maonesho hayo, jumla ya wadau wa biashara 577 waliweza kuwasilisha changamoto zao ikiwemo changamoto za kupata masoko, usajili wa biashara, kodi, mitaji, ubora na viwango vya bidhaa na matumizi ya vipimo zilitatuliwa kupitia Taasisi wezeshi kibiashara 26. Vilevile, ajira za muda mfupi 21,518 zilipatikana wakati wa maonesho hayo katika kutoa usaidizi wa huduma mbalimbali wakati wa maandalizi ikiwemo ufundi na ujenzi wa miundombinu na mabanda ya biashara, usafirishaji, migahawa, mapambo na upagazi.

***125. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia WRRB ilitoa elimu kwa umma kupitia maonesho ya Kimataifa ya Saba Saba na Nane Nane, ambapo katika maonesho ya Saba Saba zaidi ya wadau 200 walipata mafunzo na kwa upande wa maonesho ya sikukuu ya Wakulima Nane Nane zaidi ya wadau 200 walipata mafunzo.

***126. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kuwaunganisha wajasiriamali wenye bidhaa za viwanda vidogo kuyafikia masoko ya ndani na nje sambamba na kutangaza huduma zake. Fursa za masoko zimekuwa zikitolewa kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na tovuti ya Shirika na maonesho ya Kikanda na Kitaifa. Kupitia maonesho ya Kikanda na Kitaifa ya SIDO, Wizara imewezesha wajasiriamali 906 kushiriki maonesho hayo. Kati ya wajasiriamali hao, 270 ni wanaume na 634 ni wanawake. Aidha, mitandao ya kijamii ya SIDO imeweza kutangaza bidhaa na huduma za SIDO na kuwafikia watu wengi

kwa wakati mfupi na kuwezesha bidhaa za viwanda vidogo vya ndani kutambulika kwa wananchi.

***127. Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilishiriki katika maonesho ya saba (7) ya Wiki ya Viwanda SADC yaliyofanyika nchini Zimbabwe Agosti 2024. Lengo la maonesho hayo ni kutoa fursa kwa wadau kujadili masuala ya maendeleo ya viwanda na kuhamasisha ushirikiano wa wadau ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (2015 – 2063). Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Wiki ya Viwanda ya SADC ilikuwa "Kukuza Ubunifu ili Kufungua Fursa za Ukuaji Endelevu wa Uchumi na Maendeleo kuelekea SADC ya Viwanda".

***128. Mheshimiwa Spika;*** Kupitia maonesho hayo, nchi ilifanikiwa kuonesha bidhaa zinazozalishwa na baadhi ya viwanda na wajasiriamali wanawake. Viwanda hivyo ni pamoja na Kiwanda cha Kahawa cha AMIMZA; Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha (Tanzania Biotech Products Limited); Kiwanda cha Kuchakata Mkonge cha *Aja International Limited; Mohamed Enterprises Tanzania Limited (METL); na CAPS Limited.* Maonesho hayo yaliiwezesha nchi kupokea tuzo za ubora kupitia kampuni za *METL* na *Caps Limited* ambazo zilipewa Tuzo ya Ubora ya Viwango ya SADC ( SADC Quality Award) kwa mwaka 2024.

**ii. Majukwaa ya Kitaifa na Kimataifa**

***129. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikwa kuratibu ushiriki wa Tanzania katika majukwaa ya kibiashara kwa lengo la kutangaza na kuimarisha biashara katika masoko ya Kimataifa. Aidha, Wizara imewezesha kampuni 234 za Tanzania kushiriki katika majukwaa nane (8) ya Kimataifa ya kibiashara yaliyofanyika nchini na katika nchi za Msumbiji, Comoro, China na Indonesia. Vilevile, ushiriki huo ulilenga kutoa fursa kwa kampuni za Tanzania kufahamu mazingira ya biashara, kupata taarifa na mahitaji ya wafanyabiashara, na kunadi wasifu wa kampuni na biashara wanazofanya.

***130. Mheshimiwa Spika;*** Matokeo ya ushiriki wa kampuni hizo umewezesha yafuatayo:- Kutangaza bidhaa za Tanzania ikiwemo kahawa, chai, bidhaa za urembo, nguo na mavazi katika Maonesho ya 59 ya Biashara ya Kimataifa ya Msumbiji yaliyofanyika kuanzia Agosti hadi Septemba, 2024; Kupatikana kwa fursa ya kuuza mboga na vitunguu tani 2,500 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 2.5 nchini Comoro baina ya Kampuni ya Kilimo ya SUGECO na kituo cha mauzo Moroni nchini Comoro Agosti, 2024; Kufanyika kwa mkutano wa utiaji saini itifaki ya kuuza asali katika soko la China Agosti, 2024. Makubaliano hayo yataiwezesha Tanzania kuwa na soko jipya la asali lenye kununua zaidi ya tani 4,809 kwa mwaka likiwa na thamani zaidi ya dola za Marekani milioni 43,388; na Washiriki 28 walipata uelewa wa taratibu za kusafirisha bidhaa kwenda soko la Ulaya kupitia nchi ya Italia na kutangaza biashara katika kongamano la tano (5) la Biashara na Uwekezaji kati ya Italia na Tanzania lililofanyika Februari, 2025.

***131. Mheshimiwa Spika;*** Matokeo mengine ni kufanyika kwa makongamano ya maadhimisho ya miaka 50 ya mahusiano baina ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) yaliyofanyika Desemba, 2024 Tanzania na UAE. Katika makongamano hayo jumla ya wafanyabiashara 22 kutoka Tanzania walishiriki Kongamano lililofanyika nchini UAE na wadau 391 walishiriki Kongamano lililofanyika nchini Tanzania (345 kutoka Tanzania na 46 kutoka UAE). Kupitia makongomano hayo, Kampuni ya *Lico Global* ya Tanzania ilingia makubaliano na kampuni ya *Tech Flyers Air Cargo LLC ya UAE* ya kuiuzia Tani 20 za karafuu zenye thamani ya dola za Marekani 240,000.

***132. Mheshimiwa Spika;*** Aidha, kupitia Maonesho ya Saba (7) ya Biashara ya Kimataifa ya China (CIIE) yaliyofanyika Novemba, 2024 nchini China, kampuni 17 za Tanzania zilishiriki maonesho hayo. Kupitia maonesho hayo, hati tatu (3) za makubaliano zilisainiwa baina ya Kampuni ya Sisalana kutoka Tanzania na kampuni tatu (3) za *Shanghai Linghang, Qarnan Packaging* na *Ashake Essential Limited*. Kampuni hiyo kutoka Tanzania itauza bidhaa za mkonge kwa kampuni hizo.

#### *3.2.5. Maendeleo ya Rasilimali Watu*

#### A. Kuajiri watumishi wa Kada na Ngazi Mbalimbali

**133.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara na Taasisi zake imeajiri jumla ya watumishi 360. Kati ya watumishi hao, watumishi 267 wameajiriwa kwa masharti ya kudumu katika Utumishi wa Umma kupitia Sekretarieti ya ajira na watumishi 93 ni ajira za mkataba. Mchakato wa ajira za watumishi hao umekamilika kwa kuwafanyia uhakiki wa vyeti vyao vya taaluma pamoja na kuingiza taarifa zao kwenye mfumo wa mishahara. Kufuatia ajira hizo nguvukazi ya Wizara imeongezeka kwa kiasi kikubwa.

#### B. Kuwajengea Uwezo Watumishi

**134.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara imeendelea kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Katika kipindi hicho jumla ya watumishi 1,342 wamewezeshwa kushiriki mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Aidha, watumishi 417 wamegharamiwa mafunzo ya muda mrefu yaani shahada ya kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu. Watumishi 925 wamewezeshwa kushiriki mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo haya yamesaidia kuboresha utendaji kazi wa watumishi pamoja na kujipatia sifa za kimuundo.

### 3.3. Mafanikio ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Kipindi cha Miaka Minne (2021-2024) Katika Serikali ya Awamu ya Sita

**135.** ***Mheshimiwa Spika****;* Kwa kipindi cha miaka minne (4) cha Serikali ya Awamu ya Sita (6), Wizara imepata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo uendelezaji wa miradi ya kielezo na kimkakati; upanuzi na ujenzi wa viwanda; uendelezaji wa teknolojia mbalimbali; atamizi na ubunifu; utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania ndani na nje ya nchi; ubora wa bidhaa na ushindani wa kibiashara; na utatuzi wa migogoro. Mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

### *3.3.1. Sekta ya Viwanda*

### A. Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo na Kimkakati

#### Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga

**136.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imefanikiwa kulipa fidia ya shilingi bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 wanaopisha utekelezaji wa Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga. Aidha, Serikali imefanikiwa kupata mwekezaji mpya ambaye ni Kampuni ya "Shudao Investment Group Company Limited (SDIG)" inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Majadiliano na mwekezaji huyo yanaendelea vizuri ambapo matarajio ni kuwa kabla ya mwaka 2024/2025 kuisha, majadiliano na mwekezaji yatakuwa yamekamilika na mradi kuanza utekelezaji.

#### Mradi wa Magadi Soda Engaruka

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuendeleza mradi wa Magadi Soda Engaruka, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 5.8 ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya shilingi bilioni 5.7 zimelipwa kwa wafidiwa 528 kati ya wafidiwa 595 sawa na asilimia 88 ya wafidiwa wote. Zoezi la ulipaji fidia linaendelea kwa wafidiwa 67 waliobaki. Vilevile, mradi umetangazwa ili kupata wazabuni watakaotekeleza mradi.

#### iii. Kufufua Kiwanda cha Kilimanjaro Mashine Tools (KMTC)

**138.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imefanikiwa kufufua Kiwanda cha Kilimanjaro Mashine Tools (KMTC) ambacho kwa sasa kinaendelea na uzalishaji. Kiwanda hicho kilisimama uzalishaji kwa zaidi ya miaka 30 ambapo katika kipindi cha miaka minne (4) jumla ya shilingi bilioni 4.07 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ya kiwanda. Miundombinu hiyo ni pamoja na; ujenzi wa tanuru lenye uwezo kuyeyusha kilo 500 za vyuma kwa mkupuo mmoja, ujenzi na usimikaji wa mtambo mkubwa wa kuweka utandu kwenye chuma, ukarabati wa mfumo wa umeme na mitambo mingine, ujenzi wa mtambo

mdogo wa kuweka utandu wa kuzuia kutu kwenye chuma, mtambo wa kubeba vitu vizito na ukarabati wa majengo ya kiwanda. Aidha, mashine mpya na za kisasa za kukunja chuma, kusokota chuma (Sheet Roller Machine) na kukata chuma (Gantry Plasma Cutting Machine) zimenunuliwa na kuanza kutumika. Kufuatia kufufuliwa kwa KMTC, jumla ya mashine 47 na vipuri 132 vimezalishwa na jumla ya mauzo ya shilingi 323,429,000 yamefanyika. Aidha, kwa sasa kiwanda kimekuwa ni tegemeo kubwa la vipuri kutoka kwenye viwanda vya ndani vikiwemo kiwanda cha sukari (TPC), Kiwanda cha Bia (TBL), *Kili Leather,* viwanda vya mkonge na mashamba ya maua.

**B. Ujenzi na Upanuzi wa Viwanda Nchini**

**139.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha miaka minne (4), Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji wa viwanda nchini. Kupitia juhudi hizo za Serikali, viwanda vikubwa vimejengwa na kupanuliwa vikiwemo *Kiwanda cha Wild Flower and Grains Ltd; Kiwanda cha Chokaa cha Maweni (Huaxin Cement Co Ltd)*; Viwanda vya kuunganisha magari (Kiwanda cha *GF Trucks and Equipment Ltd* na Kiwanda cha Saturn Corporation Limited); Kiwanda cha kutengeneza vioo (Sapphire Float Glass (Tanzania) Company Limited); Kiwanda cha Sukari cha Kilombero; Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi na Kiwanda cha Sukari Kagera. Maelezo kuhusu viwanda hivyo ni kama ifuatavyo:-

**i. Kiwanda cha Wild Flower and Grains Ltd**

**140.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *Wild Flower and Grains* kipo katika Mkoa wa Singida. Ujenzi wa kiwanda hicho ulianza Mei, 2022 kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya kula ya alizeti. Kiwanda hicho kimewekeza mtaji wa kiasi cha takriban shilingi bilioni 63.5 na kutoa ajira 100. Hadi kufikia Machi, 2025 kiwanda kimezalisha jumla ya tani 3,200 za mafuta zilizotokana na kuchakatwa tani 10,900 za mbegu za alizeti ambazo zimeuzwa katika Mkoa wa Singida pamoja na mikoa mingine. Ujenzi wa Kiwanda hicho umekamilika kwa asilimia 97. Kiwanda kitakapokamilika kitakuwa na uwezo uliosimikwa wa kusindika takriban tani 225 za mbegu

kwa siku ambao ni sawa na kuzalisha tani 75 za mafuta ya alizeti kwa siku na kutoa ajira takriban 500.

### *ii. Kiwanda cha Chokaa na Saruji cha Maweni Limestone Limited (Huaxin* **Cement Co. Ltd.)**

**141.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji. Kuboreshwa kwa mazingira hayo kumewezesha upanuzi wa mradi wa kiwanda cha *Maweni Limestone Limited* cha kuzalisha saruji aina ya Huaxin kilichopo katika Jiji la Tanga. Awali kiwanda hicho kilikuwa hakizalishi *clinker,* baada ya upanuzi kiwanda kimefanikiwa kuzalisha *clinker* kwa ajili ya uzalishaji wa saruji kwa matumizi yake na matumizi ya viwanda vingine. Upanuzi wa mradi huo umegharimu dola za Marekani milioni 30 na umeajiri jumla ya watu 906 ambapo wazawa ni 424, wageni 82 na wenye mikataba kutoka kwa mzabuni ni 400. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha *clinker* tani milioni 1.24 kwa mwaka na saruji tani milioni 1.5 kwa mwaka.

### *iii. Kiwanda cha Fortune Cement (T) Co* **Limited**

**142.** ***Mheshimiwa Spika***; Serikali imewezesha kuanzishwa kwa kiwanda cha kuzalisha saruji nyeupe cha *Fortune Cement (T) Co Limited* kilichopo Mkoa wa Pwani. Kiwanda hicho ni miongoni mwa viwanda vichache vinavyozalisha saruji nyeupe katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Uwezo uliosimikwa ni kuzalisha saruji tani 150,000 kwa mwezi ambapo kwasasa uzalishaji halisi ni tani 75,000 kwa mwezi. Aidha, kiwanda kimefanikiwa kuuza jumla ya tani 22,897.96 za saruji nyeupe katika nchi ya Uganda, Kenya, Rwanda, Zambia na Malawi. Vilevile, kiwanda kimefanikiwa kutoa ajira za moja kwa moja 60 na zisizo za moja kwa moja 180.

### **iv. Viwanda vya Kuunganisha Magari**

**143.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina viwanda vikubwa viwili (2) vya kuunganisha magari ambavyo ni *GF Trucks and Equipment Ltd* kilichopo eneo la TAMCO katika Mkoa wa Pwani na *Saturn Corporation Limited* kilichopo Mkoa wa Dar es Salaam. Kiwanda

cha *GF Trucks and Equipment Ltd* ambacho kilianza uzalishaji kwa kutumia majengo ya Wizara yanayomilikiwa na NDC, kina uwezo wa kuunganisha magari 12 hadi 15 kwa siku na kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 13. Hadi kufikia Machi, 2025 kimefanikiwa kuunganisha magari 3,445 na kutoa ajira za moja kwa moja 167 na zisizo za moja kwa moja 43. Kwa upande wa Kiwanda cha *Saturn Corporation Limited* ambacho kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 99.45 kina uwezo wa kuunganisha vichwa vya magari 900 na magari aina ya tipa 270 kwa mwezi. Hadi kufikia Machi, 2025 kiwanda kimefanikiwa kuunganisha magari 1,350 na kutoa ajira 250.

### v. Viwanda vya Sukari

***144. Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na sukari inayotesheleza mahitaji ya wananchi kwa kufanya jitihada mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi. Kiwanda hicho, kilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Agosti, 2024 na kina uwezo wa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka. Tangu kiwanda kuanza uzalishaji wake Julai, 2024, kimezalisha tani 19,124 za sukari ya majumbani na kimetoa ajira za moja kwa moja 2,172 na ajira zisizo za moja kwa moja 8,000.

***145. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, upanuzi unaohusisha usimikaji wa mitambo yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha sukari na inayotumia teknolojia ya kisasa umeendelea katika kiwanda cha Sukari cha Kilombero na Kiwanda cha Sukari cha Kagera. Katika Kiwanda cha Kilombelo upanuzi unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 132,000 za sasa hadi tani 271,000 za sukari ifikapo mwaka 2025/2026 na kutoa ajira 4,634. Aidha, upanuzi huo utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 570 hadi utakapokamilika. Hadi kufikia Machi, 2025 upanuzi umefikia asilimia 98 ambapo majaribio ya kuendesha mitambo yanaendelea. Kwa upande wa kiwanda cha Kagera, upanuzi unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 131,000 kwa sasa hadi tani 170,000 za sukari ifikapo mwaka 2025/2026. Kiwanda hicho kimetoa ajira za moja kwa moja 10,500 na ajira zisizo za moja kwa moja 60,000.

### *vi. Kiwanda cha Bidhaa za Kibailojia (TBPL)*

***146. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jitihada za kukiendeleza kiwanda cha *Tanzania Biotech Company Limited (TBPL)* kilichopo Mkoa wa Pwani ambacho kinazalisha dawa za kibaiolojia (Bio-Products) za viuadudu vya kuua mazalia ya mbu na viuatilifu hai kwa ajili ya kuua wadudu dhurifu kwenye mazao. Jitihada hizo ni pamoja na Serikali kutumia shilingi bilioni 5 kununua viuadudu na kuvisambaza kwenye Halmashauri mbalimbali zenye maambukizi makubwa ya malaria nchini. Kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha miaka minne (4) kiwanda kilizalisha na kuuza jumla ya lita 703,608 zenye thamani ya shiling bilioni 9.15 ambapo kati ya hizo, lita 415,164 zimesambazwa katika Halmashauri 123 na wadau wengine na lita 288,444 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.6 zimeuzwa katika nchi mbalimbali zikiwemo Kenya, Angola, Niger, Botswana, Namibia, Eswatini, Mozambique na Uganda.

### C. Uvumbuzi, Utafiti na Uendelezaji wa Teknolojia za Viwanda

***147. Mheshimiwa Spika;*** Serikali katika kuhakikisha inapunguza utegemezi wa uagizaji wa vifaa tiba nchini, Wizara kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) imefanikiwa kupata ithibati inayoruhusu kusanifu na kutengeneza vifaa tiba mbalimbali. Hadi kufikia Machi, 2025 shirika limefanikiwa kutengeneza majokofu nane (8) ya kuhifadhia maiti, vitanda vya kawaida 452, kabati za kuhifadhia vitu 426; *dripstand* 306, *hospital screen* 24, *na* vichomea taka ngumu 30 ambavyo vimesambazwa katika hospitali mbalimbali nchini zikiwemo:- Hospitali za rufaa za (Iringa, Manyara, Morogoro na Tanga); Hospitali za wilaya (Chunya, Gairo, Nyasa, Ngorongoro, Buhingwe, Siha, Bagamoyo, Mafinga, Nzega na Kilolo,); Viwanja vya ndege (Julius Nyerere, Arusha na Mwanza); Vyuo (UDSM – Tawi la Mbeya na State University of Zanzibar); na Makao makuu ya Shirika la Viwango (TBS).

***148. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) imefanya zoezi la

ukusanyaji wa taarifa za viwanda, uibuaji wa fursa za uwekezaji nchini (Industrial mapping) katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Mwanza na Shinyanga. Zoezi hilo limebaini uwepo wa viwanda vikubwa 331, vya kati 514, vidogo 16,046, na vidogo sana 22,760. Aidha, TIRDO imeunda mfumo wa kitaifa wa kuhifadhi na kuchakata taarifa za viwanda nchini (NIIMS) ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati. Hadi kufikia Machi, 2025, Shirika limefanikiwa kuingiza taarifa za mikoa saba (7) kwenye mfumo huo. Vilevile, mfumo huo umeimarisha uwazi na upatikanaji wa taarifa, kurahisisha ufuatiliaji wa sekta ya viwanda, na kutoa mwongozo kwa wawekezaji kuhusu maeneo yenye fursa bora za uwekezaji, hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini.

***149. Mheshimiwa Spika;*** TIRDO imefanikiwa kupata ithibati ya maabara ya mikrobaiolojia ya chakula kupitia kiwango cha ubora cha kimataifa (ISO/IEC 17025: 2017) na kuhakiki wataalamu sita (6) na kuwawezesha kuwa wabobezi katika kuhakiki ubora wa bidhaa za viwandani. Ithibati hiyo imewezesha maabara ya mikrobaiolojia ya chakula kuwa miongoni mwa maabara chache zitakazokuwa Maabara za Rufaa za Utatifi na Ubunifu Nchini (National Reference Industrial Research and Innovation Laboratories) ambazo zitaleta mafanikio makubwa katika sekta ya viwanda na elimu. Vilevile, maabara ya nishati, *Non-Destructive Testing* (NDT), Ngozi, na maabara zingine zimeboreshwa kwa kuwekewa vifaa vya kisasa.

***150. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) imeimarisha Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) katika Mikoa ya Lindi, Kigoma, Mbeya, Iringa, Shinyanga na Kilimanjaro kwa kusimika mitambo na mashine mpya zilizoongeza tija na ufanisi katika uzalishaji. Uimarishaji huo umewezesha uzalishaji wa mashine 3,091 na vipuri 9,643 ambavyo vitasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati katika uzalishaji. Aidha, SIDO imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu, mitaji, na kutoa mafunzo ambayo yamewezesha uanzishwaji wa viwanda vipya 2,784 vilivyozalisha ajira za kudumu 84,715. Vilevile, Wizara ina mitaa ya viwanda katika mikoa 23 ya Tanzania Bara, ambayo ina miundombinu muhimu kama vile ofisi za kutolea huduma,

majengo ya viwanda, umeme, maji, barabara na mawasiliano kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo na vya kati. Pia, Wizara imefanikiwa kujenga majengo mapya ya viwanda katika Mikoa Manyara, Morogoro, Katavi, Mtwara, Mwanza,Tanga, Singida na Geita ambayo yanatumiwa na viwanda.

***151. Mheshimiwa Spika;*** Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) kimeendelea kulinda soko la ndani dhidi ya zana dhaifu za kilimo na teknolojia za vijijini kwa kufanya majaribio yanayopelekea kuthibitishwa kwa zana na teknolojia hizo. Katika kipindi cha miaka minne (4), Wizara kupitia CAMARTEC imethibitisha jumla ya modeli 113 za zana za kilimo zilizofuzu vigezo vya ufanisi na uhimili baada ya majaribio kwenye mazingira ya Tanzania. Zana hizo ni pamoja na matrekta, mitambo ya kuvunia (combine harvesters), mashine za kunyunyizia dawa shambani, mashine za kupakia miwa (cane loader), majembe ya matrekta, *power tiller,* zana zinazokokotwa na wanyama kazi na zana za kilimo za mkono.

***152. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, CAMARTEC imefanikiwa kubuni jumla ya sampuli kifani za zana modeli 34 ambapo kati ya hizo, sampuli kifani mbili (2) ni za zana za kuandaa shamba; sita (6) ni zana za kupandia; mbili (2) ni teknolojia za usafirishaji vijijini; 20 ni za teknolojia za kuchakata mazao ya kilimo; moja (1) ni ya teknolojia za kuboresha matumizi ya nguvu kazi shambani; tatu (3) ni za teknolojia za kuwashia; na sampuli kifani tatu (3) ni za kuzimia moto kwenye hifadhi za wanyama Kati ya hizo, modeli 11 zimehawilishwa na kuundwa kibiashara ambapo kati ya hizo moja (1) ni sampuli kifani ya zana ya kuandaa shamba; mbili (2) ni za zana za kupandia; moja (1) ni ya teknolojia ya usafirishaji vijijini; nne (4) ni za teknolojia za kuchakata mazao ya kilimo; na tatu (3) ni za sampuli kifani za teknolojia za kuwashia na kuzimia moto kwenye hifadhi za wanyama.

### D. Atamizi na Ubunifu

***153. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia taasisi zake za TIRDO, TEMDO, SIDO na CBE imeanzisha na kuendeleza programu atamizi

na uanagenzi, kwa lengo la kutekeleza dira ya Serikali ya kuwaandaa vijana kukabiliana na soko la ajira nchini. Katika kipindi cha miaka minne (4) taasisi hizo zimeendelea na programu atamizi kwa wabunifu 808 ambao wako katika hatua mbalimbali za uendelezaji wa bunifu zao.

***154. Mheshimiwa Spika;*** Programu hizo zimewezesha kuanzishwa na kuendelezwa kwa kampuni 12 ambazo ni: *Plant Biodeferender Ltd* inafanya uzalishaji wa viuatilifu vya kibaiolojia vinavyoitwa "Vuruga"; Preyo Company Ltd inajihusisha na kuchakata taka ngumu za plastiki; *Innovex Solutions and Merchants* (Detergent Processing) inajihusisha na utengenezaji wa sabuni za maji; *H.O.P Electronics Technologies* inajihusisha na utengenezaji wa vifaa janja vya matumizi ya nyumbani; *Innovasie Company Ltd* inajihusisha na utengenezaji wa mifumo ya tehama kama vile *software MyHI* (My Health Insurance) na Sheria 365 (application ya sheria); *Albetus technologies* inajihusisha na uundaji wa *networking applications* na utengenezaji wa *CCTV cameras*; *Ammacom* inajihusisha na utengenezaji wa *software na application* mbalimbali; *Survey Fish Market Company* inajihusisha na usindikaji wa matunda, mbogamboga na ukaushaji wa samaki wabichi kwa kutumia kaushio la jua lilobuniwa. Vilevile, kampuni za *Bivac Co. Ltd; Rest Food Process Ltd; Upendo Food Process Ltd;* na *Simba and Alice Food Process Ltd* zimeendelea kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na mazao ya kilimo. Aidha, kampuni hizo zimewezesha upatikanaji wa ajira za moja kwa moja 60 na zisizo za moja kwa moja 100.

### *3.3.2. Sekta ya Biashara*

### A. Mauzo ya Bidhaa Nje ya Nchi

#### i. Soko la EAC na SADC

***155. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jitihada za kukuza mauzo ya bidhaa nje ya nchi ambapo katika kipindi cha miaka minne (4) mauzo katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,161.2 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,163.8 mwaka 2024 sawa na

ongezeko la asilimia 0.22 Vilevile, mauzo katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,303.4 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,968 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 127.7. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali za kuboresha mazingira ya biashara nchini na kukuza viwanda na uzalishaji pamoja na kuimarika kwa uzalishaji wa bidhaa ambazo zinasoko kubwa katika Jumuiya hizo. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi katika soko la EAC na SADC ni pamoja na madini, pamba, chai, parachichi, vigae, vyandarua, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka.

***ii. Soko la Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA)***

***156. Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizosaini na kuridhia Mkataba wa Soko la Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) mwaka 2021. Kuridhiwa kwa mkataba huo kumetoa hamasa kwa wafanyabiashara kutumia fursa zinazopatikana katika soko hilo. Katika kipindi cha miaka minne (4), mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuridhiwa kwa mkataba huo ni pamoja na kutolewa kwa vyeti vya uasili wa bidhaa 226. Vyeti hivyo vinajumuisha bidhaa za nyuzi za mkonge tani 6,150 kwenda nchi za Nigeria, Ghana, Morocco na Misri; Vioo (float glassess) tani 1,433 kwenda Misri; mchele tani 433 kwenda Burkina Faso na Ivory Coast; na Kahawa tani 273 kwenda Algeria. Aidha, tangu usafirishaji wa shehena ya kwanza ya bidhaa kwa kutumia kanuni za uasili wa bidhaa za AfCFTA uliofanyika Mei 2023, nchi imepiga hatua kubwa ambapo hadi kufikia Machi, 2025 tumefanikiwa kusafirisha bidhaa mbalimbali 21 na kupanua wigo wa masoko kwa kufikia Mataifa 18 ya Afrika ambayo tulikuwa hatutangamani nayo.

**157. *Mheshimiwa Spika;*** Kwa ujumla, Tanzania imekuwa na mwenendo mzuri wa mauzo katika nchi za Bara la Afrika ambapo kwa mwaka 2024 mauzo yalikuwa dola za Marekani milioni 3,946.76 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,447.63 kwa mwaka 2021 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 61.2. Ongezeko hilo, lilitokana na kuongezeka kwa masoko mapya chini ya AfCFTA yanayojumuisha nchi za Morocco, Nigeria,

Senegal, Ghana, Misri, Ethiopia, Algeria, Djibuti, Somalia na Guinea. Bidhaa zilizochangia mauzo hayo ni pamoja na kahawa, tumbaku, vioo, nafaka (mchele na mahindi), viungo na nyuzi za mkonge.

**iii. Soko la AGOA**

**158.** ***Mheshimiwa Spika;*** Nchi imeendelea kunufaika na Mpango wa AGOA ambapo mauzo kwenda Soko la Marekani kupitia mpango huo yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 33.06 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani milioni 85.4 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 158.3 **(Jedwali Na. 9).** Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni nguo na mavazi, kahawa, mbogamboga na madini. Baadhi ya viwanda vilivyouza bidhaa katika soko hilo ni pamoja na *Mazava Fabrics and Production E. A. L, Tanzania Tooku Garments Co. Ltd, Red Earth Co. Ltd* na *21st Century Textiles Ltd*.

**iv. Soko la Umoja wa Ulaya**

**159.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa upande wa Soko la Umoja wa Ulaya, mauzo ya bidhaa katika soko la Nchi Wanachama wa Umoja wa Ulaya yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 891.5 kwa mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,234.3 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 38.5. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na maharage, tumbaku, samaki, parachichi, kahawa, kokoa, asali, mafuta ya alizeti, madini, chai (black tea), maua, matunda, pamba gafi, mbogamboga, ngozi na madini ya *tanzanite.*

**B. Kutatuliwa kwa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa Vya Kiushuru (NTBs)**

**160.** ***Mheshimiwa Spika***; Katika kipindi cha miaka minne (4) jumla ya Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa Vya Kiushuru (NTBs) 64 vilijadiliwa, NTBs 50 zilipatiwa ufumbuzi na NTBs 14 zinaendelea kufanyiwa kazi baina ya Tanzania na Kenya. Kwa upande wa NTBs na changamoto za biashara baina ya Tanzania na Zambia, jumla ya changamoto na NTBs 30 zilijadiliwa, 20 zilitatuliwa na 10

zinaendelea kushughulikiwa. Utatuzi huo wa NTBs pamoja na changamoto mbalimbali za biashara baina ya Tanzania na nchi hizo jirani umeleta manufaa ya kuwezesha biashara kufanyika na umesaidia kuimarisha ushirikiano wa biashara na uchumi na nchi hizo. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu mikutano ya Kikanda ya uondoaji vikwazo (NTBs) pamoja na kuratibu Mikutano ya Uwili (Bilateral) ya utatuzi wa vikwazo (NTBs) na nchi jirani.

***C. Kuwajengea Uwezo na Kuwawezesha Wajasiriamali na Wafanyabiashara***

**161. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali na wafanyabiashara ambapo katika kipindi cha miaka minne (4) jumla ya wajasiriamali 115,733 walipatiwa mafunzo. Mafunzo hayo yalijikita katika:- Uzingatiaji wa dhana ya ubora katika uzalishaji; Elimu ya biashara na ujuzi; Matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala; na Utafutaji wa masoko. Vilevile, juhudi za kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali zimeendelea ambapo, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (NEDF) unaoratibiwa na SIDO umetoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati 10,113 ambapo wanawake ni 4,902 na wanaume 5,313 yenye thamani ya shilingi billioni 26.225 na kuwezesha ajira 23,535 **(Jedwali Na. 10).**

**D. Kudhibiti Ubora wa Bidhaa na Ushindani wa Kibiashara Nchini**

***162. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeendelea na juhudi za udhibiti wa ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini kwa kutumia Mpango wa Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa (Product Certification Scheme). Kutokana na juhudi hizo, Wizara imefanikiwa kutoa leseni za nembo ya ubora wa bidhaa 2,569 kwa wazalishaji mbalimbali wa bidhaa hapa nchini. Kati ya leseni hizo, jumla ya leseni 1,135 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo. Leseni hizo zimewezesha wazalishaji kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi, hivyo kukuza biashara, kuongeza wigo wa ajira, kupunguza umaskini na hatimaye kukuza uchumi. Aidha, TBS imefanikiwa kusajili bidhaa za chakula na vipodozi

6,677 kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa hizo.

***163. Mheshimiwa Spika;*** Shirika la TBS limeendelea kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini kwa kutumia mfumo wa *Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards* (PVoC) pamoja na kufanya ukaguzi pindi bidhaa zinapowasili nchini (Destination Inspection) na hatimaye hutoa vyeti kwa shehena zinazokidhi matakwa ya viwango (Certificate of Conformity - CoC). Katika kipindi cha miaka minne (4), TBS kupitia mawakala wake imefanya kaguzi kama ifuatavyo: - Imekagua shehena 131,072 kabla hazijaingizwa nchini; Imekagua jumla ya bidhaa 286,709 kutoka nje ya nchi baada ya kufika nchini; na Imekagua jumla ya magari 176,122 yaliyotumika nje ya nchi.

***164. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kipindi cha miaka minne (4) imefanikiwa kusajili makampuni 58,637, majina ya Biashara 109,292, na Alama za Biashara na Huduma 13,153. Vilevile, imetoa Leseni za Biashara kundi 'A' 65,442, Leseni za Viwanda 1,002 na Hataza 290.

***165. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha miaka minne (4), Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA), imehakiki vipimo 3,410,663. Kati ya vipimo hivyo, vipimo 102,969 vilikutwa na mapungufu ambayo yalirekebishwa na kuruhusiwa kuendelea kutumika na vipimo 5,607 vilikataliwa. vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni pamoja na uhakiki wa pampu za kuuzia mafuta; uhakiki wa kiasi cha gesi kwenye mitungi ya gesi; uhakiki wa mizani itumikayo kuuzia bidhaa kama nafaka katika masoko, madukani; uhakiki wa vipimo vinavyotumika kuuzia vifaa vya ujenzi mfano; uhakiki wa malori yabebayo kokoto na mchanga; uhakiki wa usahihi wa ujazo/ kiasi kilichoandikwa cha mbolea na pembejeo kwenye vifungashio husika; uhakiki wa ujazo wa matanki makubwa ya kuhifadhia mafuta; uhakiki wa vipimo vitumikavyo kujaza mafuta kwenye matanki ya magari yabebayo mafuta; na uhakiki wa usahihi wa mizani inayotumika kupima magari ya mizigo na mabasi.

***166. Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia WMA imefanikiwa kuanzisha vituo vipya vitano (5) katika mikoa yenye mipaka na kufanya kuwa na jumla ya vituo vya ukaguzi 13 Tanzania Bara. Lengo la vituo hivyo ni kuhakiki usahihi wa kiasi/idadi iliyotamkwa (decraled quantity) kwa bidhaa zinazoingia nchini. Vituo hivyo ni Sirari (Mara), Mtukula (Kagera), Namanga (Arusha), Holili (Kilimanjaro), Tunduma (Songwe), Tarakea (Kilimanjaro), Horohoro (Tanga), Kasumulu (Mbeya), Manyovu (Kigoma), Bagamoyo (Pwani), Kwara (Pwani), Bandarini (Dar es Salaam) na Mbweni (Dar es Salaam).

***167. Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia WMA imeendelea kufanya uhakiki wa kiasi cha mafuta (jamii ya petroli na mafuta ya kula) yanayoingia nchini kupitia bandari za Dar es salaam, Tanga na Mtwara. Katika kipindi cha miaka minne (4), jumla ya lita bilioni 30.6 za mafuta kwa meli 546 zilihakikiwa ambazo zimetumika ndani na zile zilizosafirishwa nchi za jirani. Aidha, WMA imehakiki jumla ya *metric tonnes* 958,593.2 za gesi zilizoshushwa na meli 210 nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Vilevile, imefanikiwa kuanzisha mikoa mitano (5) ya kivipimo ambayo ni Kinondoni, Temeke, Ilala, Kituo cha Misugusugu (Pwani), Kitengo cha Ukaguzi wa Bidhaa zilizofungashwa zinazoingia nchini na Kitengo cha Bandari. Hali hiyo imesaidia kusogeza huduma kwa jamii pamoja na kuwezesha kushirikiana na Mamlaka zingine za Serikali kwa karibu kama vile Mamlaka za Serikali za Mitaa.

***168. Mheshimiwa Spika;*** Katika jitihada za kutatua migogoro, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) imefanikiwa kutatua migogoro kwa kushughulikia mashauri ya rufaa 70 kati ya mashauri 93 yaliyopokelewa. Mashauri 23 yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Matokeo ya maamuzi ya mashauri ni pamoja na kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kukuza ubunifu, kuwezesha matumizi ya rasilimali yenye ufanisi na kumlinda mlaji.

***169. Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha miaka minne (4) Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeridhia maombi 207 ya miungano ya kampuni kutoka Sekta za Kilimo, Madini, Mawasiliano, Benki, Michezo ya Kubahatisha, Nishati, Nyumba,

Afya, na Utalii. Miungano hiyo inajumuisha ombi la *Etablissments Maurel & Prom S.A* kununua haki zote za umiliki wa *Wentworth Resources Plc* katika kitalu cha uchimbaji gesi asilia cha Mnazi Bay; Kampuni ya Minara Tanzania Limited kununua Minara iliyokuwa ikimilikiwa na kampuni ya simu ya *Airtel Tanzania*; Kampuni ya *Honora Holdings* kununua kampuni ya *MIC Tanzania Plc* baada ya wawekezaji wa awali kuondoka Tanzania; Kuungana kwa Kampuni ya *Azam Media Limited* na *Azam TV Limited* zinazomilikiwa na mtu mmoja kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha mazingira ya biashara nchini; na Kuridhiwa kwa Kampuni ya Helios Tanzania kununua minara mbalimbali iliyokua inamilikiwa na Kampuni za Mawasiliano.

***170. Mheshimiwa Spika;*** Matokeo ya kuridhiwa kwa miungano hiyo ni pamoja nakuiwezesha Serikali kuwa na umiliki wa asilimia 40 wa gesi asilia yote itakayokuwa inazalishwa katika kitalu cha *Mnazi Bay*; kuwezesha kampuni za wazawa kushiriki katika uzalishaji wa gesi asilia kwa kuwa na umiliki wa moja kwa moja na hivyo kuweza kushindana katika masoko ya ndani na nje ya nchi; na kuongezeka kwa ufanisi zaidi katika utoaji wa huduma za mawasiliano nchini.

***Kuweka Mazingira Wezeshi ya Kuchochea Maendeleo ya Biashara Nchini.***

***171. Mheshimiwa Spika;*** Katika jitihada za kuboresha mazingira ya biashara nchini, Wizara imefanikiwa kukamilisha marejeo ya Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 toleo la mwaka 2023 ambayo ilizinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Julai, 2024 jijini Dar es Salaam. Masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Sera hiyo ni pamoja na kuimarisha maendeleo ya biashara ya ndani; Kuimarisha ushirikiano wa biashara za Kikanda na Kimataifa; kuongeza matumizi ya fursa za soko la nje; kuimarisha miundombinu ya masoko; kusimamia Sheria na Haki na ulinzi kwa walaji; kuboresha uwezeshaji biashara; kuimarisha miundombinu ya biashara mtandao na matumizi ya teknolojia za kidijitali; kuboresha upatikanaji wa mitaji ya biashara; kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika ufanyaji

biashara; na kuzingatia masuala mtambuka katika ufanyaji wa biashara. Utekelezaji huo utasaidia kuimairisha Sekta ya biashara katika kuchangia Pato la Taifa.

***Utafutaji wa Masoko kwa Bidhaa Zinazozalishwa Nchini.***

***172. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) iliratibu huduma ya Kliniki ya Biashara kwa kushirikiana na Taasisi wezeshi za Serikali 24 zikiwemo TRA, BRELA, TBS, WMA, TIC. Kupitia kliniki hizo, jumla ya wafanyabiashara 3,256 walihudumiwa ambapo changamoto 1,298 zilitatuliwa. Vilevile, kampuni 482 zilisajiliwa na kampuni 137 zilipata alama za ubora na vifungashio vinavyokidhi viwango vya soko la kimataifa. Aidha, wafanyabiashara 238 waliunganishwa na wanunuzi wa ndani na nje kupitia mikutano ya B2B na B2G na 312 walipatiwa elimu kuhusu biashara, forodha, na kodi, hatua iliyosaidia kuboresha ushindani wao katika soko.

***173. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade imeratibu ushiriki wa Tanzania katika matukio mbalimbali ya ukuzaji biashara ndani na nje ya nchi yakiwemo Maonesho ya 45 hadi 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF), Maonesho ya Bidhaa za Viwanda, Maonesho ya Expo 2020 Dubai na Maonesho ya Kimataifa ya Mbogamboga na Matunda ya Expo 2020 Doha. Kupitia matukio hayo, mafanikio mbalimbali yalipatikana yakiwemo:- Ushiriki wa kampuni 20,484 kutoka ndani na nje ya nchi; Mauzo ya papo kwa papo yenye thamani ya shilingi bilioni 13.993; na Kusainiwa kwa Hati za Makubaliano 46 baina ya Kampuni mbalimbali za ndani na nje ya nchi zenye thamani ya shilingi trilioni 17.52. Maonesho hayo yametoa fursa kwa Taasisi za sekta Binafsi na Serikali kutangaza bidhaa na huduma wanazozalisha pamoja na miradi ya kimkakati katika masoko ya kimataifa.

***174. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imeendelea kuhamasisha wakulima kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala ambapo, katika kipindi cha miaka minne (4) mazao yanayotumia mfumo wa stakabadhi za ghala yaliongezeka kutoka mazao 11 hadi kufikia mazao 16.

Mazao hayo ni Ufuta, Kakao, Asali, Maharage, Mihogo, Dengu, Choroko, Vitunguu swaumu, Mahindi, Mpunga, Mbaazi, Korosho, Chai, Mchele, Soya na Kahawa. Aidha, jumla ya tani 654,928.06 za mazao ziliuzwa kupitia mfumo huo na kuwezesha upatikanaji wa shilingi trilioni 4.9 kwa wakulima na kutengeneza ajira 6,983. (***Jedwali Na. 11***).

## 4. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2025/2026

**175.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera za kisekta; Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026); maelekezo ya viongozi wakuu wa kitaifa pamoja na mipango mbalimbali ya kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

### 4.1. Vipaumbele

**176.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

(1) Kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa Viwanda nchini;

(2) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ya Sekta;

(3) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mitaa ya viwanda (*Industrial Clusters*) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati;

(4) Kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa Sekta binafsi;

(5) Kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini;

(6) Kuchochea Maendeleo ya watu kwa kuboresha miradi na programu kwa Jamii inayohusisha elimu na Mafunzo ya Ujuzi; na

(7) Kuimarisha Usimamizi wa Ubora na Usalama wa Bidhaa Nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vipodozi.

### 4.2. Kazi Zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi Zake

**177.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara pamoja na taasisi zake zitatekeleza shughuli zifuatazo:

#### 4.2.1. Sekta ya Maendeleo ya Viwanda

#### A. Idara ya Maendeleo ya Viwanda

**178.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika Idara ya Maendeleo ya Viwanda:

i. Kukamilisha marejeo na kutekeleza Sera Endelevu ya Maendeleo ya Viwanda;

ii. Kufanya mapitio ya Mkakati wa Ngozi na Mafuta ya Kula;

iii. Kuandaa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Viwanda;

iv. Kufanya Mapitio ya Sheria ya Chuma Chakavu; na

v. Kuandaa Mkakati na Muongozo wa kuunda na kunganisha magari.

**B. Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC)**

**179.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Shirika limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo yafuatazo:

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya Mchuchuma, Liganga na mradi wa Magadi Soda Engaruka;

ii. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya Kimkakati ya Chuma Maganga Matitu, Makaa ya mawe Katewaka; Makaa ya Mawe Mhukuru pamoja na kulipia leseni za uchimbaji;

iii. Kuboresha utendaji wa kiwanda cha KMTC;

iv. Kuboresha kiwanda cha Tanzania Biotec Limited kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa ya viuatilifu hai na Mbolea hai na kukamilisha upatikanaji wa Ithibati ya Ubora wa Kimataifa;

v. Kuendelea na ufufuaji wa kiwanda cha Mang’ula;

vi. Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu katika Kongani ya TAMCO na Kange pamoja na kuendeleza eneo la Viwanda la Kimanjaro Machine Tools ili kuvutia wawekezaji zaidi;

vii. Kuendeleza mashamba ya miti ya mpira kwa ajili ya kuzalisha malighafi viwanda na kutunza mazingira;

viii. Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya Shirika ikiwemo ukarabati wa majengo na ofisi, na

ix. Kuboresha mfumo wa kitaasisi kwa kuimirisha mifumo ya kisheria, technolojia na kujenga ubobezi wa wataalamu wa shirika

### C. Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)

**180.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Shirika limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea kufanya tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji katika kanda za ziwa (Kagera, Geita, Mara na Simiyu) na kanda ya Kasikazini (Arusha na Manyara);

ii. Kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala ili kutoa nafasi ya kuanzisha kituo cha Taarifa za Viwanda (NIIMS) na ubashiri wa teknolojia na viatamizi kwa wabunifu wa teknolojia katika Shirika;

iii. Kuanzisha Maabara ya Nishati na Madini Mkoa wa Njombe na kutoa elimu ya utengenezaji na matumizi ya Nishati mbadala;

iv. Kuendelea na ukamilishaji wa kubadili ithibati za maabara na kuboresha Maabara za mazingira, kemia, makaa ya mawe, mafuta na gesi.

v. Kuendelea kuimarisha idara ya uhandisi katika maabara ya ngozi na nguo kwa kuongeza wataalam na vifaa;

vi. Kuendelea kufanya tafiti na kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora;

vii. Kuendelea kukamilisha uandaaji wa kanuni za Shirika wa kurejea Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO ambayo imefanyiwa maboresho; na

viii. Kufanya utafiti wa uwezekano wa kiteknolojia na kiuchumi wa madini katika mkoa wa Kagera- Kyerwa

(tantalum, tungsten na Zinc), Singida-Ilamba (Titanium na Zinc) na Dodoma- Mpwapwa (Chuma) ili kubaini wingi na kuweka utaratibu wa ujenzi wa viwanda katika maeneo hayo kwaajili ya kunufaika kiuchumi kwa Taifa.

**D. Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC); Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO); na Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO)**

**181.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, CAMARTEC, SIDO na TEMDO zimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kusanifu na kuendeleza utengenezaji wa vifaa tiba vya hospitali awamu ya tatu;

ii. Utengenezaji wa kibiashara wa viwanda vidogo vya kuchakata sukari (sugar mill mini-processing plant - Capacity 200 TCD);

iii. Kuimarisha na kuanzisha Mitaa ya Viwanda na viwanda darasa kwa ajili ya kongani za viwanda na biashara katika Wilaya moja kila Mkoa ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;

iv. Kuhawilisha teknolojia ili kurahisisha uchakataji wa mazao mbalimbali yanayozalishwa nchini;

v. Kuendelea kufanya utafiti na uanzisha Kiwanda Darasa cha kuchakata zao la chikichi mkoani Kigoma;

vi. Kuendelea kulinda taifa na wananchi dhidi ya zana dhaifu za kilimo na teknolojia za vijijini kwa kufanya majaribio na kuzithibisha zana hizo kwa matumizi nchini; na

vii. Kubuni mitambo ya kutengeneza Nishati Mbadala na Teknolojia za Wachimbaji Wadogo wa Madini (ASM).

### 4.2.2. Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

**Idara ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

**182.** ***Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo:

i. Kuhamasisha na kuendeleza uanzishwaji wa Kongani Nchini;

ii. Kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa utengaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;

iii. Kuhamasisha urasimishaji wa shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati;

iv. Kuhamasisha wajasiriamali wadogo na wa kati kuchangamkia masoko ya ndani na nje; na

v. Kuratibu mafunzo kwa lengo la kuelimisha wajasiriamali wadogo na wa kati wanaozalisha vyakula kutumia teknolojia ya kuongeza virutubisho kwenye vyakula.

### 4.2.3. Sekta ya Biashara

**Idara ya Mtangamano wa Biashara**

**183.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika kuendeleza Mtangamano wa Biashara:-

i. Kusimamia na kuratibu majadiliano ya ushirikiano wa biashara kati ya Nchi na Nchi;

ii. Kusimamia na kuratibu majadiliano ya biashara na utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda ya Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), Jumiuya ya Afrika Mashariki

(EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Eneo Huru la Biashara la Utatu (TRIPARTITE);

iii. Kusimamia na kuratibu majadiliano ya biashara na utekelezaji wa Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO);

iv. Kuimarisha utendaji wa kamati za Uwezeshaji Biashara na kutatua changamoto za biashara ili kuboresha mazingira ya biashara na kuhakikisha utekelezaji wa sera na taratibu za ushirikiano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa; na

v. Kubaini fursa za biashara na masoko kwa bidhaa na huduma nje ya nchi kupitia majukwaa na jumbe za biashara.

**B. Idara ya Maendeleo ya Biashara**

**184.** ***Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika kuendeleza Biashara:

i. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini kwa kufanya marejeo ya Sera na Mikakati pamoja na marekebisho ya Sheria mbalimbali mfano kufanya marejeo ya Sera ya Masoko ya Mazao (Agricultural Marketing Policy)

ii. Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na mazao ndani na nje ya nchi kwa kuratibu matukio ya ukuzaji biashara ikiwemo maonesho na misafara ya kibiashara;

iii. Kufanya intelijensia ya masoko (market inteligence) kuhusu upatikanaji wa fursa za masoko ya mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini;

iv. Kuimarisha na kuboresha huduma na mifumo ya upatikanaji wa Taarifa za Mazao, Biashara na Masoko; na

v. Kuratibu mwenendo wa ufanyaji biashara ya mipakani ikiwa ni pamoja na urasimishaji wa biashara hizo.

**C. Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**

**185.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Shirika litatekeleza yafuatayo:

i. Kutayarisha viwango 740 vya Kitaifa Katika Sekta/Nyanja Mbalimbali;

ii. Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 1,000 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo;

iii. Kusajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 14,000;

iv. Kusajili bidhaa 2,200 za chakula na vipodozi;

v. Kukagua na kutoa vibali 140,000 kwa bidhaa zitokazo nje ya nchi ambapo kati ya hizo, vibali 44,000 ni kwa bidhaa zitakazokaguliwa nje ya nchi na vibali 96,000 ni kwa bidhaa zitakazokaguliwa nchini;

vi. Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 50,000 za magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini; vii. Kutoa mafunzo na semina kuhusu viwango na udhibiti ubora kwa wadau 1,800 wa sekta ndogo tano;

vii. Kuthibitisha kampuni 16 chini ya mifumo ya ubora na uongozi;

viii. Kupima sampuli 40,000 za bidhaa mbalimbali;

ix. Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 12,000; xi. Kuweka kinasaba katika lita 4,200,000,000 za mafuta ya petrol, dizeli na mafuta ya taa;

x. Kuendelea na ujenzi wa Viwango House Mwanza, maabara na ofisi ya Kanda ya Ziwa; na

xi. Ujenzi wa maabara na ofisi katika kanda ya kaskazini (Arusha).

**D. Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)**

**186.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Wakala itatekeleza yafuatayo:-

i. Kusajili Kampuni 19,640, Majina ya Biashara 33,800, Alama za Biashara na Huduma 3,640, Maombi ya Hataza 85 na kutoa Hataza 40 na vyeti vya Viwanda 65;

ii. Kutoa Leseni za Biashara kundi ‘A’ 21,582 na za Viwanda 437 pamoja na vyeti vya usajili wa Viwanda 65;

iii. Kuendelea kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kufanya sajili mbalimbali za kibiashara zinazotolewa na Wakala na kutoa elimu juu ya mabadiliko ya sheria;

iv. Kufanya kaguzi elimishi 16 za Leseni za Biashara kundi ‘A’ na Viwanda;

v. Kuendelea kuboresha na kuimarisha mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma;

vi. Kukamilisha mapitio ya Sheria za Usajili na Leseni;

vii. Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi, idadi ya watumishi, kutoa mafunzo kwa watumishi na kuongeza

vitendea kazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma; na

viii. Kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi Dodoma.

**E. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)**

**187.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Bodi imepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

ii. Kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

iii. Kufanya upanuzi wa Utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa kuongeza bidhaa za kilimo na zisizo za kilimo katika mfumo;

iv. Kuendelea na taratibu za kuifanya Stakabadhi ya Ghala kuwa na thamani ya fedha;

v. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala na majukumu ya Ofisi;

vi. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa ithibati ya ubora wa kimataifa (ISO:9001); na

vii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini kwa shughuli za Mfumo na Bodi.

**F. Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tan Trade)**

**188.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2025/2026, Mamlaka imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania;

ii. Kuimarisha ushindani wa kibiashara nchini;

iii. Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ufanyaji Biashara; na

iv. Kuimarisha uwezo wa Taasisi kujiendesha kiufanisi.

**G. Wakala wa Vipimo (WMA)**

**189.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026 Wakala imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya utoaji wa huduma ya kumlinda mlaji;

ii. Kuboresha mazingira ya utendaji kazi pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uhakiki wa vipimo;

iii. Kuimarisha programu za mafunzo kwa watumishi ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao; na

iv. Kutoa elimu ya matumizi ya vipimo sahihi kwa wananchi.

**H. Tume ya Ushindani (FCC)**

**190.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Tume itatekeleza yafuatayo:

i. Kuboresha Hali ya Ushindani na ulinzi wa mlaji katika Soko;

ii. Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Alama za Bidhaa, 1963;

iii. Kuendelea na mapambano dhidi ya bidhaa bandia katika soko; na

iv. Kufanya tafiti tatu (3) kuhusu ushindani na ulinzi wa mlaji.

### I. Baraza la Ushindani (FCT)

**191.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Baraza litatekeleza yafuatayo:

i. Kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri ya rufaa 50 yanayowasilishwa katika Baraza;

ii. Kuimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu ya Baraza;

iii. Kufanya utafiti wa kisheria na kiuchumi kuhusu ushindani wa kibiashara na udhibiti wa Soko; na

iv. Kuongeza uelewa kwa wadau na jamii kuhusu shughuli za Baraza na haki katika ushindani wa soko.

### J. Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE)

**192.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Chuo kimepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kujenga jengo jipya la ghorofa kumi (10) la Vipimo na Viwango katika Kampasi ya Dar es Salaam;

ii. Kujenga madarasa ili kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika eneo la Nzuguni - Kampasi ya Dodoma;

iii. Kujenga ukumbi wa mihadhara katika Kampasi ya Mwanza;

iv. Kujenga vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Kampasi ya Mbeya;

v. Kutafuta eneo kwa ajili ya upanuzi wa Kampasi ya Dar es Salaam;

vi. Kuanzisha Kampasi ya Chuo cha Elimu ya Biashara katika ukanda wa Kaskazini;

vii. Kuboresha miundombinu ya TEHAMA; na

viii. Kuendeleza rasirimali watu kwa mafunzo ya muda mrefu.

## 5. SHUKRANI

***193. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2024/2025. Ufanisi huo ulipatikana kutokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Wizara wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Benki mbalimbali na wananchi kwa ujumla. Kwa kuwa Kidole kimoja hakivunji chawa, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi wakiwemo Baraza la Taifa la Biashara (Tanzania National Business Council – TNBC); Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (Tanzania Private Sector Foundation – TPSF); Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania Industries – CTI); na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chambers of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara.

***194. Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, natambua kwa dhati mchango wa wajasiriamali wa kada zote, wakiwemo mafundi mchundo, maseremala, mafundi uashi, wabunifu wa kazi za mikono na watoa huduma wa viwango mbalimbali ambao wanachangia kuinua uchumi kupitia Sekta ya Viwanda na Biashara. Wahenga walinena "Akili ni mali, na jasho ni mtaji na pia kidole kimoja hakivunji chawa", hivyo mafanikio tunayoyashuhudia leo ni matokeo ya jitihada za pamoja baina ya Serikali na Sekta binafsi.

***195. Mheshimiwa Spika;*** Nawashukuru pia wamiliki na waandishi wa vyombo vya habari na wasanii wote kwa mchango wao katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zake kwa ujumla. Nawaomba

tuendeleze ari hiyo ili tuweze kupanua wigo wa elimu kwa umma na hatimaye washiriki kikamilifu katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara na kutia chachu zaidi katika mafanikio tuliyoyapata. Kwa hakika, "neno likitumiwa vyema, hujenga Taifa", na mchango wao katika kutoa taarifa sahihi, kuelimisha na kushirikisha jamii ni sehemu muhimu ya maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

***196. Mheshimiwa Spika;*** Maji ya kisima hayachimbiwi mbali, nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kisarawe kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo kwani ukaribu wetu ndiyo msingi wa mafanikio. Nawapongeza kwa jitihada zao za kuleta maendeleo katika jimbo na ninawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yao ndani na nje ya Bunge ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kushamiri na hatimaye kutupatia matokeo ya mtu mmoja mmoja na kuongeza mchango wake kwa Taifa kwa ujumla. Wakumbuke kuwa "mkono mmoja hauchinji ng'ombe", kwa unyenyekevu mkubwa nawaomba waendelee kunishika mkono tufanikishe kwa pamoja.

***197. Mheshimiwa Spika;*** Mtumbwi mmoja huvushwa kwa pamoja, Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa Viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Mheshimiwa Exaud S. Kigahe - Naibu Waziri na Mbunge wa Mufindi Kaskazini; Dkt. Hashil T. Abdallah, Katibu Mkuu; Dkt. Suleiman H. Serera, Naibu Katibu; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake. Nawapongeza sana. Aidha, nawashukuru wachapishaji wote akiwemo Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha nyaraka mbalimbali ya Wizara kwa wakati.

***198. Mheshimiwa Spika;*** Mwenda tezi na omo, marejeo ni ngamani, Maneno haya ya wahenga hutufundisha kuwa, licha ya shughuli na majukumu ya kila siku, familia ni mahali pa faraja, nguvu na matumaini. Utekelezaji wa majukumu yangu ambayo muda mwingi nipo nje ya nyumbani usingekuwa rahisi bila maombi na dua njema kutoka kwa watu wangu wa karibu. Nawaombea Pepo ya Firdaus wazazi wangu Saidi Ally Jafo na

Khadija Amiri Madega ambao wametangulia mbele ya haki kwa malezi yao bora kwangu kwa kipindi chote cha uhai wao. Vilevile, napenda kuwashukuru wake zangu, Rehema binti Disanura, Aisha binti Shame na Salma binti Dibibi pamoja na watoto wangu kwa upendo, uvumilivu na ushirikiano wenu unaonipa nguvu na ari ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo, uzalendo na ueledi wangu wote. Vile vile, nawashukuru sana viongozi wangu wa Dini, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kuendelea kuniombea kwa Mola ili niendelee kulitumikia Taifa letu. Nawaahidi nyote na Watanzania kwa ujumla kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa kutanguliza maslahi ya Taifa mbele.

***199. Mheshimiwa Spika;*** Kwa namna ya pekee noomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**6. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026**

**200.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2025/2026, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya shilingi 135,788,232,000 katika Fungu 44. Kati ya fedha hizo, shilingi 93,900,697,000 ni matumizi ya kawaida, na shilingi 41,887,535,000 ni matumizi ya Maendeleo. Katika shilingi 93,900,697,000 za matumizi ya kawaida, shilingi 75,819,380,000 ni Mishahara na shilingi 18,081,317,000 ni matumizi mengineyo. Aidha, kati ya shilingi 41,887,535,000 zinazoombwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, shilingi 27,870,710,000 ni fedha za ndani na shilingi 14,016,825,000 ni fedha za nje.

***201. Mheshimiwa Spika;*** Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara **www.mit.go.tz.**

***202. Mheshimiwa Spika;*** Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ukiona mtu mwingine hanenepi ujue kuna kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kwa sababu ya muda ninaomba taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara unatokana na Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6(1)(a) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inahusu uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Machi, 2025, Kamati ilichambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hii inatokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa inahusu maeneo yafuatayo:-

(i) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara kufikia mwezi Februari, 2025;

(iii) Uzingatiaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayozungumzia Muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu maelezo ya jumla kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya Pili inaelezea Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(c) Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri wa Kamati na Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaliomba Bunge lako Tukufu lifuatilie mtiririko wa Taarifa hii ili kupata msingi wa ushauri unaotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Uchambuzi na Tathmini; sehemu hii ya Taarifa inazungumzia msingi wa ushauri wa Kamati uliotokana na hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mara baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na: -

(i) Hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; na

(iv) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa shilingi bilioni 29.8 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara ilipokea shilingi bilioni 11.4 sawa na 38.27% tu ya Fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo siyo wa kuridhisha, kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilipokea 38.27% tu ya fedha zilizoidhinishwa. Hali hiyo imeathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuliomba Bunge, kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha kwa Wizara hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha kukamilisha utekelezaji wa miradi iliyopangwa kabla mwaka wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayoitaka Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Geita, Tabora na Dodoma kuanzia tarehe 11 hadi 20 Machi, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo, Kamati iliutembelea Mradi wa Kuongeza Wigo wa Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani *(WRRB - Shinyanga*) Mradi Na. 6260 uliopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Ukaguzi wa Mradi; uchambuzi wa Kamati ulibaini uwepo wa mafanikio na changamoto katika Mradi uliotembelewa na ilitoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wadau kutouelewa vizuri mfumo. Wapo baadhi ya wadau ambao hawana uelewa mzuri wa mfumo wa stakabadhi za ghala ambao hueneza taarifa zisizo sahihi kwa wakulima na kuwatia hofu. Hali hii inasababisha mwitikio mdogo wa wananchi kwani hususan wakulima kwani baadhi yao hawapeleki mazao kwenye vituo na hivyo kuchangia zoezi hili kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, elimu kuhusu matumizi sahihi ya mfumo huu, manufaa yanayopatikana na hasara inayoweza kupatikana kwa kuuza nje ya mfumo iendelee kutolewa na kuwafikia wananchi wengi hususan wakulima wenyewe hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upungufu wa Mazao; lipo tatizo la upungufu wa mazao katika maeneo ambapo mfumo umepelekwa kutokana na baadhi ya wakulima na wadau kuyaficha, kwa mfano zao la choroko kwa lengo la kuuza nje ya mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa wakulima wahamasishwe kupeleka mazao ambayo yapo kwenye mfumo ili kuleta ufanisi wa mfumo, kuiwezesha Serikali kupata kodi yake na mkulima kutopunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufinyu wa Bajeti; kiwango cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Bodi kupitia bajeti ya Serikali ni kidogo kulingana na kazi kubwa iliyopo. Aidha, mapato ya ndani hayatoshelezi utekelezaji wa shughuli zilizopo kutokana na sehemu ndogo ya maeneo yanayotekeleza mfumo nchini na idadi ya mazao yanayouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuiongezea fedha Bodi iweze kutanua wigo wa shughuli zake na kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa kuwapa elimu kuhusu matumizi ya mfumo, uhifadhi na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa maghala; maghala ya kuhifadhia chakula yaliyounganishwa na mfumo yapo mbali na wakulima na katika maeneo machache. Suala hili linasababisha mazao mengi kutoingia kwenye mfumo kutokana na umbali na gharama ambazo wakulima wanaziingia kusafirisha mazao hadi kuyafikisha kwenye maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na Sekta Binafsi kujenga maghala ya kutosha karibu zaidi na wakulima na yawe yanafikika nyakati zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida; kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Viwanda na Biashara yaani Fungu 44 iliidhinishiwa shilingi bilioni 81.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aliwasilisha mbele ya Kamati ufafanuzi kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama Kielelelezo Na. 1 kinavyoonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umeonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ulikuwa pungufu kwa 4.56% ya lengo, ambapo Wizara ilipokea 61.44% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha unachangia kukwamisha baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka husika wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati; Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Fungu 44 yaliyotolewa wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maagizo 10 yaliyolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu yake. Taarifa ya mtoa hoja ilionesha kuwa, Serikali imetekeleza

maagizo ya Kamati na baadhi yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa maagizo yaliyotekelezwa ni pamoja na:-

(a) Suala la uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji ili Sekta Binafsi iendelee kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vitakavyoongeza ajira, uongezaji thamani na mapato ya fedha za kigeni na kuhakikisha wananchi wote ambao maeneo yao yanatwaliwa wanalipwa fidia stahiki haraka kulingana na thamani ya ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI), imetekeleza Programu mbalimbali kwa lengo la kuboresha taratibu za udhibiti. Aidha, Wizara imetekeleza Programu hizi ili kuepuka mwingiliano wa majukumu, kukuza uwazi na kuanzisha muundo wa ufuatiliaji na tathmini wenye ufanisi katika kukuza biashara na uwekezaji nchini kwa kufanya yafuatayo: -

i. Kukamilika kwa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2023;

ii. Kufanya mapitio ya Sheria zilizobainika kukwamisha au kuchelewesha uanzishwaji na uendeshaji wa uwekezaji na biashara ambapo Serikali imepitia na kurekebisha Sheria na Kanuni 61 kati ya 88 zilizoibuliwa wakati wa kufanya tathmini; na

iii. Kufanya mapitio ya tozo ambazo ni kero na kupendekeza kupunguza au kufutwa ambapo Serikali imefuta au kupunguza tozo, ada na faini mbalimbali zipatazo 383 zilizobainishwa kuwa kero katika ufanyaji biashara.

(b) Kamati ilielezwa kuwa Azimio kuhusu upatikanaji wa Masoko kwa Bidhaa zinazozalishwa nchini limetekelezwa kwa kuendesha warsha na ziara mbalimbali za kutambua na kuwezesha wafanyabiashara kufikia masoko ya nje ya nchi katika Mkoa wa Tanga na Kilimanjaro. Lengo kuu lilikuwa ni kutambua wafanyabiashara na kutoa mafunzo kuhusu namna ya kutumia vyema fursa zinazotokana na majadiliano ya uwili, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia Maagizo iliyopewa katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuipatia Wizara hii fedha ilizoidhinishiwa na Bunge kwa wakati ili iweze kukamilisha utekelezaji wa maagizo iliyopewa kwa kuwa baadhi ya maagizo hayajatekelezwa kutokana na kukosekana kwa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Tarehe 25 Machi, 2025 Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara – Fungu 44 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi huo ulilenga kujihakikishia iwapo Mpango na Makadirio haya umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara – Fungu 44 inaomba kutengewa jumla ya shilingi bilioni 135.8, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 93.9, sawa na 69.15%, ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 41.9, sawa na 30.85%, ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio ya bajeti yameongezeka kwa 22%. Ongezeko zaidi lipo kwenye fedha za maendeleo za nje, ambazo mwaka jana, 2024, hazikuwepo. Ongezeko hili litakuwa na tija ikiwa fedha hizo zitapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiongezea Bajeti Wizara hii kwani kwa kufanya hivi kutawezesha kazi ya utafiti wa viwanda na masoko kufanyika. Nchi zilizoendelea zimepata mafanikio hayo kwa sababu ya kuwekeza kwenye viwanda vya ndani. Hata hivyo, kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuiongezea fedha Wizara hii, ili iweze kufikia mapinduzi ya nne ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu – 44) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Upatikanaji wa Fedha na Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. Pamoja na kuiongezea fedha Wizara hii, Kamati inaona upo umuhimu wa kuendelea kuiongezea fedha zaidi, ili iweze kufikia mapinduzi ya viwanda yanayokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Iendelee kuongeza Bajeti ya Wizara hii kila mwaka ili kufanikisha mapinduzi ya viwanda; na

(b) Ihakikishe kuwa, bajeti inayoidhinishwa na Bunge kila mwaka inatolewa yote kwa wakati ili shughuli zilizopangwa zitekelezeke kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Magadi Soda, Engaruka. Serikali imetoa shilingi bilioni 6.3 kwa ajili ya mradi huu, ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.9 zimetumika kulipa fidia kwa watakaopisha mradi. Kamati inashauri kuwa, Serikali ikamilishe taratibu za kupata mwekezaji wa kutekeleza mradi huu haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mradi huu ukikamilika utasaidia upatikanaji wa malighafi ya chuma na makaa ya mawe yatakayotumika kwenye viwanda vya nondo, simenti, mabati, umeme na chuma hapa nchini. Pamoja na majadiliano yaliyofanyika, Kamati inaishauri

Serikali utekelezaji wake uanze haraka iwezekanavyo, ili kuokoa gharama za kuagiza malighafi kutoka nje ya nchi. Aidha, Kamati inashauri mpango mkakati wa utekelezaji wa mradi huu uandaliwe na utekelezwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto ya Lumbesa; pamoja na Serikali kujitahidi kutoa elimu kuhusu lumbesa katika maeneo mbalimbali nchini, bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wameendelea kutumia mfumo huu unaowanyonya wakulima na pia, unaikosesha Serikali mapato. Kamati inashauri kuwa:-

(a) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi sehemu mbalimbali kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi (mizani) na athari inayopatikana kwa kutumia lumbesa; na

(b) Serikali itoe mwongozo maalum utakaotumiwa na Halmashauri zote nchini ili kuondoa mkanganyiko kuhusu matumizi ya mizani. Aidha, izitake Halmashauri zote zisimamie kwa uwiano ambao utaleta manufaa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani; pamoja na mfumo kufanikiwa kuongeza mazao 14 ghalani, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Kuvisimamia Vyama vya Msingi na kuhakikisha vinawalipa Wakulima fedha zao kwa wakati mara taratibu za mauzo zinapokamilika ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima baina ya Serikali na wananchi;

(b) Kuhakikisha kuwa tozo na ushuru wa mazao ya wakulima zinapunguzwa kwa kuwa baadhi zinasababisha kero. Marekebisho ya tozo na ushuru yanayolenga kuwapunguzia gharama wakulima yatawapa imani zaidi wakulima hao kwa Serikali yao na hivyo kujitokeza kuuza bidhaa zao kwenye masoko halali badala ya kutumia mifumo isiyo rasmi; na

(c) Kuendelea kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wadau wa mfumo wa stakabadhi ghalani kuhusu kutumia mfumo rasmi kuuza na kununua bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upatikanaji wa Umeme wa Uhakika Viwandani; Kukosekana kwa umeme wa uhakika kunaongeza gharama za uzalishaji na hivyo kuwa mzigo kwa mtumiaji wa mwisho. Kamati inaishauri Serikali kuwa, Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ukikamilika, umeme uingizwe kwenye Gridi ya Taifa na usambazwe viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishaji wananchi katika Ujenzi wa Masoko. Suala la ushirikishaji wananchi katika miradi mbalimbali, ikiwemo ujenzi wa masoko kuanzia hatua za awali za utambuzi wa maeneo, ni jambo muhimu kwa kuwa linasaidia kujenga kwenye maeneo yenye uhitaji. Kamati inashauri kuwa, Serikali itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa masoko na wananchi wa maeneo husika washirikishwe kuanzia hatua za awali za utambuzi wa ujenzi huo, ili kuepuka kupeleka masoko kwenye maeneo ambayo hayahitajiki na/au ambayo jiografia yake haifikiki kirahisi na hivyo, kukwamisha shughuli za ufanyaji wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Bidhaa Zisizokidhi Viwango; hivi sasa lipo wimbi la uingizwaji wa bidhaa ambazo hazikidhi viwango; kwa mfano, nondo ambazo siyo bora, vifaa vya umeme ambavyo havidumu, mabomba mabovu, mabati yanayotoboka ndani ya muda mfupi tangu kuezekwa. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha udhibiti wa bidhaa katika soko, pamoja na kuwachukulia hatua wanaobainika kukiuka taratibu za ubora wa bidhaa na kusababisha hasara au madhara kwa wateja. Hatua hii pia, itaenda kulinda wawekezaji wazawa wa ndani ambao wana viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa hizi tena kwa ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufufuaji wa Viwanda Vilivyofungwa; viwanda vingi hivisasa havifanyi kazi ipasavyo na vingine vimefungwa kwa sababu mbalimbali kutokana na kukosekana kwa malighafi ya kutosha. Vipo vilivyofungwa

kufuatia ubinafsishaji na pia, vipo vilivyofungwa baada ya waliomilikishwa kushindwa kuviendesha. Viwanda hivi vikifanya kazi ya uzalishaji vitaongeza pato la Taifa, ajira kwa vijana na upatikanaji wa bidhaa kwenye masoko yetu. Kamati inashauri kwamba, viwanda vilivyofungwa vifufuliwe vifanye kazi na ambavyo wamiliki wameshindwa kuviendesha wanyang'anywe wapewe watu wenye uwezo wa kuviendesha waviendeshe, tuweze kuifikia Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uboreshaji wa Mazingira ya Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga); biashara inafanyika vizuri endapo mazingira yanakuwa nadhifu na yenye kuvutia. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwatengenezea mazingira rafiki Machinga na Mama Ntilie, ili wafanye kazi katika mazingira mazuri zaidi. Vilevile, *TBS* itoe elimu inayolenga kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo wanaofanya biashara ya bidhaa zinazofungashwa, ili watumie vifungashio vyenye ubora, vipimo na viwango vinavyokubalika na vinavyolinda afya za watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho; naomba kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, kwa kuliongoza Bunge hili la Kumi na Mbili kwa umahiri. Binafsi namwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe uhai mrefu, afya na siha njema, maana nina uhakika kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atarudi kuwa Mbunge na Spika wetu wa Bunge la Kumi na Tatu. Kama Mabunge yote duniani yamemwamini na sifa hiyo inarudi kwa Wanambeya, sidhani kama Wanambeya wako tayari kutia doa ama kuipoteza sifa hiyo. Kizuri kinajiuza na kibaya kinajitembeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kipekee kukupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. Kule Ilala wanakuita mzee jaza ujazwe na kwa taarifa nilizozipokea asubuhi hii, kwa Mkoa wa Dar es salaam, kwa wale Wabunge ambao wanatajwatajwa kurudi, basi wewe ni namba moja. Nakupongeza wewe na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuongoza Vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili kwa umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwanza kwa kuniamini na kunichagua kuwa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. Kamati hii imesheheni Wajumbe wazito wenye sifa kubwa sana, wamo wafanyabiashara wakubwa, wamo Madaktari, wamo Maprofesa, wamo Mawaziri Wastaafu, yupo *First Lady* Mstaafu, yumo Spika Mstaafu, wamo hadi wa-*NEC* wa chama, hakika Wajumbe wameniheshimisha sana. Pia, kwa ushirikiano walioutoa kwa Mwenyekiti na kwangu, kipindi chote cha uongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila kipekee kwa kushirikiana kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha Maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa kweli, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu, kama wanarudi, basi Mwenyezi Mungu awarudishe tena kwa ushindi wa kishindo. Kutokana na ufinyu wa muda, sitaweza kuwataja kwa majina, lakini niombe majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Wenyeviti wa Kamati hii niliofanya nao kazi. Kwanza, Mheshimiwa Kihenzile, ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Uchukuzi, namshukuru sana na ninamtakia kila la kheri. Kipekee, Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mzungu wa roho, Mbunge wa Njombe Mjini na Mwenyekiti wa Bunge, kwa malezi, miongozo yake kwangu na kunipa fursa ya kukua kwa kunituma kumwakilisha kwenye majukumu mazito. Namwombea kila la kheri na nina uhakika hana mpinzani kule Njombe Mjini, ila anakamilisha tu utaratibu na atarudi Bungeni na kwa Baraka za Mwenyezi Mungu namtabiria makubwa zaidi hapo mbele. Ahsante sana *Chairman.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuiamini Wizara hii muhimu ya Viwanda na Biashara kwa kupeleka fedha na kutatua changamoto za muda mrefu ambazo zimeongelewa sana na Bunge lako Tukufu; mabadiliko ya Sera na Sheria, upunguzwaji wa

tozo na ushuru sumbufu. Leo hii Mradi wa Engaruka ulioshindikana zaidi ya miaka 20 kauweza na uko hatua nzuri sana, Mradi wa Liganga na Mchuchuma kauweza na upo hatua nzuri sana. Kwenye sekta hii kwa kweli, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hana deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru Dkt. Suleiman Said Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara. Siku anaapishwa aliambiwa asikae Wizarani na kweli tunamwona *field* na mitaani, hadi Kariakoo anaenda mpaka usiku. Tangu aingie kwenye Wizara hii mabadiliko chanya ni makubwa mno, *"mwenye macho haambiwi tazama",* tunamtakia kila la kheri huko Kisarawe arudi na azidi kuaminiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa ushirikiano anaotupa kamati. Tunamtakia kila la kheri jimboni kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana nimpongeze Dkt. Hashil Abdallah, Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara. Huyu ni bingwa wa mahusiano na amekuwa *shock absorber* wa Wizara hii. Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Suleiman Hassan Serera, kijana msomi na makini, Mungu amjalie kesho njema sana, pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara, bila kuwasahau Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa kuwa mstari wa mbele kutoa ushirikiano kwa Kamati muda wote walipohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard. Pamoja na ugeni wake, lakini ameonesha umahiri mkubwa kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu iliyopangiwa kwa ufanisi. Vilevile niwapongeze sana Makatibu na msaidizi wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Kilimo na Mifugo kwa namna wanavyotusaidia Wajumbe wa Kamati hii kwa bidii, nidhamu ya hali ya juu na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia, kuishukuru sana familia yangu, lakini kipekee kumwombea dua na kumshukuru mama yangu mzazi, Hadyat Yasira Ditopile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, siyo kwa umuhimu; ninaomba kukishukuru sana chama changu, CCM, pamoja na wanawake wa Mkoa wa Dodoma, kupitia Jumuiya ya UWT kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuwa mtumishi wao kwenye Bunge hili Tukufu la Kumi na Mbili. Kipekee, niishukuru Kamati ya Siasa ya CCM, Wilaya ya Kondoa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Kondoa Mji kwa kunipa fursa ya kuwatumikia wananchi wa Kondoa, kama Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM, Wilaya Kondoa na Wananchi wa Halmashauri ya Kondoa Mji, kama Diwani, ndani ya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Kondoa Mji. Nawaomba sana waendelee kunitumia kwani nia, ari, dhamira na nguvu ya kuendelea kuwatumia bado ninayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu – 44, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU – 44 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara unatokana na Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6 (1)(a) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inahusu uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 25 Machi, 2025 Kamati ilichambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taarifa hii inatokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa inahusu maeneo yafuatayo: -

i. Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

ii. Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara kufikia Mwezi Februari, 2025;

iii. Uzingatiaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

iv. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 1.4 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayozungumzia Muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya **Kwanza** inahusu maelezo ya jumla kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya **Pili** inaelezea Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(c) Sehemu ya **Tatu** inatoa Maoni, Ushauri wa Kamati na Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, naliomba Bunge lako Tukufu lifuatilie mtiririko wa Taarifa hii ili kupata msingi wa ushauri unaotolewa na Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya Taarifa inazungumzia msingi wa ushauri wa Kamati uliotokana na Hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mara baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na:-

i. Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

ii. Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

iii. Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; na

iv. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

#### 2.2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa **Shilingi 29,784,516,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia

Mwezi Februari, 2025, Wizara ilipokea **shilingi 11,399,772,122.02,** sawa na **asilimia 38.27** tu ya Fedha zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo siyo wa kuridhisha, kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilipokea **asilimia 38.27** tu ya fedha zilizoidhinishwa. Hali hiyo imeathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuliomba Bunge, kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha kwa Wizara hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha kukamilisha utekelezaji wa Miradi iliyopangwa kabla mwaka wa fedha kumalizika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayoitaka Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Geita, Tabora na Dodoma kuanzia tarehe 11 hadi 20 Machi, 2025. Katika ziara hiyo Kamati iliutembelea Mradi wa Kuongeza Wigo wa Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (WRRB – Shinyanga) – Mradi Na. 6260 uliopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

### 2.2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Mradi

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini uwepo wa mafanikio na changamoto katika Mradi uliotembelewa na ilitoa ushauri ufuatao: -

#### (i) Baadhi ya wadau kutouelewa vizuri mfumo

**Mheshimiwa Spika,** wapo baadhi ya wadau ambao hawana uelewa mzuri wa mfumo wa stakabadhi za ghala ambao hueneza taarifa zisizo sahihi kwa wakulima na kuwatia hofu. Hali hii inasababisha mwitikio mdogo wa wananchi kwani baadhi yao

hawapeleki mazao kwenye vituo na hivyo kuchangia zoezi hili kudorora.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwa, elimu kuhusu matumizi sahihi ya mfumo huu, manufaa yanayopatikana na hasara inayoweza kupatikana kwa kuuza nje ya mfumo iendelee kutolewa na kuwafikia wananchi wengi zaidi hapa nchini.

**(ii) Upungufu wa Mazao**

**Mheshimiwa Spika,** lipo tatizo la upungufu wa mazao katika maeneo ambapo mfumo umepelekwa kutokana na baadhi ya wakulima na wadau kuyaficha, kwa mfano zao la choroko kwa lengo la kuuza nje ya mfumo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa wakulima wahamasishwe kupeleka mazao ambayo yapo kwenye mfumo ili kuleta ufanisi wa mfumo, kuiwezesha Serikali kupata kodi yake na mkulima kutopunjwa.

**(iii) Ufinyu wa Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** kiwango cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Bodi kupitia bajeti ya Serikali ni kidogo kulingana na kazi kubwa iliyopo. Aidha, mapato ya ndani hayatoshelezi utekelezaji wa shughuli zilizopo kutokana na sehemu ndogo ya maeneo yanayotekeleza mfumo nchini na idadi ya mazao yanayouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuiongezea fedha Bodi iweze kutanua wigo wa shughuli zake na kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa kuwapa elimu kuhusu matumizi ya mfumo, uhifadhi na masoko; na

**(iv) Uchache wa maghala**

**Mheshimiwa Spika,** maghala ya kuhifadhia chakula yaliyounganishwa na mfumo yapo mbali na wakulima na katika maeneo machache. Suala hili linasababisha mazao mengi

kutoingia kwenye mfumo kutokana na umbali na gharama ambazo wakulima wanaziingia kusafirisha mazao hadi kuyafikisha kwenye maghala.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kujenga maghala ya kutosha karibu zaidi na wakulima na yawe yanafikika nyakati zote.

### 2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Viwanda na Biashara - **Fungu 44** iliidhinishiwa **Shilingi 81,115,206,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.


**Mheshimiwa Spika,** Waziri aliwasilisha mbele ya Kamati ufafanuzi kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama **Kielelelezo Na. 1** kinavyoonesha.

**Kielelezo Na. 1: Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa 2024/2025 na kiasi cha fedha zilizopatikana kufikia Mwezi Februari, 2025 - Fungu 44**

| **Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2024/2025 - Fungu 44** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Kilichoidhinishwa** | **Kilichopokelewa** | **Asilimia** |
| Mishahara | 68,352,946,000.00 | 42,146,880,470.49 | 61.66 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 12,762,260,000.00 | 7,688,634,332.01 | 60.25 |
| **Jumla** | **81,115,206,000.00** | **49,835,514,802.50** | **61.44** |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 29,784,516,000.00 | 11,399,772,122.02 | 38.27 |
| Fedha za Nje | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **29,784,516,000.00** | **11,399,772,122.02** | **38.27** |
| **Jumla Kuu** | **110,899,722,000.00** | **61,235,286,924.52** | **55.22** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara*

**Kielelezo Na. 2: Ufafanuzi kuhusu upatikanaji wa fedha kwa asilimia-Fungu 44**




**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ulikuwa pungufu kwa **asilimia 4.56** ya lengo, ambapo Wizara ilipokea **asilimia 61.44** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha unachangia kukwamisha baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka husika wa Fedha.

### 2.2.5 Hali ya Uzingatiaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Fungu 44 yaliyotolewa wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa Maagizo kumi yaliyolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu yake. Taarifa ya Mtoa Hoja ilionesha kuwa, Serikali imetekeleza maagizo ya Kamati na baadhi yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Maagizo yaliyotekelezwa ni pamoja na:-

(a) Suala la uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji ili Sekta Binafsi iendelee kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vitakavyoongeza ajira, uongezaji wa thamani na mapato ya fedha za kigeni na kuhakikisha wananchi wote ambao maeneo yao yanatwaliwa wanalipwa fidia stahiki haraka kulingana na thamani ya ardhi yao. Kamati ilielezwa kuwa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI), imetekeleza Programu mbalimbali kwa lengo la kuboresha taratibu za udhibiti. Aidha, Wizara imetekeleza Programu hizi ili kuepuka mwingiliano wa majukumu, kukuza uwazi na kuanzisha muundo wa ufuatialiaji na tathmini wenye ufanisi katika kukuza biashara na uwekezaji nchini kwa kufanya yafuatayo:-

i. Kukamilika kwa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2023;

ii. Kufanya mapitio ya sheria zilizobainika kukwamisha au kuchelewesha uanzishwaji na uendeshaji wa uwekezaji na biashara ambapo Serikali imepitia na kurekebisha Sheria na Kanuni 61 kati ya 88 zilizoibuliwa wakati wa kufanya tathmini; na

iii. Kufanya mapitio ya tozo ambazo ni kero na kupendekeza kupunguza au kufutwa ambapo Serikali imefuta au kupunguza tozo, ada na faini mbalimbali zipatazo 383 zilizobainishwa kuwa kero katika ufanyaji biashara.

(b) Kamati ilielezwa kuwa Azimio kuhusu upatikanaji wa Masoko kwa Bidhaa zinazozalishwa nchini limetekelezwa kwa kuendesha warsha na ziara mbalimbali za kutambua na kuwezesha wafanyabiashara kufikia masoko ya nje ya nchi katika Mkoa wa Tanga na Kilimanjaro. Lengo kuu lilikuwa ni kutambua wafanyabiashara na kutoa mafunzo kuhusu

namna ya kutumia vyema fursa zinazotokana na majadiliano ya uwili, kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia Maagizo iliyopewa katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuipatia Wizara hii fedha ilizoidhinishiwa na Bunge kwa wakati ili iweze kukamilisha utekelezaji wa maagizo iliyopewa kwa kuwa baadhi ya maagizo hayajatekelezwa kutokana na kukosekana kwa fedha.

### 2.3 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 25 Machi, 2025 Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara – Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi huo ulilenga kujihakikishia iwapo Mpango na Makadirio haya umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Viwanda na Biashara - **Fungu 44** inaomba kutengewa jumla ya **Shilingi 135,788,232,000**. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 93,900,697,000** sawa na **asilimia 69.15** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 41,887,535,000** sawa na **asilimia 30.85** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. (**Kielelezo Namba 3).**

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Fedha zilizoombwa kwa Mwaka 2024/2025 na Fedha zinazoombwa 2025/2026**

| **Ulinganisho wa Bajeti Fungu 44 kwa Mwaka 2024/2025 na 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **2024/2025** | **2025/2026** | **Ongezeko/ Pungufu** | **Asilimia** |
| Mishahara | 68,352,946,000 | 75,819,380,000 | 7,466,434,000 | 11 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 12,762,260,000 | 18,081,317,000 | 5,319,057,000 | 42 |
| **Jumla Ndogo 1** | **81,115,206,000** | **93,900,697,000** | 12,785,491,000 | 16 |
| Maendeleo (Ndani) | 29,784,516,000 | 27,870,710,000 | -1,913,806,000 | -6 |
| Maendeleo (Nje) | 0 | 14,016,825,000 | 14,016,825,000 | 100 |
| **Jumla Ndogo 2** | **29,784,516,000** | 41,887,535,000 | 12,103,019,000 | 41 |
| **Jumla ya ulinganifu** | **110,899,722,000** | **135,788,232,000** | **24,888,510,000** | **22** |

*CHANZO:* ***Randama ya Wizara - Fungu 44***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Makadirio ya Bajeti yameongezeka kwa **asilimia 22,** ongezeko zaidi lipo kwenye fedha za Maendeleo za Nje ambazo mwaka jana hazikuwepo. Ongezeko hili litakuwa na tija ikiwa fedha hizo zitapatikana kwa wakati;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiongezea Bajeti Wizara hii kwani kwa kufanya hivi kutawezesha kazi ya utafiti wa viwanda na masoko kufanyika. Nchi zilizoendelea zimepata mafanikio hayo kwa sababu ya kuwekeza kwenye viwanda vya ndani. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee

kuiongezea fedha Wizara hii ili iweze kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali: -

#### (a) Upatikanaji wa Fedha na Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuiongezea fedha Wizara hii, Kamati inaona upo umuhimu wa kuendelea kuiongezea fedha zaidi ili iweze kufikia Mapinduzi ya Viwanda yanayokusudiwa. Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i. Iendelee kuongeza Bajeti ya Wizara hii kila mwaka ili kufanikisha Mapinduzi ya Viwanda; na

ii. Ihakikishe kuwa bajeti inayoidhinishwa na Bunge kila mwaka inatolewa yote kwa wakati ili shughuli zilizopangwa zitekelezeke kikamilifu.

#### (b) Mradi wa Magadi Soda, Engaruka

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetoa **Shilingi 6,304,672,959** kwa ajili ya Mradi huu; ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 5,895,890,224** zimetumika kulipa fidia kwa watakaopisha Mradi. Kamati inashauri kuwa, Serikali ikamilishe taratibu za kupata mwekezaji wa kutekeleza Mradi huu haraka.

### (c) Mradi wa Liganga na Mchuchuma

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ukikamilika utasaidia upatikanaji wa malighafi ya chuma na makaa ya mawe yatakayotumika kwenye viwanda vya nondo, sementi, mabati, umeme na chuma hapa nchini. Pamoja na majadiliano yaliyofanyika, Kamati inaishauri Serikali utekelezaji wake uanze haraka iwezekanavyo ili kuokoa gharama za kuagiza malighafi kutoka nje ya nchi. Aidha, Kamati inashauri Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Mradi huu uandaliwe na utekelezwe ipasavyo.

### (d) Changamoto ya Lumbesa

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kujitahidi kutoa elimu kuhusu lumbesa katika maeneo mbalimbali nchini, bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wameendelea kutumia mfumo huu unaowanyonya wakulima na pia unaikosesha Serikali mapato. Kamati inashauri kuwa:-

i. Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi sehemu mbalimbali kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi (mizani) na athari inayopatikana kwa kutumia lumbesa; na

ii. Serikali itoe mwongozo maalum utakaotumiwa na Halmashauri zote nchini ili kuondoa mkanganyiko kuhusu matumizi ya mizani. Aidha, izitake Halmashauri zote zisimamie kwa uwiano ambao utaleta manufaa kwa wakulima.

### (e) Mfumo wa Stakabadhi Ghalani

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mfumo kufanikiwa kuongeza mazao 14 ghalani, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i. Kuvisimamia Vyama vya Msingi na kuhakikisha vinawalipa Wakulima fedha zao kwa wakati mara taratibu za mauzo zinapokamilika ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima baina ya Serikali na Wananchi;

ii. Kuhakikisha kuwa tozo na ushuru wa mazao ya Wakulima zinapunguzwa kwa kuwa baadhi zinasababisha kero. Marekebisho ya tozo na ushuru yanayolenga kuwapunguzia gharama wakulima yatawapa imani zaidi wakulima hao kwa Serikali yao na hivyo kujitokeza kuuza bidhaa zao kwenye masoko halali badala ya kutumia mifumo isiyo rasmi; na

iii. Kuendelea kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wadau wa mfumo wa stakabadhi ghalani kuhusu kutumia mfumo rasmi kuuza na kununua bidhaa mbalimbali.

**(f) Upatikanaji wa Umeme wa Uhakika Viwandani**

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa umeme wa uhakika kunaongeza gharama za uzalishaji na hivyo kuwa mzigo kwa mtumiaji wa mwisho. Kamati inaishauri Serikali kuwa, Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ukikamilika, umeme uingizwe kwenye Gridi ya Taifa na usambazwe viwandani.

**(g) Ushirikishaji Wananchi katika Ujenzi wa Masoko**

**Mheshimiwa Spika,** suala la ushirikishaji wananchi katika Miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa masoko kuanzia hatua za awali za utambuzi wa maeneo ni jambo muhimu kwa kuwa linasaidia kujenga kwenye maeneo yenye uhitaji. Kamati inashauri kuwa, Serikali itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa masoko na wananchi wa maeneo husika washirikishwe kuanzia hatua za awali za utambuzi na ujenzi huo ili kuepuka kupeleka masoko kwenye maeneo ambayo hayahitajiki na au ambayo jiografia yake haifikiki kirahisi na hivyo kukwamisha shughuli za ufanyaji wa biashara.

**(h) Udhibiti wa bidhaa zisizokidhi viwango**

**Mheshimiwa Spika,** hivi sasa lipo wimbi la uingizwaji wa bidhaa ambazo hazikidhi viwango; kwa mfano, nondo ambazo siyo bora, vifaa vya umeme ambavyo havidumu, mabomba mabovu, mabati yanayotoboka ndani ya muda mfupi tangu kuezekwa.

Kamati inaishauri Serikali kuimarisha udhibiti wa bidhaa katika soko pamoja na kuwachukulia hatua wanaobainika kukiuka taratibu za ubora wa bidhaa na kusababisha hasara au madhara kwa wateja.

**(i) Ufufuaji wa Viwanda Vilivyofungwa**

**Mheshimiwa Spika,** viwanda vingi hivi sasa havifanyi kazi ipasavyo na vingine vimefungwa kwa sababu mbalimbali kutokana na kukosekana kwa malighafi ya kutosha. Vipo vilivyofungwa kufuatia ubinafsishaji na pia vipo vilivyofungwa baada ya waliomilikishwa kushindwa kuviendesha. Viwanda hivi vikifanya kazi ya uzalishaji vitaongeza pato la Taifa, ajira kwa vijana na upatikanaji wa bidhaa kwenye masoko yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba, viwanda vilivyofungwa vifufuliwe vifanye kazi na ambavyo wamiliki wameshindwa kuviendesha wanyang'anywe wapewe watu wenye uwezo wa kuviendesha waviendeshe tuweze kufikia Tanzania ya Viwanda.

**(j) Uboreshaji wa Mazingira ya Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga)**

**Mheshimiwa Spika,** biashara inafanyika vizuri endapo mazingira yanakuwa nadhifu na yenye kuvutia. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwatengenezea mazingira rafiki Machinga na Mama Ntilie ili wafanye kazi katika mazingira mazuri zaidi. Vilevile, TBS itoe elimu inayolenga kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo wanaofanya biashara ya bidhaa zinazofungashwa ili watumie vifungashio vyenye ubora, vipimo na viwango vinavyokubalika na vinavyolinda afya za watumiaji.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri. Vilevile,

naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Naibu Spika - Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wa Bunge, kwa kukusaidia kuongoza Vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili kwa umahiri.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha Maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyoonekana hapa chini na kwa ruhusa yako, naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Deodatus Mwanyika, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Francis Isaack Mtinga, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Atupele Alfred Mwakibete, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Salim Hassan Turky Toufiq, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Pauline Phillip Gekul, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Dkt. Suleiman Said Jafo, Mb - Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe, Mb - Naibu Waziri, Dkt. Hashil Twaibu Abdallah - Katibu Mkuu, pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa kuwa mstari wa mbele kutoa ushirikiano kwa Kamati muda wote walipohitajika.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu iliyopangiwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya **Wizara ya Viwanda na Biashara** – **Fungu 44** kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

14 Mei, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kusoma kwa weledi mkubwa sana hongera sana. Waheshimiwa tunaanza uchangiaji tunaanza na Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa ajiandae Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi na moja kwa moja niungane na Wajumbe wenzangu wa Kamati kupongeza kazi kubwa ambayo inafanywa na Waziri wetu na wasaidizi wake, Katibu Mkuu pia na Msaidizi wake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika Kamati yetu lakini katika Wizara yenu ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nitaanza kukupongeza Mheshimiwa Waziri nadhani kwenye hotuba yetu tume-*acknowledge* kazi kubwa ambayo umeifanya hasa kutkeleza malekezo ya Mheshimiwa Rais kwenye habari ya wafanyabiashara wa kigeni ambao sasa imefikia *stage* wanafanya mpaka shughuli zetu za umachinga na vitu vingine kama hivyo. Umefanya kazi kubwa tuzidi kukupongeza, lakini tuombe na vyombo vingine ambavyo vinahusika na utoaji wa vibali vikuunge mkono. Usifanye kazi wewe halafu wengine wakaendelea kutoa vibali. Kwa hiyo washirikiane ili kazi hii kubwa na maono haya ambayo Mheshimiwa Rais ameyaona kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wadogo yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi tunawalinda hawa wafanyabiashara wadogo Kamati yako ilitembelea baadhi ya viwanda na tukawa tunajaribu kujiridhisha. Tumeenda kwenye viwanda vinavyotengeneza mabati, lakini tumetembelea viwanda vinavyotengeneza nondo halikadhalika na bidhaa zingine za chuma. Tuombe labda kupitia Bunge hili na kupitia nafasi ambayo tumeipata kwa mfano tulitembelea kiwanda cha Lovia kule Mkuranga Mheshimiwa Waziri atakuwa anakumbuka. Kiwanda kile *capacity* yake ni kubwa, kipindi cha nyuma hata uagizaji wa nondo kwenye tenda tulikuwa tunaweka *imported*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipindi walikuwa wanasema nondo zinaitwa *imported* badala ya kusema *BS500* kwa sababu ndiyo tulikuwa tunatumia kwa sehemu kubwa, lakini tumeona juzi nondo hizi zenye kiwango cha juu za *BS500* zinazalishwa pale Mkuranga na zimetumika kwenye miradi mingi sana hapa nchini. Kwa hiyo sasa sehemu mojawapo ya kuzidi kulinda uwekezaji huu mkubwa wa ndani tumeona hata *ALAF* sasa wameanza kufanya uzalishaji wa mabati yale ya rangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uweze kulinda viwanda hivi lazima tunagalie *tariff* za uingizaji hapa pale ambapo tunahisi kwamba wanaoingiza walikuwa wanapata *incentive* kubwa hatubani *importation* kwa sababu ni soko huria, lakini lazima tujaribu kuwa na *control* kwa sababu nchi nyingi ili kulinda uwekezaji wa ndani wamejaribu kuweka *control* hasa *tariffs*

kwamba anayeingiza basi Serikali ipate zaidi kwa sababu kodi zitaongezeka tuangalie *tariff* ya kodi ili sasa wakati huo bidhaa zinaingizwa halikadhalika nchi iweze kunufaika na ukusanyaji wa kodi, lakini pia ilinde ajira za wazawa wa hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nimekuwepo nacho. Jana pia katika semina nadhani tulikuwa tumeongelea suala la uwekezaji katika vinywaji. Tumeona wawekezaji wakubwa wazawa. Kwa mfano kuna Kiwanda hiki cha *Mult Super Brand* cha Babati yule ni mzawa tena bahati nzuri ni mzawa wa kutoka Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, hata sisi tumekuwa na shida, tuna ndizi zinaharibika huko na tuna vitu vingine. Nimsihi kupitia hapa; uwekezaji alioufanya Babati ni mkubwa na ni uwekezaji wa mfano. Huyu bilionea Mulokozi, ndugu yangu, aone jinsi ya kuokoa ndizi ambazo zinaoza shambani huko. Kama anaweza akatengeneza *spirit* inayotumia ndizi tunazozilima nyumbani huko itatusaidia na tutaweza kwenda sawa; ili kipindi uwekezaji huu unashamirisha watu wengine hali kadhalika asiisahau ardhi ya nyumbani Kagera, aje atuwekee uwekezaji mwingine tuweze kuuza ndizi zetu pale na hatimaye soko na uchumi wa Wanakagera uzidi kunyanyuka kama ulivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yako pia ilifanya ziara mwaka jana. Mwaka jana tulitembelea taasisi yetu ya uhandisi na mitambo, taasisi ya *TEMDO*. Tulitembelea *TEMDO* Arusha; kwa kweli kazi zinazofanywa pale *TEMDO* ni kazi kubwa sana. Tumekwenda pale tukaona hawa watu wameanzisha mpaka kitengo maalum cha kutengeneza vifaa tiba; na sasa wana wateja, wanauzia baadhi ya maeneo kama Bugando na hata Uhuru *Hospital* wameshanunua, hospitali zetu za jeshi na hospitali za polisi wote wananunua pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, *one of the complaints* ambazo tulikutana nazo pale, ambapo ninaomba Serikali isikilize na itupatie *solution;* tumekuwa tunashindwa kuelewa, ni kwa nini *sometimes* Serikali inaanzisha vitu halafu yenyewe haiwezi kujiunga mkono? Tunashangaa, kwa sababu mnunuzi na *supplier*

mkubwa vifaa vya Serikali ni *MSD,* lakini mpaka sasa *MSD* hachukui vifaa pale. Hivi kweli kwa *stage* tuliyopo leo hata ile *stand* ya kutundikia *drip* nayo inaagizwa nje; hivi *are Waheshimiwa serious* kweli, lakini hawa watu wanazalisha pale!

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo ambacho kimekuwepo *MSD* anawaambia hawana uwezo wa kuzalisha. Nikikupa *order* kubwa utashindwa ku-*supply* kwa wakati; lakini *order* kubwa ni *accumulation,* kwa sababu *no one is consuming it in a single day*. Kama unaagiza vitanda, vitanda vile havilaliwi siku moja vyote kwa pamoja; kama unaagiza baadhi ya viti, havikaliwi siku moja vyote kwa pamoja. Hata kule tunapoagiza wanakupatia *minimum order* na wanakupatia *time of production,* lakini sisi hapa tunataka tukihitaji kitu unatoa siku 60 *delivery,* hujui *material* na yapo, hujui chochote, mtu akishindwa unamwambia ninakwenda kuagiza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nje siku zilezile utakuja ukute ule mzigo umeuleta hapa baada ya miezi sita. Sote ni mashahidi, tunatoka majimboni huko, *order* nyingi zimekuwa zinalala *MSD* vituo vyetu vya afya na hospitali zetu wakati mwingine *order* inachukua mpaka mwaka mzima; lakini ukimwambia aagize *TEMDO* anasema haiwezekani. Sasa tulione hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kizuri zaidi ni kwamba makubaliano kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya yalikwishasainiwa, lakini *TEMDO* wenyewe wana makubaliano na *MSD,* lakini hiki kitu kinakuwa hakifanyiki. Sasa, tunaposema kwamba tukuze soko la ndani na tuondoe *importation* maana yake tutunze fedha za kigeni. Maelekezo ya *BOT* yako *very clear,* kwamba hata leo manunuzi ya ndani wenyewe tumekataza tusilipe kwa kutumia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama *BOT* wanaweka *control,* lakini mmojawapo bado anataka pesa zizidi kwenda nje uchumi wetu wanaurudisha nyuma. Hii ni kodi ya Watanzania, kwa nini zisitumike za ndani ambazo zikasaidia kutengeneza ajira

za vijana wetu, itasaidia kutengeneza mazingira mengine mazuri ili iweze kutusaidia. Kwa hiyo, tulione hilo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** ... ili liweze kutusaidia. Kwa kumalizia; tulipotembelea *TEMDO* tulikuta pale wanazalisha kiwanda kidogo cha sukari; kiwanda cha kutengeneza mpaka tani 20 kwa siku; lakini nilivyokuwa na-*calculate* pale zile *calculation* zao nimejaribu kufuatilia hapa nikawa ninasoma *document,* kile kiwanda wanachosema ni cha tani 20 kwa siku ukijaribu kuangalia *input* na *output* yake kwa siku ukifanya masaa 48 kinaweza kikaenda mpaka tani...

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Ezra ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwani ni dakika ngapi? Hazijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Hoja?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara halafu Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, tulikuwa naye TAMISEMI akiwa Waziri na mimi nikiwa Naibu Waziri mchapa kazi kwelikweli. Mimi nimeshindwa tu kumweka kuwa na wale akina mama wengi. Hilo ninalifikiria na kulitafakari, lakini kwa maana ya kuchapa kazi na kukimbia kimbia usiku na mchana. Hilo tuko pamoja mzee wangu, Mheshimiwa Jafo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nichangie kwenye viwanda na biashara kama Mwalimu na Mwalimu ni popote. Mheshimiwa Waziri atanisikiliza na baadaye kuna maeneo nitahitaji majibu hata kama siyo ya moja kwa moja. Kwenye kizazi tulichonacho ni lazima tuwa-*impact* wananchi wetu na hasa vijana, *analytical skills;* namna ya kuweza kufakari mambo, kuyafanyia kazi na kujipangia malengo ya muda mrefu, muda mfupi na malengo ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wachache wanaweza wakafanikiwa sana, ambapo tunaita ni *extra ordinary cases,* akapata manufaa hapa katikati na maisha yakaenda; lakini ni lazima vijana waandaliwe kutafuta maisha kwa muda mrefu zaidi na wawe wabobezi katika fani mbalimbali. Ndiyo maana leo tunazungumzia kupitia sayansi, mambo ya *e-commerce, e-medicine, wireless phones, paperless* na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi karibuni kumekuwa na mjadala wa mambo ya *betting;* na mimi ni Mwalimu wa hesabu. Jana nililazimika kwenda kwenye duka la vitabu pale nikaenda nikatafuta niangalie kama *topic* zimebadilika mwaka huu. Kwenye *syllabus* mpya kitabu cha *form four* ile *topic* ipo na nikaangalia *form three* na pia nikaangalia na kitabu cha *Chemistry form two, three,* na *four* nikagundua kwamba Wizara ya Elimu wamefanya kazi nzuri sana kwa kutafsiri. Kabla ya kila *topic* mnaeleza malengo ya hii *topic* baadaye yatakuwa ni yapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimeona watu wamejadili. Siwalaumu sana wanaojadili habari ya mambo ya *betting;* lakini kwa lugha rahisi *betting* ni *gambling* na *gambling* ni *probability* na *probability* ni *predictions.* Sasa lugha rahisi tu wale wanaofanya *betting* halafu tunalaumu, nitakuja sasa kwa Mheshimiwa Waziri, lakini niseme kwamba hili somo ni *topic* ipo kidato cha nne na mimi nimeisoma *form four,* nimeisoma *advance,* inaenda mpaka vyuo vikuu na kuna watu wamebobea katika eneo hilo. Kwa hiyo, unapoona maeneo ya Casino, *Premier League* na ligi mbalimbali siyo bahati mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hivi; kwa lugha rahisi tu, ukiwa unataka kubeti; tuchukulie mpira wa Tanzania, Simba na Yanga wanacheza hiyo tarehe inayokuja wapeleke timu. Sasa matokeo ni matatu tu. *Expected* au *possible outcomes* ni tatu tu. tunaweza kushinda, kupoteza au kutoa *draw;* ni *win, lose or draw;* ni matatu. Hizo ndizo *possible outcomes.* Sasa tutafute uwezekano wa Simba kuishinda Yanga. Ukifanya hivyo maana yake uwezekano wa kushinda ni mmoja tu; hakuna kushinda mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama una *total events possible outcomes, probability* ya kupata ushindi ya *win* ni namba ile ya ushindi ambayo ni moja *out of* zile tatu maana yake ni moja ya tatu. Ukikadiria ni 0.33, kwenye asilimia ni 33.3%. Sasa, kama mtu anaenda kubeti kwenye mpira halafu anakwambia kwamba Simba ikiishinda Yanga utachukua mke wake, anajua ana 33%, kwanza lazima atapoteza. Sasa huyu hatuwezi kumlaumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa Waziri, kwa hiyo, hoja ya *betting* si kosa na wala dini haijasema kwamba ukiwa hukufanya *betting* ni dhambi. Kilichopo hapa kwenye nchi hii ni biashara holela. Nchi za wenzetu wanachukua mashine za kubeti na hiyo michezo kwenye *Casino* ambako ni eneo ambalo unapaswa kwenda kama akili yako umepanga kwenda. Wanaangalia umri wa watu ambao wanahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini hapa Tanzania Serikali imeruhusu mashine za kubeti za Kichina zimepachikwa shule za msingi zilipo, sekondari, Machinga *Complex* na kila mahali. Hata mtoto akitumwa kwenda kununua chumvi ana shilingi mia mbili anaenda kucheza kamari pale, halafu tunaanza kulaumiana. Mheshimiwa Waziri hii kazi anaiweza. Waende wakapitie sheria zetu; kwamba ni leseni gani ya biashara ya ku-*bet* walitoa kwa wale wahusika? Waliwaambia wafanye biashara katika maeneo gani? Wamehimiza ni umri gani wanapaswa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya ku-*bet* ninasema hili ni jambo la kitaalam na ni jambo la kisayansi. Wenzetu wamechungulia fursa wameitumia tusilalamike. Twende kwenye sheria zetu tuwa-*squeeze* kwenye hizi sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninalotaka nilizungumze ni kwenye habari ya viwanda. Nimepitia *topic* hizi mbalimbali hapa ambazo zinaeleza; yaani iko *very proper*. Ukienda kwenye *topic* zetu hizi unazungumzia habari ya viwanda; ukienda kwenye *functions* imeelezwa kwenye mambo ya *demand and terms,* yamezungumzwa mambo ya *statistics,* mambo ya sensa na *circle and sphere*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua wenzetu walioendelea hata mpira, kwenye *sports* hauchezwichezwi tu; unakadiria kwamba lile goli ni mita ngapi unapiga ili uweze kufunga. Ndiyo maana sisi hapa unafanya kazi ya kwenda kwa mganga wa kienyeji. Wenzako wanafanya *structural* ya mipira wewe unafanya kwa mganga wa kienyeji kwenda kuvunja nazi kwa sababu watu hawasomi haya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimshauri Mheshimiwa Waziri, kwa maana ya *topic* ambazo zimeandaliwa na Wizara ya Elimu na kazi wanayoifanya ninataka nimwombe, hakuna namna ambavyo ataendelea na viwanda hivi kama tutaacha shule ya sayansi na tukaacha watu wafanye mambo kiholela na kienyeji. Waende waka-*connect topic* zile ambazo watu wanafundishwa ili twende katika uzalishaji *material* mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninazungumza habari ya vitu ambavyo Mheshimiwa Ezra amezungumza; lakini niulize, kwa mfano zile dawa za kusafisha vyoo tu wako akinamama wanatengeneza hapa Tanzania; amewapandisha akinamama wangapi, amewapa mikopo wangapi wachache ili badala ya kuagiza dawa za chooni kutoka nje tufanye hapahapa? Unataka viwanda vya sabuni, akinamama wanasambaza sabuni mitaani *locally.* Amewawezesha akinamama wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mtindo hapa; kwa mfano sasa hivi nchi kama India kuna kazi ambazo wame-*limit* kuna watu wanakuja kufanya biashara hapa; kimsingi siyo wafanyabiashara, ni machinga. Kazi ambazo Watanzania wameweza kufanya wanafanya wao. Kwa nini wasiweke

masharti? Apimwe, kwamba ana mtaji kweli? Anataka kufanya biashara gani na atalipa kodi kiasi gani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** *(Aliendelea kuzungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:...** Mheshimiwa Waitara...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** *(Aliendelea kuzungumza bila kutumia kipazasauti)*

**NAIBU SPIPA:** Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Waitara. Hii imekuwa ni tabia yako mara nyingi sana sasa. Unachukua muda wa mchangiaji mwingine. Kaa chini na karatasi yako.

Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, wajiandae Mheshimiwa Kenneth Nollo na Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Ninaomba ulinde muda wangu kwa sababu Mheshimiwa Waitara alichukua muda wangu. Kwanza kabisa, nianze kwa kukupongeza wewe uliye hapo mbele na Mheshimiwa Spika. Ninampongeza Waziri na Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara. Ninampongeza sana Dkt. Samia kwa kazi nzuri anayoifanya na kuweza kutenga fedha kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia mradi ambao umechukua muda mrefu lakini sasa hivi umepata muafaka mzuri sana. Siyo mradi mwingine, ni Mradi wa Mchuchuma Liganga. Mradi wa Mchuchuma Liganga kama tulivyoeleza, kwamba sasa hivi wako kwenye maongezi na maongezi yanakwenda vizuri. Kuja kufikia mwaka ujao bila shaka tutakuwa tumekwishafikia muafaka. Ninashauri kuwa jinsi walivyopanga uende hivyo hivyo kusudi utekelezaji wake uweze

kutekelezeka. Mradi huu ni mradi muhimu sana kwa upande wa vyuma kwa sababu tuna uhitaji sana kwenye viwanda vyetu. Kwa hiyo, ninaamini kuwa utatekelezwa kadri ulivyopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusiana na kufufua viwanda ambavyo havifanyi kazi. Ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kukiona Kiwanda cha Mang'ula ambacho kiko Morogoro Wilaya ya Kilombero na ambacho kinafanyiwa kazi na hivi karibuni kitafufuliwa na kitaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hivyo, Mkoa wetu wa Morogoro ulikuwa ni mkoa wa viwanda, lakini viwanda vingi havifanyi kazi, ikiwemo kiwanda cha *MOPROCO* ambacho ni cha mafuta ya kula, kiwanda cha ngozi ambacho kilikuwa kinatengeneza viatu na mikoba ya akinamama. Sasa hivi havifanyi kazi. Viwanda vingine katika mikoa mingine kama viwanda vya Tanga navyo vingi havifanyi kazi. Kwa hiyo, licha ya kuanzisha viwanda vingi, ninapongeza, Mheshimiwa Rais ameanzisha viwanda vingi nchini kwetu. Kwa mfano, Mkoa wa Pwani wanaongoza. Hata hivyo, viwanda hivi ambavyo havifanyi kazi vifufuliwe, hasa kwa Mkoa wa Morogoro, kwa sababu viwanda hivi vinasaidia katika kutoa ajira hususani kwa vijana pamoja na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwa taasisi nyingine ambazo ni *TEMDO, KAMATEC* na *SIDO;* hizi ni taasisi nzuri ambazo zinafanya kazi nzuri sana chini ya Wizara. Kwa mfano *KAMATEC;* inafanya kazi ambayo inatengeneza vifaa vingi vya kilimo kama vifaa vya kubangua korosho, matrekta madogo ambayo ni ya bei rahisi. Kwa hiyo, ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge watembelee *KAMATEC, TEMDO* na taasisi hizi zote zilizo chini ya viwanda; zinafanya kazi vizuri. Kwa mfano tumesema kuwa *TEMDO* wamefikia hatua wanatengeneza majokofu ya kusitiri miili ya wapendwa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazishukuru taasisi na Wizara ambazo zimeanza kutumia vifaa hivi, lakini wengine bado. Ninaomba sana wale ambao hawajaanza kuvitumia waanze

kuvitumia; na tuendelee kutangaza kusudi waweze kutumia hivi vifaa ambavyo tunavitengeneza hapa ndani. Kwa mfano *KMTC* inatengeneza vifaa vingi vizuri ambavyo vinaweza kutumika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninashauri Mheshimiwa Waziri pamoja na wananchi wote wa Tanzania waweze kuzitembelea taasisi hizi ili waone zinafanya nini na hivyo tuweze kuvilinda viwanda vyetu vya ndani na tuweze kutumia vitu vyetu vya ndani. Tuache kupenda kutumia vitu vya nje na huku tunaacha vitu vetu vya ndani. Wamefikia hatua wanatengeneza na vitanda vya wagonjwa. Kwa hiyo, tutumie hivi vya ndani ili tuweze kuokoa na kuona nchi yetu inakwenda vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa nchi yetu sasa hivi umekua na unaendelea vizuri kutokana na mambo haya ambayo tunayatengeneza ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu stakabadhi ghalani. Huu ni mfumo mzuri sana ambao umeenea na unatumika sasa hivi. Mfumo huu uko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Huu mfumo ukitumika vizuri utamsaidia muuzaji na yule anayenunua ili kuona soko zuri, la kupanga bei na ambalo linaweza kumnufaisha yeye pamoja na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu, ushauri wangu, elimu iweze kuwafikia wananchi kujua kuwa mfumo huu ni mzuri na ambao unaweza kutumika kwa mazao mengi kuliko kutumika kwa mazao machache. Kwa hiyo, ninaomba sana tuweze kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya mbolea. Kama tunavyojua, sasa hivi wakulima wanatumia sana mbolea. Sasa hivi Tanzania tuna viwanda vya mbolea, lakini viwanda vikubwa ni Minjingu pamoja na *Intracome* ambacho kiko hapa Dodoma. kwa hiyo, ninaomba sana hivi viwanda vidogo vidogo viweze kuboreshwa ili viweze kuzalisha mbolea kwa wingi na hivyo tuweze kuzalisha mazao kwa wingi ambayo yatatumika kwenye viwanda na hivyo tunaweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* linafanya vizuri sana. Tunaomba sana tuliangalie shirika letu la *TBS* kwa sababu limepata ithibati mbalimbali na linatambulika kimataifa na hapa nchini Tanzania; linafanya vizuri sana shirika hili. Hata hivyo wana tatizo moja tu ambapo watumishi siyo wengi. Wapate watumishi wa kutosha ili waweze kufanya kazi hii vizuri. Ninashauri waendelee na utafiti ili kuweza kuleta...

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vyetu vya sukari. Ninafurahi sana kusema kuwa hadi kufikia mwaka kesho; kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, tunaweza tukaepukana kuagiza sukari kutoka nje kwa sababu tuna viwanda vya Mtibwa na Kilombero na ambavyo vyote viko Morogoro; Kiwanda cha Kagera ambacho kiko huko huko, Kiwanda cha *TPC* Manyara pamoja na viwanda vingine ambavyo vipo na vinazalisha takribani tani 638 *point,* kadhaa pamoja na kuzalisha ajira. Kadri tunavyopanua uzalishaji, kadri tunavyopanua mashamba ndivyo tunavyopata sukari nyingi ya kutosha na ajira za kutosha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili hiyo.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, wajiandae Mheshimiwa JaneJelly na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Hivyo, nianze kwa kuunga mkono hoja ya hii Bajeti ya Wizara ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue *tune* aliyomaliza nayo ndugu yangu Mheshimiwa Waitara. Duniani kote na mfumo wa dunia yetu viwanda ni utu, viwanda ni *power* ya nchi, viwanda ni

kila kitu kwa maana ya usalama wa nchi na kwa maana ya *influence* ya nchi ni viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona duniani hapa kati ya mvutano uliopo katika Taifa la Marekani na China; Taifa la Marekani kupandisha zile *tariff* katika kuleta bidhaa katika nchi yake, kwamba, zikija bidhaa kutoka nchi zingine *tariff* yake inakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara siyo dini, biashara ni vita ambayo haionekani, lakini sisi tumekuwa na huruma, tumekuwa na ulegevu, tumekuwa na muhali wa kuona aibu kusema hiki hapana huwezi ukaingiza vitu vya hovyo hovyo katika nchi yetu. Kwanza, niseme hata kitendo cha Waziri kwenda Kariakoo kusukumana kufanya *ambush* lile si jambo zuri katika heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke sheria, tuweke utaratibu, hawa wanaofika Kariakoo wamepitaje kwenye mipaka yetu? Wameingizaje vitu vyao? Ni ulegevu wa sheria. Kwa hiyo, kama ndugu yangu Mheshimiwa Waitara alivyopata moto hata mimi ninashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kariakoo wale ndugu zetu wa China, tunavyoenda vile kuwafukuza vile ni ulegevu wa sheria zetu, hatujaweka sheria sawasawa ndio maana wanauza bidhaa pale. Mtawatoa wa China watakuja watu wengine kwa sababu hakuna *room* ya sheria. Hata ile kuunda kamati ya uchunguzi, unachunguza nini? Wanatakiwa wale watoke kwa sababu hujaweka sheria madhubuti ya kuzuia jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kusema nchi yetu kwanza sisi wenyewe tunaoneana wivu, akitoka ndugu yangu Edgar Chilatenga kwenda kutafuta mkopo wa bilioni sita, saba, nane, tisa, kumi hachukuliwi kama ni mtu *serious.* Akija mtu mwingine ana ngozi tu tofauti na ya kwake anapewa kwanza na kahawa ndio aanze kusikilizwa na hii ni ndani ya nchi yetu.

Wanakuja wageni hawana fedha, fedha za biashara wanapatia hapa, kwa hiyo tatizo tunalo sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unataka viwanda vyetu vishindane na wageni wanaokuja kuanzisha viwanda hapa. Sisi hapa mkopo wa kuanzisha kiwanda ni kama mkopo ambavyo mtu anaanzisha biashara hizi za kawaida za uchuuzi, sasa atapata lini faida? Wenzetu riba 6% sisi hapa tunashindwa nini? Tumeona juzi Wizara ya Kilimo imeanzisha Benki ya Ushirika na lengo lake ni kuinua wakulima, kwa nini tusianzishe mikopo ya mashine kwa ajili ya watu wanaotaka kuanzisha viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiona katika nchi yetu hatuna utashi kwanza wa kulinda biashara zetu, wa kulinda wafanyabiashara wanaoanzisha viwanda vilevile na kufanya *incubation* kwa ujumla katika sekta ya viwanda. Nondo zinaagizwa kutoka nje zinaingia Tanzania, lakini tuna viwanda vikubwa vya nondo na wanafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Lodhia kwa mfano *steels* wale wamefika katika kiwango ambacho Serikali hata ingewekeza kule kwa maana ya kuwapa *incentive* za kutosha vilevile kuweza kupanua zaidi ili waweze kufanya vizuri. Kwa hiyo, lipo tatizo la kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuseme zipo biashara za kufanya wageni, zipo biashara za kufanya wazawa. Kama ambavyo tumefanya kwenye Sheria ya Manunuzi tumeongeza wigo wa *50 billion* kuanzia mradi huo kwamba hawezi kufanya mgeni…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa ndugu yangu mchangiaji kwamba maneno yake yanagusa mioyo ya wafanyabiashara wengi wa nchi hii na uhalisia ni kwamba, mfanyabiashara wa Tanzania sasa hivi hawezi kukua hata kidogo kwa sababu hata hao waliokuja kwa dhamana ya kwamba, ni wawekezaji hawalipi kodi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hiyo siyo taarifa sasa unachangia.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa yake ni ukweli wa dhati kabisa, ni lazima tuweke kwamba hizi biashara wazawa watafanya na hizi biashara kweli mgeni aje afanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka *incentives* mtu anaanzisha kiwanda cha kuzalisha mkate ni mgeni, mnampa mpaka *incentives*. Kwanza kuna viwanda ambavyo mgeni hatakiwi kufikiriwa hata kuvifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu isione aibu, ukienda nchi zingine hata nchi kubwa kama tunayoisema ambayo tunawafukuza watu wake pale Kariakoo kwenye mahoteli hairuhusiwi mtu mwingine wa kawaida afanye kwenye biashara za *research* na kwenye viwanda vikubwa hairuhusiwi. Sasa kwa nini sisi tunaona aibu? Kwa nini tunaoneana muhali? Tuna hii diplomasia kwamba ukisema hiki itaonekana kwamba umeleta ubaguzi.

**MHE. DKT. RITTA A. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Jafo ni lazima tuwe na uchungu na ni lazima tuwe wazalendo katika kulinda viwanda vyetu, katika kukuza Sekta ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ntale, jiandae Mheshimiwa Mpina.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ni Ntate siyo Ntale.

**NAIBU SPIKA:** Unasema?

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane…

**NAIBU SPIKA:** Ulikuwa unasemaje?

**MHE. JANEJELLY NTALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Ntate siyo Ntale.

**NAIBU SPIKA:** Basi kaa chini siyo wewe. *(Kicheko)*

Haya endelea. *(Kicheko)*

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Niungane na wote waliompongeza Mheshimiwa Jaffo kwa kazi unayofanya na Naibu Waziri wake. Nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda Daktari Hashil, sisi kwa watumishi tumemwona ni simba ambaye haogopi kuachia madaraka yake. Pale alipoamua Miradi mizito ya Liganga, Lichuchuma, Engaruka na kadhalika kwamba, aisimamie Daktari Suleiman Serera kuwa Mwenyekiti wa majadiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze na Liganga na Mchuchuma. Liganga na Mchuchuma ni jambo ambalo lilikuwa haliwezekani lakini Awamu ya Sita limewezekana. Kwenye Liganga na Mchuchuma tumelipa fidia ya bilioni 15.4 kwa wananchi, lakini majadiliano yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Liganga na Mchuchuma ina faida nyingi kwa Tanzania. Leo hii ukiangalia Kilimanjaro *tools machine* tumeweka bilioni 4.7 hiki ni kiwanda ambacho tumekifufua, lakini kinategemea chuma itakayotoka Liganga na Mchuchuma. Kwa

hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri majadiliano yafike mwisho na leo hii ikimpendeza basi atuambie huu mradi unaanza kazi lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Maganga Matitu, mradi huu ni wa chuma ghafi ambao niwapongeze sana mkataba wake umesainiwa na unaenda kuanza kazi sasa, sasa tuone ni lini inaanza. Kuna Engaruka *Soda* hii hapa nilikuwa ninateta na Profesa ameanza akauacha, lakini sasa tunaona unaenda tayari tumeshalipa wananchi bilioni 5.8 na inafurahisha sana, lakini na wawekezaji wako tayari kuweka dola milioni 700 sawasawa na trilioni 1.5 hela za Kitanzania. Sasa tuombe na wenyewe uende uanze kazi mara moja. Hata hivyo, haya mambo yote yanafanyika chini ya *NDC* shirika ambalo ni kongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa fedha hizi wameweza kuzisimamia kwa kuanzia 2020/2021 kwa miaka miwili mfululizo wamepata hati safi ya *CAG*. Kwa hiyo, hili siyo shirika la kulibeza ni shirika ambalo tunatakiwa tulitie moyo ni shirika ambalo tunatakiwa tulipe rasilimali watu na kulipa rasilimali fedha liendelee kufanya kazi bila kuunganishwa na shirika lolote lingine lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee biashara kwa wageni. Mchangiaji aliyepita amesema Mheshimiwa Dkt. Jafo, kwa nini ameenda Kariakoo? Tumeona Naibu Waziri Mkuu, Daktari Biteko akiwa kwenye sherehe za kumsimika Askofu. Alimwambia Baba Askofu ukienda kwa upole wasipokuelewa badilika. Kwa hiyo, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Jafo, alibadilika, ameenda kuwaonyesha yanayofanyika hayataki, ameenda kuwaonyesha wanaosimamia sheria wajue sasa kwamba, Waziri msimamia sera hataki vinavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niseme lazima wasimamia sheria, wasimamie sheria barabara. Kama sera imelegalega ya uwekezaji basi twende tukairejeshe ibadilishwe isimamie kabisa. Hatuwezi mtu anaingia kama mwekezaji, lakini anabadilika anakuwa machinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watoto wetu wa Kitanzania watafanya nini? Hapa Mheshimiwa Dkt. Jafo aendelea kusimama usikatishwe tamaa, usivunjwe moyo, endelee kuvamia na masoko mengine, avamie Dodoma, avamie Mbeya, hiyo ndiyo kazi yake, avamie! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa wafanyabiashara wa Kitanzania, kwa kweli sijui tumekosea wapi. Nikitaka kufanya biashara sijaanza nimeshapigiwa kodi, nimeshaambiwa nilipe zile kodi, lakini akija mwingine kuja kuwekeza kutoka nje anapewa *grace period* ya *tax holding. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ameandaliwa mazingira ambayo siwezi kushindana naye. Niombe tu na kwenye Wizara ya Fedha kwenye bajeti nitachangia sana. Niombe na sisi Watanzania tuwekewe hizo *incentive* kama tunataka kweli Watanzania tuonekane tunafanya biashara, tuonekane tunawekeza hiki wanachopewa wenzetu, tupewe sisi kwanza, *charity starts at home*. Tukipewa sisi ndio waje wapewe na hao wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga hoja mkono na ninakubaliana na taarifa ya Kamati yote. Ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mpina, wajiandae Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Mkinga.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na wenzangu waliopongeza sana Serikali juu ya kukamilisha ulipaji wa fidia katika Mradi mkubwa wa Mchuchuma na Liganga na kwamba, mazungumzo ya awali yamekwishafanyika na kuna makubaliano ambayo tayari kama mgawanyo wa hisa na muundo wa uwekezaji, kiwango cha mtaji na muda wa uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya hapa ni moja, ametuletea *blank* amesema tu maneno hajatueleza huo mgawanyo wa hisa utakuwaje? Viwango vya mtaji

kinachotakiwa kitakuwaje? Muundo wa uwekezaji utakuwaje, na muda wa uwekezaji utakuwaje? Kwa sababu kwa mujibu wa *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act No. 5 of 2017* na *TEITA Act* ya Mwaka 2015 zinakataza majadiliano ya siri katika miradi ya uziduaji. Kwa hiyo, hayo mambo yanatakiwa kuwekwa wazi ili wote twende kwa pamoja hasa katika mradi mkubwa kama huu ambao tuliutegemea kwa muda katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kuangalia mwenendo wa biashara na uwekezaji nchini tunavyoenda. Taarifa ya mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia dirisha la huduma ya uwekezaji la pamoja *(one stop facilitation center)* inaonyesha kuwa miradi 240 ilisajiliwa yenye thamani ya dola 4387.17 sawa na shilingi trilioni 11.4 miradi 94 ni ya wageni, miradi 89 ilikuwa ni ya Watanzania na 57 ya wabia. Kwa hiyo, wageni walikuwa wanaongoza katika miradi iliyowekezwa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023/2024 inaonyesha maombi kwenye tume ya kugawa ardhi kwa ajili ya uwekezaji yalikuwa maombi 191 ambao kati ya maombi hayo 130 sawa na 68% yalikuwa ni kampuni za wageni na maombi 61 sawa na 32% yalikuwa ni ya Watanzania. Kwa hiyo, na hapo inaonyesha kwamba, wageni wanaongoza katika kupewa ardhi ya uwekezaji, wanaongoza katika uwekezaji kuliko wazawa na Watanzania waliomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wawekezaji wa ndani wanalalamika kunyang'anywa kazi na wageni. Mfano, mfanyabiashara maarufu hapa nchini Mbunge Mstaafu wa Igunga Mheshimiwa Rostam Aziz alinukuliwa na vyombo vya habari akilalamika wazawa kunyimwa kazi nyingi na kupewa wageni huku akionya kuwa hakuna nchi duniani iliyowahi kupata maendeleo kwa kutegemea wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ilitegemewa iwe ni rufaa ya huzuni na mateso ya wafanyabiashara, iwe rufaa ya huzuni na mateso ya wakulima na wafugaji wa nchi, lakini badala yake imekuwa ni kinyume. Imekuwa ni wizara ambayo ikihalalisha

kuuawa kwa biashara nchini, imekuwa ni wizara ambayo imekuwa ikihalalisha kuuwa uwekezaji nchini, ajira na hata kodi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Wizara ambayo inabariki na kusaidia na kuwa wakala hata wa bidhaa za kutoka nje ya nchi kupata soko hapa nchini, huku mazao na bidhaa za nchi zikiwa zinauwawa bei zake kila siku na kuruhusu mambo ambayo hayaruhusiwi kwa mujibu wa sheria kuingia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu hapa wamezungumza. Leo tunazungumzia suala uingizaji wa bidhaa zisizokuwa na ubora na kamati imezungumza suala la uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora. Ni kwa nini bidhaa zisizo na ubora ziingie nchini wakati tuna mfumo uliokamilika ndani ya nchi? Mamlaka zinazohusika na *enforcement* ya kuzuia bidhaa zisizo na ubora ziko wapi mpaka bidhaa ziingie hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza mpaka nondo zinaingia nchini, nondo zikiingia nchini ambazo hazina ubora maana yake tunaenda kujenga madaraja ambayo hayana ubora, tunakwenda kujenga zahanati ambazo hazina ubora, tunakwenda kujenga vitu ambavyo havina ubora na vyenye madhara makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna viwanda bubu vingapi vinavyotengeneza? Wananchi wetu wanakunywa vinywaji ambavyo havina ubora kutoka kwenye viwanda hivyo, mamlaka zinazohusika zipo, Wizara inayohusika ipo. Leo hii kupitia Wizara hii hii waliondoa suala la kigezo cha *COC* kwa kigezo cha kuingiza bidhaa nchini; Cheti hicho kuwa ni kigezo muhimu cha kuingiza bidhaa hapa nchini ikaondolewa hapa tukakataa leo bidhaa feki zimejaa kila kona kila mtu anakiri leo, Kamati imekiri bidhaa zisizokuwa na ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vifaa vya umeme ambavyo havina ubora, wananchi wetu wanalipukiwa kule. Leo hii wananchi wanapata ajali kila leo kununua matairi ambayo hayana ubora, vifaa vya magari ambavyo havina ubora halafu

tuna Waziri ambaye anasimamia Wizara hii, tuna taasisi ambazo zinasimamia Wizara hii wote wapo na wanakuja leo mbele yetu kuja kuomba pesa tena ili wakaruhusu watu wetu waendelee kupata ajali waendelee kupata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba kama Wizara hii haina uwezo wa kusimamia majukumu iliyopewa na kama labda ilianzishwa kimakosa basi Bunge hili liazimie hii Wizara ifutwe kati ya Wizara za Serikali kwa sababu haina sababu za kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama ni udhaifu wa watendaji basi tukaweke hiyo historia kwa sababu hatuwezi kuwa na karoti tu kila siku twende na kwenye *stick approach*. Haiwezekani Bunge hili linashiriki kupitisha leo bajeti ya watu kwenda kuwaidhinishia bilioni 93, halafu wanachoenda kufanya ni kwenda kuangusha uchumi wa nchi, kuharibu afya ya Watanzania, kuua kodi za Watanzania na kuua uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kama imeshashindikana leo *TBS* wapo, *FCC* wapo, *BRELA* wapo, mifumo mingine yote ya udhibiti ipo mbona mambo mengine tukitaka kuyadhibiti tunaweza…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa ninaongeza muda mpaka tutakapomaliza, endelea.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** …hapa kunakuwa na changamoto gani ambayo inatufanya tushindwe kusimamia na kama mtu anashindwa kusimamia sheria zinampa uwezo wa kusimamia, ameshindwa kusimamia, kuna mambo mawili. Moja, ni mdhaifu katika usimamizi; jambo la pili, kama siyo mdhaifu kwenye usimamizi, maana yake biashara zinazofanyika za hovyo ni za kwake au ana ubia na hao watu ambao wanazifanya biashara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jambo hili lilivyo nyeti ambalo linagusa afya za Watanzania, linagusa uchumi wa Watanzania, linagusa kodi za Watanzania na hatuwezi kukutana hapa kila siku

tena kuzungumza hayo hayo, kama siyo Wizara kuvunjwa basi kama ni utendaji mbovu wa watu walioshindwa kusimamia, Waziri na watu wake ikiwezekana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina ahsante.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja tu nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kuna wachangiaji wengine kama 18 hapa, ninakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliongia Bungeni muda mchache uliopita.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Kapt. Mstaafu Mheshimiwa John Chiligati, Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda cha Mbolea. Mheshimiwa Chiligati aliwahi kuwa Mbunge, aliwahi kuwa Waziri humu ndani, hongera sana kwa majukumu mengine mapya. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Twaha Malate, kaka wa Mheshimiwa Waziri, hapa nikiona ndugu wa Waziri huwa ninapata hofu daah, hapa kuna…! *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Jafo, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Mameneja wa Mikoa kutoka Shirika la Maendeleo na Viwanda vidogo *(SIDO)* *(Makofi)*

Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Pwani. Wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Mwinshehe Mlao, Viongozi wa Dini kutoka Mkoa wa Pwani, wawekezaji Sekta ya Viwanda, viongozi kutoka Sekta Binafsi, wadau kutoka Benki ya *NMB,* Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania, viongozi wanawake wafanyabiashara na watumishi kutoka Ofisi ya Mbunge. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Mtinga na Mheshimiwa Gallos wajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Wizara nyeti sana ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Jafo, ninampongeza sana kwa kazi yake anayoifanya nzuri, Naibu wake Mheshimiwa Kigahe anafanya kazi nzuri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kuongoza watu tunatunga na sheria mbalimbali duniani hakuna siku maendeleo yanaweza kukoma. Nchini Marekani kuna vyombo vingi sana vya usalama lakini bado leo watu wanauawa hawajaweza kusema Serikali ijiuzulu. Kwa hiyo, kazi ya kulinda watu na kutunga sheria ipo pale pale, kitu cha msingi ni kuendelea kushughulikia makosa ambayo yanaonekana, lakini huwezi kusema kila kosa likionekana tufukuze watu, tutamaliza watu duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na wengi wamempongeza sana hapa, kiukweli leo tunapozungumza Liganga na Mchuchuma na ndoto yetu leo inasema tunakwenda kusaini mikataba, kiukweli tumpongeze sana mama kiukweli, ni moja ya mikataba ambayo imezungumzwa hata na mtangulizi wake aliyetoka kama ni moja ya mikataba michafu iliyokuwepo, kazi ya kusahihisha mikataba ilikuwa kubwa sana, tumpongeze mama kwa kazi nzuri aliyofanya kwa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna pia kiwanda kinaitwa *KMTC,* kiwanda cha mashine kile cha Kilimanjaro, kimekuwepo miaka 30 kimefungwa na kinatengeneza vipuri vya nchi yetu, Mama amekifufua kinafanyakazi, tunamshukuru sana mama kwa kazi hiyo ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi kuna Mradi huu wa Engaruka wa Magadi Soda umekuwa ni shida kuuanzisha, lakini

sasa watu wamelipwa bilioni sita na pointi waweze kuhama hicho kiwanda kiendelee kuwepo, tunamshukuru sana mama kwa namna hiyo ambayo anafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine humu ndani hawajui tunapozungumza bilioni bilioni hawajui kama ni bilioni kiasi gani? Ukipewa bilioni moja una nyumba ya kulala nzuri na una mashamba na wewe una umri mdogo, bilioni moja ukiila kwa elfu hamsini na senti sabini na tano unaweza kukaa nayo miaka hamsini na nne. Kama wewe ni mwanamahesabu chukua siku za mwaka mzima ni siku 365 zidisha mara miaka 54 ambayo unaishi, chukua bilioni moja gawia hiyo kitu uone, ina bilioni elfu hamsini kwa kila siku na unaishi miaka hamsini na nne. Kwa hiyo, tunaposema bilioni sita, bilioni kumi na tano watu wasifikirie mchezo hapa, *billions* hii ni kazi ngumu hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda sasa wa kulinda viwanda vyetu vya ndani ni muda, muda umefika tusione aibu, tusione aibu kulinda viwanda vyetu vya ndani. Hivi kuna haja gani ya kuwa viwanda vingi tunavyo halafu sasa hatuvilindi? Sasa hivi kweli utaruhusu bidhaa kutoka nje kwa bei nafuu na huku kwetu tunatengeneza viwanda kwa malighafi hii ambayo ina bei juu, hatuwezi kushindanisha viwanda hivi, *is unfair*, tunafanyaje kazi hiyo? Kwa hiyo, imefika muda sasa tulinde viwanda vyetu vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, *Lodhia Industries* ni kiwanda kikubwa sana hapa Tanzania, kinatoa mabati bora, kinatoa nondo bora, kinatoa plastiki bora, sasa viwanda kama vile tukiviacha vinakufa, tuna viwanda vya vinywaji ambacho kipo Babati cha *MATI Industrials* cha mabilioni. Sasa ikiwa bilionea huyo ukimwacha aende hivi bila kulinda mali yake itakuwa kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bilionea wa Kihaya wa Babati lazima tulinde viwanda vyake, kuna watu wanazungumza mambo ya vinywaji, pombe nini, jamani duniani sigara zipo zinalindwa, hapa leo tuna makorokoro yanaitwa kamari yale ya Wachina yanaenda mpaka vijijini hatuyalindi, sasa tuendelee

kuwalinda. Suala ni kuelimisha watu unakunywaje pombe, unavutaje sigara na mambo mengine, kwa sababu ulevi ni wa kila kitu, tunaomba kwamba hawa watu walindwe, wafanyabiasha maarufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja ya wageni wa Kariakoo. Sasa kuna mtu amesema wageni wale Waziri anaenda kufanya nini pale? Sasa mimi nitawashangaa kwani Mahakimu wanafanya nini kwenye Mahakama? Mahakimu Mahakamani wanafanya kazi gani? Si ni kulinda sheria? Waziri kama kuna jambo amelitengeneza la Serikali linalinda watu na limevunjwa ataenda kuona na anachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyokwenda akaona vile akachukua hatua. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Jafo, hoja yangu ni moja ile ripoti ya Profesa imesema hivi, Wizara ya Biashara iangalie sera ya biashara ya kutenganisha, kuangalia biashara ya wageni, Sera ya 2003, toleo la 2023, itenganishe biashara ya wageni na biashara ya wenyeji, iwe wazi tuweze kujua biashara ya wageni ni ipi na biashara ya wenyeji ni ipi? Lingine wamesema ile Kariakoo iwe Kanda Maalum na waitengenezee maeneo maalum ya kuishia tujue na *data base* yake tujue wafanyabiashara wakubwa na wafanyabiashara wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo kazi Mheshimiwa Jafo ameifanya? Maana yake sijaiona hapa! Kwa hiyo ndiyo ninaomba lakini vinginevyo ninamshukuru sana, anafanya kazi nzuri sana tuendelee kupambana, hakuna Waziri anayemaliza matatizo yake hakuna, kama yupo atuambie, nilikuwa kwenye Wizara fulani nikamaliza matatizo. Kwa sababu tuliona kuna biashara zingine zilikuwa zinafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, tulipokuwa na Waziri wa Uvuvi kipindi hicho, alikuwa anakamata makokoro anafunga, anafanya nini alikuwa anachukua hatua, hatukusema sheria zimevunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtinga, Mheshimiwa Gallos na Mheshimiwa Kamonga wajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hii Wizara muhimu sana ambayo tunaitegemea kuweza kutimiza ajira milioni nane ambazo Chama chetu kilitaka zipatikane, hapa ndipo mahali tunapopategemea sana baada ya kilimo, kupata ajira rasmi ni kwenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia mambo mawili tu makubwa. Kwanza ni umuhimu wa kulinda viwanda vyetu vya ndani lakini pili bajeti kwenye Wizara. Ninampongeza sana Waziri na timu yake, timu hii iko vizuri na inafanya kazi vizuri sana. Katibu Mkuu ameipanga vizuri sana safu yake na ni mtu ambaye ni rahimu, anafikika, watumishi wake wanampenda nasi Kamati tunampenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtetee pia Mkurugenzi wa *TBS,* Ashura Katunzi anafanya kazi kwa weledi ni mwanadada ambaye kwa kweli Rais amepatia sana kumchagua pale. Tatizo liliopo ni kwamba nchi yetu ni kubwa na ina mipaka mingi na mipaka mingi ni *porous* na hivyo sasa udhibiti wa vifaa kuingia nchini unakuwa ni mgumu sana, lakini ugumu unaongeza zaidi kwa kuinyima bajeti Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ni ndogo, iko mipaka leo katika nchi yetu haina hata *scanner* kwa sababu ya bajeti ndogo. Kwa hiyo, kuna bidhaa zinapita haziwi *scanned* kwenye mipaka, sasa hapo unategemea nini? Tutalindaje viwanda vyetu vya ndani iwapo vitu vinaingia na hata vile vinavyoingia kwenye njia sahihi baadhi ya vifaa bado havina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe sana Mama yangu, Rais wangu mpendwa kwa jinsi ambavyo amekuwa akiachia bajeti kwenye Wizara nyingi na mafanikio tunayaona

hapa na kwenye bajeti hii kuna kila sababu ya kuongeza fedha kwenye hii Wizara, uzuri watumishi waliopo sasa ni wachapakazi ambao wanafanya vizuri, wakipata fedha mambo haya yatakuwa mazuri sana. Hilo lilikuwa ni sehemu ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kulinda viwanda kama ambavyo wenzangu wamesema, viwanda vyetu vya ndani haswa kwenye *material* ambayo Watanzania wanayatumia kwa wingi bati, nondo, mabomba kwa sababu suala la kujenga nyumba ni suala la lazima kila Mtanzania aliyezaliwa katika nchi hii anawaza kwamba afike mahali ajenge nyumba, aishi na familia yake na kujenga nyumba ni jambo la mara moja. Katika kujenga nyumba *material* makubwa ni bati, nondo, sasa haya *material* baadhi ya wenzetu ambao tumewapa uhuru wa kuja kuuza bidhaa kwenye nchi yetu wanatuletea bidhaa feki sana. Bati la rangi ukiiezeka baada ya miezi mitatu linakuwa na rangi ambayo hata huijui ni rangi gani kutokana na jinsi ambavyo ulinunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni hatukuwa na hivi viwanda ambavyo vilikuwa na uzalishaji, tulikuwa hatuna namna ilikuwa inabidi tu-*import* tu, lakini kwa sasa viwanda vyetu vya ndani vinazalisha *excess* zaidi ya kiwango. Mabati ya rangi tunayotakiwa kutumia kwa nchi yetu ni tani 130,000, leo viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha tani 260,000, kwa hiyo tuna ziada ya tani 130,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama isingekuwa masuala ya kuangalia angalia sijui nini tungepiga *ban* kabisa tusiingize bidhaa, kwa sababu ya biashara huria basi tuweke kodi ambayo itasababisha wale wanaotaka kuleta wasiwe na hamu kubwa ya kuleta. Kama una hamu sana ya kuja kuuza Tanzania basi pale mpakani atuchangie fedha ya kutosha. Kwa hiyo niiombe Serikali, niiombe sana Wizara ya Fedha kwenye *Finance Bill* na mambo yanayokuja tuongeze kodi kwenye bidhaa za bati, bidhaa za nondo, bidhaa za mabomba kwa sababu viwanda vyetu vina uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa macho yangu nimekwenda pale Lodhia *Industries* kuanzia chuma kinapoanza kusafishwa, kinayeyushwa, nondo inatengenezwa mpaka inatoka ni kifaa unakiona kabisa kwa macho ni bora. Nimeangalia bati inavyoanza kutengenezwa, bati ya *gauge* 30 ukiishika ni sawa na bati ya *gauge* 28, bati ya *gauge* 32 ukiishika kwa mkono kama vile ina 30 pale *Lodhia Industries* na mzigo umejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda *godown* mzigo umejaa nikawauliza huu mzigo kwa nini umejaa? Wanasema kule sokoni kuna shida bati zetu zikienda zinaonekana zina bei kubwa, zile za wenzetu wageni, sitaki kutaja ni nchi gani mnaijua zina bei chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bati wakati linagongwa likianguka kutoka juu likafika chini, linatoboka utafikiri limetobolewa na majani jinsi ambavyo ni duni, kwa hiyo ninaiomba sana Serikali tuongeze kodi, tulinde viwanda vyetu vya ndani kwa sababu vinaajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lodhia pale kuna ajira 500, *MMI Steel* kuna ajira 300 za *direct* ambazo ni vijana wetu wa Kitanzania wameajiriwa, kwa hiyo kuna faida ya kodi, kuna faida ya ajira, kuna faida ya bidhaa bora kwa Watanzania, tutakuwa tumewatendea haki sana tukilinda viwanda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni tulikuwa tuna haja ya ku-*import,* lakini sasa hatuna haja ya ku-*import* kwa sababu viwanda hivi vinaweza, simenti tumeweza, sasa kwenye bati tunaenda, nondo tumeweza, sukari usiseme miaka mitatu ijayo habari ya vibali itakuwa haipo tena, kwa hiyo nchi yetu inakuwa na hii ni kutokana na uwezo mkubwa wa Rais wetu, jinsi ambavyo anaziacha fursa, anaachia bajeti mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana Wizara hii iko vizuri, watendaji wa timu Rais ameipanga nzuri tuongeze bajeti Waziri wa Fedha kwenye *Finance Bill* tafadhali kaka yangu mahali popote alipo, aangalie namna ya kurekebisha kodi za watu wanaoingiza hizi bidhaa nchini ili tulinde viwanda, tulinde ajira za

vijana wa Kitanzania. Viwanda hivi vikifungwa kuna ajira nyingi sana zitapotea, nilitaka niseme hilo kwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika viwanda vya vileo kuna maneno mengi sana hapa, ooh! vileo vinaharibu watu na nini? Hiyo ni tabia ambayo inabidi tuwajenge watoto wetu na wazazi wetu, unywaji wa pombe uendane na maadili, hatuwezi kuzuia viwanda vya pombe kwa sababu vimeajiri. Kwa mfano, hiyo *super brand*, hiyo *MATI brand* aje na kule kwangu Mkalama Ndugu yangu, maana yake tatizo nadhani wanasema wanang'ang'ania huku Babati kwa sababu ya maji, nasi tutapata maji ya Ziwa Victoria hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri alete kiwanda na huko Mkalama, aajiri na huku watu wetu, najua wengi watatoka pale pale, hawa Watanzania wanaotengeneza hivi viwanda vya ndani ambavyo vinaleta ajira tuwalinde, tusiwavunje moyo, kama unywaji wa pombe unakwenda kinyume, basi ile Wizara inayohusika na maadili twende tujipange vizuri, Bunge hili tujipange vizuri tuhakikishe kwamba pombe inayonywewa na watu wenye umri unaohusika, wenye kipato kinachohusika kwa kiwango kinachohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa unyenyekevu ninaunga mkono hoja, hongera sana Mawaziri waendelee na kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gallos, Mheshimiwa Kamonga, na Mheshimiwa Kunti wajiandae. (*Makofi)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kabisa kwa kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Wizara nzima na Watendaji wote tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu wa hii Wizara hapendi kusifiwa hata tukiwa kwenye Kamati tunapata shida tunapomsifu. Sasa tutaacha kumsifu lakini tutamshukuru kwa mambo makubwa

anayoyafanya na anayoisaidia Serikali na nchi hii. Hapendi mwenyewe nadhani kwa sababu hataki kulewa sifa, lakini sisi tutampongeza kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya nchi hii, kwa kujitoa usiku na mchana kuhakikisha Taifa hili linakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri na Naibu Waziri wake, kaka yetu Mheshimiwa Jafo tunampongeza. Ninaanza kumpongeza kwa kitendo cha juzi uaichokwenda Kariakoo, huu ndiyo uzalendo, haiwezekani ndugu zetu wa Kariakoo wanafanyabiashara kuna watu wageni wanafanyabiashara pasipo kufuata utaratibu. Twende tufanye tathmini nchi tunazozitembelea tuangalie Watanzania wangapi wapo kwenye mataifa ya nje wanaopewa vibali vya kufanya kazi au wana uwezo wa kuweka hata kibanda cha kusema yeye anauza *chips* na mishkaki ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu nampongeza, muda mchache nilimsikia mtu anasema Wizara ifutwe, hii Wizara haifutwi. Wizara hii ni kati ya Wizara zinazowasaidia Watanzania, ajira nyingi za vijana wa Tanzania ziko kwenye Wizara ya Viwanda. Kaka yangu Jafo ninakuomba endelea na Watendaji wa hii Wizara maana watendaji wote ni wazuri, angalieni namna mtakavyowakomboa vijana wa kitanzania kwenye suala la ajira, jibu kubwa la vijana wa Tanzania ni suala la upatikanaji wa ajira, njia rahisi ni suala la kuongeza viwanda na kuona nini tunakifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza kwenye suala la Mchuchuma kwa kuwa nami ni Mjumbe wa Kamati hii, ninaelewa kinachoendelea kwa undani. Ninampongeza kwa hatua aliyofika si chini ya bilioni 15.4 zinaendelea kulipwa wananchi. Naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri aendelee, kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Liganga na Mchuchuma ni majibu pia kwa viwanda vyetu vya ndani. Sasa hivi kaka yangu katoka kuzungumzia kuna Kiwanda cha Lodhia, Mheshimiwa Waziri alitupeleka kwenda kukagua, tulikwenda Mkuranga

kukagua. Baada ya ziara hii ndipo tunapokuja kufanya kazi Kamati tukiwa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wawekezaji waliomo ndani ya Tanzania mtiririko wa kodi walionao kodi zote wanalipa halafu viwanda vyao, bidhaa zao hazifanyi kazi! Huu kwetu tumeweka mkakati maalum kama Kamati kuwasemea wazalishaji wa ndani maana ni jukumu letu kama Kamati. Haiwezekani kuwaona wanadidimia sisi tunaridhia bidhaa zinazotoka nje na sisi ni jukumu letu kama Wabunge kusema alindwe kwanza aliyewekeza ndani, hatukatai wa bidhaa kutoka nje lakini tuchukue fursa, Mheshimiwa Waziri achukue fursa ya kumlinda mwekezaji wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amfikirie mwekezaji wa ndani, ametengeneza ajira ngapi? Amfikirie mwekezaji wa ndani ananunua malighafi ngapi kutoka ndani? Liganga na Mchuchuma nayo itakuwa miongoni mwa wao kuweza kuendesha biashara zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili linalozungumzwa la pombe, suala la pombe takribani kwa Tanzania ukija kwa dini zetu kubwa zote mbili ya Kiislamu na ya Kikristo pombe hairuhusu, lakini kwa maadili pia tunayolelewa kama Watanzania pombe hairuhusiwi. Kama tumeamua Serikali haina dini, tumeamua kuacha watu wafanye biashara tuangalie penye tatizo, tuangalie tatizo liko wapi? Mimi Tauhida kusikia vijana wa hii nchi wanaharibikiwa kwenye suala la pombe siridhii, lakini nimejiridhisha kwa kuuliza na kuhoji ubora wa hizo pombe kali zinazotengenezwa, Mheshimiwa Waziri kuna namna ya kuchukua hatua, moja ya hatua ni kufanya uchunguzi kwenye maduka ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Tanzania hii halijulikani duka la pombe, duka la chakula, au duka la nyama. Leo tutamchukulia kama kaka yangu, ndugu yangu mmoja anaitwa Mati yupo Babati niliwahi kumsikia dada yangu Mheshimiwa Gekul. Tutaenda kusema kwamba, labda uwekezaji wake siyo sahihi,

hapana tusimhukumu; ametumia fursa na fedha aliyokuwa nayo kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililokuwepo ni unyonge wa sheria yetu. Dada yangu Ashura aangalie, akiwa kama mama maeneo gani tunaweza kuitetea na kuisaidia Tanzania. Aangalie eneo hili na kwenye hii Sheria yetu ina miaka 57 tunarekebisha wapi? Leo hakujulikani pombe kama iuzwe mchana au usiku. Tusimhukumu mwekezaji wakati yeye hana kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna suala la *TANTRADE*. Dada yetu Latifa amejitahidi vya kutosha, *TANTRADE* zamani ilikuwa inaonekana kwamba ni suala la Sabasaba. Hivi ndiyo tulivyokuwa tukielewa sisi Wabunge ndani na nje, lakini tuiangalie sasa imefika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanawake wamo ndani ya Wizara, ninatamani niwataje wote maaana ninawafahamu wanafanya kazi nzuri. Leo angalia, sisi maonesho ya mwisho tuliyokwenda tunahoji lakini kulikuwa na ushiriki wa nchi 10 lakini sasa hivi kuna ushiriki wa nchi 24 za kigeni na watu wanakuja kufanya biashara hapa. Kwa nini inapostahili Wizara kupewa pongezi isipewe pongezi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dada yetu jina nimelisahau anasimamia kwenye masuala ya elimu ya biashara na yeye ni mwanamke anafanya vizuri; ninatamani jina lake ningelipata. Mheshimiwa Waziri ana wafanyakazi wazuri, Katibu Mkuu mzuri, Naibu Katibu Mkuu na watendaji waliopo ndani ya Wizara hii ni wazuri, wasukumeni Tanzania. Waziri ana *speed* ambayo Mheshimiwa Rais anataka twende. Mheshimiwa Rais anatumia nguvu, akili na uwezo wake kama mama kuona Taifa linasonga mbele. Tusonge naye tusimame naye. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante kwa hayo machache. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Kamonga wakati huo Mheshimiwa Kunti, Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Lulida, wajiandae.

Mheshimiwa Kamonga hayupo? Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia wasaha, ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii. Nianze kwa kuwapongeza Wizara. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, lakini baadaye ikabadilishwa tukaletewa viwanda, maji ikatoka. Huko nyuma kabla ya kuingia kulikuwa na sintofahamu nyingi mambo yalikuwa hayaendi, lakini baada ya uwepo wao, Rais kubadilisha, kaka ame-*fit* (anatosha na *change* inabaki) yeye pamoja na timu yake yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna mambo kadhaa ninatamani niyaseme na kwa kuwa ninajua wao ni wasikivu na ni watu ambao wanatamani Taifa letu na wafanyabiashara wetu ndani ya Taifa letu waweze kufanya biashara na Taifa letu tuweze kujenga huu uchumi, nina hakika watayachukua na watayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni suala la upatikanaji wa leseni kwa wafanyabiashara wetu ndani ya Taifa letu. Mheshimiwa Waziri suala la upatikanaji wa leseni huko nyuma tuliwaambia wananchi wetu kwamba, watakuwa wanapewa muda wa miezi sita afanye biashara ndipo alipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwa uhalisia uliopo nje huko mtaani kwa wafanyabiashara wetu, anapokwenda Manispaa kuchukua leseni ya kuanza kufanya biashara anatakiwa kuwa na *TIN number.* Ili awe na *TIN number* ni lazima akadiriwe. Huyu mtu anakadiriwaje ilihali hajaanza kufanya biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sheria hii ibadilishwe. Hicho kitendo na kauli waliyoisema Serikali, wafanyabiashara kupata miezi sita ili waweze kufanya biashara ndipo walipe kodi, basi Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara ya Fedha wakae chini watengeneze mfumo ulio bora wa kuweza kuwasaidia wafanyabiashara wapate leseni kabla ya makadirio, wafanye biashara na hatimaye ndiyo waende wakalipe kodi ndani ya Taifa lao. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye biashara hiyo hiyo na mwaka jana nilisema kwamba, kwenye suala la biashara leo upatikanaji wa leseni pamoja na ulipaji wa kodi. Mfanyabiashara leo ana kodi lukuki kwenye taasisi mbalimbali. Hizi taasisi Mheshimiwa Waziri tunamwambia haya kwa sababu yeye ndiye mratibu wa shughuli za biashara. Ndiyo tunajua yupo na wafanyabiashara. Huyu mfanyabiashara anatakiwa kwenda Manispaa*, TRA, OSHA*, na *Fire*, ana mlolongo wa taasisi anazotakiwa kuzifuata. Akiamua kwenda kutafuta leseni ama kulipa na kuchukua hizo *control number* anatakiwa kupoteza siku mbili mpaka tatu anahangaika na hizi taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeweza kuweka vituo jumuishi kwenye mipaka yetu, tunashindwa nini kuweka vituo jumuishi kwenye halmashauri zetu ili wananchi wetu wakapata huduma kwa wakati na wakaweza kufanya shughuli zao nyingine kuwapunguzia huo muda wanaoupoteza? Kwa hiyo, niombe pia walione suala zima la kuwa na kituo jumuishi ndani ya halmashauri zetu, ili hawa watu wote wawekwe eneo moja na hatimaye mfanyabiashara wetu anapokwenda kutafuta huduma apate kwenye eneo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; kwenye suala hilo la kupata hizo huduma ni suala zima la uchangiaji wa hizo kodi. Tunawaomba TAMISEMI, Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri yeye ambaye ndiye msimamizi wa biashara wazungumze. Hizi fedha tuziweke kwenye kapu moja huyu mfanyabiashara anapokwenda kulipa, akalipe kwenye kapu moja. Watengeneze mfumo wa kuzisambaza kwenye hizo taasisi ili tumwondolee mfanyabiashara mzigo wa kuhangaika na kutapatapa na *control*

*numbers* za kila taasisi. Kwa hiyo, tunamwomba sana kwenye hilo aweze kuwasaidia wafanyabiashara wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine limesemwa pia na Wabunge wenzangu ni suala la *scanner* kwenye mipaka yetu. Leo mipaka yote ya nchi nzima tuna *scanner* mmoja tu kwenye mpaka mmoja. Mheshimiwa Waziri tunapoteza mapato. Ninaomba Waziri kama msimamizi wa Wizara lakini ndiye anayesimamia sera, azungumze na Waziri wa Fedha atusaidie kununua *scanner* kwenye hii mipaka, ili tuweze kukusanya hizo kodi ambazo zitakuwa stahiki kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, nimwombe sana suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninatamani kulisema ni suala la stakabadhi ghalani. Nishukuru mfumo huu lakini ninachotamani kuwaomba Wizara ya Viwanda kupitia stakabadhi ghalani wakishirikiana na Wizara ya Kilimo; la kwanza, ni elimu kwa wananchi wetu na la pili, watusaidie kuondoa mtu kati ambaye ndiye anaharibu mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu huko wapo salama lakini huyu ambaye halimi, hafanyi chochote ndiye anatuharibia huu mfumo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Waziri wa Kilimo wasimamie, wasaidie wakulima huyu mtu kati anayekuja hapa kama hawawezi basi wawaache wakulima wetu waende wao ndiyo wafanye hiyo biashara wauze mazao yao kwa uhuru, ili waweze kupata hiyo faida badala ya kuja kuendelea kuwanyonya wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye stakabadhi ghalani; Mheshimiwa Waziri maeneo mengi hatuna maghala. Niwaombe Wizara waone namna bora ambayo wanaweza kutuletea maghala yanayohamishika ama yanayotembea, ili kwenye yale maeneo ambayo hayana maghala watusaidie kuyasogeza. Moja; watawasaidia wananchi wetu kupata hiyo huduma na kuhifadhi, pia na gharama za usafirishaji na upotevu wa mazao utapungua kwa kiasi kikubwa kuliko leo ambavyo tunahangaika kusafirisha mazao kutoka eneo moja kwenda lingine ambalo pia ni la umbali mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie Bunge lililopita, kuna watu wa *Vodacom* walikuja hapa na hili ninamwambia Waziri kwa sababu ni mtu wa biashara. Tulipewa semina kuhusu hisa za *Vodacom* na baadhi ya Wabunge na Watanzania huko nje walinunua hizo hisa, lakini mpaka leo hisa zile hatujui kinachopatikana, zilishapotelea wapi, hakuna chochote kinachojulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atusaidie, hisa za *Vodacom* ambazo tulikuja Wabunge tukaelimishwa hapa ndani na zikatangazwa huko nje, wananchi wakanunua hisa zile mpaka leo kumekuwa kimya. Mtu ana hisa za shilingi milioni 10, analipwa shilingi 120,000 kwa kipindi cha miezi sita. Huu ni utapeli kama utapeli mwingine na hiyo haiwezekani Taifa letu tukawa tunaendelea kuleta watu wanatangaza fursa nzuri lakini matokeo yake kwenye utekelezaji unakuwa ni tofauti. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante. Mheshimiwa Paresso, wajiandae Mheshimiwa Lulida na Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na wachangiaji wote kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya kusimamia Sekta ya Biashara na Viwanda nchini. Matumaini yetu sisi kama Wabunge ni makubwa juu yao, lakini matumaini ya wenye viwanda na wafanyabiashara kwa ujumla pia ni makubwa wakiamini kabisa kwamba changamoto zilizoko kwa namna moja ama nyingine zitaenda kwisha na kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo nipongeze sana Shirika la *TBS* kwa kazi kubwa wanayoifanya ambayo kwa kweli yanaendana na mazingira ya sasa. Pamoja na kwamba kuna nyakati fedha wanazotengewa hazitoshi kutimiza majukumu yao, lakini wanajitahidi na nimpongeze sana Mkurugenzi Dkt. Ashura kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na anayoendelea kuifanya; tunamtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TBS* Mheshimiwa Waziri kwa hali ya sasa hatutegemei tuwe na maabara moja peke yake ya kupeleka sampuli mbalimbali Dar es Salaam. Kwa kweli kwa karne ya leo kulingana na changamoto ya kimazingira tuliyonayo tulishapaswa kuwa na maabara kwenye kila mkoa na si kila kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kupitia bajeti hii ambayo tunaipitisha sasa tunatarajia kuwa na maabara nyingine Arusha ambayo ni moja tu. Bado uhitaji ni mkubwa, kwa hiyo ni lazima tufikirie umuhimu wa kuwa na maabara kwenye mikoa yetu ili kupanua wigo na kufanya kazi za Shirika ziwe rahisi. Sampuli ziwe zinafika kwa wakati, zinafanyiwa vipimo na kuja na majibu. Pia, hawa ambao wanaohitaji huduma waweze kupata kwa urahisi tuondokane na hii dhana ya kufikiria tu sampuli lazima iende Dar es Salaam kwenye maabara iliyopo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kuhusu wakulima na hasa wakulima wa zao la vitunguu na kwa kipekee kabisa katika eneo la Wilaya ya Karatu. Kuna changamoto kubwa sana ya vifungashio vya mazao ya vitunguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kifungashio sahihi kilichothibitishwa ambacho wakulima wanakitumia na ndicho ambacho kinaeleweka ni uhalisia wa kilo ngapi au idadi ngapi. Sisi kule Karatu kwenye Bonde la Eyasi, hivyo vifungashio vinavyoitwa neti, vina majina yake. Kuna Neti ya Magufuli, Neti ya Samia, Neti ya Mkenya na Neti ya Mganda, lakini ukiangalia hizi neti ambazo wakulima mazao yao vitunguu yanawekwa pale, kila neti ina ujazo wake ambao haueleweki. Kila neti ina *style* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imekuwa ikiwakandamiza sana wakulima kwa sababu hizi neti zina ujazo kupitiliza. Mtu anaweza kukwambia mnunuzi anaenda anasema hii neti nanunua kitunguu hiki lakini nitatumia neti husika labda Neti ya Mkenya, Samia, au Magufuli ambayo ina viwango tofauti vya ujazo. Imekuwa ikiwaumiza wakulima kwa kiwango kikubwa sana sambamba na ujazaji wa vipimo kupitiliza maarufu kama lumbesa ambayo imewaumiza wakulima muda mrefu sana, mkulima ananyanyaswa. Tunatamani kuona Wakala wa Vipimo wanasimamia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wameziachia halmashauri, lakini hazina uwezo kwa kiwango hicho. Yaani halmashauri hiyo ipambane na madaraja, shule, wafanyabiashara wawe na leseni, mengine na ipambane tena na lumbesa? Kwa kweli uwezo ni mdogo na hawana watu wa kusimamia haya. Mheshimiwa Waziri tunaomba sana Wakala wa Vipimo wakasimamie suala la ujazo kupitiliza ambalo linawaumiza wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea leo wakulima wa nchi hii siwaongelei tu wa Karatu. Ukisema unabananisha Karatu wanahama, wanakimbia kwenda Moshi au Singida kwenda kununua vitunguu. Hili linatakiwa liwe agizo na kusimamiwa kwa nchi nzima. Wakati mwingine tuna sheria nzuri sana, lakini utekelezaji na usimamizi wa sheria ndiyo changamoto kwa sababu hatuna rasilimaliwatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninaomba niwasilishe kilio cha wakulima wa vitunguu katika Bonde la Eyasi, Jimbo la Karatu; kwanza, wanaomba wawafikie, wazungumze nao, wakubaliane, mkulima afaidike na kilimo chake siyo anapata hayo manyanyaso ya kiwango hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopiga marufuku tupige kwa nchi nzima, ili kama wakiona Bonde la Eyasi mambo yamekuwa magumu akienda Singida anakuta *the same,* akienda *West Kilimanjaro* anakuta *the same* na kwingineko anakuta *the same.*

Tunaomba sana tusimamie upimaji wa vitunguu hivi viwe kwa kilo na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni changamoto ya wageni kufanya biashara. Imekuwa ikizungumziwa sana hapa na nimpongeze Mheshimiwa Waziri tumemwona kule Kariakoo akiingia *field* kuangalia. Ni lazima tufike mahali tu-*categorize* na kuona ni biashara ipi ambayo atapaswa kufanya mgeni kwa mtaji upi katika eneo na mazingira yapi. Tukiachia mpaka Wachina wanaenda kuuza nyanya na mchicha, mama zetu wafanye nini? Haiwezekani, yaani tutakuwa na nchi ambayo haina utaratibu au wastaarabu, hatuwezi kuwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe na nchi ambayo kwanza inawajali watu wake, lakini haiwakatazi watu kuja kutoka nje na waje kwa utaratibu, sheria na kuwaainishia maeneo ya kufanya kazi na biashara. Hapo tutakuwa tumewasaidia wafanyabiashara wetu, pia akinamama na vijana wa nchi hii, ambao kwa namna moja ama nyingine wamekuwa na changamoto ya kukutana na vikwazo katika ufanyaji biashara katika maeneo mbalimbali.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tena?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha hamna taarifa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele bado. Jambo la mwisho; tusiwe na dhana ya kufikiria kutunga sheria kuweka vizingiti vikubwa kwa kuhofia watu kuja kutoka nje eti wasiwekeze. Tukiwa na ubora wa vitu vyetu *automatic nature* ita-*take place*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Paresso. Kwa mujibu wa kanuni kama bado una hoja nyingine mwandikie Waziri na atapokea atakujibu.

Mheshimiwa Lulida, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Dkt. Jafo na Naibu wake, Katibu Mkuu Dkt. Hashil Abdallah na Naibu Katibu Mkuu, Suleiman Serera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nimpongeze Mwenyekiti wa Wafayabiashara Tanzania Ndugu Khamis Livembe akishirikiana na wadau wake wakiwemo akina Mariam Lulida ambao wanakwenda katika kongamano kubwa la kuhamasisha Watanzania kuingia katika biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kwa muda huu wa miaka michache wa Utawala wa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, tunaona mabadiliko makubwa katika upande wa viwanda. Ninakwenda Lindi kutoka Dar es Salaam mpaka unamaliza Mkuranga yote ni eneo la viwanda. Hii inakwenda mpaka Mkiu ni eneo kubwa kote humu ni viwanda, hayo ni mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuranga ilikuwa inaonekana kama ni Wilaya za watu maskini sana, lakini sasa hivi imeleta ajira kubwa na mabadiliko makubwa katika maeneo hayo. Kutoka Dar es Salaam – Kibaha mpaka Chalinze ni maeneo ya viwanda. Uwekezaji wa ndani ndio una maslahi makubwa kwa vile ajira zinakuwa za ndani na zinawasaidia watu wa ndani kutoka kupata uchumi kupitia ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana katika uwekezaji mkubwa ambapo Kamati tulikwenda kutembelea kule Kigamboni Kiwanda cha *Saturn* ambacho kinatengeneza *truck* kubwa na sasa hivi inatoa *trucks* angalau 1,000. Tanzania ni mabadiliko ambayo tulikuwa tunayatamani, ilikuwa kila siku

tunaagizia magari kutoka nje. Kumbe Tanzania yenye maendeleo chini ya Utawala wa Mheshimiwa Rais inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatembelea Mkiu wewe unatoka huko. Mkiu leo ndiyo wanatengeneza *tiles* zote unazoziona zinakwenda Rwanda, Kenya, Uganda, Burundi Malawi, yote hii ni Tanzania tunatengeneza vile viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitembelea Kiwanda cha *Gypsum* kinaitwa *KNAUF*. Kwa kweli zile *gypsum* zake, tulikuwa tunaagizia *gypsum* ukikaa muda mfupi tu unaona zimeanguka, lakini tuna *gypsum* bora kabisa ambazo zinatoka Mkuranga. Hii ni maendeleo tunayoyataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maendeleo haya ninataka nitoe angalizo moja, nina hoja ambayo nilikuwa nayo kwa muda mrefu. Tusione aibu Mheshimiwa Waziri amepewa nafasi na Mwenyezi Mungu na mama Mheshimiwa Rais amemwamini. Akishirikiana na timu yake, nina hoja ambayo inanifanya kwa muda mrefu ninasikitishwa sana. Tulikuwa na Viwanda vya Korosho 13 vimefungwa mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninaomba tafadhali aje anipe majibu anauweza huu mfupa wa kuhakikisha viwanda hivi vinarudi na vinafunguliwa? Kama wapo wawekezaji ambao ni wa ndani wanafanywa nini mpaka sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vile vilikuwa ni vya korosho, mojawapo ilikuwa ni Kiwanda cha Lindi, Mtama, Newala, Mtwara na Kibaha, vyote vimefungwa toka mwaka 1997, tunazungumza miaka mingapi leo viwanda hivi vimefungwa? Wanataka korosho zetu zipelekwe nje *as a raw material,* kupeleka ajira nje. Kwa kweli siridhiki na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba *CAG* au Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tafuteni njia ya kuwaita wafanyabiashara hawa, wasirudishe nyuma maendeleo ya Tanzania. Tunataka kwenda na maendeleo ya *12G*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kiwanda kikubwa cha *General Tyre,* Arusha, tukatengeneza mpaka miti ya kutoa mpira. Kile kiwanda kilikuwa, Tanzania miaka hiyo ya nyuma, tuna *tyres* bora za magari yetu kutoka Arusha. Kile kiwanda kimefungwa. Nani amefunga?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kama kuna Sheria ije irekebishe, apatikane mwekezaji mwingine kazi iendelee. Tulikuwa na viwanda vya nguo Tanzania; Kiwanda cha Urafiki, Kiwanda cha *Mutex*, Kiwanda cha *Mwatex*, *Sunguratex*, *Kiltex*, vimekuwa *godowns* sasa hivi. Hizi ni juhudi za makusudi zilifanywa kufanya uchumi wa Tanzania udorore, ili wao watuletee nguo mbovu kutoka nje; haikubaliki! Tanzania ya maendeleo ya viwanda chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na viwanda vya mafuta ya chakula, nitavitaja; kulikuwa na Kiwanda cha Mafuta ya *Okay* Tanzania, tulikuwa tunakula *Tanbond* yetu Tanzania, *Super G* yetu kutoka Tanzania, lakini kwa kweli, kwa makusudi na uhuni walioufanya wafanyabiashara hawa, wamehakikisha viwanda hivi havifanyi kazi. Mbegu za pamba zilikuwa zinatoa mafuta ambayo unaona kabisa ni mafuta safi, mpaka nchi za nje walikuwa wanachukua mafuta kutoa kwetu. Jamani, tumefikia mahali ambapo hatuwezi kukubali kufanyiwa mambo kama haya, *enough is enough*!

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania yenye uchumi wa viwanda inawezekana na Waziri, Mheshimiwa Dkt. Jafo, aliyepewa nafasi ninamwomba tafadhali, aliangalie na lipewe macho hili ili angalu vile viwanda vifunguliwe. Kwa nini vile viwanda vifungwe? Lindi peke yake ilikuwa inaajiri watu 1,000; nenda Lindi, hakuna kiwanda hata kimoja! Kwa nini wanavifungia? Kwa sababu gani wanavifungia? Ninaomba Waziri atakapokuja baadaye anipe majibu kwa nini kile kiwanda cha Lindi kimefungwa? Kwa nini kiwanda cha Mtwara kimefungwa? Kwa nini kiwanda cha Nachingwea kimefungwa? Kwa nini wananyima ajira kwa Watanzania kwa kuwaachia watu hawa kwa kuona aibu na muhali? Muhali umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote tushirikiane tuhakikishe hawa waliovichukua, viwanda, wanavirudisha kwa heshima na taadhima waliyopewa na Mheshimiwa Rais. Wamekaanavyo kwa muda mrefu, toka Mwaka 1997 mpaka leo, maana yake ni hawana dhamira nzuri. Ninaomba Mungu aibariki Tanzania na hawa waliowekeza warudi, kama ni Watanzania, wasitufanyie uhuni. Tumechoka, tumechoka, tumechoka! Tunataka mabadiliko ya kweli ya viwanda ili yamkomboe mtu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vinashirikiana na kilimo. Leo nikilima korosho yangu, Tandahimba, ninapeleka katika Kiwanda kilichopo Newala, nikilima korosho Mtwara ninapeleka Mtwara. Leo wamevifunga, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wametufungia ili kutufanya sisi tuwe maskini. Hakuna Mtanzania atakaye huu umaskini... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Lulida, kengele ya pili.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, nikiwa na hoja zangu hizo za viwanda virudishwe na sisi tuko tayari kusimamia. Ninakushukuru sana sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kushukuru sana Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri wanayofanya. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita nimepata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwako Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii nina masuala mawili, ambayo ningependa kuchangia na ikimpendeza

Mheshimiwa Waziri nipate ufafanuzi wakati wa kuhitimisha hoja yake:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Wilaya ya Kilolo katika eneo la Mbigili ilitenga na kukabidhi eneo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *CBE* na ahadi yako Mheshimiwa Waziri ilikuwa ujenzi huo ungeanza mara moja. Hadi sasa hakuna dalili zozote za ujenzi huo kuanza. Ningeomba Wizara yako ianze ujenzi huo kama ilivyokuwa imeahidiwa kwa kuwa eneo hili lilitolewa bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara iliahidi kufanya majaribio ya Kiwanda cha Sukari katika eneo la Mahenge, Wilaya ya Kilolo. Nimekuwa nikifuatilia *TEMDO* kwa muda mrefu na majibu ni kwamba, Wizara haijatoa fedha, kwa ajili ya ukamilishaji wa kiwanda hicho. Ombi langu ni kwamba, kiwanda hicho kiwekwe kwenye bajeti na ujenzi ukamilike ili majaribio yaweze kufanyika kwani uwekezaji huo una tija kubwa kwa Taifa na ni hatua kubwa kuwa na mitambo ambayo imezalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuishukuru Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa ya ukamilishaji wa Kiwanda cha Chai katika Wilaya ya Kilolo.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususani barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kinachoishia Aprili, 2025 Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya viwanda na pia kuna mwelekeo mzuri wa kuboresha mazingira ya biashara *(blueprint)*. Pia kwa kusimamia vizuri diplomasia ya uchumi, imejenga imani kubwa kwa wawekezaji ambao wameonesha nia

ya kuwekeza kwenye maeneo muhimu ya uchumi wetu. Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, imeendelea kutekeleza miradi mingi ya viwanda na pia kuboresha mazingira ya biashara *(blueprint)* kwa kuondoa tozo, ada na kodi ambazo zimekuwa kikwazo katika shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *blueprint,* Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Pamoja na jitihada za Serikali, bado kuna mahitaji makubwa ya viwanda vya kuongeza thamani ya madini, kuongeza thamani ya mazao yetu vijijini na pia kuna changamoto za uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza Serikali iendelee na msukumo wa kujenga viwanda vya mazao ili tuweze kuongeza thamani hapa nchini na pia kuzalisha ajira. Kutokana na neema ya kijografia, nchi yetu inazalisha mazao ya aina mbalimbali ikiwemo zao la pareto na Tanzania inaongoza Afrika, pia ni ya pili duniani kwa uzalishaji wa pareto. Uwekezaji zaidi kwenye Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kuna fursa kubwa ya kuzalisha mbolea na hata viuatilifu kutokana na pareto inayolimwa hapa nchini. Serikali ichukue hatua za kutafuta wawekezaji wa viwanda vya viuatilifu ambavyo mahitaji yake ni makubwa hapa nchini na hata soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina neema ya madini ambayo ni malighafi ya kutengeneza aina mbalimbali za mbolea. Madini aina ya *calcium* (chokaa ya kilimo) na *phosphate* inapatikana kwa wingi hapa nchini na malighafi muhimu kutengeneza mbolea aina ya *CAN* na *DAP* na hata *NPK.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa gesi ni fursa nyingine kwa viwanda vya mbolea aina ya *Urea* ambayo mahitaji yake ni makubwa sana Tanzania na duniani kote. Pamoja na madini hayo kuna madini adimu duniani kama vile *Niobium* ya Pandahill, Mbeya ambayo kuna fursa ya kujenga kiwanda cha kuchakata hayo madini ili kutengeza *Ferroniobium* ambayo mahitaji yake ni makubwa hapa nchini na pia nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, ninapendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya *Niobium* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani, ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *Niobium* ambayo inapatikana Milima ya Pandahill, Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inakabiliana na athari za kiuchumi kutokana *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium,* ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.* Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(modern manufacturing plant and smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa itachangia huduma za kijamii *(corporate social investment in community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana fursa za kijiografia, napendekeza msukumo zaidi kwenye *EPZ* na *industrial parks* hasa kwenye bandari zetu na maeneo yanayozunguka viwanja vya ndege kikiwemo Kiwanja cha Kimataifa cha Songwe kilichopo Wilaya ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali ichukue hatua za haraka kubadilisha matumizi ya eneo ya iliyokuwa *Tanganyika Packers* litumike kwa *EPZ* na *industrial parks* hasa kwa mahitaji ya viwanda mbalimbali ikiwemo vya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wimbi la wageni hasa Wachina kujishughulisha na viwanda vidogo vidogo na hata biashara ndogo ndogo. Ongezeko hili la wageni linaleta wasiwasi wa kuhatarisha ushindani wa kuelemea biashara na viwanda vinavyomilikiwa na wazawa kutokana na wageni kusaidiwa mitaji na nchi zao. Kutokana na wimbi hili la wageni, malalamiko yanazidi kusikika kuhusu namna raia wa kigeni, hususan Wachina, wanavyohodhi biashara na kuwapiku wafanyabiashara wa Kitanzania. Serikali iendelee kuchukua hatua za haraka kudhibiti wageni kufanya biashara au kuanzisha viwanda vidogo vidogo kinyume na sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza mkakati wa Serikali kwa kuanzisha Soko la Bidhaa *(The Tanzania Mercantile Exchange (TMX)*. Wizara ya Viwanda na Biashara iwe mstari wa mbele kuimarisha hili soko la bidhaa ambapo wauzaji na wanunuzi wanakutana na kubadilishana bidhaa na fedha katika mtindo wenye mpangilio na utaratibu maalum. Kuanzishwa kwa soko la bidhaa kutamwezesha mkulima kuweza kuuza mazao yake katika utaratibu unaoeleweka bila kulanguliwa. Pia soko la bidhaa linatupa mwanga na mwanzo mzuri wa kuboresha soko la madini kuwa sehemu ya *TMX*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo na Naibu wake Mheshimiwa Exaud Kigahe, Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Hashil T. Abdallah, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Suleiman H. Serera na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwenye changamoto zinazoikabili Sekta ya Viwanda hapa nchini na nini kifanyike kuzitatua. Ninachangia kwenye hili kwa sababu katika vipaumbele vya Wizara katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ni pamoja na kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda ni mojawapo ya nguzo muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu, kwa sababu uwepo wa viwanda huchangia kuzalisha ajira, kuongeza thamani bidhaa za ndani na mwishoni kuchangia uchumi wa washiriki na wa Taifa kwa ujumla. Viwanda vina umuhimu mkubwa katika kuongeza uzalishaji wa bidhaa na kujenga soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wake mkubwa, Sekta ya Viwanda inakabiliwa na changamoto nyingi zinazoweza kuathiri ukuaji wake na kufikia malengo ya kuchangia katika uchumi wa nchi tetu. Changamoto hizi ni kama vile ushindani wa bidhaa kutoka nje, ukosefu wa mitaji, gharama kubwa za uzalishaji, changamoto za kiteknolojia na upungufu wa ujuzi kwa wafanyakazi, upatikanaji wa malighafi za uzalishaji, ukosefu wa masoko ya bidhaa za ndani na ukosefu wa umeme na miundombinu ya usafirishaji. Mchango huu utajadili changamoto hizi na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuzitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto inayovikabili viwanda vyetu hapa Tanzania ni ushindani wa bidhaa za kigeni na uagizaji wa bidhaa nyingi kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya ndani hapa Tanzania vinakabiliana na changamoto ya ushindani mkubwa kutoka kwa bidhaa za kigeni zinazouzwa kwa bei nafuu. Bidhaa za nje huleta ushindani mkali na kufanya bidhaa za viwanda vya ndani kuwa ghali zaidi. Kwa mfano, wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati ninayohudumu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo tulipokea malalamiko kutoka kwa wenye viwanda vya mabati, mabomba, nondo, mabomba ya plastiki, sigara, bia na sukari kwamba wanakabiliana na ushindani kutoka kwa bidhaa kama zao za bei

nafuu zinazotoka nchi nyingine, hali inayosababisha viwanda vya ndani kushindwa kushindana na bidhaa hizo. Baadhi ya wenye viwanda walisema kwamba kuna kosa linafanyika la kuingiza baadhi bidhaa nchini bila kulipa kodi na bidhaa hiyo hiyo inayozalishwa nchini inakuwa na kodi lukuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hali hii, ninaishauri Serikali izuie uagizaji kutoka nje wa bidhaa zinazotengenezwa na viwanda vyetu ili kuhamasisha na kusisimua uzalishaji wa ndani. Pamoja na hili, ni muhimu mno kuhakikisha tunaweka utaratibu mzuri wa kisera na kisheria wa kulinda bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu vya ndani. Ni vyema viwanda vya wazawa vipewe kipaumbele cha msamaha wa kodi na kuweka kodi kubwa kwenye bidhaa kutoka nje ili kuchochea ukuaji wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni ya uhitaji wa mitaji mikubwa kwa uwekezaji wa awali katika ujenzi wa viwanda. Uanzishaji wa viwanda unahitaji mitaji mkubwa jambo ambalo ni changamoto kwa wananchi wanaotaka kuanzisha viwanda katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Hivyo basi, ni vyema Serikali na sekta binafsi wakashirikiana katika hatua mbalimbali ili kuwatafutia wananchi mitaji inayotosha kuanzisha viwanda. Vilevile Serikali inaweza kutoa vivutio kwa wawekezaji kama misamaha ya kodi, mikopo yenye riba nafuu na mazingira bora ya biashara ili kuchochea uanzishaji na ukuzaji wa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ujio wa teknolojia mpya za viwanda kutoka nje, viwanda vingi katika nchi yetu vinakabiliwa na changamoto ya kutokuwepo teknolojia za viwanda hivyo. Changamoto hii ni kubwa na kwa kiasi kikubwa huathiri ufanisi wa viwanda pale vinapoharibika. Kutokana na hili, ni vyema Serikali ikawasaidia wenye viwanda kuwekeza katika teknolojia mpya na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa ndani ili wasaidie kurekebisha kasoro zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikaongeza ushirikiano na wadau wa kimataifa ili kusaidia kupata teknolojia za

kisasa, kubadilishana maarifa na hapo baadaye haya yatasaidia kuboresha ufanisi wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupata suluhisho la muda mrefu na la kudumu, ni vyema kuimarisha mafunzo ya ufundi na teknolojia hapa nchini. Kwa kuwa na vituo vya mafunzo ya ufundi nchi inaweza kuongeza idadi ya wataalam katika Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni upatikanaji wa malighafi za uzalishaji; viwanda vingi vya hapa nchini vinahitaji malighafi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali. Kwa mfano, vifaa vinavyozalisha bidhaa za chuma, bati, plastiki, vioo huagiza malighafi hizi kutoka nje. Upatikanaji wa malighafi hizi kwa gharama nafuu ni changamoto kubwa. Gharama na kodi kubwa inayotozwa na Serikali kwenye malighafi hizi huongeza gharama za uzalishaji na kuathiri uwezo wa viwanda kuzalisha na kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali ifanye uwekezaji wa kimkakati ili rasilimali zetu za asili kama vile chuma, bati, magadi soda, gesi asilia viibuliwe na kutumika kwenye uzalishaji wa bidhaa za ndani hapa nchini. Kwenye zile malighafi za kuagiza kutoka nje, ni vyema Serikali ikatoa msamaha wa kodi kwa viwanda vinavyoagiza ili kutoa nafuu ya bei kwa walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni ile ya ukosefu wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hapa nchini; baadhi ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zimekuwa zikikosa soko la ndani kutokana na ushindani kutoka kwa bidhaa za kigeni zinazoingizwa bila kuzingatia kuvilinda viwanda vya ndani. Kwa mfano, viwanda vya nondo, sukari na mabati hapa nchini Tanzania vinakabiliwa na ushindani wa bidhaa zao dhidi ya zile zilizoingizwa kwa bei nafuu kutoka nje. Hali hii inafanya viwanda vya ndani kupoteza wateja na kupunguza mapato, hali inayodhoofisha Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali iimarishe Kitengo cha Intelijensia ya Biashara pamoja na kusaidia kufungua masoko

mapya ili kuhamasisha uuzaji wa bidhaa za viwanda vyetu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ya upatikanaji umeme katika maeneo mengi ya viwanda hapa nchini; umeme ni sehemu muhimu katika uzalishaji viwandani, lakini upatikanaji wa umeme wa uhakika imekuwa kikwazo kwa uendeshaji wa viwanda katika maeneo mengi hapa nchini Tanzania. Viwanda vingi hutumia umeme kwa ajili ya uendeshaji wa mashine na mitambo, lakini upatikanaji umeme wa uhakika ni changamoto. Kutokana na changamoto hii, viwanda vingi hutumia jenereta kuzalisha umeme kuendesha viwanda, jambo ambalo husabadisha gharama za uzalishaji kupanda. Changamoto hii huathiri ufanisi wa viwanda na hupunguza faida kwa wamiliki wa viwanda na hivyo kufanya bidhaa zinazozalishwa kuwa ghali zaidi katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali iwekeze kikamilifu na kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo yote ya viwanda nchini. Kama Serikali imeweza kupeleka umeme karibu vijiji vyote nchini, sioni sababu ya msingi ya kushindwa kupeleka umeme kwenye viwanda vinavyozalisha na kulipatia Taifa fedha. Kupeleka umeme wa uhakika viwandani itasaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni ukosefu wa miundombinu ya usafirishaji bidhaa kutoka viwandani; katika maeneo mengi hapa nchini kuna changamoto ya miundombinu duni ya barabara na reli ambazo zinatumika kusafirisha bidhaa kutoka viwandani na kwenda mikoani. Changamoto hii husababisha gharama kubwa za kusafirisha bidhaa na kuzifikisha kwa walaji. Ninaishauri Serikali iwekeze katika ujenzi wa barabara, reli na ununuzi wa miundombinu mingine ya mawasiliano kama meli na ndege ili kurahisisha usafirishaji wa malighafi na bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe kwa kusema kwamba changamoto zinazoikabili sekta ya viwanda ni nyingi na zinahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa Serikali, wamiliki wa viwanda na

wadau wengine ili kuzitatua. Ni vyema kwa pamoja washughulikie masuala ya mitaji, teknolojia, soko, ujuzi wa wafanyakazi na upatikanaji umeme ili kuimarisha Sekta ya Viwanda na kuongeza mchango wake katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uchapakazi wake, hakika Watanzania tunajivunia na wanawake tunajivunia yeye. Pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa uchapakazi wao na kuhakikisha wanaendelea kutatua changamoto za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue fursa hii kuendelea kuweka nguvu kwenye viwanda vidogo vidogo ili kuendelea kuzalisha ajira zaidi kwa wajasiriamali hasa akinamama, lakini pia kuendelea kuwasaidia wakulima kupata elimu ya kusindika mazao yao ili kuwasaidia zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, jiandae mtoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuchangia kwenye hoja hii iliyoko mbele yetu, lakini ninaomba nitoe maelezo kidogo kabla ya kuchangia. Kwanza kwa kuanza kuunga mkono hoja, kwa maana bajeti ya Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara ili tuhakikishe anatekeleza yale ambayo amepanga kwenye bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ambaye ametujalia uzima kukutana siku hii ya leo. Tatu, shukrani za pekee na pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameendelea kuiongoza na kuisimamia Wizara hii kwa weledi mkubwa, lakini zaidi kwa kuendelea kuniamini na mimi

kumsaidia Mheshimiwa Waziri, kama Naibu Waziri, katika Wizara hii muhimu. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais kwamba, nitaendelea kufanya kazi kwa weledi, utii na umakini mkubwa, ili kuhakikisha yale malengo na maono yake, ambayo ameyapanga kwa nchi hii yaweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua pia nafasi hii kukushukuru sana wewe, Mheshimiwa Spika, Wenyeviti, pamoja na Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano mnaotupa sisi, kama Wizara, ambao tumeendelea kuupata kutoka kwenu. Zaidi, ninachukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa kuendelea kunisaidia na kunipa ushirikiano mkubwa, ili niweze kutekeleza majukumu yangu nikiwa hapa Bungeni, lakini pia na kuwatumikia wa kule nyumbani. Ninajua kuna mambo mengi ambayo tunaendelea kuyafanya pamoja na ninawaahidi nitaendelea kufanya kazi kwa weledi kuhakikisha nchi yetu na Wanamufindi Kaskazini nao wanaweza kufaidika na weledi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kuishukuru sana familia yangu; kwanza mke wangu mpendwa, Rehema Mponzi, watoto wangu, pamoja na ndugu zangu wote ambao wameendelea kunitia moyo na kuhakikisha ninaendelea kufanya kazi vizuri ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia machache katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kijana mwenzangu, kwa weledi mkubwa na kwa upendo, ameendelea kuniongoza, kuhakikisha ninamsaidia katika nafasi hii ili yale ambayo ninayapanga yatekelezeke. Niseme kutoka moyoni, nimefanya na Mawaziri wengi, lakini huyu kwa kweli, ameweza kunifundisha namna ya kufanya kwa upendo na kutekeleza mambo yangu kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia maeneo mengi, lakini niseme machache kwa sababu ya muda. Moja, katika vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, karibu vyote vya mwaka huu

vimegusa maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, katika kipaumbele cha kwanza amesema tunataka tuendelee kuanzisha na kuendeleza viwanda vilivyopo, ambavyo tayari wamesema sana kwamba, tuvilinde. Pili, ni kutekeleza miradi ile ya kielelezo, ambayo wamesema mojawapo, kama Mchuchuma na Liganga, lakini pia, Mradi ule wa Magadi *Soda* na mengine. Zaidi tumesema kwenye vipaumbele, ni kuimairsha uzalishaji wa viwanda vya ndani, ili kuhakikisha sasa tunaendelea kutumia bidhaa zetu badala ya kuingiza zile bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi tumesema tunaendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara. Hili limesemwa sana na hasa tukiangalia kwa maana ya ukuajia wa Sekta Binafsi ya ndani ya Wazawa, lakini zaidi Mheshimiwa Waziri amesema tunataka tuone ni namna gani ya kuimarisha masoko ya ndani na ya Kimataifa. Moja ya maeneo ambayo yamesemwa sana ni hili la bidhaa zetu za ndani wakati mwingine kutokutumika au kukosa soko kwa sababu ya kuingiza au kupenda bidhaa za nje. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri alisema tuna ile Kaulimbiu yetu ya kusema 'Nunua Tanzania, Jenga Tanzania'. Maana yake ni, tununue bidhaa zetu, ili tuweze kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele kingine, Mheshimiwa Waziri amesema, ni namna ya kuboresha miradi na programu kwa jamii, ambayo inahusisha elimu, mafunzo na ujuzi na zaidi katika hili tunasema nini? Katika Wizara yetu chini ya taasisi zetu tumeanza, sasa kuna kitu kinaitwa 'Atamizi na Ubunifu'. Chini ya Wizara, Taasisi za *TIRDO*, *TEMDO*, *SIDO*, *CBE*, lakini nimepita na vyuo vingine, nao wameanzisha ujasiriamali, kwa ajili ya wabunifu vijana. Tunataka kusema nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tuendeleze mawazo ya ubunifu, ili vijana waweze kuja na miradi na ubunifu mzuri ambao utasaidia kuzalisha au kuongeza kipato. Mheshimiwa Mwita amesema kwa uchungu mkubwa pale, lakini na wengine pia. Tunataka vijana wetu hawa badala ya kufanya *betting* waje na

mawazo ambayo yatawasaidia kuingiza kipato na kujenga uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda pale Mzumbe, tayari nao wana bunifu za ujasiriamali. Kuna kijana mmoja alitoa *testimony* kwamba, alikuja na wazo akiwa mwanafunzi, amekosa *boom*, kwenye akaunti kuna 2,000, katika ile 2,000 akatoa 500 akatuma *message* kwa watu fulani anaowajua, akasema ninaomba nitume nifanye kazi, ili nipate kula. Alivyotuma mara ya kwanza amepata watu kumi, wanamtuma akanunue vitu wanampa 1,000, 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye akapata wengi wanahitaji kumtuma kwa hiyo, kupitia ubunifu huo ameajiri na wengine. Anatumwa, anapata 2,000. Siku ya kwanza alipata 30,000 kwa kutumwa kufanya shughuli fulani, lakini ametuma *message,* ujumbe kwamba, nitume nifanye kazi unipe hela ya kula.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Tunataka tuone vijana wabunifu ambao watazalisha, wataongeza uchumi, badala ya kucheza Bahati Nasibu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema. Hili litatusaidia pia, kuhakikisha hawa vijana wabunifu tunawaatamia kupitia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo yamesemwa kuhusiana na kuhakikisha tunatekeleza na kulinda viwanda vya ndani; moja ya maeneo ambayo Serikali inaweka jicho la mkazo sana ni kuhakikisha tunalinda viwanda vya ndani. Hapa hoja imesemwa kwamba, Sheria zipo, basi tusimamie. Sisi tunawahakikishia kwamba, kama Wizara, tutaendelea kufanya hivyo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la lumbesa, masoko ya mazao ya kilimo na maeneo mengine, kumesemwa sana hapa. Leo nimepata kifungashio kingine kinaitwa *net*. Wizara ya Viwanda na Biashara tumesema, na hii elimu tutaendelea kuifanya kwamba, vipimo si vifungashio, kifungashio siyo kipimo. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa elimu hiyo na hili tunawahakikishia

Waheshimiwa Wabunge, kwa ushirikiano wenu, ninaamini tutaenda kukomesha, kupunguza, bila kuharibu mahusiano kati ya taasisi zetu, kwa maana ya Wakala wa Vipimo na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka mkakati wa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Kilimo tuone ni namna gani katika maeneo tofauti tofauti tunaweka masoko. Katika masoko yale tutaweka mizani, ili wananchi, wakulima, wanavyouza waende kuuzia pale, sehemu moja, halafu wanapima, ili mfanyabiashara achukue, anunue, kutokana na vipimo badala ya kwenda kuwafuata kwenye mashamba ambako ndiyo wanafanya hivyo vifungashio vya *net* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara, tutaendelea kushirikiana na Bunge lako Tukufu kuhakikisha mawazo yote, ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge tunayafanyia kazi, kama nilivyosema. Bahati nzuri mengi yako kwenye vile vipaumbele saba ambavyo Mheshimiwa Waziri ameviweka katika mwaka wa fedha ujao, 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, mwenye hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mola, ambaye ametupa afya na uzima siku ya leo, nilipoweka hotuba hii ya Bajeti ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mapenzi yake makubwa sana katika Taifa letu hili. Mheshimiwa Rais analipenda Taifa lake na ndiyo maana mara nyingi huwa hapumziki, muda wote anahangaika, kwa ajili ya Watanzania. Mungu amwezeshe Rais wetu aendelee kuhakikisha

kwamba, anadumu na afya njema wakati tunaelekea katika Uchaguzi wa mwaka huu 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru wewe, kwanza kwa weledi wako wa *style* zako za kuendesha Bunge. Wewe ni Naibu Spika wa viwango sana na ninadhani watu wa Ilala lazima waige mfano huo, kwamba, wana kiongozi bora, ambaye anafanya kazi kule Ilala na hapa Bungeni kwetu. Hakika tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, ambaye ni Spika wetu, tunamshukuru sana kwa weledi mkubwa wa kuliongoza Bunge hili, pamoja na Wenyeviti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba ku-*respond* baadhi ya hoja. Kwanza ninaomba niseme nchi yetu inasonga mbele kwa kiwango kikubwa sana. Hili tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na tumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa weledi wake wa uongozi. Hakika amefanya mambo makubwa katika upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Ndiyo maana hapa nilisikitika sana, hata rafiki yangu Mheshimiwa Mpina, kana kwamba haoni chochote. Nilishangaa sana wakati akiwa ni Waziri, alikuwa ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binadamu lazima tufike wakati tuweze ku-*appreciate*. Ukifika muda kwamba, wewe kila siku huna jema, utaonekana una matatizo binafsi. Kama Serikali hii chochote inachofanya inaonekana haina jema, hata ku-*appreciate* chochote! Inawezekana utakuwa na matatizo binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtani wangu, niseme una *style* nyingi nyingi, lakini kwa kweli, mimi binafsi ni kijana mwenzako. Una kila sababu, Serikali inapofanya, ku-*appreciate* hata kwa *minimum*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu leo hii imeonesha. Kwa mfano miaka mingi, kihistoria, nchi yetu likuwa inaagiza mabati kiwango kikubwa; Kiwanda cha *ALAF* peke yake ndiyo kilikuwa

cha historia, kinatengeneza mabati hapa nchini. *Demand* ya mabati ya rangi nchini mwetu ni tani 130,000. Leo hii kupitia Kiwanda cha *ALAF* ambao wamefanya *expansion* ya kiwanda kupitia Kiwanda cha *LODHIA*, kupitia *MMI*, kupitia *King Lion*, uzalishaji wa mabati yetu umefikia tani 260,000. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nchi inasonga mbele. Kama tulikuwa hatufikii mahitaji yetu ya mabati leo hii tuna *surplus*, *demand* yetu ni tani 130,000 leo hii tumefika tani 260,000 halafu mtu anasema hakuna lolote linalotokea! Hakika ni ajabu kwa kweli. Katika hili tuseme kwamba, Serikali inaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pili ni mahitaji ya *cement*. Kazi kubwa imefanyika, mahitaji ya *cement* ni tani milioni saba, leo hii uzalishaji wetu umeenda tani milioni nane, milioni tisa, mpaka inaenda tani milioni 10. Tuna *surplus* ya tani milioni mbili katika nchi yetu, hii haijawahi kutokea nchi kuhakikisha tunafanya uwekezaji huo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tumeshuhudia uwekezaji mkubwa wa viwanda vya magari. Ukienda pale *Jef Trucks*, juzi nilikuwa kwenye kiwanda cha *Saturn*; mahitaji ya malori nchini mwetu ni wastani wa malori 11,000. Kiwanda cha *Saturn* peke yake...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina ninaona unaandika. Unasikia majibu yako huku?

Aah, kaa tu, sijakwambia usimame. Kaa tu. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ni malori 11,000. Leo hii *Saturn* peke yake wana *capacity* ya kuzalisha malori 9,000 ni kazi kubwa inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna viwanda, tulikuwa tunaagiza vioo nchini mwetu. Kiwanda cha *Sapphire* peke yake leo hii kimeweza kuhakikisha mahitaji ya ndani yote yanapatikana na kuweza ku-*supply* nje ya nchi. Hii ndiyo Tanzania ya

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo inafanya kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu, leo hii nenda Sekta ya Sukari, sisi nchi yetu tumekuwa *importer* mkubwa wa sukari, lakini leo hii angalia kazi kubwa iliyofanyika. Kiwanda cha Kagera *capacity* yake ni tani 131,000, Kiwanda cha Kilombero ilikuwa tani 130,000. *Expansion* ya Kilombero tunaweza kuzalisha tani 270,000; Kiwanda cha Mtibwa ni tani 80,000. Kiwanda cha Kilimanjaro ni tani 100,000 na kiwanda cha Mkulazi ambacho ni kipya, cha Serikali, ni tani 50,000. *Bagamoyo Sugar* imetengenezwa kipindi hiki, ni tani 50,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijumlisha kwa pamoja unapata tani 681,000. Mahitaji ya sukari nchini mwetu ni tani 802,000 ambapo *industrial sugar* ni tani 250,000 na *brown sugar* matumizi ya nyumbani ni tani 552,000. Ukijumlisha *buffer* utapata ni karibu tani 600,000 *plus*. Leo hii ukiangalia *capacity* hiyo, kama kutakuwa na *full capacity* ya *production*, maana yake tutakuwa na tani 681,000. Hii ni *brown sugar*. Ni nini maana yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya kipindi kifupi kinachokuja hatutokuwa na haja tena ya ku-*import* sukari katika nchi yetu. Haya maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kuonesha Serikali, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inafanya kazi kubwa sana. Leo hii kuna uwekezaji mkubwa, ukienda pale Rufiji kuna kiwanda, wenzetu wa *Lake Group* wanatengeneza kiwanda ambacho *capacity* yake kitazalisha tani 200,000 kwa mwaka. Tutapofika huko mbele maana yake tutakuwa hatuna haja kabisa ya kuagiza sukari ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa *tyres*. Leo hii uzalishaji wa *tyres* umekuwa mkubwa, umekamata mahitaji ya ndani na kuweza ku-*export*. Maana yake ni kwamba, nchi yetu inaenda kufanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilikuwa *importer* mkubwa wa *wall putty*. Tulikuwa tunaagiza *wall putty* kutoka nchi mbalimbali ikiwemo Nchi ya Misri. Leo hii ndugu zangu Watanzania na Wabunge ninaomba niwaambie, Nchi ya Tanzania *a wall putty* yote inazalishwa Tanzania, tena yenye ubora wa hali ya juu. Hii yote ni kazi kubwa mabayo imeendelea kufanyika katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Ndugu zangu ninaomba niwaambie, ukiangalia dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita, Mradi wa Mchuchuma na Liganga, mnafahamu ni mradi wa kihistoria, ulijadiliwa katika Bunge hili kwa miaka mingi sana, haijawahi kutokea. Kwa mara ya kwanza leo, Serikali ya Awamu ya Sita imeweza kutoa shilingi bilioni 15.5 kuweza kulipa fidia kwa wananchi wote. Piga makofi tafadhali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haijawahi kutokea. Angalia, tunafahamu mradi ule ulikuwa na kizungumkuti muda mrefu, leo hii Serikali imekubali, mpaka *share* za mwanzo za Serikali zilikuwa 20%. *Negotiation* inapanda mpaka *share* karibu 36%. Mradi ule ulikuwa ni mradi wa kudumu wa miaka yote. Kazi nzuri inaendeshwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemkabidhi kijana mwenzetu Dkt. Serera, ameongoza *negotiation* kwa uzalendo wa hali ya juu. Sasa leo hii leseni imeenda miaka 25, haijawahi kutokea katika Taifa letu hili, ni kazi kubwa. Ndugu zangu mnakumbuka Mradi wa Magadi *Soda?*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni *importer* mkubwa wa Magadi *Soda* nchini. Kwa mara ya kwanza utoaji wa fidia, ambao nimezungumza pale awali, watu wa Engaruka, watu wa Monduli, leo hii sasa maana yake tunaenda kutekeleza Mradi wa Magadi *Soda*. Kwa mara ya kwanza Afrika uzalishaji mkubwa utakuwa unatoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii yote ni kazi kubwa ambayo ninaomba niwaambie inataka *commitment* kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Rais

anayeongoza na sisi Wabunge. Ninaomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge. Wengi wamekuwa *supportive* sana. Ninaomba niishukuru Kamati ya Bunge. Hakika muda wote imekuwa ni mwalimu wa Wizara yetu, tunawashukuru sana. Hakika hatutawaangusha katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande mwingine ni suala zima la *TBS* kuhakikisha inakuwa na ofisi katika maeneo mbalimbali, upande wa maabara. Tunafanya uwekezaji, sasa hivi tunajenga maabara Mwanza, tunajenga maabara kubwa hapa Dodoma ambapo ukienda pale, eneo kama unaenda Nanenane, kuna maabara kubwa, ambayo mwezi Juni tutaenda kuweka jiwe la msingi. Matarajio yetu ni kwamba, maabara ile itakuwa ni kubwa zaidi kuifungua ndani ya mwaka huu 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule Arusha, halikadhalika, ujenzi wa maabara unafanyika. Kwa hiyo, suala zima la upatikanaji wa maabara ni kwamba, nchi yetu sasa, kupitia *TBS,* tunafanya uwekezaji mkubwa katika upande huo, lengo letu kubwa ni kuhakikisha tunapata fursa za watu kunafanya *testing* katika maeneo mbalimbali bila kutoa gharama yoyote ya kusafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia hoja mbalimbali na hasa za msingi, suala zima la viwanda. Mheshimiwa Mama Lulida, Mheshimiwa Mama Ishengoma na wengine wote; viwanda vilivyobinafsishwa, lakini havifanyi kazi. Ni kweli tuna viwanda vya korosho, ambapo kule Lindi, ukienda Tunduru, hivi vimekuwa ni changamoto kubwa. Ndiyo maana watakumbuka katika ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tulipokuwa Mkoani Tanga, alitoa maelezo mahsusi ya kuhakikisha jinsi gani baadhi ya viwanda vinaweza kufufuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, kupitia Msajili wa Hazina kazi hii inafanyika. Imani yetu kubwa ni yale ambayo yatawezekana, ambayo hayataleta mgogoro wa kisheria, tuweze kuhakikisha viwanda vile wanapewa watu wengine na kuona kwamba, viwanda vile vinaendelezwa. Lengo kubwa ni kwamba, nchi yetu ipate fursa kubwa sana. Tunafanya hivi kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu ya vijana wa Kitanzania. Takwimu zinatuonyesha Mwaka 2021 *graduates* walikuwa 54,000.8 leo hii wamepanda, wamefika karibu 67,000. *Absorption capacity* siyo ya Serikai ya Tanzania peke yake, isipokuwa dunia nzima. Hakuna Serikali, hasa kwa nchi zinazoendelea, itaweza kuajiri watu wote; *Private Sector*, viwanda na biashara ndiyo sehemu ya lango la kuajiri. Ndiyo maana katika eneo hili, ninaomba niwahakikishie kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sasa hivi itakuja na mpango mahsusi wa ujenzi wa viwanda wa miaka sita, utakaoanza mwaka huu mwishoni mpaka mwaka 2031.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yetu ni kujenga viwanda karibu 9,048 vitakavyoajiri watu milioni 6.5. Ajira za moja kwa moja ni watu 1,040,000. Wale milioni tano *plus* waliobaki hizi zitakuwa ni *indirect employment*. Lengo letu ni kwamba, eneo hili tutafungua suala zima la ajira kwa vijana wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kazi kubwa, lakini ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge. Sisi tumeyapokea yote. Lengo letu ni kwamba, haya tunaenda kuyafanyia kazi kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Ninaomba niwahahikishie tumejipanga vizuri, mimi, Naibu wangu na timu yetu Wizarani, Dkt. Hashil, Dkt. Suleiman Serera na watumishi wetu wote. Tumejipanga kuhakikisha kwamba, nchi yetu inasonga mbele. Ninaomba niwahakikishie hatutawaangusha hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, siyo kwa umuhimu, huu ni mwaka wa uchaguzi. Tumwombee sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hilo jambo kubwa. Tumwombee sana Mama, lakini kubwa, tuendelee kuliombea vilevile Taifa letu amani na usalama. Ninaomba niwaambie ndugu zangu, tunapojadili biashara hapa, viwanda haviwezi kuwepo bila amani na usalama. Kwa hiyo, jambo kubwa tuliombee Taifa letu. Ni kwamba, twende kwenye uchaguzi tuwe salama na amani, tusifanane na nchi nyingine ambazo zilipoingia katika mgogoro watu walisambaratika, mabwana wakabadilika kuwa watwana. Nchi hizo mnazifahamu hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, sina Taarifa rasmi ya mshahara wa Waziri. Kwa hiyo, Katibu tunakwenda kwenye *guillotine*.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 44 – Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………..………....Sh. 21,234,680,862
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*................Sh. 907,547,600
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…...............Sh. 3,142,724,000
Kifungu 1004 – *Government and Communication Unit*………………….……....................Sh. 627,960,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*……......…..............Sh. 603,560,000
Kifungu 1006 – *Legal Services Unit*…….……...............Sh. 687,973,000
Kifungu 1007 – *Management Information System*…………………………..........................Sh. 599,888,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*…………………………….............Sh. 658,671,110

Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*……………………...……………….........Sh. 585,692,000
Kifungu 2001 – *Industry*.............................................Sh.12,586,306,324
Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises Division*................................................Sh. 8,531,584,596
Kifungu 3001 – *Trade Integration Unit*........................Sh. 2,317,680,000
Kifungu 4002 – *Commodity Market Development*……………………….Sh. 41,416,429,508
Kifungu 5002 – *Economic Empowerment and Private Sector Development*............................................Sh. 0
Kifungu 6001 – *Research and Innovation Unit*……..................……Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 44 – Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……..………………........Sh. 1,150,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.................Sh. 22,666,825,000
Kifungu 2001 – *Industry*............................................Sh. 15,099,515,120
Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises Division*................................................Sh. 2,971,194,880

Kifungu 5002 – *Economic Empowerment and Private Sector Development*............................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**NAIBU SPIKA:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ninachukua nafasi hii kukupongeza sana kwa kazi kubwa uliyoifanya, wewe, Naibu wako, watendaji wako, Katibu Mkuu, Naibu na taasisi zako zote. Kwa kweli, maelekezo ya Mheshimiwa Rais mmeyatekeleza vizuri na mnafanya vizuri. Tulipotoka, tulipo na tunakokwenda ni tofauti sana. Sasa hivi yapo mabadiliko makubwa, tunaona baadhi ya viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa. Kwa hiyo, hongereni sana na *4R* za Mheshimiwa Rais zinafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Tunawashukuru wadau, Jumuiya ya Wafanyabiashara, ninaona wako hapa na kiongozi wao Mheshimiwa Severini. Endeleeni kushirikiana na Serikali na Mama Samia ameweka Tume Maalum ya Kodi, ili mlipaji apate haki na Serikali ipate haki; ya Kaisari iende kwa Kaisari na ya Mungu iende kwa Mungu. Kwa hiyo, hongereni sana wafanyabiashara kwa namna mnavyochangia uchumi wa Taifa letu na mnavyolipa kodi. Hongereni sana. *(Makofi)*

Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri mliyofanya. Kwa kutoa michango mizuri na Serikali imepokea na itakwenda kuifanyia kazi.

Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.45 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 15 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*